**21 APRILI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 21 Aprili, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**WAZIRI WA NISHATI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi Hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi Hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuingia kwenye Kipindi cha Maswali, kuna Mwongozo wa Spika Kuhusu Kitendo cha Mheshimiwa Ado Shaibu Ado kuendelea kuchangia hoja bungeni baada ya uda wake kwisha.

Waheshimiwa Wabunge, Tarehe 17 Aprili, 2026 katika Kikao cha 11 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge, wakati wa jioni, Bunge lilipokuwa limerejea, Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, Mbunge, alipata fursa ya kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mara baada ya muda wake kuchangia kwisha, Kiti kilimjulisha juu ya suala hilo, ili kutoa fursa kwa Wabunge wengine. Baada ya maelekezo hayo Mheshimiwa Ado aliendelea kuzungumza na hata baada ya kisemeo chake kuzimika, kuashiria kwamba muda wake wa kuchangia ulikuwa umekwisha. Kitendo hicho kilimuibua Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge, ambaye aliomba Mwongozo wa Spika ili kujua kama suala hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi.

Waheshimiwa Wabunge, Kiti kina mamlaka ya kuhakikisha utaratibu wa uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge unazingatiwa wakati wa mjadala. Vilevile, kanuni zimeweka masharti kwamba, uamuzi wa Spika kuhusu utaratibu ni wa mwisho. Haya yamefafanuliwa chini ya Kanuni ya 85(1) ya Kanuni za Bunge ya Mwaka 2025.

Waheshimiwa Wabunge, sote tunapaswa kuzingatia masharti ya kikanuni kuhusu muda wa kuzungumza Bungeni, na vilevile kutii Maelekezo ya Kiti kila yanapotolewa. Sasa kwa kuwa, Mheshimiwa Ado wakati alipokuwa anachangia hakuzingatia hayo kwa kuendelea kuzungumza wakati muda wake umekwisha na vilevile hakuacha kuzungumza baada ya kuelekezwa na Kiti, na vilevile, mpaka sasa tumeona kuna baadhi ya Wabunge wanafanya makosa kama hayo, hivyo, ni vyema kujirekebisha ili kujiepusha na vitendo hivyo vya utovu wa nidhamu.

Kwa mantiki hiyo, inaelezwa kuwa, endapo suala hili litajitokeza tena, taratibu za kikanuni zitachukuliwa kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za 2025. Kwa hiyo, namsamehe Mheshimiwa Ado kwa ugeni.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ni kwamba, Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, katika mchango wake aligusia kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2023/2024. Taarifa hiyo, pamoja na Taarifa za Ukaguzi za mwaka 2024/2025 zimepelekwa kwenye Kamati za Kudumu za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za umma, ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ambayo Mheshimiwa Ado Shaibu Ado ndiye Mwenyekiti wa Kamati hiyo. *(Makofi)*

Taarifa ya *CAG* aliyorejea ipo kwenye Kamati anayoiongoza na bado haijafanyiwa kazi. Kwa mantiki hiyo, nasisitiza na kuelekeza kuwa, masuala ambayo yamepelekwa kwenye Kamati, Wenyeviti wa Kamati hizo hawapaswi kuyazungumza nje ya vikao vya Kamati, ili kuzingatia taratibu zilizowekwa na Kanuni za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili ni chombo cha Wawakilishi wa Wananchi. Kwa mantiki hiyo, Bunge ni sauti halisi ya wananchi wa Tanzania kwa ustawi wa jamii zetu na kwa mustakabali wa Taifa letu. Hivyo basi, ni muhimu kuzingatia kanuni zinazosimamia taratibu za mijadala Bungeni kwa sababu, tunapozingatia taratibu hizo, hii mijadala itakuwa ina tija, na haitapotosha umma. Kwa kufanya hivyo, tunapunguza upotevu wa muda, hivyo kuwezesha Wabunge wengi zaidi kupata fursa ya kuchangia hoja.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kutumia fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuongoza mijadala Bungeni, tuendelee kuwapa ushirikiano kama mnavyofanya kwangu. Nasisitiza kuwa, kwa muda wote viongozi hawa wanapoendesha Vikao vya Bunge wanakuwa wanatekeleza Madaraka ya Spika. Kwa msingi huo, maelekezo ya Mwenyekiti wa Bunge yanayotolewa Bungeni ni maelekezo ya Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge za 2023. Hivyo, ni lazima tutambue na kuwapa heshima inayostahili.

Waheshimiwa Wabunge, Ripoti ya CAG 2023/2024, kama mnavyofahamu haijaletwa Bungeni bado. Kwa hiyo, maono ya CAG bado siyo maamuzi sahihi ya Bunge. Mheshimiwa Ado ndiye atatuletea Ripoti ya CAG 2023/2024 – 2024/2025 kwa pamoja. Kwa vile mwaka 2023/2024 uhai wa Bunge umekwisha, ripoti ile bado ipo mikononi mwa Kamati ya Mheshimiwa Ado. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ado ukimaliza ripoti yako utakuja kutuletea mapendekezo ndani ya Bunge hili na Bunge litatekeleza mapendekezo yako mtakapotushirikisha, mtakapotuamulia kwenye Bunge.

Ninaseme kwa Lugha ya Kiswahili, au lugha nyepesi. Tukikaa sisi hapa, sisi ni ma-*referee* siyo makocha. Hata mpirani wakati kocha anabadilisha mchezaji, mchezaji haingii bila ruhusa ya refa, na humu ndani kila kitu kinasimamiwa na Kiti. Ninaomba sana, tuna ugeni, tuendelee kujifundisha.

Katibu.

**21 APRILI, 2026**

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali. Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Mheshimiwa Profesa Lazaro Ndalichako.

Na. 144

### Ujenzi wa Barabara za Jimbo la Kasulu

**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Kasulu – Kigondo na Habitat – Hwazi, kupitia Mradi wa *TACTIC*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Kasulu ni miongoni mwa halmashauri za miji 45 inayotekeleza Mradi wa *TACTIC* nchini. Mji wa Kasulu uko kundi la tatu la utekelezaji wa Mradi wa *TACTIC* lenye miji 18. Katika mradi huu, Halmashauri ya Mji wa Kasulu imetengewa shilingi billioni 10.87.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *TACTIC* umekamilisha usanifu wa miradi ya Mji wa Kasulu wa Barabara za Makaburi – Kigondo, kilometa 3.77, Habitat – Hwazi, km 2.04, jumla ya kilometa 5.8. Mradi huu unahusisha pia ujenzi wa Stendi ya Mabasi ya Murus na Soko la Kumsenga, Kasulu. Baada ya kukamilisha usanifu wa miradi hii yote, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaendelea na taratibu za

maandalizi ya kuanza utekelezaji wa miradi katika kundi hili, ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Kasulu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndalichako.

**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Swali langu la msingi lilikuwa, ni lini ujenzi wa barabara hizo utaanza? Barabara ya Hwazi – Habitat ni mbaya sana na haitengewi fedha yoyote kwa sababu, tayari ipo kwenye Mpango wa *TACTIC*. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri awaambie wananchi wa Kasulu, ni lini mradi huu wa *TACTIC,* barabara hizo kilometa 5.8 zitaanzwa kujengwa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Tunafahamu mvua kubwa ambazo zinanyesha zimeleta uharibifu mkubwa wa barabara na Jimbo la Kasulu Mjini limeathirika. Kwa mfano, Barabara ya Kasulu – Kabanga – Muganza, Heru Juu – Munyegera na Kanazi – Msambara – Kabanga, zimeharibika na tumeziombea fedha za dharura. Je, ni lini fedha hizo za dharura zitapelekwa ili barabara hizo ziende kutengezwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Kasulu umewekwa kwenye mpango wa ujenzi wa barabara na miundombinu mingine kupitia *TACTIC*. Miongoni mwa miji 45, na halmashauri hii iko awamu ya tatu.

Mheshimiwa Spika, tulianza na awamu ya kwanza, utekelezaji unaendelea, awamu ya pili utekelezaji unaendelea na awamu ya tatu tuko hatua za mwisho za usanifu, kwa ajili ya kuanza kupata makandarasi na kuanza ujenzi wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Prof. Ndalichako kwamba, Serikali inaendelea kufanya taratibu za ukamilishaji wa usanifu, na mara baada ya kukamilisha

usanifu hatua za utekelezaji wa ujenzi wa barabara hizi na miundombinu mingine itaanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ni kweli kwamba, mvua imeleta athari kwenye barabara zetu na Serikali inaendelea kufanya tathmini mpaka wiki iliyopita. Tunahitaji kiasi cha shilingi bilioni 98, kwa ajili ya ujenzi wa barabara, kwa maana ya dharura, katika maeneo mbalimbali kote nchini ili kurejesha barabara kwenye hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hii aliyoitaja ni miongoni mwa barabara ambazo zitapelekewa fedha za dharura ili ziweze kupitika wakati tunasubiri mradi wa *TACTIC* kuanza kutekelezwa, kama ambavyo imepangwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Mji wa Isaka ni bandari kavu ndipo ambapo *Station* ya *SGR* inajengwa pale katika Mji wa Kahama, je, ni lini Serikali itaweka mpango wa kuujenga ule mji kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, barabara zetu zinaendelea kujengwa kwa awamu, na Serikali imetambua maeneo yote ambayo yanahitaji kujengwa barabara za changarawe, barabara za lami na tunaendelea kutambua maeneo hayo kulingana na uhitaji, na Serikali inatambua kwamba, Mji wa Isaka ni wa kibiashara unaokua haraka.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna *station* ya *SGR*, lakini pia, shughuli za kiuchumi zimeendelea kuongezeka. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu na kufanya tathmini ili kuweza kujenga

barabara hizo kwa kiwango cha lami au changarawe kwa kadri ambavyo itakuwa inawezekana.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera.

Na. 145

**Ujenzi wa Majengo Muhimu Hospitali ya Wilaya, Butiama**

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa majengo muhimu yanayohitajika katika Hospitali ya Wilaya Butiama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, naomba kumjibu Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera, Mbunge wa Jimbo la Butiama:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Butiama ni moja kati ya hospitali 25 ambazo zimejengwa katika awamu ya tatu ya ujenzi wa hospitali za halmashauri ambao ujenzi ulianza mwaka 2021/2022. Jumla ya majengo tisa yamejengwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Butiama kwa gharama ya shilingi bilioni 3.02.

Mheshimiwa Spika, majengo yaliyokamilika ni pamoja na jengo la *OPD*, maabara, *EMD*, jengo jumuishi la uzazi, yaani *martenity complex*. Aidha, jengo la *OPD* limekamilika na huduma za wagonjwa wa nje zimeanza kutolewa mwezi Novemba, 2024.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama imetengewa shilingi milioni 500, kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo yaliyosalia. Serikali itaendelea

kutenga bajeti kwa awamu, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu muhimu katika hospitali za Halmashauri Wilaya ya Butiama.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mahera.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kwanza kuishukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo saba, ambayo yanaendelea kujengwa kwa sasa. Uhakika ni kwamba, majengo ambayo yamekamilika ni manne. Sasa majengo tisa ambayo bado yanahitajika, kwa mfano jengo la huduma ya macho, jengo la kuhifadhia maiti, majengo ya huduma ya kinywa na meno, pamoja na karakana ya hospitali na jiko, haya ni majengo muhimu sana ambayo yanahitajika.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani kuongeza kasi kuhakikisha kwamba majengo haya yanakamilika ili wananchi wa Butiama waweze kupata huduma nzuri ya afya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri ikiwezekana mwezi wa Saba tuambatane naye aende kuangalia hali halisi ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Butiama, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, tunaendelea kusisitiza ukamilishaji wa majengo haya na tunawaelekeza wataalamu wetu kuwa waadilifu katika kazi hii. Tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, imetuma baadhi ya timu yetu kwenda kuangalia ujenzi wa mejengo haya ili yakamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nikijibu swali lake la pili, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tuko tayari muda wowote kufanya ziara. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, baada ya Bunge lako hili Tukufu la Bajeti

tutaongozana naye kwenda Butiama kujionea miundombinu hii, ili iweze kutoa huduma kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dotto Bahemu.

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Sisi Hospitali yetu ya Wilaya ya Ngara, na ya Mbuba, pia kuna ujenzi ambao unaendelea, lakini jengo la mochwari, jengo la wodi za wagonjwa pamoja na *theatre* vilevile bado hayajakamilika. Je, ni mpango gani wa Serikali kuhakikisha kwamba haya majengo yanakamilika ili wananchi waendelee kupata huduma bora sana. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, sote tutakumbuka kwamba Serikali katika bajeti ya mwaka 2026/2027 tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 52.25 kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo, miundombinu katika hospitali zetu za Halmashauri 105. Nimhakikishie Mheshimiwa Bahemu, yupo ndani ya mpango, tutakwenda wote pamoja kuhakikisha kwamba hospitali hii tunakwenda kuikamilisha katika miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba niishukuru Serikali kwa kupeleka fedha awamu ya kwanza kujenga Kituo cha Afya cha Tarafa ya Nyakakika. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha awamu ya pili ili kukamilisha kituo cha afya? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, tayari tulishapeleka fedha awamu ya kwanza, na tayari tumeshaomba fedha Hazina awamu ya pili ili kuhakikisha tunakamilisha kwa wakati

vile vituo vyote ambavyo tulivianzisha ambavyo tulivitengea shilingi milioni 250. Nimhakikishie Mheshimiwa Bashungwa, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tutaendelea kutoa ushirikiano wa dhati kuhakikisha kituo hiki kinakamilika kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Morris.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Ninaomba kumwuliza Naibu Waziri atusaidie, Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kukarabati kituo kikongwe cha afya cha Umbwe ambacho kipo Kibosho Magharibi, kituo ambacho kinawanahudumia Tarafa yote ya Kibosho yenye Kata sita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, tayari tuna mpango mkakati pale Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha vituo vya afya kongwe, na hospitali zile kongwe tumezitengea bajeti kwa ajili ya kwenda kuzikamilisha, ikiwa ni pamoja na kurekebisha miundombinu chakavu ili ziendelee kutoa huduma kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tutaendelea kutenga bajeti ili kukamilisha vituo kongwe kama ambacho amekiongelea.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Charles Mhando Njama.

Na. 146

**Ujenzi wa Majengo Mapya Hospitali ya Magunga**

**MHE. CHARLES M. NJAMA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kujenga majengo mapya katika Hospitali ya Magunga badala ya kuendelea kuweka viraka kila mwaka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Mhando Njama, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Magunga ni moja ya hospitali kongwe nchini ambayo imejengwa mwaka 1952 na inahitaji ukarabati mkubwa. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Serikali imetoa jumla shilingi bilioni 1.06 kwa ajili ya ujenzi wa jengo jumuishi la huduma za uzazi *Maternity Complex* kwa muundo wa ghorofa. Taratibu za kibali na michoro zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga fedha shilingi milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa *theatre* pamoja na ukarabati wa jengo la kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Magunga. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mipya inayohitajika katika Hospitali ya Magunga ili iweze kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhando.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa namna ambavyo wameendelea kutoa jicho lao kwa ajili ya ukarabati wa majengo yale, lakini kwa kuwa hali ya majengo yale ni chakavu mno na hayaridhishi kabisa, tunaomba aweze kupanga safari yeye pamoja na wataalam wake ili twende tukaone hali halisi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, ninaamini baada ya kuiona tunaweza tukawa na mpango wa pamoja ambao utatufanya tuharakishe zaidi kufanya matengenezo, kwa kuwa kiasi cha milioni 600,000,000 kwa mwaka wa fedha 2026/2027 bado ni kidogo mno ukilinganisha na hali ya uhitaji uliokuwepo katika majengo yale.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je ni lini ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Kwamndolwa utaanza, kwa kuwa imekuwa ahadi ya muda mrefu kwa wananchi wa Kwamndolwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, pongezi ambazo amezitoa Mheshimiwa Mbunge zinaelekea moja kwa moja kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu yeye alifanya ziara na aliahidi fedha hizi ziende kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ambayo imetajwa.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, baada ya Bunge lako Tukufu, tutapanga ratiba ili twende ziara katika hospitali yetu hii kujionea uchakavu wa miundobinu na pia thamani ya fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya kukamilisha miundobinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba katika swali lake la pili la nyongeza kuhusu kituo cha afya, tukiwa katika ziara hii tutapita kwenye kituo cha afya alichokitaja ili tuone namna gani ya kuendelea kutenga fedha ili kukamilisha miundobinu ya ujenzi wa kituo hicho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haiderali.

**MHE. HAIDERALI H. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Ninataka kujua, ni lini Hospitali ya Manispaa ya Mpanda itapata jengo la *emergency*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu kwenye majibu ya awali, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Hospitali ya Mpanda nayo imo katika mpango wa zile hospitali 105 ambazo tumeshatenga bajeti katika mwaka wa fedha 2026/2027, jumla ya shilingi bilioni 52.25, ambazo tutazielekeza katika kukamilisha baadhi ya miundombinu muhimu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli jengo la *emergency* ni muhimu sana kwa sababu linatoa huduma kwa wakati na baadhi ya wagonjwa huishia tu kutibiwa *emergency* na kwenda nyumbani. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa jengo hili muhimu.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Lugomela.

**MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa tuna Kata ya Ipililo, kimejengwa kituo cha afya katika Kata ile na Kata ya Ipililo ndiyo Kata yenye wakazi wengi katika Jimbo la Maswa Mashariki. Ninaomba kuuliza, je, kituo cha afya hiki kitaanza kufanya kazi lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge aliuliza swali la nyongeza kuhusu kituo cha afya Kata ya Maswa. Kwanza tumejielekeza kutoa katika vile vituo ambavyo havijakamilika kwanza viweze kutoa huduma zile za *OPD*. Kwa hiyo, mimi na Mheshimiwa Mbunge tutakaa chini baada ya Bunge hili leo, ili tuone namna gani katika kituo chetu hiki cha afya kitaanza kutoa huduma za msingi kwa ajili ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kija.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii ili na mimi niulize swali. Kituo cha Afya cha Katoro kinapokea wagonjwa wengi sana kuliko Hospitali ya Wilaya ya Katoro. Je, ni lini Kituo cha Afya cha Katoro kitapata jengo la *emergence* ili kuongeza ufanisi kuhudumia wananchi wa Katoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ni kweli pale Katoro kuna ongezeko kubwa sana la watu ndiyo maana wananchi wetu wanaona bora waende kwanza wakapate huduma katika kituo cha afya, lakini tayari Katoro wanayo hospitali ya wilaya inayotoa huduma za msingi, na wana jengo bora kabisa la *emergency*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunawaomba wananchi waendelee kwenda kupata huduma hizo katika jengo la dharura la hospitali yetu ya Wilaya huku tukiendelea kujielekeza kuboresha miundobinu rafiki na miundobinu ya dharura katika kituo chetu cha Afya cha Katoro.

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Mheshimiwa Nassor Said Nassor.

Na. 147

**Hatua za Kimkakati za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi**

**MHE. NASSOR SAID NASSOR MAROO** aliuliza:-

Je, Serikali kupitia Wizara ya Muungano na Mazingira inachukua hatua gani za kimkakati za kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Nassor Said Nassor, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kimkakati za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hatua hizo ni pamoja na kuendelea kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao kwa kuzingatia kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha uwezo wa nchi kustahimili ukame, mafuriko na mvua zisizokuwa na uhakika.

Mheshimiwa Spika, aidha, tunaendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ikiwemo jua, upepo, joto ardhi, gesi asilia na umeme ili kupunguza utegemezi wa matumizi ya kuni, mkaa na mafuta machafu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi inayotekelezwa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Sera na mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo Dira 2050 hususan nguzo ya tatu inayohusu mazingira na uhimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 na mkakati wake wa utekelezaji unaoanzia 2021 – 2030, Mpango Kabambe wa Mazingira 2022 - 2032 na Mpango wa Taifa wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi 2025 - 2035.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nassor.

**MHE. NASSOR SAID NASSOR MAROO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi ya maswali ya nyongeza. Je, Mheshimiwa Wizara imetenga kiasi gani cha bajeti katika kushughulikia suala hili hasa la tabianchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kwenda katika Jimbo langu la Chake Chake kuziangalia hizo athari za tabianchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kupitia bajeti za sekta mbalimbali ndani ya Serikali ikiwemo bajeti ya maji kwenye kilimo, kwenye miundobinu, kwenye nishati, kwenye misitu ambayo matokeo yake kwa ujumla yanatufanya tuweze kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kule Pemba mwaka 2024/2025 Serikali ilipeleka fedha shilingi milioni 300 kwa ajili ya kujenga kuta za kuzuia athari za maji zinazotokana na bahari kwenye ufukwe wa Sipwese huko Pemba na mwaka uliofuata 2025/2026, Serikali imepeleka shilingi milioni 392 kukamilisha ujenzi wa ukuta huo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ukuta huo umefikia 95% kwenye mwaka huu wa fedha. Kwenye bajeti itakayosomwa leo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, itaeleza kiwango kilichotengwa kwenye eneo hili Jimbo la Chake Chake.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Maryam Mwinyi.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Bonde la Tibirinzi lililopo Chake Chake Pemba limeathirika na mabadiliko ya tabianchi na maji ya bahari kuingia katika bonde hilo na wakulima kushindwa kuendelea na kilimo, je, nini mkakati wa Serikali kujenga tuta katika shamba hilo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, Serikali imeshayaainisha maeneo yote ambayo yameathirika kutokana na mabadiliko ya tabianchi kule Pemba. Kama nilivyotangulia kusema kwenye jibu langu la nyongeza, ni kwamba kwenye mwaka huu wa fedha 2026/2027, kwenye bajeti ambayo tutaiwasilisha hapa leo, tumeangalia vizuri na kuyaangazia maeneo yote ya Pemba ambayo yameathirika na tutaanza utekelezaji wake hatua kwa hatua.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Abdul Yussuf.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza uwekezaji katika suala hili la mabadiliko ya tabianchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mikakati mbalimbali ya uwekezaji kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Tunayo mikakati ambayo imejikita katika maridhiano ya Kimataifa ambayo tumeyafanya.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa tumeshiriki maridhiano ya Rio de Janeiro yaliyofanyika mwaka 1992. Vivyo hivyo tumeridhia makubaliano ya Tokyo yaliyofanyika mwaka 1997. Pia tumeridhia makubaliano ya Paris yanayofanyika mwaka 2015, tunatekeleza na tumeweka mipango kazi ya kutekeleza maridhiano yote hayo.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, Serikali imeendelea na mpango wa kuhakikisha Watanzania wote wanatumia nishati safi na salama, na kwenye hili la nishati safi na salama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan dunia imemtambua kama *champion* wa usimamizi wa nishati safi na salama na mtunzaji wa mazingira namba moja ndani ya Tanzania, ndani ya Afrika na nje ya mipaka ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, tafiti zilizokuwa zimefanyika zinaonyesha kwamba kila mwaka Tanzania tunapoteza hekta karibia laki 370 za misitu ambayo inatokana na kukata miti kwa ajili ya matumizi ya mikaa na na uharibifu mwingine unaofanyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kukabiliana na uharibifu huu ili tuweze kupunguza athari zinazoweza kutokea za mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, tumeendelea na zoezi la upandaji miti na Waziri atakaposimama hapa leo, atataja mkakati kabambe wa upandaji miti ambao tunao kwa nchi nzima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, Ziwa Babati limevamiwa na magugu na linaenda kupotea. Nini mpango wa Serikali katika kulinusuru Ziwa hilo ambalo ni muhimu kwa wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Babati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango endelevu wa kukabiliana na athari za mazingira ambazo zimetokea kwenye maziwa yetu, siyo tu Ziwa Babati, tunalo Ziwa Victoria, Ziwa Jipe pamoja na na maziwa mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa Ziwa Babati, cha kwanza ambacho tumeweka mkakati ni kushirikiana na Wizara ya Maji ambao ndio wanaohusika na mabonde pamoja na maji ili kwanza tuweke mipaka kwa maana ya kuweka *beacons* za mipaka ambazo zitaonyesha ukomo wa eneo la shughuli za kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali itaendelea kuwatafutia wananchi wa maeneo yanayozunguka maziwa shughuli mbadala ambazo hazitaathiri maeneo haya ambayo tunalenga kuyahifadhi.

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na utalii. Mheshimiwa Jacqueline Kainja uliza swali lako.

Na. 148

**Elimu kwa Wananchi Wanaoishi Karibu na Hifadhi ya Ugalla**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa elimu ya kutosha kwa wananchi wanaoishi maeneo ya karibu na Hifadhi ya Ugalla Wilaya ya Urambo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Kainja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla mwaka 2019, Serikali imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi ambapo jumla ya mikutano ya hadhara 60 ilifanyika na kuwafikia wananchi 10,000 pamoja na vipindi 505 vya elimu ya uhifadhi vilivyowafikia wananchi 58,100.

Mheshimiwa Spika, pia, hifadhi ilishiriki kutoa elimu ya uhifadhi kwenye mikutano ya vijiji 102 na kuwafikia wananchi 8,000 na kutoa elimu ya uhifadhi kwenye vipindi 160 kwenye shule mbalimbali katika Wilaya ya Urambo, Kaliua na kuwafikia wanafunzi 15,000.

Mheshimiwa Spika, vilevile, hifadhi imekuwa na *program* ya kutoa elimu ya uhifadhi kwa njia ya sinema, ambapo jumla ya mikutano kupitia njia za sinema 49 ilifanyika na kuwafikia wananchi 8,500. Katika kuimarisha mahusiano na jamii iliyopo jirani na hifadhi, hifadhi iliandaa ziara mbili za elimu ya uhifadhi kwa njia ya

kutembelea hifadhi ambazo zilihusisha wananchi 130 na kuratibu michezo miwili iliyowashirikisha wananchi 470.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka ujao, hifadhi imejipanga kupanua wigo zaidi wa kutoa elimu ya uhifadhi kwa kuyafikia makundi mbalimbali ya jamii, hususan vijana na wanafunzi ili kuongeza uelewa na kuchochea mabadiliko ya tabia chanya juu ya shughuli za uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hiyo, jumla ya vipindi 112 vimepangwa kufanyika vikilenga kufikia zaidi ya wananchi 11,860 ikijumuisha mikutano ya hadhara, mikutano ya vijiji, vipindi mashuleni, maonesho, maonesho ya sinema, ziara ya kutembelea hifadhini, michezo na vikao. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mwakyembe.

**MHE. LUCY E. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza...

**SPIKA:** *Sorry,* Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi niweze kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ambayo Wizara imetupatia, Wilaya yetu ya Urambo katika Hifadhi ya Mto Ugalla imezungukwa na Kata Nne kubwa ambazo zinazunguka hifadhi hiyo, lakini majibu haya hayajaonesha ni namna gani Kata hizi za Kasisi, Ukondamoyo, Nsenda na Ugalla yenyewe itafikiwa na elimu hiyo. Ninataka kujua, ni lini sasa Kata hizi zote zitapatiwa elimu ya uhifadhi?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Bado wananchi hawana elimu ya kutosha ya kujihami na wanyama wakali. Je, ni lini Simba na Tembo wataweza kudhibitiwa kutokwenda kwenye makazi ya watu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu, ninaomba ni mpongeze sana Mheshimiwa Jacqueline kwa namna anavyofuatilia suala hili na anavyo wapambania wananchi wake wa Urambo na Tabora kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, suala la kutoa elimu ni suala endelevu na la kila siku. Nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba zile kata ambazo hazijafikiwa, zitafikiwa ndani ya mwaka huu wa fedha. Kila ambaye hajapata elimu, atapata elimu hiyo kwa njia mbalimbali ambazo tumeziandaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, Serikali kupitia hifadhi zetu zinafanya doria za mara kwa mara katika sehemu zote ili kutoa elimu ya kujihami na wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, nitoe maelekezo kwa Kamishna wetu wa Hifadhi wa *TAWA* na *TANAPA* waende Urambo, ambako anasema ndugu yangu Mheshimiwa Mbunge kwamba wanyama hao wako kwenye vijiji sasa hivi, waende kuwaondoa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mwakyembe.

**MHE. LUCY E. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Tanzania imepata bahati mwaka 2027 kuendesha michezo ya *AFCON* katika upande wa Bara na Zanzibar, ninataka kujua, kwenye upande wa utalii, wafanyabiashara ndogo ndogo na wajasiriamali nao ni sehemu ya fursa ambayo wameipata kwa ugeni utakaoingia. Je, ni elimu gani imetolewa mpaka sasa, au Serikali imejipanga vipi kutoa elimu kwa wafanyabiashara ndogo ndogo pamoja na wajasiriamali, hususan wanawake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, imejipanga vya kutosha kupokea mashindano hayo ya *AFCON*. Hivi ninavyokwambia, wataalamu wetu wako *site,* wameshaanza mafunzo na taratibu

mbalimbali za wajasiriamali wetu ili kusudi waweze kupokea vizuri, na wanapokuja watu kutoka nje kwa ajili ya michezo, wasiwe wameondoka tu na michezo, bali waende kwenye vivutio vyetu na wajasiriamali wetu nao wawe wanufaika kupitia mashindano hayo ya *AFCON*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benjamin.

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kuniona. Ninaomba kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri, kwamba kutokana na kukua kwa shughuli za kibinadamu na kuongezeka kwa idadi ya watu katika Mji wa Kahama, je Serikali ina mpango gani wa kumega eneo dogo la Hifadhi ya Pori la Nkweni ambalo lipo kati ya Kahama na Wilaya ya Ushirombo ili kuwapatia wananchi waweze kufanya shughuli zao za kibinadamu kama ufugaji na kilimo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, eneo ambalo amelitaja kwa sasa, Serikali haina mpango wa kumega kwa ajili ya matumizi ya wanadamu, lakini, kama kuna haja kubwa ambayo anaiona yeye Mheshimiwa Mbunge, basi tukae tu mezani mimi na yeye, twende *site* tuone. Kama ipo haja ya kufanya hivyo, Serikali inaweza ikachukua hatua siku zijazo.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Yohana Stephen Msita.

Na. 149

**Kero ya Wanyama Waharibifu – Itigi**

**MHE. YOHANA S. MSITA** aliuliza: -

Je, upi mpango wa Serikali wa kuondoa kero ya wanyama waharibifu kama tembo kwenye Jimbo la Itigi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yohana Msita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu katika Jimbo la Itigi, ikiwemo kuendelea kutumia kituo cha kudumu cha Askari kilichopo katika Kijiji cha Doroto na kambi za muda mfupi tatu kwenye Vijiji vya Chisingisa, Sanjaranda, na Kitaraka kwa ajili ya kuitikia kwa haraka kwenye matukio na kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, kuendelea na kuimarisha doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu; kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mbinu rafiki za kudhibiti wanyamapori hao; kuendelea kugawa nyenzo na vifaa rafiki kwa wananchi ili kudhibiti na kuzuia wanyama waharibifu hao, tembo, kwa vijiji mbalimbali; kuendelea kutumia teknolojia ya ndege nyuki; na kuendelea kushirikiana na wadau.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la *Southern Tanzania Elephant Program (STEP)* imetengeneza vihenge 24 vya kuhifadhi mazao yaliyoboreshwa. Sambamba na hatua hizo, Serikali imevuna tembo wawili waliokuwa wakihatarisha usalama wa maisha na mali za wananchi katika Vijiji vya Doroto na Sanjaranda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yohana. Waheshimiwa mko *active* wengi kwenye *mic* zenu. Mheshimiwa Getere zima *mic* yako.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwanza ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali langu. Naomba kuuliza kwamba, kwa kuwa athari ni kubwa katika Vijiji vya Doroto, Kitaraka, Kihanju, Sanjaranda, Gurungu, Njirii, Aghondi, Kamenyanga, Kashangu na Idodyandole; na kulingana na

majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba wamevuna tembo wawili: -

(a) Je, Serikali haioni sasa iko haja ya kuendelea kuvuna angalau hata tembo 20 ili kupunguza adha kwa wananchi kwa sababu athari ni kubwa sana?

(b) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuambatana pamoja na mimi ili kwenda kujionea hali halisi ya athari iliyopo Jimbo la Itigi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Yohana, kwani sasa amekuwa ni sehemu ya hifadhi, na pia anakuwepo ofisini mara kwa mara kutetea wananchi wake kwa usumbufu ambao wanaupata kutokana na wanyamapori hawa wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli alichosema, kwamba Serikali imewahi kuvuna tembo wawili; na nimeona na nimesikia pendekezo lake kwamba tuendelee kuvuna, lakini kuvuna wanyama hawa ni lazima tufuate sheria, kanuni na taratibu. Kwa hiyo, tutaangalia taratibu, zikiruhusu, basi wale wanyama ambao wamekuwa ni wakali sana na ni waharibifu, inawezekana.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, mimi niko tayari kabisa kufuatana na ndugu yangu ili twende jimboni, tuone kadhia hiyo ili tuhami wananchi wetu, waweze kuendelea kuishi kwa tabasamu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Johannes.

**MHE. DKT. JOHANNES L. LUKUMAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kulipa shilingi milioni 5.9 kwa wananchi 26 wa Kata za Kisongo, Musa na Mwandet ambao wameathiriwa na wanyamapori wakali sana.

Mheshimiwa Spika, wanyama hawa wamebadili tabia, wakawa wanashambulia watu na wahifadhi. Pia kuna majangili wanatumia silaha za kisasa, wanawashambulia wananchi na wahifadhi wa maliasili. Je, lini Serikali itawapatia wahifadhi wa maliasili waliopo Jimbo la Arumeru Magharibi silaha sitahiki aina ya *SMG* au *AK-47* ili wahifadhi waweze kuokoa maisha ya wananchi na mali zao; pia wahifadhi wawalinde wanyamapori wetu ili wasiendelee kuuawa na hawa majangiri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua ni lini watapewa silaha hizo? Kwa mujibu wa sheria na kanuni zetu, wahifadhi wetu wana viwango maalumu vya umiliki wa silaha. Siyo kila aina ya silaha wanaweza kutumia.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kumhakikishia ni kwamba, Askari wetu wa hifadhi wataendelea kupewa silaha zinazostahiki kwao ili kuhami wanyamapori wetu na kupamba na majangili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Moja ya kero kubwa, ndani ya Jimbo la Nanyumbu ni ongezeko la wanyama waharibifu, hasa tembo. Mheshimiwa Rais alipokuja wakati wa kampeni aliahidi kufungua kituo pale ndani ya jimbo langu, kwa maana ya kuongeza Askari na kutupatia ndege nyuki. Je, ni lini agizo hili la Serikali litatekelezwa ndani ya jimbo langu?

**SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Yahya kwa namna anavyofuatilia suala hili la wanyama wakali na waharibifu na namna anavyowahami na kutoa elimu na yeye kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimtoe shaka Mheshimiwa Yahya kwamba kituo hiki kitajengwa kwa kiwango kikubwa mwaka ujao wa fedha. Sasa hivi Askari wetu wapo *site* kufanya doria za mara kwa mara ili kuwarejesha hifadhini wanyamapori hao wakali na waharibifu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya Serikali namna wanavyoshughulikia suala la wanyama waharibifu, hasa tembo, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali, kwani zile ndege nyuki kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara na hasa Jimbo langu la Mtama, kwa kweli zimekuwa na msaada mkubwa. Tatizo lililopo ni kwamba ndege nyuki zipo kidogo, tatizo likitokea mpaka ije ifukuze wale wanyama inachukua muda mrefu. Je, Serikali iko tayari kuongeza idadi ya ndege nyuki kwenye maeneo yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari, na hivi ninavyozungumza mwaka wa fedha ujao tutaongeza ndege nyuki zisizopungua 100 na tutapeleka katika eneo hilo ndege nyuki kama inavyostahiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa umri wa kuishi tembo ni miaka 60 hadi miaka 70 na kuendelea. Kwa kuwa hatuna uwezo wa kuvuna tembo kwa kuwaua, je, lini Serikali itaanzisha uzazi wa mpango kwa kuzuia tembo kuongezeka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**MBUNGE FULANI:** Mtambo! Wawachome sindano!

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni vigumu kuzuia wanyama ambao wanazaa, ni vigumu. Kwa hiyo, kuongozeka kwake kwa sababu ya kizazi, ninaomba tuvumilie tu.

Serikali itachukua hatua ya kudhibiti, kujenga uzio ili wasiweze kufika kwenye makazi ya watu.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga.

Na. 150

**Malipo ya Mkandarasi wa Mradi wa Bwawa la Maji Nsekwa – Katavi**

**MHE. THOMAS K. MAGANGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha malipo ya mkandarasi wa Mradi wa Bwawa la Nsekwa ili akamilishe kazi hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga, Mbunge wa Jimbo la Katavi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kufuatia ujenzi wa Bwawa la Nsekwa kufikia hatua nzuri, Serikali inaendelea na ujenzi wa mradi wa miundombinu ya kutibu na kusafisha maji yanayotokana na bwawa hilo lililopo Wilayani Mlele Mkoa wa Katavi. Utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 10% na unatarajia kuwanufaisha zaidi ya wananchi 68,426 waishio katika vijiji 16 vya Wilaya ya Mlele.

Mheshimiwa Spika, mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.5, ambapo tayari Serikali imelipa fedha za malipo ya awali *(advance payment)* kiasi cha shilingi 226.5 kwa mkandarasi na yupo eneo la kazi akiendelea na utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kupeleka fedha za utekelezaji wa mradi huo kadiri hati za madai zitakavyowasilishwa ili

kukamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Thomas.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa mujibu wa mkataba wa mradi huo, mkataba unatarajiwa kukamilika Juni. Kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, mpaka sasa mradi uko 10%, je, Serikali ina kauli gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza kwa ufuatiliaji wa karibu sana wa utekelezaji wa mradi huu; na pili, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu utekelezaji huu unaenda sambasamba na kukagua huu mradi mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulichelewa kwa sababu ya changamoto ya kifedha, na sasa Serikali imeshatatua changamoto hiyo. Baada ya kuwa wamepelekewa fedha, wakandarasi wameanza kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, tutatendelea kufuatilia kwa ukaribu sana, na vyombo vyetu vya usimamizi viko kule vinasimamia vizuri, wataalamu wetu, watendaji wakuu, Mheshimiwa Waziri pia anaendelea kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika kwa wakati na wenye thamani halisi ya fedha, kwa kuhakikisha kwamba ubora wake uendane na mahitaji halisi ili wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Kampala wapate huduma ya maji iliyokusudiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zodo.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ujenzi wa Bwawa hili la Kwenkambala katika Jimbo la Handeni Mjini, ambao umekamilika katika hii Awamu ya Kwanza. Je, ni lini sasa Serikali itajenga chujio na kupandisha maji

kwenye tenki kwa ajili ya wananchi kuendelea sasa kutumia maji haya? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Zodo. Kwanza ninampongeza sana kwa kazi nzuri anayoifanya kwa akina mama, hasa wa Mkoa wa Tanga. Ninampongeza kwa sababu amekuwa karibu sana na Wizara ya Maji kwa kushirikiana kutoa taarifa.

Mheshimiwa Spika, tunapochimba bwawa ama tunapokamilisha bwawa, kazi inayofuatia ni kuhakikisha kwamba tunajua *queue* ile ya maji ili tuweze sasa kufanya usanifu wa mtandao ambao utaenda kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu, Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya usanifu wa kuhakikisha kwamba unajenga tenki ili maji yaanze sasa kupelekwa kwa wananchi kama ilivyokusudiwa, ili wananchi wapate huduma ya majisafi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fagason.

**MHE. FAGASON A. NKINGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo. Jimbo langu la Mbogwe linazo kata 17, vijiji 87, vitongoji 335, lakini wananchi hawa hawana majisafi na salama. Je, ni lini Serikali italeta maji kwenye Jimbo langu la Mbogwe kutoka Ziwa Victoria?

**SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, labda niweke takwimu sahihi kwamba, siyo kwamba Jimbo la Mbogwe hakuna majisafi na salama. Tunafahamu kwamba mpaka sasa tuna zaidi ya 69% ya wananchi wa Mbogwe wanaopata huduma ya maji safi na salama. Nimtoe hofu, tunayo miradi inayoendelea ndani ya Jimbo la Mbogwe. Tutahakikisha kwamba tunaisimamia na tunapeleka fedha wakandarasi waweze kukamilisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia hatutamsahau katika maji kutoka Ziwa Victoria kwa sababu yeye yuko katika njia ambayo inaenda katika maeno ya Bukombe pamoja na Kahama. Hivyo, tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa wananchi wake wa Mbogwe watapata maji kutoka Ziwa Victoria bila ya kuwa na shida yoyote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Serikali iliahidi kuanza ujenzi wa kuleta maji kutoa Ziwa Tanganyika kuyaleta Mpanda Mjini. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi huo ili wananchi waweze kunufaika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama sijamsikia vizuri kwenye hilo.

**SPIKA:** Unaweza ukarudia tena Mheshimiwa Kakoso swali lako?

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuleta maji kutoka Ziwa Tanganyika kuyaleta Makao Makuu ya Mkoa wa Katavi Mpanda Mjini. Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza mradi huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, katika mpango mahususi wa ujenzi wa gridi ya Taifa ya maji, moja ya maziwa na vyanzo vya uhakika ni pamoja na Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, pamoja na mito mingine mikubwa mikubwa kama Malagarasi, Momba, Pangani na mingineyo. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba maji tunayatumia kwa kuyapeleka katika makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari imeshampata mtaalamu mshauri kwa ajili ya kuanza kufanya *feasibility study* ya kuyatumia maji ya kutoka Ziwa Tangayika ili yaende Kigoma, Mpanda, mpaka Rukwa. Lengo ni kuhakikisha

kwamba wananchi wote wanaunganishwa na huduma ya maji yenye vyanzo vya uhakika, likiwemo Ziwa Tanganyika. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Benjamin Lukubha.

Na. 151

**Ujenzi wa Chujio la Maji Buzwagi na Tenki la Maji Shunu/Lugela**

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa chujio la maji la Buzwagi na tenki la maji la Shunu/Lugela ili kupunguza kero ya kukatika kwa maji Kahama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Benjamin Lukubha Ngayiwa, Mbunge wa Jimbo la Kahama Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi inaendelea na mradi wa ujenzi wa mtambo wa kutibu na kusafisha maji *(treatment plant)* katika eneo la Buzwagi Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga. Utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 79% na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Lugela unaojumuisha ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa lita 75,000 katika eneo la Lugela Kata ya Nyahanga wilayani humo. Kazi nyingine zinazotekelezwa ni pamoja na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa tisa ambapo umeanza kutoa huduma kwenye baadhi ya maeneo ya Lugela.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi huo umefikia wastani wa 78% za utekelezaji na unatarajiwa kukamilika Juni, 2026 na kunufaisha wananchi wapatao 2,682 wanaoishi katika eneo la Lugela.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benjamin.

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Wizara, ninaomba sasa nipate uhakika wa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, je, yuko tayari kuambatana na mimi kwenye uzinduzi wa miradi hii ambayo amesema itakamilika mwezi Juni pamoja na kutembelea miradi mingine ya Kilago na Mondo ili kuwapatia wananchi wetu huduma ya maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Lukubha kwa kazi nzuri na kuwa sauti imara ya Wanakahama Mjini kwa kuendelea kuwatetea na hasa katika sekta yetu ya maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali dhamira yake ni kuendelea kushirikiana na Wabunge wote. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali kupitia Wizara ya Maji, tuko tayari kuambatana naye kwenda kukagua utekelezaji wa miradi; pili, kuhakikisha ubora wa mradi uliokamilika; tatu, kuangalia thamani halisi ya mradi uliotekelezwa. Baada ya hapo uzinduzi wa miradi utatokea katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, sisi Serikali hasa Wizara ya Maji tutaendelea kushirikiana naye.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cornel.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ninapenda kujua kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba mradi mkubwa wa maji uliojengwa kwenye Mji wa Chato ambao ni miongoni mwa miradi ya maji katika miji 28 sasa umekaribia kukamilika kwa 90%, lakini mpaka sasa sijaona kama hatua ya upelekaji maji imeanza.

Katika vile vijiji 23 ambavyo mradi mkubwa umepita, vinavyotoka katika kata za Vikome, Ijamchele, Katende na Muungano, je, kauli ya Serikali ni nini juu ya mradi huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa miji 28 katika Mji wa Chato, na kweli uko katika hatua nzuri kabisa, lakini sera yetu ya maji ni kuhakikisha kwamba pale ambapo chanzo cha maji kinatoka, wananchi wa eneo hilo wanakuwa wanufaika namba moja. Hilo la kwanza; pili, pale ambapo bomba kuu *(transmission line)* inapopita, wananchi *left and right* kilometa 12 wawe wanufaika wa maji ambayo yanachukuliwa kutoka kwenye chanzo; na tatu, kule sasa kulikokusudiwa kupeleka maji ndipo sasa watakuwa walengwa namba tatu.

Mheshimiwa Spika, hili tutaendelea kulisimamia isipokuwa kuna miradi ambayo tunaanza kwanza kwa kujenga bomba kuu, na baadaye zinaanza kupatikana *offtake* kulingana na vijiji sasa ambavyo vimepitiwa katika lile bomba kuu.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu kwamba vijiji vyake tutahakikisha tunafanya usanifu na kufanya ile *needs assessment* ili kuhakikisha wananchi wa vijiji na kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, zinapitiwa na kunufaika na mradi huo wa maji kutoka miji 28.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mbangala umekuwa ukiahidiwa maji au utekelezaji wake kwa miaka mitatu mfululizo, na miongoni mwa watu ambao waliahidi ni yeye mwenyewe Naibu Naibu Waziri na tulikwenda naye mpaka kule kwenye kijiji cha Lupaso. Ni lini mradi huu utaanza kutekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa niliongozana na Mheshimiwa Mchungahela, tukaenda mwaka 2024, tulifika katika jimbo lake na hasa katika mradi huu wa Mbangala.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mradi huu haujaanza kutekelezwa, lakini nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba bajeti ya 2026/2027 mradi huu tunahakikisha kwamba unakuwa kipaumbele ili sasa wananchi wa Mbangala waweze kwenda kupata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba tunayo miradi mingi inayoendelea, lakini kila mradi Serikali iko makini na imejizatiti kuhakikisha kwamba itachukua hatua kila fedha inapokuwa inapatikana. Lengo ni kwamba uwekezaji huu ukalenge kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka.

Na. 152

**Ujenzi wa Mradi wa Maji - Chunya**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Mradi wa Maji Chunya uliosainiwa na kutengewa fedha utaanza ?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Jimbo la Lupa, kama ifuatavyo :-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilisaini Mkataba wa ujenzi wa mradi wa maji kwa Mji wa Chunya mwezi Juni, 2022 ambapo ulikuwa ukitekelezwa kwa kushirikiana na Serikali ya India kwa gharama ya

Dola za Marekani Milioni 6.59. Pamoja na kazi nyingine, Serikali ilipanga kuchimba jumla ya visima saba kama chanzo cha maji ambapo baada ya uchimbaji wa visima vya majaribio kufanyika ilionekana havikuwa na matokeo mazuri ya wingi na ubora wa maji unaokubalika kwa matumizi ya binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, matokeo hayo yalipelekea Serikali kutafuta chanzo cha maji mbadala ambacho ni Mto Gwaziva ambapo baada ya usanifu wa marejeo, sasa mradi huo unatarajiwa kugharimu jumla ya Dola za Marekani milioni 16 badala ya Dola za Marekani milioni 6.59 za awali.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi huo ikiwemo majadiliano ya kina na Serikali ya India ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi huo unaanza katika mwaka wa fedha 2026/2027.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali ambayo imeweza kuyatoa, lakini wananchi wa Chunya wamenituma maji. Kwa kuwa Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuweza kutekeleza mradi huu ambao utekelezaji wake utachukua zaidi ya miaka miwili, je, kwa nini sasa Serikali isianze kutekeleza mradi huu kwa kiasi cha fedha kilichokuwepo (dola milioni sita) ambazo takribani ni zaidi ya shilingi bilioni 13 ili kuanza hatua za mwanzo, kwa maana ya kwenye chanzo, pamoja na tenki na *power house,* ili fedha nyingine zinazopatikana utekelezaji wake uweze kukamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa mji wa Chunya Mjini una changamoto kubwa sana ya maji na mradi huu utekelezaji wake utachukua muda mrefu, je, ni upi mpango wa Serikali wa muda mfupi wa kuchimba visima vichache ili viweze kushirikiana na vilivyokuwepo ili changamoto ya maji Chunya Mjini iweze kutatulika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa ninampongeza Mheshimiwa Masache ambaye amekuwa sauti imara ya Wananchi wa Lupa hasa katika kuwatetea na kuhakikisha kwamba huduma ya majisafi na salama inaendelea kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la kwanza nimtoe hofu kwamba Serikali baada ya kubaini kwamba visima vile havina ubora unaotakiwa kupeleka maji kwa wananchi, lakini pia visima vile havina uwingi wa maji kulingana na usanifu wa mahitaji halisi ya eneo husika, tukabaini kuna chanzo kingine.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba *scope* ya kazi ikabadilika na gharama zake zikabadilika, lakini kwa sababu fedha hizi ziko *committed* kwa ajili ya kutekeza mradi huo, hatuwezi kuanza kuzitumia kabla ya makubaliano na Serikali iliyotoa hizo fedha kuhakikisha kwamba tuwe na maelewano ili watoe kibali kama ni kuendelea ama tusubiri ili waongeze fedha ili tukatekeleze na kufanya shughuli zote kwa pamoja bila kuwa na changamoto.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira katika hili kwa niaba ya wananchi wake wa Lupa, tunamhakikisha Serikali tuko makini na tunaendelea na mchakato huo na tuko katika hatua nzuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo lingine kwa swali la pili ni kuhusiana na kwamba tufanye juhudi za dharura; Mheshimiwa Mbunge ni shahidi, kwanza kabisa tunavyo visima vitatu pale ambavyo vimechimbwa na vinatoa maji takribani lita 692,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali kupitia Wizara ya Maji kwa kutumia wataalamu wetu wa ndani na kutumia mitambo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoinunua, tumechimba pale kisima ambacho sasa kinatoa lita 412,000 kwa siku ambapo tunaamini kwamba kutoka kwenye mahitaji ya milioni 4.3 tukajumlisha 692,000, tukajumlisha 412,000 mahitaji yetu yanazidi kupungua, na sasa upatikanaji wa maji unaenda kuwa zaidi ya 56% kwa Mji wa Lupa.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tuko makini na tumejizatiti kwenda kutatua huduma ya majisafi na salama katika Mji wa Lupa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kata ya Mahenge katika Jimbo la Kilolo lina chanzo kizuri sana cha maji na tayari Serikali ilishafanya upembuzi yakinifu. Je, ni lini sasa watapatiwa mradi wa maji ili wananchi waweze kupata majisafi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali nchini, lakini cha kwanza kabisa ni kufanya mapitio ya mahitaji ya maji na baadaye tunafanya upembuzi yakinifu. Baada ya kufanya upembuzi yakinifu tunafanya usanifu wa kina ili ku-*establish* gharama za mradi unaoenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu upembuzi yakinifu umeshakamilika na sasa tunaandaa kwenda kufanya usanifu wa kina ili tuweze kupata gharama za mradi ili tuende kutekeleza na wananchi wake wa Jimbo la Kilolo wapate huduma ya majisafi na salama kutoka kwenye chanzo cha uhakika ambacho Mheshimiwa Mbunge amekigusia.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Silvery Luboja.

Na. 153

**Ujenzi wa Barabara ya Mwanangwa – Misasi –
Salawe – Kahama**

**MHE. SILVERY L. SALVATORY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamrejesha mkandarasi wa ujenzi wa Barabara ya Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Silvery Luboja Salvatory, Mbunge wa Misungwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama yenye urefu wa kilometa 149 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha kwa kuanza na sehemu ya Mwanangwa hadi Manawa kilometa tatu ambapo utekelezaji wake umefika 40%. Kwa sasa, Serikali inaendelea na taratibu za kupata fedha ili kumlipa mkandarasi madai yake aweze kuendelea na kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Silvery. Waheshimiwa ambao mko *off record* mngezima *mic* zenu.

**MHE. SILVERY L. SALVATORY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza ninakubaliana na mpango wa Serikali wa kutengeneza barabara kwa awamu kwa sababu za kibajeti, lakini majibu ya Mheshimiwa Waziri ni tofauti kabisa na hali halisi iliyoko *site* kwa kuwa Serikali haijasema kweli. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana na mimi kwenda kujionea hizo 40% za ujenzi wa kilometa tatu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ninaomba Serikali sasa iwaambie wananchi wa Mwanangwa, Misasi, Buhingo, Busongo, na Nunduru, ni lini barabara yao itaanza kujengwa kiukweli? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mkandarasi alishafanya kazi na ndiyo maana alishaomba hata malipo baada ya kufanya kazi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa

Mbunge kwamba tulichoandika hapa, niko tayari kwenda na Mheshimiwa Mbunge kuona kile ambacho kimefanyika, lakini huku Serikali ikiwa inaandaa malipo ya huyo mkandarasi ili aweze kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Spika, pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni dhamira ya Serikali na ndiyo maana tumeanza kuijenga kwa awamu tukisubiri kupata fedha nyingi ambayo tutakamilisha kuijenga barabara hiyo ya Misungwi mpaka Kahama.

Mheshimiwa Spika, tusingekuwa na dhamira ya dhati tusingeanza, lakini tumeona wakati tunapata fedha kiasi, basi tuendelee kupunguza kazi, lakini tutakapokuwa tumepata fedha yote, mpango wa Serikali ni kujenga barabara yote kutoka Misungwi hadi Kahama kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo. Waheshimiwa, mmoja wenu azime *mic* yake.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Ninaishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa na kumlipa mkandarasi wa barabara ya Mbulu - Garbabi - Haydom. Je, kwa kuwa mkandarasi huyu hadi sasa hajarudi *site,* ni lini mkandarasi wa Mbulu - Garbabi - Haydom atarudi na kuanza kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna vipande viwili Mbulu - Garbabi na Labay - Haydom ambapo mkandarasi anayetekeleza ni mkandarasi mmoja na tumeshamlipa fedha aliyokuwa anatudai. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mkandarasi atarudi *site* kwanza kufanya kazi ya kuhakikisha kwamba zile njia za *diversion* zinapitika, lakini pia kuendelea na kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumwagiza Meneja wa Manyara ahakikishe mkandarasi anarudi *site* na kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yalikuwa na changamoto za kutopitika

yanapitika wakati anaanza kuijenga hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami katika vipande hivyo viwili.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku kwa niaba yake Mheshimiwa Najma.

Waheshimiwa, mmoja wenu azime *mic* yake.

Na. 154

**Ujenzi wa Barabara ya Ifakara – Lupilo Hadi Malinyi kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA K.n.y. MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka Ifakara – Lupilo hadi Malinyi kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Ifakara – Lupilo hadi Malinyi kwa kiwango cha lami kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huu ilikuwa ni kukamilisha ujenzi wa daraja la Magufuli (meta 384) katika Mto Kilombero pamoja na barabara ya maingilio (kilometa 9.143) ambalo lilikuwa kikwazo kikubwa katika barabara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, Serikali imesaini mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Ifakara – Lupilo – Mtimbira yenye urefu wa kilometa 112 ambapo taratibu za malipo ya awali kwa Mkandarasi ili

aweze kuanza kazi zinaendelea. Kwa sehemu zilizobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Najma. Waheshimiwa mmoja wenu azime *mic* yake.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanamalinyi, ninaishukuru sana Serikali kwa majibu yenye kuleta matumaini. Nina swali moja la nyongeza. Barabara ya Malinyi - Natumbo ni barabara mtambuka na inaweza kuunganisha mikoa zaidi ya miwili. Je, Serikali itatimiza lini ahadi yake ambayo imeitoa kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hiyo barabara inaunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Ruvuma na ni barabara kuu. Awali tulitakiwa tujenge barabara yote hiyo, lakini kwa sababu za kibajeti ndiyo maana tumeanza kuigawa kwa vipande.

Mheshimiwa Spika, kwa awamu ya kwanza tutajenga kilometa 112, na tumesema kwenye jibu la msingi, tayari tumeshasaini hata mkataba na huyo mkandarasi. Kilichobaki sasa ni kumlipa fedha ya awali ili aanze kuijenga hiyo barabara kilometa 112, na baada ya hapo mpango ni kukamilisha hadi Mkoa wa Ruvuma pale Songea, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Mburarugaba.

**MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa maslahi mapana ya wananchi wa Mkoa wa Kagera, ni lini Barabara ya Nyakahura – Rulenge - Murugarama itajengwa kwa kiwango cha lami? Tunafahamu barabara hiyo ina kilometa 141 na ni barabara ya kimkakati ndani ya Wilaya ya Ngara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara aliyoitaja kwanza tunaitambua, ndiyo barabara ambayo inaenda kwenye machimbo ya Nikeli. Kwa hiyo, kama Serikali ninapenda umhakikisha Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Ngara kwamba Barabara ya Nyakahura, Muguga, Rulenge hadi Ngara yenyewe, ipo kwenye mpango.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mtupitishe bajeti kwa sababu iko kwenye mpango wa kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Ninadhani ataiona kwenye bajeti yetu siku tutakapokuwa tunaisoma hapa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tinnar Chenge.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni sera ya Serikali kuhakikisha kwamba kila makao makuu ya mkoa yanaunganishwa na mikoa jirani kwa barabara za lami. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Bariadi na Gangabilili – Mwanhuzi – Sibiti - Iguguno na Singida? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, hili swali linafanana na swali la msingi kwa sababu ndiyo barabara ambazo zinatakiwa zijengwe zote. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa kwa awamu hii tumepanga kujenga kiwango cha lami kilometa 50 katika hiyo barabara ya Bariadi – Sibiti kuja Singida.

Mheshimiwa Spika, tayari tuna mkandarasi, na tunachosubiri ni kulipa malipo ya awali ikiwa ni pamoja na kujenga barabara kwa kiwango cha lami katika lile daraja la Sibiti ambapo kutakuwa na upande wa Sibiti kwa maana ya Simiyu na upande wa Singida, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Chikota, rudia tena.

Na. 155

**Ujenzi wa Majengo Mapya ya Mahakama ya Mwanzo Nanyamba**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza: -

Je, lini majengo mapya ya Mahakama ya Mwanzo Nanyamba yatajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania inaendelea kutekeleza Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026. Kutokana na uhaba wa majengo ya Mahakama hususan majengo ya Mahakama za Mwanzo katika maeneo mbalimbali nchini, majengo haya yanajengwa na kukarabatiwa kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, tunakamilisha kutengeneza Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama awamu ya tatu. Aidha, ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Nanyamba utazingatiwa katika Mpango huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nimeridhika na majibu ya Serikali. Ushauri wangu ni kwamba wakati wa ujenzi wa majengo ya Mahakama wakumbuke vilevile na nyumba kwa ajili ya watumishi wa Mahakama. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ado.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Katika Wilaya ya Tunduru, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa Mahakama ya kisasa ya ngazi ya wilaya. Kwa miezi mitano hivi sasa ujenzi ule umesimama.

Swali langu ni kutaka kujua, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mahakama ile ili tuweze kupata huduma inayokusudiwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, Wakili Msomi, kwa swali lake zuri lenye lengo la kufuatilia upatikanaji wa haki katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niendelee tu kumsisitiza Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inatekeleza mradi wa kimkakati kabisa ambao unatokana na mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama na kwa sasa Mahakama inatekeleza mpango huu wa pili na imetumia wastani wa shilingi bilioni 524.9 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Mahakama kuanzia katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo mpaka Makao Makuu ya Mahakama kama tunavyoliona jengo letu la *Judiciary Square*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa Mahakama ya Wilaya ya Tunduru aliyoitaja tayari imeshafikiwa na mpango huu wa pili, na tayari mkandarasi yupo *site* anaendelea na ujenzi wa Mahakama hiyo, nimhakikishie kwamba ni dhamira ya Mahakama kuhakikisha wananchi wanapata majengo bora ya kisasa kwa ajili ya upatikanaji wa haki. Kwa hiyo, jengo hilo litajengwa na litakamilishwa ili wananchi wake waweze kupata huduma bora kabisa za upatikanaji wa haki katika jimbo lake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Adonis Alfred.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tunashukuru Wilaya ya Muleba tumejengewa Mahakama ya Mwanzo katika Kata ya Izigo, lakini tuna Mahakama ya Wilaya ambayo ina changamoto ya ufinyu wa nafasi, ni chakavu na imejengwa miaka mingi na

haiendani na ukubwa wa Wilaya ya Muleba yenye idadi ya watu karibu 650,000 na majimbo mawili ya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani kujenga jengo jipya la Mahakama ambalo litakidhi mahitaji ya Wilaya ya Muleba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufanya ufuatiliaji wa karibu kabisa kuhakikisha kwamba kwenye jimbo lake utoaji wa haki unaendelea kuimarishwa. Ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kama nilivyotangulia kusema kwamba, Mahakama kwa wakati huu inatekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu, mpango wa pili ambao umegharibu wastani wa bilioni 524.9.

Mheshimiwa Spika, mpango huu haujikiti tu kwenye kuboresha miundombinu kwa maana ya majengo ya Mahakama pekee, lakini pia hata katika kujenga mifumo ya kidijiti. Ndiyo maana mtaona kwa wakati huu mwananchi anaweza akafungua shauri kidijiti kupitia mfumo wa Mahakama wa *ECMS*, pia mwananchi anaweza akahudhuria shauri lake kupitia mifumo ya kidijiti kupitia Mahakama Mtandao.

Mheshimiwa Spika, pia kuna mifumo mingi ambayo inamwezesha mwananchi kupunguza gharama kusafiri kufika Mahakamani na kupata huduma zilizo bora na za kisasa. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mahakama itafika na kuhakikisha kwamba jengo katika Wilaya hii ya Muleba inakuwa ni bora na la kisasa kwa sababu ndiyo mpango uliopo na ndiyo mpango unaotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, jengo litajengwa na wananchi wa Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo hili la Muleba watapata miundombinu iliyo bora katika upatikanaji wa haki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kiteto ina Mahakama kongwe sana ya muda mrefu. Tumeshaleta maombi na tukaambiwa ipo kwenye bajeti ya 2024/2025. Nini kauli ya Serikali kuhusu majibu ya ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya kisasa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Olelekaita Edward ambaye amekuwa akifanya ufuatiliaji wa mambo mengi sana katika sekta hii muhimu ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake kuhusu ujenzi wa Mahakama hii ya Wilaya ya Kiteto, kama nilivyotangulia kusema, kwa wakati huu Mahakama inatekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama ikiwemo Mahakama za Wilaya. Mahakama hii ya Wilaya ya Kiteto ipo katika mpango huu wa pili na tayari tenda ilishatangazwa kwa ajili ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hii.

Mheshimiwa Spika, kwa wakati huu bado majadiliano yanaendelea kwa ajili ya kusaini mkataba ili sasa ujenzi wa Mahakama ya kisasa kabisa uweze kuanza na wananchi wa Mheshimiwa Mbunge wapate majengo mazuri kwa ajili ya huduma za Kimahakama.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Taska Mbogo, uliza swali lako.

Na. 156

**Ufafanuzi kuhusu Mbegu za Mahindi**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza: -

Je, kwa nini Mahindi yanayovunwa kutokana na Mbegu za kisasa hayawezi kupandwa kwa mara ya pili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mkulima hulazimika kununua mbegu kila msimu ili aweze kupata tija iliyodhamiriwa kwa sababu mbegu anazonunua katika maduka ya pembejeo huwa zimepitia majaribio ya kisayansi katika maabara ili kuthibitisha ubora wa sifa mbalimbali ikiwemo kiwango cha uzalishaji, uhimilivu wa magonjwa na ukame. Mkulima anapovuna mazao na kutumia mbegu kwa mara ya pili au zaidi husababisha sifa stahiki za mbegu husika kupungua au kupotea.

Mheshimiwa Spika, asilimia kubwa ya mbegu zinazotumiwa na wakulima nchini ni mbegu aina ya chotara ambazo utengenezaji wake hutumia aina mbili au zaidi tofauti za mbegu wazazi kutoka jamii moja. Kutokana na sababu hiyo, iwapo mbegu hizo zitatumika kama mbegu kwa mara ya pili au zaidi husababisha kupotea au kupungua kwa ubora wa mbegu hizo na hivyo kuchangia kushuka kwa tija na uzalishaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, tangu mwaka 2021 Wizara ya Kilimo ilianzisha utaratibu wa kusafisha, lakini kutambua mbegu za asili na pia kufanya utafiti ili mbegu hizo za asili ziweze kutumika kibiashara.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini mbegu hizo zitaanza kutumika kwa sababu mwaka 2025 aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe alizindua aina za mbegu 17 zikiwemo mahindi, maharage, na mbegu mbalimbali za karanga, mpunga na kadhalika. Je, ni lini mbegu hizo zitaanza kutumika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mbegu ndiyo msingi wa chakula nchini Tanzania, lakini mbegu ndiyo msingi wa kilimo. Zipo kampuni za Kitanzania zinatengeneza mbegu zinaipatia Wakala wa *ASA*

*(Agriculture Seed Agency),* lakini *agency* ya *Agriculture Seed Agency* hailipi haya makampuni ya Kitanzania ilhali ikijua kwamba mbegu ndiyo msingi wa kilimo.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itazilipa kampuni za Kitanzania zinazotengeneza mbegu nchini kwetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, moja, ni kweli Serikali tunafanya utafiti. Pili, jukumu ambalo Mheshimiwa Rais ametuelekeza ni kuhakikisha kwamba tunalinda mbegu za asili. Jukumu hilo linafanywa na taasisi yetu ya *TARI. TARI* wameendelea kufanya utafiti wa kuhakikisha tunazilinda.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhakikisha kwamba zinaongeza tija ya uzalishaji kwa wakulima. Kwa hiyo, jambo hili limeshakuwa likifanyika na tumeshatambua mbegu kama Mheshimiwa Mbunge alivyoainisha mbegu 17 na matumizi yake yamekuwa yakitangazwa kwa wananchi kuendelea kutumia lakini bado uzalishaji wa mbegu za asili hapa nchini ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, tatu, kwenye hili suala la mbegu asili, moja ya jukumu kubwa ambalo tunalifanya, kwa mfano sasa hivi kule Arusha tunajenga benki ya mbegu *(gene bank)* pale Seriani Arusha ili kuhakikisha tunahifadhi mbegu zote za asili katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu kwa wananchi, matumizi yanaendelea, lakini uzalishaji ndiyo bado haujawa mkubwa, watarajie tu kwamba tutakavyoongeza uzalishaji maana yake na usambazaji wake kwa wananchi utafika kama ambavyo tumekusudia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakala wa mbegu wa Taifa nchini kwa maana ya *ASA* kutokulipa wadai wake ni kwamba walikuwa na changamoto ya kifedha na sasa hivi Wizara ya Fedha ilishatuahidi kutupatia fedha ili kuweza kuwalipa mawakala hao. Kwa hiyo, wapo ambao tumeshawalipa kwa awamu ya kwanza, wapo ambao

tutawalipa kwa awamu ya pili na kuhakikisha kwamba wanaendelea na shughuli hiyo. Kwa hiyo, jukumu hili lipo, na tunalifanyia kazi, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninapenda kufahamu Wizara imechukua hatua zipi kutokana na changamoto iliyojitokeza ya mbegu feki kwa wakulima waliolima msimu huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninamshukuru Mheshimiwa Neema Mwandabila. Ni kwamba, moja ya hatua ambazo Serikali tumechukua kupitia taasisi yetu ya *TOSCI*, imewakamata wale mawakala waliosambaza mbegu feki kwa wananchi na kuhakikisha kwamba tumewafutia leseni ili katika msimu unaokuja hawatafanya biashara ya mbegu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pia, tumeipa *TOSCI* jukumu la kuhakikisha wanaendelea kuelimisha wananchi kwamba kwenye kila mbegu inayouzwa hapa nchini inakuwa imeandikwa vocha ambapo mwananchi anakwangua ile vocha na kutuma zile namba katika ile kodi iliyowekwa pale chini ambapo ataitambua mbegu ile kwamba ni mbegu halali ama ni mbegu feki kwa sababu zile namba ziko *registered* na zinajitegemea kwa namba moja moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatua ambazo tutaendelea kuzichukua ni kuhakikisha wale wanaokiuka tunawachukulia hatua za sheria. Pia nitoe rai kwa wananchi kwamba wahakikishe wanaponunua zile mbegu ambazo zimethibitishwa na *TOSCI* wahakikishe wanaituma kwa sababu ile namba ni bure ili kujua kama mbegu aliyonunua ni halali?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, inatusaidia sisi ku-*trace* kumjua yule aliyesambaza ni nani, na kuwahi kuchukua hatua kabla, kuliko wananchi wanakuwa wamezitumia zile mbegu halafu wanakuja

kuleta matokeo baadaye. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hatua ambayo tunaifanya.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa.

Na. 157

**Hitaji la Mawasiliano ya Simu Vijiji vya Kata ya Nyamigogo**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka Mawasiliano ya simu katika Vijiji vinne vya Kata za Nyamigogo na maeneo mengine yenye uhitaji Wilayani Biharamulo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaomba kujibu swali la Mhandisi Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imejenga Minara 11 ya Mawasiliano katika awamu mbalimbali (Awamu ya Kwanza A, Awamu ya Pili B na Awamu ya Nne B) katika kata kadhaa zilizopo katika Wilaya ya Biharamulo, ikiwemo Biharamulo Mjini, Kalenge, Kaniha, Lusahunga, Nemba, Nyabusozi, Nyakahura, Nyarubungo na Ruziba.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijiti Awamu ya Kwanza Minara 13 imejengwa katika kata 13 na tayari inatoa Huduma za Simu na *data* kwa teknolojia za *2G, 3G* na *4G*. Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa Mnara mmoja katika Kata ya

Lusahunga chini ya Mradi wa Mawasiliano Vijijini Awamu ya 10, unaotarajiwa kuhudumia Kijiji cha Kikoma na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado kuna changamoto ya huduma za mawasiliano katika baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Biharamulo, hususan katika Kata za Nyamigogo, Runazi, Nemba na Nyakahura.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *UCSAF* imebaini uwepo wa changamoto ya Huduma za Mawasiliano katika Vijiji vya Nyamigogo, Kagoma, Kasozibakaya, Songambele na maeneo mengine katika Vijiji vya Migango, Kaluguyu na Busiri. Kwa sasa, upembuzi yakinifu unaendelea ili kuyaingiza maeneo hayo katika Mpango Mkakati wa Ujenzi wa Minara wa Mwaka 2025 – 2030.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa nafasi. Pia, ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri ambayo wameyatoa na ninashukuru kwa miradi hii ambayo imefanyika. Ni kweli minara hii imejengwa na haya maeneo yanapata mawasiliano, lakini kama Serikali ilivyojibu Kata ya Nyamigogo ina vijiji vinne na vyote hakuna hata kijiji kimoja chenye mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, eneo hili la Migango, Kata ya Runazi, ambalo umelitaja lina wakazi zaidi ya 10,000 lakini hawana mawasiliano kabisa. Ninajua mmesema ipo kwenye mpango; mpango ni 2025 – 2030. Kwa kuwa hawa watu ni wengi na wanategemea mawasiliano, ninaweza kupata kauli thabiti ya Serikali inayonihakikishia kwamba haitaweza kusubiri mpaka mwishoni kwa sababu bajeti inafanyika kila mwaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipate kauli ya Serikali inayoweza kuni-*assure* kwamba mpango utakapoanza, hawa wananchi watapelekewa hiyo huduma haraka ili waweze kupata *sub-station* kwa sababu ni wengi na wanahitaji huduma ya simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Mheshimiwa Waziri amesema Kijiji cha Busiri *feasibility study* inaendelea, lakini jirani na Busiri kuna eneo moja linaitwa Iloganzara kwenye Kata ya Nyakahura. Kuna Kata ya Bisibo eneo la Rwakilinda na Muungano, ni maeneo yenye watu wengi sana lakini hawana mawasiliano pia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba kupata kauli ya Mheshimiwa Waziri na Serikali kwamba hata haya maeneo mawili yatakuwa *considered* kwenye kufanya *feasibility study* ili mtakapoanza kujenga hii minara Biharamulo, basi na wao waweze kupata mawasiliano haya kwa ajili ya kuendeleza huduma za wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika maeneo yote aliyoyataja, kwa sababu amesema kuna changamoto kubwa ya mawasiliano, tutayapa kipaumbele kikubwa katika mkakati wetu tunaoendelea kuutekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya udharura alioueleza, ninamwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *UCSAF* apeleke wataalamu kule katika hali ya udharura ili wakague na kufanya tathmini katika maeneo hayo kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunaweka mawasiliano mapema ili wananchi wengi aliowataja katika maeneo hayo waweze kupata mawasiliano ya uhakika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Spika, viko baadhi ya vijiji mpaka leo havina minara kama alivyosema hapo Mheshimiwa Waziri. Kipekee ninaomba nizungumzie Kijiji cha Mtengashari kilichopo Kata ya Ligunga katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru. Kijiji kile hakina mawasiliano kabisa, wananchi wale

wanapata shida. Ni nini sasa mkakati wa Serikali katika kuhakikisha tunakwenda kujenga minara katika kijiji kile na wananchi wetu waendelee kupata huduma ya mawasiliano? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali katika kujenga minara tumeuweka katika mkakati wetu mahsusi wa Serikali wa miaka mitano ambapo tunakusudia kuyafikia maeneo yote yenye changamoto ya mawasiliano nchini ukianza na maeneo ambayo yana changamoto kubwa. Tumeyatenga katika maeneo yenye changamoto kubwa sana, changamoto za kati na changamoto ndogo.

Mheshimiwa Spika, tutaanza na maeneo yenye changamoto kubwa katika mkakati wetu wa miaka mitano na ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafika pia katika maeneo yake kwa ajili ya kuweka mawasiliano ya uhakika kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia kwamba ndani ya hii miaka mitano mkakati wetu utakapokamilika kila eneo lenye changamoto ya mawasiliano hapa nchini litakuwa limepata mawasiliano ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Japhael Lufungija.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi. Jimbo la Ulyankulu ni miongoni mwa majimbo yenye hali ngumu ya kimawasiliano hasa katika Kata ya Uyowa, Kijiji cha Mwamnange chenye wakazi wengi na kijiji cha kibiashara Kata za Sasu, Ilege na Nhwande kwa maana ya Kata ya Mwongozo. Lini Wizara itakwenda kujenga minara kwenye maeneo hayo ili wananchi waweze kunufaika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, tunatambua changamoto ya mawasiliano iliyopo katika jimbo hili na hivi karibuni, ninadhani wiki hii iliyopita wataalamu wa *UCSAF* walikuwa kwenye eneo la jimbo hili kufanya tathmini. Tunasubiri taarifa yao ili utekelezaji uanze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya taarifa hiyo ya wataalamu kuwasilishwa Wizarani tutafanya mpango wa dharura wa kuhakikisha kwamba katika maeneo ambayo hayana mawasiliano kabisa katika Jimbo lake la Ulyankulu yanafanyiwa kazi, ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Mtima.

**MHE. RASHID M. MTIMA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itatatua tatizo la upatikanaji wa simu katika maeneo yafuatayo katika Jimbo la Newala Mjini: Kata ya Nanguruwe, Kijiji cha Nanguruwe, Mnanje, na Mtawe; Kata ya Mcholi I, Kijiji cha Chikwedu na Chiunjila; Kata ya Namiyonga, Kijiji cha Nakachela na Mandumba; Kata ya Mnekachi Kijiji cha Kazamoyo; na Kata ya Mtumachi, Kijiji cha Mcholi Godauni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimekuwa nikieleza katika majibu yangu kwamba Serikali imeandaa mkakati wa miaka mitano wa kuyafikia maeneo yote nchini ambayo yana changamoto ya mawasiliano. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge katika mkakati wetu wa miaka mitano maeneo yake hayo pia tutayafikia, lakini kwa sababu ameeleza kwamba ana changamoto kubwa, tutayapa kipaumbele wakati wa kutekeleza mkakati wetu huu wa Serikali, ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. Ninaomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mamba Kusini katika Jimbo la Vunjo imekuwa na changamoto kubwa sana ya mawasiliano. Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu ili tuweze kupata mawasiliano ya uhakika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kata aliyoieleza Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo la Vunjo pia itahusishwa katika mkakati wetu wa Wizara, kwa sababu pia amesema kwamba ina changamoto kubwa. Ni kati ya zile kata ambazo na sisi tumepanga kwamba katika maeneo yenye changamoto kubwa tutayapa kipaumbele tunapoendelea na utekelezaji wa mkakati wetu huu wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatoa kipaumbele kikubwa kwa Jimbo lake la Vunjo katika maeneo yote yenye changamoto kubwa, hasa wakati wa utekelezaji wa mkakati mahsusi wa Wizara wa hii miaka mitano tunayoendelea na utekelezaji wake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Mifugo, Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni.

Na. 158

**Hitaji la Ardhi kwa Wananchi - Kata ya Mkoe na Mbuluma**

**MHE. EDIFONSI J. KANONI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ardhi ya kilimo kwa wananchi wa Kata ya Mkoe na Mbuluma kutoka katika eneo la *NARCO*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo wa Uvuvi ninaomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ranchi ya Kalambo ni moja kati ya ranchi 15 zinazomilikiwa na Kampuni ya Ranchi za Taifa, yaani *NARCO*. Ranchi hii inapatikana katika Wilaya za Nkasi na Kalambo, Mkoani Rukwa. Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, ranchi imepakana na Kata za Mkoe na Mbuluma, ambapo kuna Kijiji cha Katapulo (Kata ya Mkoe) na vijiji vya Mbuluma na Lolesha (Kata ya Mbuluma).

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha ufugaji wa kisasa kwa lengo la kuongeza mchango wa sekta ya mifugo katika uchumi wa Ttaifa, Serikali kwa kuzingatia maelekezo ya Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati wa kufungua rasmi Bunge hili la Kumi na Tatu, ya tarehe 14 Novemba, 2025, pamoja na maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025/2030, Serikali inaendelea kutekeleza maelekezo hayo kwa kutenga, kupima na kumilikisha kwa wafugaji maeneo ya shughuli za ufugaji kutoka hekta milioni 3.46 hadi hekta milioni sita pamoja na kuyaboresha maeneo hayo kwa kuyapatia huduma muhimu zikiwemo maji, majosho, malisho na huduma za ugani.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali kupitia Ranchi ya Kalambo haina eneo la ziada na la kutosha kwa ajili ya kuwezesha shughuli nyingine kwa wahitaji kutoka katika Kata za Mkoe na Mbuluma kwa ajili ya kilimo, kwa kuwa maeneo yote yaliyotengwa kwa sasa yana matumizi mahsusi yanayoendelea.

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai kwa halmashauri zote hapa nchini kuhakikisha kuwa zinatenga, zinapima, kumilikisha, kulinda na kuhifadhi maeneo yote ya kimkakati yaliyotengwa kwa shughuli za

mifugo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mifugo ili kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kanoni.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, ninapongeza sana kwa majibu ya Serikali, lakini pia ninasema katika Wilaya ya Kalambo, Kata za Mbuluma na Mkoe Wananchi wa Kijiji cha Lolesha, Kalemasha, Mbuluma, Mao, Katapulo, Mkoe pamoja na Ilimba wana changamoto kubwa sana ya shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuomba Serikali iwasaidie hiyo ardhi kwa ajili ya mifugo. Je, ni utaratibu upi unaotumika ili kuweza kukodi hayo maeneo na hasa kipaumbele katika hayo maeneo ambayo nimeyataja katika vijiji hivyo ambavyo nimevitaja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mheshimiwa Waziri, upo tayari kuambatana na mimi Mbunge kwenda mpaka kwenye eneo hilo katika Wilaya ya Kalambo, Kata ya Mbuluma na Mkoe ili wananchi waweze kuwasilisha kero mbele ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kupambania maslahi ya wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niyajibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja. Mheshimiwa Mbunge amehitaji kujua ni utaratibu gani unaotumika kukodi maeneo hayo? Swali lake la awali lilikuwa linahitaji kujua ni namna gani tunaweza tukatenga maeneo hayo ambayo yamepimwa mahususi kwa ajili ya mifugo ili yatumike kwa ajili ya kilimo?

Mheshimiwa Spika, ninarudia tena kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika vijiji hivi tayari kuna maeneo 31 ya ranchi ambayo yameshatengwa na kutolewa kwa wananchi. Katika Kijiji cha Mbuluma tumetenga hekta 3,167 na Kijiji cha Lolesha hekta 2,107 ambazo tayari wameshapewa wananchi na wanaendelea kwa shughuli za mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa vile tayari Serikali ina *commitment* ya kuongeza maeneo ya ufugaji kutoka hekta milioni 3.4 mpaka hekta milioni sita, maana yake tayari katika maeneo yetu hatuna maeneo ya ziada kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge amehitaji kujua kama tuko tayari kuambatana naye kwa ajili ya kwenda kusikiliza kero za wananchi wake. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, hilo ndiyo hasa jukumu letu kubwa. Kwa hiyo, muda na wakati ambao tutapanga kwa pamoja tutaambatana na kwenda kuwasikiliza wananchi wetu hasa wafugaji katika kata hizi ili tuweze kutatua changamoto zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa maswali yetu yamekwisha, Mheshimiwa Waziri hongera sana. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, nitaanza na wageni waliokaa jukwaa la Spika. Wageni wa Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yusuf Masauni, Waziri Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira, ambao ni viongozi wakuu na viongozi wa Chama cha Mapinduzi; nao ni Dkt. Richard Muyungi, Katibu Mkuu; Ndugu Abdallah Mitawi, Naibu Katibu Mkuu, Muungano; Balozi Baraka Luvanda, Naibu Katibu Mkuu, Mazingira; Ndugu Mwanasha Tumbo, Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; na Dkt. Albina Chuwa, Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni. *(Makofi)*

Pia yupo, Dkt. Immaculate Semesi, Mkurugenzi Mkuu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*. Mkurugenzi Mkuu hongera kwa kazi nzuri unayoifanya. *(Makofi)*

Vilevile yupo Ndugu Kathryn Kigaraba, Afisa Mtendaji Mkuu, Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni; Ndugu Edwin Makamba, Katibu wa Makamu wa Rais; Ndugu Amne Kagasheki, Mjumbe wa Bodi ya Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni; Dkt. Ladislaus Kiyaruzi, Mjumbe wa Bodi ya Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni; Dkt. Philipina Shayo, Mjumbe wa Bodi ya Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni; Ndugu Mohamed Ibrahim Razalee, Mstahiki Meya wa Zanzibar; Ndugu Abdallah Manzi, Mjumbe wa Halmashauri Kuu Zanzibar; na Ndugu Hamid Mbwana Said, Mwenyekiti CCM Wilaya ya Mjini. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mhandisi Masauni, ni familia yake kutoka Zanzibar. Yupo Ndugu Thania Ali Abdulla, mke wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Riziki Hamad Masauni, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Sadiq Masauni, kaka wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Masauni Masauni, baba mdogo wa Mheshimiwa Waziri; na Ndugu Darlin Said, mjomba wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Prof. Adolf Faustine Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ni marafiki zake kutoka Rombo, Mkoani Kilimanjaro, karibuni. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, ni mpiga kura wake anaitwa Ndugu Isack Noe Kitali kutoka Longido Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Wapo wageni 29 wa Mheshimiwa Ayoub Mohammed Mahmoud, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; hawa ni Madiwani na Watumishi wa Manispaa ya Kaskazini A kutoka Zanzibar, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Mohamed Abdullah Makame, ambao ni Madiwani kutoka Jimbo la Kwahani Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Mohammed Kassim Salum, ni Madiwani kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, ni wafanyakazi wa *Clouds Media Group* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Amour Seif Abdalla, ni wafanyabiashara kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, ni ndugu zake kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, ni familia yake kutoka Mpanda Mkoani Katavi. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Amani – Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ni wanakwaya kutoka Chamwino Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo.Yupo Ndugu Victoria Lukigo kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam; Ndugu Devota Bulugu kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam; na Ndugu Hypolite Makassy kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia wapo Wanafunzi 75 na Walimu 16 kutoka Shule ya Awali na Msingi *New Precious* ya Jijini Dodoma, karibuni. (Makofi)

Pia wapo Wanafunzi 142 na Walimu watano wa Shule ya Sekondari *Efforts Academy* kutoka Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Chatanda, Mwenyekiti wa UWT Taifa, anaomba kukutana na Waheshimiwa Wabunge wanawake wote mara baada ya kuahirishwa Shughuli za Bunge, saa 7.00 mchana, Ukumbi wa Msekwa.

Sasa ninamwita Mheshimiwa Mwenyekiti, kuja kuendelea na kazi.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa ninamwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mpango wa Bajeti, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kufuatia mawasilisho yaliyotolewa na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge Katiba na Sheria, pamoja na Maji na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge, kama itakavyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kunijalia uhai na afya njema ya kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya

Makamu wa Rais kwa mwaka 2025/26 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2026/27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa tena kwa awamu ya pili kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo, kupata tena heshima na imani ya Watanzania ya kuweza kuliongoza Taifa letu kwa kipindi kingine cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, heshima hii inatokana na uongozi wake mahiri na wa kipekee katika kipindi cha kwanza cha Awamu ya Sita ambapo wote tumeshuhudia mageuzi ya maendeleo makubwa katika nchi yetu, hususan, katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniteua tena katika awamu ya pili kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na kuendelea kutekeleza vyema jukumu lake la Kikatiba la kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuliongoza Taifa letu, pamoja na kusimamia masuala ya Muungano, Mazingira na Uchumi wa Buluu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda kumshukuru kwa uongozi wake thabiti unaodhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri anayofanya katika kudumisha Muungano wetu, kusimamia hifadhi ya mazingira na kuimarisha Uchumi wa Buluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kuchaguliwa kwake

kwa mara ya pili kumetokana na uongozi wake thabiti aliouonesha katika muhula wake wa kwanza wa uongozi. Aidha, ninamshukuru kwa uongozi wake na maelekezo anayotupa katika kuimarisha mshikamano na ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali. Aidha, ninamshukuru kwa hotuba yake aliyoitoa Bungeni tarehe 1 Aprili, 2026, ambayo inatoa mwelekeo wa utekelezaji wa Shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninakushukuru kwa namna ambavyo anavyoliongoza Bunge hili Tukufu na ninaahidi kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kutoa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yake, kama yalivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kazi nzuri anayoifanya katika kumsaidia Spika wa Bunge kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupongeza wewe Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninawapongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa kamati hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati hizi mbili kwa kuendelea kunipatia ushirikiano madhubuti katika kutekeleza majukumu yangu ya usimamizi wa masuala ya Muungano, Mazingira na Uchumi wa Buluu. Vilevile, ninawapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za kudumu za Bunge waliochaguliwa kusimamia Kamati hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuaminiwa, kuchaguliwa na kupewa dhamana kubwa na wananchi ya kuwawakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Waheshimiwa Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniruhusu niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa heshima na imani kubwa waliyopata ya kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, ninawashukuru kwa ushirikiano mkubwa ambao wameendelea kunipatia wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu ya kusimamia masuala ya Muungano, Mazingira na Uchumi wa Buluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo mkunjufu, ninampongeza Mheshimiwa Hamza Saidi Johari kwa kuaminiwa na kuteuliwa tena kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia, ninamshukuru kwa ushauri wake anaoendelea kutupatia wakati wa utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Kwa muda ambao nimefanyanaye kazi, alinishauri vyema na kunisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa weledi na ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninaomba pia kumpongeza Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Uchapakazi wake utakuwa nyenzo kubwa katika kuhakikisha Ofisi ya Makamu wa Rais inafikia malengo iliyojiwekea. Hakika kwa muda mfupi ambao nimeanza kufanyanaye kazi ameonesha ushirikiano na weledi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa salamu za pole kwa Bunge hili Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi). Tunawaombea Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo na maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais kibajeti ina Mafungu mawili, ambayo ni Fungu 26, Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, na Fungu 31, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Fungu 26, katika kipindi cha mwaka 2025/2026, jumla ya shilingi bilioni 19.95 ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 18.88 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 1.07 ni, kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 31, jumla ya shilingi bilioni 47.92 ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 28.86 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 19.06 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha shilingi bilioni 4.23 kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, shilingi bilioni 6.67 kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

*(NEMC)*, na shilingi bilioni 17.95 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo inajumuisha shilingi bilioni 4.60 fedha za ndani na shilingi bilioni 14.46 fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya shilingi bilioni 15, fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Fungu 26 sawa na 75.2% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 14.4 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, sawa na 76.3% na shilingi bilioni 604.33 ni kwa ajili ya mishahara ambayo ni sawa na 56.6% ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya shilingi bilioni 14.80 zilitumika sawa na 98.6% ya fedha zilizopokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Fungu - 31 lilipokea jumla ya shilingi bilioni 27.14 fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.38 ni kwa mishahara ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, sawa na 79.8% ya bajeti iliyoidhinishwa, shilingi bilioni 4.92 ni mishahara ya Watumishi wa *NEMC*, ambayo ni sawa na 73.7% ya bajeti iliyoidhinishwa na shilingi bilioni 18.84 ni kwa matumizi mengineyo, ambayo ni sawa na 83.8% ya bajeti iliyoidhinishwa kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo, jumla ya shilingi bilioni 17.58 zilipokelewa, ambayo ni sawa na 92.2% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 10.79 na fedha za nje ni shilingi bilioni 6.78. Aidha, katika kipindi hicho, shilingi bilioni 14.18 zilizotumika, ambazo ni shilingi bilioni 9.08, zilikuwa ni fedha za ndani, sawa na 84%, na shilingi bilioni 5.19 ni fedha za nje ambazo ni sawa na 75.2%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 47(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021, Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024, Sheria ya Usimamizi wa

Mazingira, Sura 191 pamoja na marekebisho yake na kanuni zake, pamoja na Miongozo na Maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Viongozi Wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 katika masuala ya Muungano, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika mwaka huu 2026, Muungano wetu unatimiza miaka 62 tangu kuasisiwa kwake. Wote mtakubaliana nami kuwa, tuna jukumu la kuulinda, kuudumisha na kuimarisha Muungano wetu. Hivyo, hatuna budi kukumbuka tukio hili muhimu na kuendeleza mafanikio makubwa yaliyopatikana kisiasa, kiuchumi na kijamii. Aidha, ni muhimu kuendeleza amani, umoja, ushirikiano na kuheshimiana baina ya pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2025/2026, Ofisi imeendelea kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mambo yasiyo ya Muungano. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kufanya mapitio ya kuchapisha mwongozo mpya wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Toleo la 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo huo pamoja na mambo mengine, umeainisha jukumu la kujadili masuala mengine yenye maslahi mapana ya pande mbili, ikiwemo fursa zilizoko pande mbili za Muungano, na siyo kujadili hoja za Muungano pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha tunaondosha ombwe la changamoto ya uelewa wa Muungano kuhusu elimu ya Muungano, hususan kwa vijana, Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Elimu kwa Umma kuhusu Muungano. Mpango huo unahusisha shughuli mbalimbali ikiwemo semina, makongamano, *Muungano Caravan*, mashindano ya michezo, mashindano ya insha, programu za redio na televisheni na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mpango huu, ofisi ilitoa semina kuhusu masuala ya Muungano kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Vilevile, ofisi iliandaa na kuratibu makongamano kuhusu masuala ya Muungano kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu vilivyopo Zanzibar na kongamano la kumuenzi Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, lililobeba maudhui ya Mwanamajumui wa Afrika, Mwasisi wa Muungano na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar lililofanyika Dar es Salaam katika Ukumbi wa Karimjee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2025/2026, ofisi imeandaa na kuchapisha vitini, maswali na majibu kuhusu Muungano kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya Muungano, hususan, maswali yanayoulizwa mara kwa mara. Aidha, Ofisi imeendelea kukusanya Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano, kwa ajili ya uanzishwaji wa vituo vya kumbukumbu na Nyaraka za Muungano, ikiwemo kumbukumbu, nyaraka, vifaa, video na tafiti kutoka taasisi kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi imeendelea kutumia mbinu mbalimbali za kuwaelimisha wananchi kuhusu Muungano, ikiwemo kupitia makala mjongeo kwenye vyombo vya usafiri, kama vile treni ya mwendokasi *(SGR)* na maboti yaendayo kasi *(AZAM Marine)*, ambapo maudhui mbalimbali kuhusu Muungano. Pia, ofisi imeendelea kurusha vipindi kwenye vyombo vya habari *TBC*, *ZBC* Redio na TV kupitia kipindi maalum cha 'Hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.'

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba Muungano unaimarishwa kupitia michezo, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar na Wizara zenye dhamana ya michezo kutoka pande zote mbili za Muungano, pamoja na Mashirikisho ya Vyama vya Michezo Tanzania (*TFF* na *ZFF*) tumefanikiwa kurejesha Mashindano ya Muungano kwa mpira wa miguu yaliyokuwa yamesimama kwa miaka 20. Kwa mwaka huu mashindano haya yanatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 21 hadi 29

Aprili, 2026 na yatahusisha timu nane za Simba, Yanga, Azam, Singida *Black Stars, Mlandege FC*, *Mwembe Makumbi City*, *Mafunzo Sports Club* na *KVZ FC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi imeendelea na usimamizi na uratibu wa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Waheshimiwa Wabunge wa majimbo 50 ya Zanzibar, kwa mujibu wa Kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Sura Na. 96.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tarehe 26 Februari, 2026 ofisi iliandaa na kutoa semina kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wakurugenzi wa Halmashauri, Manispaa na Mabaraza ya Miji ya Zanzibar ambao ndiyo wasimamizi wa miradi inayotekelezwa na fedha hizo kwa ajili ya kupokea maoni na mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria hiyo ya Hifadhi na Usimamizi Endelevu wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu, tarehe 17 Julai, 2025 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050, ambayo mojawapo ya nguzo zake tatu inahusu Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu Dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi. Vilevile, Ibara ya 3.1.7 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 – 2030 imeweka masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kama mojawapo ya masuala muhimu ya kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhifadhi mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la kuhakikisha kuwa, Watanzania wote wanaendelea kuishi katika mazingira bora na salama. Hatua hizo ni pamoja na kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura Na.191, kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira, kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, kama nyenzo mojawapo ya kuimarisha uhifadhi wa mazingira na

kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kuhamasisha upandaji wa miti na uwekezaji katika biashara ya Kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, uhifadhi wa mazingira umeendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo uharibifu wa ardhi, ukataji hovyo wa miti na uharibifu wa misitu unaochangiwa na utegemezi wa matumizi ya nishati ya kuni na mkaa, kilimo cha kuhamahama, uchafuzi wa mazingira, upotevu wa makazi ya wanyamapori na bioanuai, uharibifu wa vyanzo vya maji, mifumo ya ikolojia ya ukanda wa pwani na bahari, kuenea kwa viumbe vamizi na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changomoto hizi zinachangiwa zaidi na uwepo wa shughuli za kibinadamu zisizo endelevu zinazofanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, miongozo, mikakati, miradi ya hifadhi ya mazingira, na kuratibu utekelezaji wa mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2025/2026 Ofisi imetoa vibali Sita vya tathmini ya mazingira ya kimkakati kwa ajili ya programu ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa Victoria Mkoa wa Kagera, Mwanza, Simiyu, Mara na Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya mifumo ya ekolojia ya mikumi, mpango kabambe wa uendeleza wa eneo la kasabi katika Halmshauri ya Kibaha Mkoa wa Pwani, Mradi wa Uboreshaji wa Bonde la Msimbazi, Kongani la Viwanda la kuchakata mazao ya kilimo. Hususan zao la korosho Halmashauri ya Nanyamba – Mkoa wa Mtwara na eneo la maalumu la kiuchumi la Buzwagi katika Halmashauri ya Kahama katika Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mpango kabambe wa Taifa wa Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira, Ofisi inaendelea kuratibu upatikanaji wa fedha kutoka katika mifuko ya Kimataifa ya mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kutekeleza miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha miradi mitano imeidhinishiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji. Miradi hiyo ni mradi wa kuboresha mifumo ya chakula Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania Bara na Zanzibar, inayotekelezwa katika Mikoa ya Njombe, Mbeya, Iringa, Kaskazini Unguja, Kaskazini Pemba na Kusini Pemba. Majimbo ya Mbarali, Makete, Iringa Vijijini, Wanging'ombe, Bumbwini, Wete na Chake Chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa usimamizi shirikishi wa hifadhi endelevu ya ikolojia ya Bonde la Wami, Ruvu unaotekelezwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani na Dodoma kwenye Majimbo ya Bahi, Chamwino, Dodoma Jiji, Mtumba, Kongwa, Mvomero, Kibaha na Ilala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa usimamizi endelevu ya ardhi na uimarishaji na ustahimilivu wa jamii katika maeneo kame na vituo vya uhamaji wa mifugo nchini Tanzania, unaotelekezwa katika Mikoa ya Simiyu, Manyara, Shinyanga, Arusha, Tabora, Dodoma na Singida ikigusa Majimbo ya Simanjiro, Chemba, Igunga, Monduli, Kishapu, Meatu na Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ni miradi ya kuendeleza uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ya ekolojia vijijini. Mradi huu unatekelezwa katika Halmshauri za Wilaya Nane ambazo ni Bunda, Serengeti, Tarime, Ngorongoro, Karatu, Meatu, Busega na Mbulu; mradi wa urejeshwaji wa hifadhi endelevu wa mifumo ya ekolojia ya Bonde la Wevu la Malagarasi Moyowosi kupitia mbinu jumuishi za hifadhi ya bioanuai utakaotekelezwa katika Mikoa ya Kigoma, Tabora. Miradi hii kwa ujumla ina thamani ya shilingi bilioni 102.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia Bunge lako Tukufu niendelee kuhimiza Wizara, Taasisi na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha wanajumuisha katika mipango yao na bajeti zao masuala mahsusi ya mazingira yanayohusu sekta zao yaliyobainishwa katika dira ya 2050 na Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi imeendelea kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji Miti Milioni 1.5 katika kila Halmashauri nchini ambapo hadi kufikia Machi, 2026 takribani 76% ya miti hiyo iliyopandwa ilikuwa imestawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuhimiza, kuhamasisha upandaji na utunzaji wa miti nchini hususan kwa kuamua kutumia kumbukumbu ya siku yake ya kuzaliwa ya tarehe 27 Januari kila mwaka kupitia kampeni ya "27 ya Kijani, Mti wa Mama," kuwa jukwaa la uhamasishaji wa upandaji miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitoe pongezi kwa Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* pamoja na Taasisi ya *Mwanamke Initiatives Foundation* kwa kutoa mchango wake mkubwa katika uhamasishaji wa kampeni hii pamoja na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania na wadau wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa Mazingira. Katika kipindi cha Mwaka 2025/2026, Ofisi iliratibu na kushiriki katika mikutano mbalimbali ya Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 30 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi *COP30* uliofanyika Belém - Brazil Tarehe 10 hadi 21 Novemba, 2025. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliongoza kundi la majadiliano la wataalamu wa Afrika kuhusu mabadiliko ya tabianchi kupitia Dkt.

Richard Muyungi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kundi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maazimio yaliyoafikiwa katika mkutano huo ni pamoja na kupitishwa kwa vigezo vitakavyotumika kufanya tathmini ya nchi zitakazonufaika na fedha za utekelezaji wa miradi kupitia ufadhili wa Mfuko wa Kushughulikia Uharibifu na Hasara *(The Fund for Responding to Loss and Damage)* zitokanazo na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nchi wanachama zilikubaliana kupitisha viashiria 59 vitakavyotumika kupima utekelezaji wa shughuli za uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Maazimio mengine yaliyoafikiwa ni pamoja na nchi zinazoendelea kukataa maombi ya nchi zilizoendelea za kutokutumia makaa ya mawe na gesi asilia ili kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi na nchi wanachama kuanza kutekeleza programu ya ubunifu wa teknolojia, uhaulishaji wake kwa nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano huu umeleta tija kwa Taifa ambapo Tanzania iliweza kupata ahadi ya fedha kutoka katika Mfuko wa Shirika wa Maendeleo na wadau mbalimbali na mkataba huo zinazotokana na mikutano ya uwili baina ya Tanzania na mashirika ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Dola za Marekani Milioni 868.42 na Euro 500,000 ziliahidiwa kutolewa kwa Tanzania kwa ajili ya programu na miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, nishati safi ya kupikia, usimamizi wa taka na uhifadhi wa bioanuai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 24 zimepatikana kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi kwenye vyanzo vya maji katika Bonde la Wami-Ruvu na katika Mto Mkondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi pia imeratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Saba wa Baraza la

Mazingira la Umoja wa Mataifa *(UNEA-7)* uliofanyika Nairobi Kenya, kuanzia tarehe 01 hadi 12 Desemba, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maazimio yaliyofikiwa katika mkutano huo ni pamoja na nchi wanachama, ni pamoja na kujenga uwezo wa nchi kukabiliana na viumbe vamizi, kuimarisha ustahimilivu wa miamba ya matumbawe, uhifadhi wa barafu ikiwemo Mlima Kilimanjaro na udhibiti wa moto holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kukabiliana na usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya madawa na udhibiti wa kemikali na taka, kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira na matumizi ya Akili Unde katika hifadhi ya mazingira. Pamoja na masuala mengine, mkutano huo ulimpitisha Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Makamu wa Rais wa Mkutano wa Baraza la Mazingira Duniani *(UNEA-7)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais, imejipanga kutekeleza Dira ya 2050 ipasavyo hususan nguzo ya tatu kuhusu uhifadhi ya mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, ambapo umeandaa Programu za Mageuzi ya Kimkakati Mazingira Endelevu *(Strategic Transmotive Programme for Sustainable Environment in Tanzania)* yenye lengo la kuimarisha uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi kwa kuongeza eneo lenye uoto wa kijani kupitia upandaji miti na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu hii inalenga kuhamasisha jamii na wadau katika kupanda na kutunza miti bilioni mbili na hekta 100,000 za bustani za kijani kwa mwaka; kuwezesha urejeshwaji na uhifadhi wa ardhi ya kilimo ardhi-oevu, misitu na nyanda za malisho zilizoharibiwa kiasi cha hekta milioni moja kwa mwaka; kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa angalau taasisi 13,000, utekelezaji wa miradi 35 ya biashara ya kaboni katika sekta ya usafirishaji, misitu, na nishati safi na usimamizi wa taka na kuchangia utekelezaji wa mpango wa kuirithisha Zanzibar ya Kijani (2023 –2030) unaolenga kupanda miti milioni tatu kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2025/2026, Ofisi iliratibu utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo usimamizi jumuishi wa mifumo ikolojia, urejeshwaji endelevu wa mazingira na hifadhi ya bioanuai Tanzania. Mradi huu unatekelezwa katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Katavi, Rukwa kwenye Majimbo ya Kalenga, Isimani, Wanging'ombe, Mbarali, Mbeya Vijijini, Kwera, Kavuu na Tanganyika ambapo kiasi cha shilingi bilioni 5.26 kimeshapokelewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine ni mradi wa kujenga uwezo wa kutekeleza mkataba wa *Montreal* kuhusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni, ambapo kiasi cha shilingi milioni 250 kilipokelewa kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa Maafisa wa Idara ya Serikali na mawakala wa forodha katika mipaka ya Holili, Horohoro, Tunduma, Bandari ya Tanga na Dar es Salaam, pamoja na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius K. Nyerere kuhusu udhibiti na uingizaji nchini wa vifaa na kemikali zinazoweza kusababisha uharibifu wa tabaka la ozoni na ongezeko la joto duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi vilevile imeendelea kutekeleza mradi wa kujenga ustahimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi Mkoani Kigoma, mradi huu unatakelezwa katika Halmashauri ya Wilaya za Kasulu, Kibondo na Kakonko. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuajiri timu ya uratibu wa mradi na ununuzi wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa umma kuhusu uhifadhi wa usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Katika kipindi cha mwaka 2025/2026, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu uhifadhi ya usimamizi ya mazingira kupitia vyombo mbalimbali vya habari, makongamano, semina, warsha na maonesho ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia kipindi maalumu kiitwacho Mazingira Yetu ni Tanzania Ijayo, jumla ya vipindi tisa vya runinga 14 vya redio vilirushwa na habari 655 za kuelimisha umma zilitolewa kupitia magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, elimu ya umma imetolewa kupitia maadhimisho ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa yanayohusu Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi ikiwemo Siku ya Ardhi oevu, tarehe 2 Februari; Siku ya Mazingira Afrika, tarehe 3 Machi; na Siku ya Misitu Duniani, tarehe 21 Machi; Siku ya Maji Duniani, tarehe 22 Machi; na Kuenea kwa Jangwa na Ukame, tarehe 17 Juni; na Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni, tarehe 16 Septemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchumi wa Buluu ni moja ya maeneo mapya ya kimkakati yenye mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za bahari, maziwa, mito, mabwawa, maji chini ya ardhi na maeneo oevu kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi, kuboresha mazingira ya jamii na uhifadhi wa rasilimali za Uchumi wa Buluu. Maeneo haya yana fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji, kukuza biashara na uwekezaji, kutoa ajira kwa vijana na wanawake, kuimarisha usalama wa chakula, pamoja na kuongeza mchango wa sekta husika katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, Serikali imeanzisha Kitengo cha Maendeleo ya Uchumi wa Buluu na Uratibu chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Hatua hii imeimarisha uratibu wa shughuli za Uchumi wa Buluu nchini na kuweka msingi wa usimamizi jumuishi kwa sekta zote zenye mnasaba wa Uchumi wa Buluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa matumizi endelevu ya rasilimali za Uchumi wa Buluu, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imeanza mchakato wa kuandaa mpango wa matumizi endelevu wa maeneo ya maji. Mpango huu ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha rasilimali ya bahari na maji baridi zinatumika kwa njia ya tija, kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi, kuboresha maisha ya jamii na hifadhi ya rasilimali za maji kwa lengo la kupunguza mgongano wa matumizi na kufungua fursa mpya za uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*. Baraza limeendelea kutekeleza majukumu

yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Mipango, Miongozo na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2026 Baraza lilifanya kaguzi katika miradi 3,408 ikijumuisha viwanda, migodi yakiwemo machimbo ya mchanga na kokoto, mitambo ya gesi, mafuta, nishati ya umeme, machinjio ya wanyama, kumbi za starehe, nyumba za ibada, hoteli, mabomba ya mafuta, maghala ya kemikali, taka zenye madhara, vituo vya mafuta, masoko, madampo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kaguzi hizo ni pamoja na kuongezeka kwa uzingatiaji wa sheria na ubora katika kuhifadhi mazingira kwa maeneo yote ambayo yamekaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2025/2026, Baraza la Usimamizi la Uhifadhi wa Mazingira *(NEMC)* limeendelea kusimamia utekelezaji wa kanuni na udhibiti wa taka hatarishi kwa mwaka 2019 na marekebisho yake ya mwaka 2021. Katika kipindi hicho, jumla ya maombi 224 ya vibali vya usimamizi wa taka hatarishi yalipokelewa, ambapo vibali 212 vilitolewa ikiwa ni sawa na 95%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Kanuni za Kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki, Baraza limeendelea kudhibiti matumizi ya mifuko hiyo, ambapo hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya tani 60 zimekamatwa na kati ya hizo tani 40 zimeteketezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza limeendelea kusimamia usajili wa miradi na maendeleo kwa ajili ya kufanya Tathmini ya Athari ya Mazingira na Ukaguzi wa Mazingira ambapo jumla ya Miradi 1,471 ilisajiliwa. Kati ya hiyo, miradi 1,180 ilisajiliwa kwa ajili ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na miradi 291 kwa ajili ya Ukaguzi wa Mazingira. Kwa kipindi hicho, jumla ya miradi ipatayo 1,030 imeidhinishwa kupata vyeti ambapo miradi 903 ni ya tathmini ya athari kwa mazingira na 127 ni miradi ya ukaguzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2025/2026, Baraza limefanikiwa kuendesha programu 78 za mazingira kupitia redio jamii na Taifa, programu 52 za runinga, makala maalumu tatu

za televisheni, habari 151 za runinga, habari 109 za redio na taarifa 563 zilisambazwa katika mitandao mbalimbali ya kijamii. Aidha, habari 278 zilichapishwa kwenye magazeti, vipeperushi 384 vya kielektroniki vyenye kuhuishwa kwenye mitandao ya kijamii ya *NEMC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Taifa cha Kuratibu Biashara ya Kaboni. Kituo cha Taifa cha Kuratibu Biashara ya Kaboni *(MCMC)* kimeanzishwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura Na. 191 iliyofanyiwa marekebisho kupitia Sheria Na. 5 ya Mwaka 2025 na kupewa Majukumu yafuatayo: Kuratibu masuala yanayohusiana na gesijoto na Biashara ya Kaboni, kuwa Msajili wa miradi ya kaboni; kuweka Mfumo wa ufuatiliaji, utoaji wa taarifa na uthibitishaji wa gesijoto; kutoa mafunzo ya uhamasishaji kwa wadau; kufuatilia utekelezaji wa Kanuni ya Biashara ya Kaboni, na kuweka Mipango ya kukuza uwekezaji na ushirikiano wa Kimataifa katika Biashara ya Kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2026 shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu muundo na majukumu ya kituo na uratibu wa biashara ya kaboni, kuwajengea uwezo wa kufanya biashara ya Kaboni taasisi na wadau mbalimbali. Aidha, elimu kwa umma kuhusu biashara ya kaboni imeendelea kutolewa kupitia njia mbalimbali ikiwemo mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kituo kimefanya usajili wa miradi 22 ya Biashara ya Kaboni ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na hivyo kufanya idadi ya miradi iliyosajiliwa kufikia 99 katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukweli kuwa biashara ya kaboni ni dhana ngeni kwa wananchi, ninaomba nitoe rai kwa umma kutumia ipasavyo kituo cha uratibu wa biashara ya kaboni nchini ili kupata ushauri wa kitaalamu na miongozo stahiki kuhusu biashara hii *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto na utatuzi wake. Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatika katika mwaka 2025/2026, Ofisi ilipitia changamoto mbalimbali za utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo uelewa mdogo wa masuala yanayohusu chimbuko, misingi, historia na fursa za Muungano; jamii kutozingatia sheria kikamilifu za usimamizi wa mazingira na Kanuni zake; na uelewa mdogo wa jamii kuhusu fursa za Uchumi wa Bluu na biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizo, ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano na fursa zake, uzalendo na mshikamano wa Kitaifa hususan kwa vijana. Kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira hususan uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Kanuni zake pamoja na fursa ya biashara ya kaboni na Uchumi wa Bluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Bajeti ya Ofisi kwa Mwaka 2026/2027 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo:-

(i) Dira ya 2050;
(ii) Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu na Utekelezaji wa Dira ya 2050;
(iii) Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031);
(iv) Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021;
(v) Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024;
(vi) Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2025/2030;
(vii) Mpango Mkakati wa Ofisi (2026/2027 - 2030/2031);
(viii) Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2026/2027;
(ix) Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira;
(x) Mabadiliko ya Tabianchi na Maagizo ya Viongozi wa Wakuu wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano kwa masuala yasiyo ya

Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa utekelezaji wa mpango kabambe wa elimu ya umma kuhusu Muungano ambao pia utahusisha maandalizi ya ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu cha Nyaraka za Muungano, (makavazi), kuratibu vikao vya pamoja vya Serikali zote mbili, pamoja na kushughulikia masuala ya Muungano ikiwemo kukamilisha utatuzi wa hoja za Muungano na kuhamasisha fursa za Muungano

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuratibu vikao vya ushirikiano baina ya Wizara, idara, na taasisi zisizo za Muungano, kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano, kuandaa Maadhimisho ya Miaka 63 ya Muungano, na kujengea uwezo Kamati za Usimamizi wa Fedha za Mifuko ya Jimbo kwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaotokea Zanzibar, na watendaji wa halmashauri kuhusu uendeshaji na usimamizi wa fedha za kuchochea maendeleo ya jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2026/2027, ofisi pia imepanga shughuli mbalimbali, ikiwemo kuratibu utekelezaji wa Dira ya 2050 katika masuala yanayohusu hifadhi ama usimamizi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Kimkakati ya Mazingira Endelevu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191. Kuratibu Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, kuimarisha uratibu na utekelezaji wa masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira katika Wizara za kisekta, taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, na wadau mbalimbali wa mazingira. Aidha, kutoa elimu ya Umma kuhusu hifadhi ya mazingira, na kuendelea kuratibu utekelezaji wa mikataba ya kikanda na Kimataifa kuhusu hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Tanzania inatarajiwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 12 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa

Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi, na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano huu unategemewa kufanyika siku ya tarehe 6 hadi 9 Oktoba, 2026 Jijini Dar es Salaam. Aidha, mkutano huu unatarajiwa kuleta manufaa katika nyanja mbalimbali, ikiwemo kupata fursa za miradi na uwekezaji, kuimarisha ushirikiano wa kikanda na Kimataifa, na kutangaza bidhaa mbalimbali za kiasili zinazotengenezwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Dira 2050, ofisi itaendelea kuratibu na kusimamia sekta zenye mnasaba na Uchumi wa Buluu ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa na Dira 2050 yanafikiwa kwa kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika Sekta ya Uchumi wa Buluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kumwezesha Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza majukumu yake, kusimamia masuala ya utawala na menejimenti ya rasilimaliwatu, kuratibu maandalizi ya maandiko ya nyaraka mbalimbali za ofisi, na kuandaa mpango na bajeti ya ofisi na taarifa za utekelezaji wa mipango mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuelimisha umma kuhusu majukumu, sera, mikakati na programu zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais; kutoa huduma ya ushauri wa masuala ya kisheria; kufanya kaguzi za fedha zilizopokelewa na matumizi yake, na kusimamia utekelezaji wa mifumo ya manunuzi na kutoa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuandaa taarifa za mapato na matumizi ya Fungu 26 na 31; kufanya ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa sera, mikakati, mikataba ya Kimataifa pamoja na programu zinazohusu Muungano, mazingira na Uchumi wa Buluu; na kuandaa, kusimamia mfumo na kutoa msaada wa kitaalamu katika masuala ya TEHAMA; pamoja na kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali inayoratibiwa na ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2026/2027 Baraza la Taifa na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* litaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kuratibu, kusimamia na kushauri utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, miongozo na mikakati ya mazingira kwa lengo la kudhibiti athari na uharibifu wa uchafuzi wa mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; kuratibu mchakato wa tathmini ya athari ya mazingira ili kuhakikisha kuwa miradi yote ya maendeleo inajumuisha masuala ya mazingira kabla ya kuanza utekelezaji wake; na kusajili na kusimamia utendaji wa wataalamu elekezi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Baraza litaendea kutoa elimu na kuhamasisha jamii na wadau kuhusu umuhimu wa kufanya tathmini ya athari ya mazingira na kuzingatia miongozo ya usimamizi wa mazingira kwa maendeleo endelevu, pamoja na kufanya tafiti mbalimbali za mazingira ili kuongeza uelewa wa mifumo ikolojia na kuhifadhi baioanuwai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Kituo cha Taifa cha Kuratibu Biashara ya Kaboni kitaendelea kutekeleza majukumu yake na shughuli mbalimbali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzisha na kusimamia rejesta ya kidigitali ili kuongeza ufanisi wa usajili na ufuatiliaji wa miradi ya kaboni, na kuongeza wigo wa usajili wa miradi ya kaboni ili kulinda mazingira na kuongeza kipato kwa jamii na Serikali; kukamilisha Mfumo wa Kidigitali wa Upimaji, Utoaji wa Taarifa na Uthibitishaji; kuimarisha uratibu wa biashara ya kaboni kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Kitaifa, Kikanda, na Kimataifa, na kutoa elimu kwa umma kuhusu biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2025/2026 yamechangiwa na ushirikiano mzuri kutoka kwa washirika wa maendeleo, sekta binafsi, taasisi za fedha nchini, asasi

zisizo za kiserikali za ndani na nje ya nchi, pamoja na wadau mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninaomba kutoa shukrani kwa wadau wafuatao: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya *Norway*; *Sweden*; *Denmark*, *Japan*, Uingereza, India, Korea Kusini, Ufalme wa Saudi Arabia, *Oman*, na *Qatar*. Wengine ni pamoja na Umoja wa Ulaya, Benki ya Dunia, Mfuko wa Mazingira wa Dunia, Mfuko wa Kimataifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi, Mfuko wa Kusaidia Nchi Zinazoendelea Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Maendeleo la Jumuiya ya Madola, na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengine ni Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda, Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani, Shirika la Fedha la Kimataifa, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa, Shirika la Umoja wa Mataifa la Huduma za Miradi, Shirika la Chakula Duniani, na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengine ni pamoja na Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo, Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Mitaji ya Maendeleo, Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi, Mfuko wa Utekelezaji wa Mkataba wa *Montreal*; Mfuko wa Dunia wa Baioanuwai, *The Good Neighbours Global Impact Foundation*, *Korea Investment Securities,* na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Sekretarieti za Mikataba ya Kikanda na Kimataifa Inayohusiana na Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wengine ni pamoja na *TNC*, *TRC, CRDB, NBC, NMB, Azam Marine, TBC, TADB, PBZ, ZFF, TFF, UpEnergy Tanzania*, *BRAC* Maendeleo Tanzania, *Save the Children*, na *CORUS International*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutumia fursa hii kuwaomba washirika wa maendeleo na wadau wengine kuendelea

kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuimarisha Muungano, hifadhi ya usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, pamoja na Uchumi wa Buluu kwa Maendeleo Endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo kwa washirika wa maendeleo, ninaomba sasa nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa ushirikiano na msaada mkubwa anaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru Dkt. Richard Stanslaus Muyungi, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais; Ndugu Abdallah Mitawi, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Muungano; Ndugu Baraka Luvanda, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Mazingira; Mhandisi Mwanasha Tumbo, Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Dkt. Albina Chuwa, Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni; Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; na Bi. Kathryn Kigaraba, Afisa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni Nchini; Menejimenti na watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, *NEMC* na *NCMC*, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na ya kipekee ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kikwajuni Zanzibar, kwa heshima ya kuwawakilisha tena hapa Bungeni kwa kipindi cha mara ya nne mfululizo. Aidha, ninawashukuru sana Chama cha Mapinduzi kwa kunipa heshima ya kugombea tena katika Jimbo la Kikwajuni, Zanzibar. Ninawaahidi wananchi wa Kikwajuni na Chama changu cha Mapinduzi utumishi wenye ari, bidii, weledi, na utiifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo mwisho kwa umuhimu, ninapenda sana, sana, sana kuishukuru familia yangu pendwa, nikianza na mke wangu kipenzi Bi. Thania Ali Abdulla, watoto wetu Riziki, Asha, Bareek, na Basit, kwa upendo wao unaonipa nguvu ya kutekeleza majukumu yangu vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2026/2027 ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 23,297,959,000 kwa ajili ya matumizi ya Fungu 26, Ofisi Binafsi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,297,959,000 ni kwa ajili ya mishahara, na shilingi 22,000,000,000 ni kwa matumizi mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe shilingi 76,686,837,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ya Fungu 31, ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 38,371,992,000 ni matumizi ya kawaida, na shilingi 4,875,325,000 ni mishahara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, na shilingi 7,096,050,000 ni ruzuku ya mishahara ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, na shilingi 26,400,617,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, fedha za miradi ya maendeleo ni shilingi 38,314,845,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 14,402,000,000 ni fedha za ndani, na shilingi 23,912,845,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninapenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, www.vpo.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/27 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/26 kufuatia mawasilisho yaliyotolewa na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Maji na Mazingira.

Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2026/27.

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai na afya njema ya kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2025/26 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2026/27.

**Salamu za Pongezi na Shukrani**

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuchaguliwa tena kwa awamu ya pili kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na hivyo kupata tena heshima na imani ya Watanzania ya kuweza kuliongoza taifa letu kwa kipindi kingine cha miaka mitano ijayo. Heshima hii inatokana na uongozi wake mahiri na wa kipekee katika sehemu ya kwanza ya awamu ya sita ambapo wote tumeshuhudia mageuzi na maendeleo makubwa katika nchi yetu hususan, katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kipekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniteua tena katika awamu ya pili kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa Balozi **Dkt. Emmanuel John Nchimbi**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na kuendelea kutekeleza vyema jukumu lake la kikatiba la kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuliongoza Taifa letu pamoja na kusimamia masuala ya Muungano, Mazingira na Uchumi wa Buluu nchini. Aidha, ninapenda kumshukuru kwa uongozi wake thabiti unaodhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri anayofanya katika kudumisha Muungano wetu, kusimamia hifadhi ya mazingira nchini na kuimarisha uchumi wa buluu.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kuchaguliwa kwake kwa mara ya pili kumetokana na uongozi wake thabiti aliouonesha katika muhula wake wa kwanza wa uongozi. Aidha, ninamshukuru kwa uongozi wake na maelekezo anayotupa katika kuimarisha mshikamano na ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa **Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.)** kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali. Aidha, ninamshukuru kwa hotuba yake aliyoitoa bungeni tarehe 1 Aprili, 2026 ambayo inatoa mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka 2026/27.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutoa pongezi zangu za dhati kwako Mheshimiwa **Mussa Azzan Zungu (Mb.),** kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninakushukuru kwa namna unavyoliongoza Bunge lako tukufu na ninaahidi kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kutoa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria za nchi.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa **Daniel Baran Sillo (Mb.),** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kazi nzuri anayoifanya katika kumsaidia Spika wa Bunge kutekeleza majukumu yake.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza pia Mheshimiwa **Najma Murtaza Giga (Mb.),** Mheshimiwa **Cecilia Daniel Paresso (Mb.),** na Mheshimiwa **Deodatus Philip Mwanyika (Mb.)** kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninawapongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mheshimiwa **Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb.),** na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira Mheshimiwa **Jackson Gedion Kiswaga (Mb.)** kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Kamati hizo. Aidha, ninawashukuru kwa dhati wajumbe wa kamati hizi mbili kwa kuendelea kunipatia ushirikiano madhubuti katika kutekeleza majukumu yangu ya usimamizi wa masuala ya Muungano, Mazingira na Uchumi wa Buluu. Vilevile, ninawapongeza waheshimiwa wenyeviti wa kamati mbalimbali za kudumu za Bunge waliochaguliwa kusimamia kamati hizo.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuaminiwa, kuchaguliwa na kupewa dhamana kubwa na wananchi ya kuwawakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba uniruhusu niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa heshima na imani kubwa waliopata ya kuteuliwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, ninawashukuru kwa ushirikiano mkubwa ambao wameendelea kunipatia wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu ya kusimamia masuala ya Muungano, Mazingira na Uchumi wa Buluu nchini.

13. ***Mheshimiwa Spika***, kwa dhati nimpongeze Mheshimiwa **Hamza Saidi Johari** kwa kuaminiwa na kuteuliwa tena kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia, ninamshukuru kwa ushauri wake anaoendelea kutupatia wakati wa utekelezaji wa Majukumu yetu.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa moyo mkunjufu ninapenda kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Festo John Dugange (Mb.)** kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Kwa muda ambao nimefanya naye kazi alinishauri vyema na kunisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa weledi na ufanisi wa hali ya juu.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba kumpongeza Mheshimiwa **Reuben Nhamanilo Kwagilwa (Mb.)** kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri - Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). Uchapakazi wake utakuwa nyenzo kubwa katika kuhakikisha Ofisi ya Makamu wa Rais inafikia malengo iliyojiwekea. Hakika kwa muda mfupi ambao nimeanza kufanya naye kazi ameonesha ushirikiano na weledi wa hali ya juu.

**Salamu za Pole**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa salamu za pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa **William Vangimembe Lukuvi** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Mheshimiwa **Jenista Joakim Mhagama** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Mheshimiwa **Halima Idd Nassor** aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi). Tunawaombea Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya salamu hizo na maelezo hayo ya utangulizi, sasa ninaomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha mwaka 2025/26 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2026/27.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26

### i. Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2025/26

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais kibajeti ina Mafungu mawili ambayo ni Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**Fungu 26:**

19. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2025/26, jumla ya Shilingi **19,946,399,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 26. Kati ya

fedha hizo, Shilingi **18,879,500,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **1,066,899,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara.

**Fungu 31:**

20. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Fungu 31, jumla ya Shilingi **47,917,792,000.00** ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **28,858,213,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **19,059,579,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha Shilingi **4,232,310,000.00** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Shilingi **6,675,287,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Shilingi **17,950,616,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo inajumuisha Shilingi **4,602,000,000.00** fedha za ndani na Shilingi **14,457,579,000.00** fedha za nje.

**ii. Fedha zilizopokelewa na kutumika hadi Machi, 2026**

**Fungu 26**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya Shilingi **15,005,068,199.97** fedha za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Fungu 26 sawa na asilimia 75.2 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **14,400,741,199.97** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia 76.3 na Shilingi **604,327,000.00** ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 56.6 ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya Shilingi **14,800,593,132.54** zilitumika sawa na asilimia 98.6 ya fedha zilizopokelewa.

**Fungu 31**

22. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Fungu 31 lilipokea jumla ya **Shilingi 27,136,065,335.56** fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **3,378,708,300.00** ni mishahara ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais sawa na asilimia 79.8 ya bajeti iliyoidhinishwa, Shilingi **4,917,620,285.56** ni

Mishahara ya Watumishi wa NEMC sawa na asilimia 73.7 ya bajeti iliyoidhinishwa, na Shilingi **18,839,736,750.00** ni Matumizi Mengineyo sawa na asilimia 83.8 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa, Shilingi **21,160,209,564.38** zilitumika, sawa na asilimia 78 ya fedha zilizopokelewa.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo, jumla ya Shilingi **17,576,799,447.45** zilipokelewa sawa na asilimia 92.2 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho, fedha za ndani ni Shilingi **10,798,369,447.45** na fedha za nje ni Shilingi **6,778,430,000.00.** Aidha, katika kipindi hicho, Shilingi **14,176,251,453.69** zilitumika ambapo Shilingi **9,076,833,816.69** ni fedha za ndani sawa na asilimia 84 ya fedha zilizopokelewa na Shilingi **5,099,417,637.00** ni fedha za nje sawa na asilimia 75.2 ya fedha zilizopokelewa.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 47(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu; Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Sera ya Taifa ya uchumi wa Buluu ya mwaka 2024; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na marekebisho yake na kanuni zake; na Miongozo na Maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Viongozi Wakuu.

## C. KAZI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI, 2025 HADI MACHI, 2026

### 1) MASUALA YA MUUNGANO

25. ***Mheshimiwa Spika***, Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mwaka huu 2026 Muungano wetu unatimiza miaka 62 tangu kuasisiwa kwake. Wote mtakubaliana nami kuwa tuna jukumu la kuulinda, kuudumisha na kuimarisha Muungano wetu. Hivyo, hatuna budi kukumbuka tukio hili muhimu na kuendeleza mafanikio makubwa yaliyopatikana kisiasa, kiuchumi na kijamii. Aidha, ni muhimu kuendeleza amani, umoja, ushirikiano na kuheshimiana

baina ya pande zote mbili za Muungano. Serikali itaendelea kuulinda, kuudumisha na kuimarisha Muungano wetu adhimu na adimu.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika mambo yasiyo ya Muungano. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:

a) **Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano**

27. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Ofisi imefanya mapitio na kuchapisha Mwongozo mpya wa Vikao vya Kamati ya Pamoja kati ya SJMT na SMZ, Toleo la 2025. Mwongozo huo pamoja na mambo mengine umeainisha jukumu jingine la vikao kuwa ni kujadili masuala mengine yenye maslahi mapana ya pande mbili ikiwemo fursa zilizopo pande mbili za Muungano na si kujadili hoja za Muungano pekee, kwa kuwa kila upande zipo fursa zinazoweza kutumika kwa pamoja au kwa kushirikiana na hivyo kuwa na uelewa wa pamoja wa fursa za pande mbili za Muungano na kuzitolea maamuzi.

28. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia mwaka 2025/26 jumla ya Hoja 22 kati ya Hoja 25 zimepatiwa ufumbuzi na hoja tatu zilizobakia zinaendelea kufanyiwa kazi. Hoja hizo ni pamoja na hoja inayohusu masuala ya kifedha (mgawanyo wa mapato yatokanayo na Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, Faida ya Benki Kuu na Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha); Usajili wa vyombo vya moto; na Uingizaji wa Sukari inayozalishwa Zanzibar katika soko la Tanzania Bara. Serikali zote mbili zina dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba hoja zote zilizobakia zinapatiwa ufumbuzi.

b) **Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Muungano**

29. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa tunaondosha ombwe la changamoto ya uelewa kwa Umma kuhusu elimu ya Muungano hususan kwa vijana, Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa Mpango Kabambe wa Elimu kwa Umma kuhusu Muungano. Mpango huo unahusisha shughuli mbalimbali ikiwemo semina, makongamano, muungano caravan, mashindano ya michezo, mashindano ya insha na programu za redio na televisheni. Miongoni mwa shughuli zilizofanyika kupitia Mpango huo ni pamoja na utolewaji wa elimu kwa makundi mbalimbali ya jamii.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ilitoa semina kwa Wahariri wa Vyombo vya Habari zilizofanyika Zanzibar tarehe 19 Desemba, 2025 na Dar es Salaam tarehe 23 Desemba, 2025.



***Wahariri wa Vyombo vya Habari mbalimbali wakishiriki Semina ya kujenga uelewa kuhusu Muungano iliyofanyika jijini Dar es Salaam Desemba 23, 2025.***



***Wahariri wa Vyombo vya HabarI mbalimbali wakishiriki Semina ya kujenga uelewa kuhusu Muungano iliyofanyika Zanzibar Desemba 19, 2025.***

31. ***Mheshimiwa Spika***, Aidha, Ofisi ilitoa Semina kuhusu masuala ya Muungano kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ukumbi wa Pius - Msekwa Jijini Dodoma tarehe 11 Februari, 2026 na tarehe 27 Februari, 2026 kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, katika Ukumbi wa Mikutano wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.



***Sehemu ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakishiriki Semina ya kujenga uelewa kuhusu Muungano iliyofanyika jijini Dodoma Februari 11, 2026.***



***Sehemu ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakishiriki Semina kuhusu Muungano iliyofanyika Unguja, Zanzibar, Februari 27,2026***

32. ***Mheshimiwa Spika***, Vilevile Ofisi iliandaa na kuratibu Makongamano kuhusu masuala ya Muungano kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya juu wa Vyuo vilivyopo Zanzibar lililofanyika tarehe 19 Februari, 2026 katika Ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.



***Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu Zanzibar wakishiriki Kongamano kuhusu Muungano lililofanyika katika Mkoa wa Kusini, Unguja Februari 19, 2026.***

33. ***Mheshimiwa Spika***, tarehe 6 Aprili, 2026 Ofisi kwa kushirikiana na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ilifanya Kongamano

la Kumuenzi Hayati Sheikh Abeid Amani Karume lililobeba maudhui ya **Mwanamajumui wa Afrika, Mwasisi wa Muungano na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar**. Kongamano hili lilifanyika Dar es Salaam katika Ukumbi wa Karimjee, Ukumbi ambao unabeba historia muhimu ya Taifa la Tanzania kwani matukio mengi muhimu ya kuanzishwa kwa Muungano yalifanyika katika Ukumbi wa Karimjee ikiwemo kuapishwa kwa Sheikh Abeid Amani Karume kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.




***Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni akiwa pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Mhe. Hamza Hassan Juma wakiwasili katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kushiriki Kongamano la Kumbukumbu ya Miaka 54 ya Kifo cha Sheikh Abeid Amani Karume lililofanyika Aprili 6, 2026.***

34. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza jitihada za kutoa elimu kwa umma, Ofisi ilifungua Akaunti mahsusi za mitandao ya kijamii kwa lengo la kuwafikia vijana na kutoa taarifa sahihi kuhusu Muungano. Akaunti hizo ni za *Instagram, Facebook, Youtube, X,* na

*Chatbox* zijulikanazo kwa jina la **miminamuungano** ambazo zinasaidia kuondoa upotoshaji unaofanywa na wasioutakia mema Muungano kupitia mitandao ya kijamii. Katika kipindi cha Januari hadi Februari, 2026 watu waliofikiwa ni 1,800,000. Aidha, jumla ya machapisho 585 yalichapishwa na kusambazwa kupitia mitandao hiyo. Naomba kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa wabunge wote na wananchi kwa ujumla kutembelea akaunti hizi za mitandao ya kijamii ya **#miminamuungano** ili kupata taarifa sahihi kuhusu muungano na kusaidia kuelimisha jamii.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imeandaa na kuchapisha vitini vya maswali na majibu kuhusu Muungano kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya Muungano hususan maswali yanayoulizwa mara kwa mara.




36. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kukusanya kumbukumbu na nyaraka za Muungano kwa ajili ya uanzishwaji wa Vituo vya Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano ikiwemo kumbukumbu, nyaraka, vifaa, video na tasnifu (tafiti) kutoka Taasisi kadhaa.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kutumia mbinu mbalimbali za kuwaelimisha wananchi kuhusu Muungano ikiwemo

kupitia makala mjongeo kwenye vyombo vya usafiri kama vile treni ya mwendokasi (SGR) na boti ziendazo kasi (AZAM Marine), ambapo maudhui mbalimbali kuhusu Muungano hurushwa ikiwemo hatua za Muungano, Faida za Muungano na Viongozi waliohudumu kwenye nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1964 hadi sasa.




***Muonekano wa makala mjongeo kwenye treni ya mwendokasi inayotoa elimu ya Muungano kwa wananchi wanaosafiri.***

38. ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 26 Agosti, 2025, Ofisi ilitoa mafunzo kwa Wakurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara zote za SJMT ambapo moja ya wasilisho lilihusu Majukumu ya Wakurugenzi wa Sera na Mipango katika kulinda na kuimarisha Muungano na umuhimu wa kuzingatia vipaumbele vinavyohusu Muungano katika mipango na Bajeti za Sekta zao.



***Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Ofisi ya Makamu wa Rais Prof. Peter Msoffe (katikati mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na Wakurugenzi wa Sera na Mipango mara baada ya kufungua kikao cha Wakurugenzi wa Sera na Mipango kutoka wizara za kisekta na taasisi kilichofanyika Dodoma Septemba 2, 2025.***

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ilishiriki na kutoa elimu kuhusu Muungano katika Maonesho ya Wakulima (Nanenane), Siku ya kumbukumbu ya Mapinduzi, Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) na Siku ya Mazingira Duniani.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliendelea kurusha vipindi katika Vyombo vya Habari vya TBC na ZBC Redio na TV kupitia kipindi maalum cha '*Hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*'.

41. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kwamba Muungano unaimarishwa kupitia michezo, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar na Wizara zenye dhamana ya michezo kutoka pande zote mbili za Muungano pamoja na Mashirikisho ya Vyama vya Michezo Tanzania (TFF na ZFF) tumefanikiwa kurejesha mashindano ya Muungano kwa Mpira wa Miguu yaliyokuwa yamesimama kwa miaka 20. Kwa mwaka huu mashindano haya yanatarajiwa kufanyika tarehe 21 hadi 29 Aprili, 2026 na yatahusisha timu nane (Simba, Yanga, Azam, Singida Black Stars, Mlandege FC, Mwembe Makumbi City, Mafunzo SC na KVZ FC).

42. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mpira wa Pete (Netiboli), kwa mara ya kwanza Timu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ilishiriki mashindano ya ligi ya Netiboli ya Muungano yaliyofanyika Zanzibar katika Viwanja vya Netiboli vya *New Amaan Complex* kuanzia tarehe 15 hadi 24 Januari, 2026. Lengo la mashindano hayo ni kudumisha Muungano, kujenga umoja na mshikamano, kuleta burudani pamoja na kuboresha afya. Aidha, mashindano ya Mieleka ya kombe la Muungano yameanzishwa kwa mara ya kwanza mwaka huu 2025/26. Ofisi ilitumia mashindano hayo kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano.




***Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa na viongozi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na wachezaji wa Timu ya Netiboli ya Ofisi hiyo baada ya kukabidhiwa Kombe na vyeti ambavyo imepata katika mashindano maalum ya Ligi ya Muungano iliyofanyika Zanzibar Januari 15 hadi 24, 2026 wakati wa Hafla ya kuwafuturisha wachezaji hao nyumbani kwake Dodoma Machi 11, 2026.***

### c) Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii

43. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu gawio kwa SMZ ambapo hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya shilingi bilioni **48.5** zilipelekwa Zanzibar. Fedha hizo zinajumuisha gawio la *PAYE* kwa watumishi wa Zanzibar wanaofanya kazi Tanzania Bara - shilingi

bilioni 14; Misaada Nafuu ya Kibajeti (GBS) - shilingi bilioni 21; na gawio la faida ya Benki Kuu - shilingi bilioni 13.5.

d) **Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Zanzibar**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea na usimamizi na uratibu wa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa wabunge wa majimbo 50 ya Zanzibar kwa mujibu wa kifungu 4(2) cha Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo Sura 96. Aidha, katika kujenga uelewa mpana juu ya usimamizi na matumizi ya fedha za Mfuko wa jimbo pamoja na kupokea maoni ya mapendekezo ya marekebisho ya sheria hiyo, tarehe 26 Februari, 2026 Ofisi iliandaa na kutoa semina kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wakurugenzi wa Halmashauri, Manispaa na Mabaraza ya Miji ya Zanzibar ambao ndio wasimamizi wa miradi inayotekelezwa na fedha hizo.




***Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla (katikati) pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Mhe. Hamza Hassan Juma katika picha ya pamoja na baadhi ya Wabunge kutoka Zanzibar walioshiriki Semina Kuhusu Usimamizi wa Fedha za***

***Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, iliyofanyika Zanzibar Februari 26, 2026.***

45. ***Mheshimiwa Spika,*** *katika mwaka 2025/26* Ofisi imeendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo 50 ya Zanzibar, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 jumla ya shilingi bilioni **2.034** zimepelekwa Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika sekta ya elimu, afya, maji, barabara na shughuli za kijamii.

**e) Kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano**

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano kama yalivyoainishwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) ambapo Wizara, Idara na Taasisi za Muungano zinatekeleza majukumu hayo.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Ofisi imeendelea kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Muungano na kuhakikisha kuwa Taasisi hizo zinatoa huduma stahiki kwa wananchi wa pande mbili za Muungano.

**f) Miradi na Programu za Maendeleo zinazotekelezwa pande mbili za Muungano**

48. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Serikali imeendelea kuwezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo. Miradi na programu hizo zimefanikiwa kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuboresha ustawi wa jamii.

49. ***Mheshimiwa Spika***, miradi na programu hizo ni pamoja na: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii chini ya TASAF; Mfuko wa Elimu chini ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA); Mradi wa kusafirisha Umeme kupitia Baharini wa Msongo wa Kilovoti 220 kwenda Zanzibar, Kilovoti 132 kwenda Pemba, na Kilovoti 33 kwenda Mafia kupitia Wizara ya Nishati ambao upo katika hatua za utekelezaji.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, *TEA* imeweza kunufaisha wanufaika 8,180 kwa Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar, wanufaika 8,720. Aidha, kwa upande wa Zanzibar TEA imefanikiwa kuanza ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Amali katika eneo la Kangagani – Pemba na ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Amali katika eneo la Kizimkazi, Unguja.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi mingine inayotekelezwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) Tanzania Bara na Zanzibar ni pamoja na: Mfumo wa mawasiliano ya redio kati ya marubani na vituo vya kuongozea ndege; Mradi unaotoa taarifa muhimu kwa marubani; na Mradi wa kwa ajili ya kubadilishana taarifa za anga kwa njia ya kidijitali baina ya Taasisi mbalimbali.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais imeendeleza ushirikiano na Zanzibar katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya Tabianchi ambapo miradi ya mazingira imekuwa ikitekelezwa pande zote mbili za Muungano. Miradi hiyo ni pamoja na Miradi ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kutokana na kuongezeka kwa kina cha Bahari ya Hindi - Sipwese Pemba; na mradi wa kuimarisha jamii na mifumo ikolojia katika kustahimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa misitu ya miombo Tanzania Bara na maeneo kame ya Zanzibar. Aidha, pande mbili zinaendelea kutafuta kwa pamoja fedha za mazingira na mabadiliko ya tabianchi kutoka katika mifuko ya kimataifa kwa lengo la kufanikisha miradi ya mazingira na kufikiwa kwa malengo ya Nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuleta mchango katika maendeleo ya Taifa.

### g) Kuratibu ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya SJMT na SMZ

53. ***Mheshimiwa Spika****,* katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea kuimarisha ushirikiano kati ya SJMT na SMZ ambapo jumla ya vikao kumi na tano (15) vya Ushirikiano na Wizara za Kisekta za (SJMT) na (SMZ) vilifanyika kwa lengo la kubadilishana uzoefu wa Sera, Sheria na utaalamu katika maeneo mbalimbali. Sekta zilizofanya vikao ni: Elimu; Mazingira; Uchumi wa Buluu; Uratibu wa

masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano; Sera na Tafiti; Uchunguzi; Mifugo na Uvuvi; Maji; Fedha; Mambo ya Ndani; Kilimo; Ujenzi; Michezo; Teknolojia ya Habari; na Biashara.



***Aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Festo Dugange pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Mhe. Hamza Hassan Juma wakiwa na watendaji waandamizi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar mara baada ya kikao cha Ushirikiano kilichofanyika Zanzibar Februari 16, 2026.***

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ilifanya ziara maalum ya kutembelea Viongozi Wastaafu wa SJMT na SMZ kwa lengo kupata maelekezo, maoni na uzoefu wao katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais hususan katika kulinda na kudumisha Muungano.



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, alipomtembelea Mhe. Dkt. Ali***

***Mohamed Shein, Makamu wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais Mstaafu wa Zanzibar katika makazi yake Unguja, Zanzibar, Januari 03, 2026.***



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi akizungumza na Rais Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume alipomtembelea katika makazi yake Unguja, Zanzibar Januari 03, 2026.***



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, alipomtembelea Makamu wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal, katika makazi yake Masaki Jijini Dar es Salaam, Januari 02, 2026.***

## 2) HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEVU WA MAZINGIRA NA ABADILIKO YA TABIANCHI

55. ***Mheshimiwa Spika,*** Kama unavyofahamu, tarehe 17 Julai, 2025 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050 ambayo mojawapo ya nguzo zake tatu inahusu Uhifadhi wa Mazingira na ustahimilivu dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi. Vilevile, Ibara ya 3.1.7 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025-2030 imeweka masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kama mojawapo ya masuala muhimu yatakayozingatiwa katika kipindi husika.

56. ***Mheshimiwa Spika***, Hii ni zaidi ya uthibitisho kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu mpendwa imetoa kipaumbele kwa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kama msingi wa ukuaji wa uchumi na ustawi wa watanzania.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhifadhi mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la kuhakikisha kuwa watanzania wote wanaendelea kuishi katika mazingira bora na salama. Hatua hizo ni pamoja na kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191, kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira, kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kama nyenzo mojawapo ya kuimarisha uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kuhamasisha upandaji miti, na uwekezaji katika biashara ya Kaboni. Hata hivyo, jitihada mbalimbali zilizochukuliwa na mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili, uhifadhi wa mazingira umeendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo: Uharibifu wa ardhi; Ukataji ovyo wa miti na uharibifu wa misitu unaochangiwa na utegemezi wa matumizi ya nishati ya kuni na mkaa; Kilimo cha kuhamahama; Uchafuzi wa mazingira; Upotevu wa makazi ya wanyamapori na bioanuai; Uharibifu wa vyanzo vya maji, mifumo ikolojia ya ukanda wa pwani na bahari; Kuenea kwa viumbe vamizi; na Athari za mabadiliko ya tabianchi. Changomoto hizi

zinachangiwa zaidi na uwepo wa shughuli za kibinadamu zisizo endelevu zinazofanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo, Mikakati, Miradi ya hifadhi ya mazingira, na kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu Hifadhi ya Mazingira na mabadiliko ya tabianchi ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama. Kwa mwaka 2025/26, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetekeleza yafuatayo:

**(a) Kuratibu Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 ikiwa ni pamoja na:

**i. Kuratibu Masuala ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira katika Wizara za kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea kuwatumia Maafisa Viungo walioteuliwa ili kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira kwenye Wizara, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizofanyika ni pamoja na kufanya:- Vikao vya kimkakati na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Dodoma kuhusu hatua za kuimarisha usafi wa mazingira na udhibiti wa taka kwa kuzingatia dhana ya uchumi rejeshi (circular economy); Wataalamu wa Mazingira (48) kutoka Sekretarieti za Mikoa na Maafisa (50) kutoka Wizara za Kisekta walijengewa uwezo kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka (2025-2030), na Mpango wa Taifa wa Kuhimili Mabadiliko ya tabianchi (2025-2030).

62. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi pia iliratibu kikaokazi na kuwajengea uwezo Wakurugenzi wa Sera na Mipango kutoka Wizara za Kisekta kuhusu ujumuishaji wa masuala ya mazingira yaliyoainishwa kwenye Dira 2050 katika mipango na bajeti ya Wizara na Taasisi za Umma; Vilevile, wajumbe (25) wa Kamati ya Kitaifa ya ushauri kuhusu Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi walijengewa uwezo kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa Sheria. Sambamba na hilo, katika kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, Ofisi iliratibu Kikao cha Mashirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kilichofanyika Zanzibar tarehe 16 - 17 Februari, 2026 ambapo pamoja na masuala mengine mikakati ya ushirikiano iliyoafikiwa ni pamoja na; kuimarisha biashara ya kaboni; kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia; kujenga uwezo wa kitaalamu katika hifadhi na usimamizi wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; Kuanzishwa kwa mashirikiano rasmi baina ya Mamlaka ya Mazingira Zanzibar (ZEMA) na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ikiwemo ukamilishwaji na utiwaji wa saini wa Hati ya Mashirikiano baina ya Taasisi hizo.



***Aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Festo Dugange (mbele katikati) akiwa na viongozi na wataalamu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) mara baada ya kikao cha ushirikiano kilichofanyika Februari 17, 2026, Zanzibar.***

### b) Kuratibu Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191

#### i. Kanuni na Mikakati ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imefanya mapitio ya Marekebisho ya Kanuni za Ada na Tozo kupitia Tangazo la Serikali Na. 494/2025. Aidha, kabla ya mwaka huu wa fedha kukamilika, Ofisi ya Makamu wa Rais itakamilisha Kanuni za Udhibiti wa Kemikali zinazodumu kwenye Mazingira kwa Muda Mrefu pamoja na Kanuni za Katazo la Matumizi ya Kuni na Mkaa.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26 Ofisi imeandaa Mipango na Mikakati mbalimbali ya usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Mipango na mikakati hiyo ni pamoja na: Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa hali ya Jangwa na Ukame (National Action Program to Combat Desertification, 2025-2030), Taarifa ya Tatu ya Mchango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Nationally Determined Contribution - NDC 3.0); Mpango wa Taifa wa kuhimili athari za Mabadiliko ya Tabianchi (National Adaptation Plan, NAP (2025 – 2035); na Mkakati na Mpango-kazi wa Taifa wa Uhifadhi wa Bioanuai (National Biodiversity Strategy and Action Plan, NBSAP, 2025 - 2030).

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (2025-2030) umejumuisha mikakati na hatua mahsusi za kuimarisha usimamizi endelevu wa ardhi, kuhifadhi na kurejesha uoto wa asili, kuboresha ustahimilivu wa jamii dhidi ya athari za ukame, pamoja na kuimarisha uratibu wa taasisi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa hatua za kukabiliana na kuenea kwa hali ya jangwa nchini. Mpango huu utatekelezwa zaidi kwenye maeneo kame na utachangia katika kupunguza kuenea kwa hali ya jangwa nchini.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Taifa wa kuhimili athari za Mabadiliko ya Tabianchi (2025 – 2035) umeainisha jitihada mbalimbali zinazotakiwa kuchukuliwa ili kuimarisha uhimilivu wa

jamii, mifumo ikolojia na sekta za ukuaji wa uchumi dhidi ya athari za mabadiliko ya Tabianchi. Mpango huu umebainisha sekta tisa (9) za kipaumbele zinazoathiriwa zaidi na mabadiliko ya Tabianchi na kuweka mikakati mahsusi ya kukabiliana na changamoto hiyo. Sekta hizo ni Kilimo, Maji, Uvuvi, Mifugo, Wanyamapori, Miundombinu, Afya, Utalii, na Rasilimali za Ukanda wa Pwani na Bahari.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo Ofisi imeratibu maandalizi ya Taarifa ya Mchango wa Taifa wa tatu wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Nationally Determined Contribution - NDC 3.0). Aidha, taarifa hiyo imezingatia vipaumbele, maslahi na mahitaji ya nchi yetu katika maeneo yanayohusu ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi pamoja na kupunguza uzalishaji wa gesijoto. Nyenzo hizi zilizoandaliwa zinatoa mwongozo wa kitaifa na kubainisha majukumu mahsusi ya wadau katika juhudi za Taifa za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uhifadhi wa bioanuai na mifumo-ikolojia, Ofisi imeratibu maandalizi ya Mkakati na Mpango-kazi wa Taifa wa Uhifadhi wa Bioanuai (2025 - 2030). Mkakati huu una malengo manne (4) yanayoendana na Mpango wa kidunia wa kuhifadhi bioanuai. Malengo hayo yanahusu masuala ya kudhibiti upotevu wa Bioanuai, kuongeza upatikanaji wa huduma za kiikolojia kwa watu na viumbe hai, upatikanaji wa fedha za kuwezesha hifadhi ya bioanuai na ushirikishwaji wa makundi mbalimbali ya kijamii ikiwemo wanawake na vijana. Mkakati huu wa kitaifa, umezingatia masuala ya hifadhi ya mazingira yaliyopo katika Dira 2050 na utatumika katika utafutaji wa fedha za ndani na nje za kuhifadhi bioanuai.

69. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba nitumie Bunge lako tukufu kuendelea kuhimiza wadau ndani na nje ya Serikali kuhakikisha kuwa wanatenga bajeti kuwezesha utekelezaji wa afua mahsusi zilizobainishwa katika mipango na mikakati hiyo ili kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya Nguzo ya Tatu ya Dira 2050 ya hifadhi ya Mazingira na ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi.

### ii. Utoaji wa Vibali vya Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK)

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imetoa vibali sita (06) vya Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK) kwa ajili ya:- Programu ya Ufugaji wa Samaki kwa njia ya Vizimba katika Mikoa ya kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Mwanza, Simiyu, Mara na Geita); Programu ya Mfumo Ikolojia wa Mikumi; Mpango kabambe wa Uendelezaji wa eneo la Kasabi katika Halmshauri ya Kibaha Mkoa wa Pwani; Mradi wa Uboreshaji wa Bonde la Msimbazi; Kongani ya Viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo hususan zao la Korosho, Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, Mkoa wa Mtwara; na Eneo la Maalum la Kiuchumi la Buzwagi, katika Halmashauri ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga.

### c) Kuratibu Utekelezaji wa Mpango . Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032)

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango huu, Ofisi imeendelea kuratibu upatikanaji wa fedha kupitia mifuko ya kimataifa ya Mazingira na kukabiliana na Mabadiliko ya tabianchi ili kutekeleza miradi mbalimbali. Aidha, Miradi mitano imeidhinishiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji. Miradi hiyo ni: Mradi wa kuboresha mifumo ya chakula Nyanda za juu kusini mwa Tanzania Bara na Zanzibar. Mradi huu utatekelezwa katika mikoa ya Njombe (Wanging'ombe), Mbeya (Mbarali na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya), Iringa (Makete), Kaskazini Unguja (Kaskazini B), Kaskazini Pemba (Wete) na Kusini Pemba (Chakechake). Mradi wa Usimamizi Shirikishi na Hifadhi endelevu ya Ikolojia ya Bonde la Mto Wami – Ruvu; Mradi huu unatekelezwa katika mikoa ya Dodoma (Bahi, Chamwino, Dodoma Jiji na Kongwa), Morogoro (Mvomero), Pwani (Kibaha) na Dar es Salaam (Ilala). Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Uimarishaji wa Ustahimilivu wa Jamii katika maeneo kame na vituo vya uhamaji wa Mifugo nchini Tanzania. Mradi huu utatekelezwa katika mikoa ya Simiyu (Meatu), Manyara (Simanjiro), Shinyanga (Kishapu), Arusha (Monduli), Tabora (Igunga), Dodoma (Chemba) na Singida (Ikungi).

**72.** ***Mheshimiwa Spika***, Miradi mingine ni mradi wa Kuendeleza Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia mifumo ikolojia vijijini. Mradi huu utatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya nane (8) ambazo ni: Bunda, Serengeti, Tarime, Ngorongoro, Karatu, Meatu, Busega na Mbulu; na Mradi wa Urejeshwaji na Uhifadhi Endelevu wa Mfumo wa Ikolojia wa Bonde Oevu la Malagarasi–Moyowosi kupitia Mbinu Jumuishi za hifadhi ya bioanuai. Mradi huu utatekelezwa katika Mikoa ya Kigoma (Kasulu na Uvinza), na Tabora (Kaliua na Urambo). Miradi hii kwa ujumla ina thamani ya kiasi shilingi bilioni 102.3.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi hii inalenga katika kukabiliana na visababishi vya uharibifu wa mazingira ambavyo vinatokana na shughuli za kibinadamu zisizoendelevu pamoja na kujenga uwezo wa jamii katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Shughuli za kimkakati zitakazotekelezwa zitahusisha: Masuala ya urejeshaji wa mifumo ikolojia ya misitu na vyanzo vya maji; Shughuli za ufugaji wenye tija na kilimo endelevu kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi; Kuwezesha upatikanaji wa maji katika ngazi ya kaya; na Shughuli mbadala za kiuchumi ambazo ni rafiki kwa mazingira.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kupitia Bunge lako Tukufu niendelee kuhimiza Wizara, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha wanajumuisha katika mipango na bajeti masuala mahsusi ya mazingira yanayohusu sekta zao yaliyobainishwa katika Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

### d) Nishati Safi ya Kupikia

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024- 2034) kwa kuhamasisha matumizi ya Nishati safi ya kupikia kwa taasisi za umma na binafsi zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku, ambapo hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya taasisi 1,350 zimeanza matumizi ya nishati safi ya kupikia zikiwemo Shule za Msingi na Sekondari; Vyuo vya Kati na Ualimu; Magereza; Hospitali; Jeshi la Kujenga Taifa; Hoteli; Migahawa; Mama na Baba lishe.



***Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni (mwenye skafu) akimsikiliza Mkuu wa Wilaya ya Geita Mhe. Hashim Komba wakati alipotembelea Shule ya Sekondari ya Wasichana Geita kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Serikali ya kutumia nishati safi kwa Taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100.***

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati iliendesha mafunzo kwa maafisa dawati 30 wa nishati safi ya kupikia kutoka katika Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es salaam, Lindi na Mtwara kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa ufuatiliaji na uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia 2024 2034.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutumia Bunge lako Tukufu kuhimiza taasisi zilizobaki zinazolisha watu zaidi ya 100 kuhakikisha kuwa zinatumia nishati safi ya kupikia kwa mujibu wa katazo la matumizi ya kuni na mkaa lililotolewa na Serikali Januari, 2024. Vilevile, natoa rai kwa sekta binafsi hususan makampuni yanayouza majiko na teknolojia za nishati safi kuendelea kuweka mazingira wezeshi na nafuu ili kuchochea matumizi ya nishati safi nchini.

### e) Elimu kwa Umma Kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa

mazingira kupitia vyombo vya habari, makongamano, semina, warsha na maonesho ya kitaifa na kimataifa. Aidha, kupitia kipindi maalumu kiitwacho **"Mazingira Yetu na Tanzania Ijayo"** jumla ya vipindi tisa (9) vya runinga, 14 vya redio vilirushwa na habari 655 za kuelimisha umma zilitolewa kupitia magazeti. Vipindi hivyo vilihusu, Matumizi ya nishati Safi ya kupikia, Udhibiti wa Taka Ngumu, Fursa za Uwekezaji katika Sekta ya Mazingira ikiwemo Biashara ya Kaboni, Kampeni ya Upandaji Miti, Udhibiti wa kemikali zinazoharibu tabaka la Ozoni, na Uhamasishaji wa Usafi wa Mazingira.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, elimu kwa umma imetolewa kupitia maadhimisho ya kitaifa, kikanda na kimataifa yanayohusu mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Maadhimisho hayo ni pamoja na: Siku ya Ardhi Oevu, tarehe 2 Februari; Siku ya Mazingira Afrika, tarehe 3 Machi; Siku ya Misitu Duniani, tarehe 21 Machi; Siku ya Maji Duniani, tarehe 22 Machi; na Kuenea kwa Jangwa na Ukame, tarehe 17 Juni; na Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni tarehe 16 Septemba.

### f) Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji Miti

**80.** ***Mheshimiwa Spika****,* Ofisi imeendelea kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji miti milioni 1.5 katika kila Halmashauri nchini ambapo hadi kufikia Machi, 2026 takriban asilimia 76 ya miti iliyopandwa imestawi.



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi akimwagilia mti aina ya mwembe aliopanda wakati alipowasili katika Ukumbi wa Chimwaga jijini Dodoma, kwa ajili ya ufunguzi wa Kongamano la Vijana katika Kumbukizi ya Miaka 104 ya Kuzaliwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Aprili 11, 2026.***

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kampeni hii, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Jiji la Dodoma imeendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kujihusisha na suala la kukijanisha Jiji la Dodoma. Hadi Machi, 2026 jumla ya miti 960,210 imepandwa katika maeneo mbalimbali ya Jiji na iliyostawi ni miti 787,372 sawa na asilimia 82. Aidha, Ofisi itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha kuwa zoezi la upandaji miti katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma linakuwa endelevu kwa ajili ya kupambana na ukame na kuboresha mandhari ya Jiji. Aidha, katika kuimarisha uhifadhi wa mifumo ikolojia ya milima na vilima katika Jiji la Dodoma, Ofisi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma imepanga kudhibiti uharibifu wa maeneo hayo kutokana na shughuli za kibinadamu zisizo rafiki kwa mazingira pamoja na kuweka utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi katika kuwekeza katika shughuli za kiuchumi ambazo zinaendana na misingi ya uhifadhi wa mazingira.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhimiza na kuhamasisha upandaji na utunzaji wa miti nchini hususan kwa kuamua kutumia kumbukumbu ya siku ya kuzaliwa kwake tarehe 27

Januari kila mwaka kupitia kampeni ya "**27 ya Kijani, Mti wa Mama,**" kuwa jukwaa la uhamasishaji wa upandaji miti.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile naomba nitoe pongezi kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kwa kutoa mchango wake mkubwa katika uhamasishaji wa Kampeni ya '27 ya Kijani, Mti wa Mama' pamoja na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na wadau wengine.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwahamasisha wananchi, taasisi na sekta binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kiraia na wadau wengine kufuata nyayo za Mheshimiwa Rais wetu kwa kuendelea kupanda miti na kuitunza hasa katika kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha.

### g) Ushiriki wa Nchi Katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi iliratibu na kushiriki katika mikutano mbalimbali ya Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kama ifuatavyo: -

#### i) Mkutano wa 30 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 30 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Belem, Brazil tarehe 10 hadi 21 Novemba, 2025. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa **Balozi Dkt. John Stephen Simbachawene**, Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Brazil akimwakilisha Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliongoza Kundi la Majadiliano la Wataalamu wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi kupitia Dkt. Richard Stanslaus Muyungi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kundi hilo.




***Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Brazil Mhe. Balozi Dkt. John Stephen Simbachawene (kushoto) akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa 30 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Belem, Brazil Novemba 10 hadi 21, 2025.***

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baadhi ya maazimio yaliyoafikiwa katika Mkutano huo ni pamoja na kupitishwa kwa vigezo vitakavyotumika kufanya tathmini ya nchi zitakazonufaika na fedha za utekelezaji wa miradi kupitia ufadhili wa Mfuko wa Kushughulikia Uharibifu na Hasara (The Fund for Responding to Loss and Damage) zitokanazo na athari za mabadiliko ya Tabianchi. Vilevile, iliazimiwa kuwa nchi nufaika zinaweza kupata ruzuku kati ya Dola za Marekani Milioni 5 hadi 20 kwa kila dirisha litakalokuwa linatangazwa na mfuko husika. Ili kupata ruzuku hizo, Tanzania inakamilisha andiko la mradi chini ya Mfuko husika.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika majadiliano kuhusu malengo ya Dunia ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi, nchi wanachama zilikubaliana kupitishwa kwa viashiria 59 vitakavyotumika kupima utekelezaji wa shughuli za uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Uamuzi huu utasaidia kuimarisha ustahimilivu na kupunguza hatari zitokanazo na athari za mabadiliko ya tabianchi na hivyo kuchangia katika utekelezaji wa Makubaliano ya Paris. Maazimio mengine yaliyofikiwa ni pamoja na: Nchi zinazoendelea kukataa maombi ya nchi zilizoendelea ya kutokutumia makaa ya mawe na gesi asilia ili

kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi; na Nchi wanachama kuanza kutekeleza programu ya ubunifu wa teknolojia na uhaulishaji wake kwa nchi zinazoendelea.




***Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Dkt. Richard Muyungi (kushoto) wakati huo akiwa Mwenyekiti wa Kundi la Majadiliano la Afrika (AGN,) akiwasilisha taarifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya Nchi 54 kwenye Mkutano wa 30 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Belem, Brazil Novemba 10 hadi 21, 2025.***

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mkutano huu umeleta tija kwa Taifa ambapo Tanzania iliweza kupata ahadi ya fedha kutoka katika Mifuko, Washirika wa maendeleo na Wadau mbalimbali wa Mkataba huo zinazotokana na mikutano ya uwili baina ya Tanzania na mashirika ya kimataifa. Jumla ya Dola za Marekani Milioni 868.42 na Euro 500,000 ziliahidiwa kutolewa kwa Tanzania kwa ajili ya program na Miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi, Nishati safi ya kupikia, usimamizi wa Taka na uhifadhi wa bioanuai. Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya kiasi cha shilingi Bilioni 24 kimepatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi kwenye vyanzo vya maji katika Bonde la Wami-Ruvu katika mto Mkondoa.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** mikutano mingine iliyofanyika chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi inajumuisha: Mkutano wa Pili wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika tarehe 8 – 10 Septemba, 2025 Jijini Addis Ababa, Ethiopia. Mkutano huo ulipitisha Azimio la Viongozi wa Afrika kuhusu mabadiliko ya tabianchi na wito

wa kuchukua hatua kupambana na mabadiliko ya tabianchi; na Mkutano wa Matumizi ya Akili Unde katika Kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi ukiwa na lengo la kuongeza ufanisi wa matumizi ya teknolojia ya Akili Unde katika sekta za Kilimo, Misitu, Maji, Umwagiliaji na udhibiti wa majanga ya asili uliofanyika Dar es Salaam tarehe 8-9 Oktoba 2025.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine makubwa yaliyopatikana katika medani ya kimataifa katika masuala ya mazingira ni pamoja na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitishwa rasmi kuwa mjumbe wa kudumu wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali ya Umoja wa Afrika kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, Umoja wa Afrika ulipitisha Azimio la kumtambua rasmi **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kuwa kinara wa uhamasishaji wa masuala ya nishati safi ya kupikia Barani Afrika.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni pamoja na: Jiji la Dar es Salaam kuwa mwenyeji wa Ofisi ya Kikanda ya Kujenga Uwezo wa nchi zinazoendelea katika kukabiliana na Upotevu na Hasara zitokanazo na athari za Mabadiliko ya Tabianchi (Regional Office for Santiago Network on Loss and Damage); na nchi yetu kuwa mwenyeji wa Kituo Mahiri cha Afrika cha Kujenga uwezo wa Vijana kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi.

### ii) Mkutano wa 27 wa Kamati ya kitaalamu chini ya Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 27 wa Kamati ya Ushauri wa Kitaalamu wa Mkataba wa hifadhi ya Bioanuai uliofanyika tarehe 20 hadi 30 Oktoba, 2025 Panama. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Dunia wa Kuhifadhi Bioanuai.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** makubaliano yaliyofikiwa katika mkutano huo ni pamoja na nchi wanachama: Kuendeleza sera zinazoimarisha kilimo rafiki kwa mazingira na kupunguza uharibifu wa

makazi asilia; Kuanzisha programu za kitaifa za kutathmini athari za kilimo kwa bioanuai; Kuwezesha mataifa kupata teknolojia, fedha na ujuzi wa utafiti kuhusu kilimo endelevu; Kuimarisha udhibiti wa viumbe vamizi katika mipaka; na kuwezesha nchi kutengeneza mifumo ya tahadhari ya mapema.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** manufaa yaliyopatikana kupitia ushiriki katika Mkutano huo ni pamoja na kujengewa uwezo kwa wataalam kuhusu tathmini ya hali ya uhifadhi wa bioanuai, rasilimali fedha zinazohitajika kuhifadhi bioanuai nchini na tathmini zingine ambazo ziliwezesha uandaaji wa Mkakati na Mpango kazi wa Taifa wa Uhifadhi wa Bioanuai (20252030). Aidha, katika ushiriki wa mkutano huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipata kiasi cha fedha jumla ya shilingi **931,791,960.00** kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kuimarisha Uhifadhi na Usimamizi wa bioanuai nchini.

### iii) Mkutano wa 15 wa nchi wanachama wa Mkataba wa RAMSAR kuhusu uhifadhi wa ardhi oevu

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano wa 15 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Ramsar kuhusu ardhi oevu uliofanyika Victoria Falls, Zimbabwe, tarehe 23 hadi 31 Julai, 2025. Maazimio ya Mkutano ni pamoja na: Kuongeza bajeti katika usimamizi na utekelezaji wa Sera, mipango, kanuni na mikakati ya kusimamia maeneo ya ardhi oevu; Nchi wanachama kutengeneza mfumo kwa kutafuta rasilimali fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa masuala ya usimamizi wa maeneo oevu ikiwemo kufanya tathmini ya uharibifu wa maeneo ya ardhi oevu; na Kuboresha mbinu za utoaji elimu ya mazingira hususan elimu ya utunzaji wa maeneo ya ardhi oevu.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mkutano huu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Wataalam wa Nchi wanachama wa Mkataba kwa nchi zilizopo Mashariki ya Bara la Afrika na mjumbe katika kikosi kazi cha

kutathmini Miji yenye hadhi ya kuitwa 'Miji yenye hifadhi ya maeneo ya ardhi oevu'.

### iv) Mkutano wa Saba (7) wa Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Saba wa Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEA-7) uliofanyika Nairobi, Kenya, kuanzia tarehe 1 hadi 12 Desemba, 2025. Ujumbe wa Tanzania katika mkutano huo uliongozwa na aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na wenye Ulemavu, Hayati **William Vangimembe Lukuvi (Mb.),** (Mungu amrehemu) ambaye alimwakilisha **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Maazimio yaliyofikiwa katika mkutano huo ni pamoja na nchi wanachama: Kujenga uwezo wa nchi kukabiliana na viumbe vamizi, kuimarisha ustahimilivu wa miamba ya matumbawe, uhifadhi wa barafu ikiwemo Mlima Kilimanjaro, na udhibiti wa moto holela; Kukabiliana na usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya madawa na udhibiti wa kemikali na taka; na Kuhakikisha Matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira na matumizi ya Akili Unde katika hifadhi ya mazingira. Pamoja na masuala mengine, mkutano huo ulimpitisha Mhandisi **Hamad Yussuf Masauni (Mb.),** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kuwa Makamu wa Rais wa Mkutano wa nane (8) wa Baraza la Mazingira Duniani (UNEA-8).



***Aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Festo Dugange (kushoto) akimwakilisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni kushiriki Mkutano wa Baraza la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEA-7) uliofanyika jijini Nairobi, Kenya Desemba 11, 2025.***

**v) Mkutano wa sita (6) wa nchi wanachama wa Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki**

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano wa sita (6) wa nchi wanachama wa Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki. Mkutano huo ulifanyika tarehe 03 hadi 07, Novemba, 2025 Geneva, Uswisi. Mojawapo ya azimio muhimu katika Mkutano huu ni nchi wanachama kukubaliana kwa pamoja kusitisha matumizi ya zebaki kama kiambata cha dawa ya kuzibia meno (Dental Amalgam) ifikapo mwaka 2034 ili kulinda afya ya binadamu na mazingira. Aidha, Tanzania ilianza matumizi mbadala ya zebaki katika matibabu ya meno kabla ya kufikiwa kwa azimio hili.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Maazimio mengine yaliyoafikiwa katika mkutano huo ni pamoja na Nchi wanachama: Kushirikiana

kukomesha biashara haramu ya zebaki; Kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu; Kuhakikisha kuwa uchafuzi utokanao na zebaki hauzidi kiwango cha 15mg/kg; na Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mkataba kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025 ambapo Tanzania imewasilisha taarifa husika kwa Sekretarieti ya Mkataba.

**vi) Mkutano wa 13 wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Bonde la Ziwa Tanganyika**

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa nchi katika Mkutano wa 13 wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Bonde la Ziwa Tanganyika uliofanyika tarehe 13 hadi 17 Oktoba, 2025 Lusaka, Zambia. Maazimio yatokanayo na Mkutano huo ni pamoja na: Nchi wanachama kutekeleza azimio la kusitisha kwa muda shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa miezi mitatu (3) ili kuweka mazingira ya utulivu kiikolojia kuwezesha kuzaliana kwa viumbe maji na kuongezeka kwa rasilimali za uvuvi; Kukamilisha taratibu stahiki za uridhiaji wa itifaki ya Ufugaji wa samaki na viumbe maji katika Ziwa Tanganyika; na Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 14 wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Bonde la Ziwa Tanganyika utakaofanyika Oktoba, 2026 Jijini Dar es Salaam. Aidha, Mkutano huo ulimpitisha Dkt. Emma Liwenga ambaye ni Mtanzania kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi ya kikanda chini ya mkataba husika kwa kipindi cha miaka mitatu (20262029).



***Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Dkt. Richard Muyungi (kushoto) akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika, Dkt. Emma Liwenga, Februari 24, 2026 baada ya kufanya mazungumzo na kumpongeza kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo.***

**h) Utekelezaji wa Nguzo ya Dira 2050 Kuhusu Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi.**

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais imejipanga kutekeleza Dira 2050 ipasavyo hususan Nguzo ya tatu kuhusu Uhifadhi ya Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi ambapo imeandaa Mpango Mkakati wa Ofisi wa mwaka 2026 – 2030. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa Programu ya Mageuzi ya Kimkakati ya Mazingira Endelevu Tanzania yenye lengo la kuimarisha uhimilivu wa mabadiliko ya Tabianchi kwa kuongeza eneo lenye uoto wa kijani kupitia upandaji miti na usimamizi wa mazingira.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Programu hii ni nyenzo muhimu ya utekelezaji wa Dira 2050 ambayo pamoja na masuala mengine itahamasisha uhifadhi wa mazingira kama ajenda ya kitaifa, itakuwa shirikishi hasa katika ngazi ya jamii, itajenga hamasa na mwamko wa kipekee nchini na itasimamiwa moja kwa moja na Viongozi Wakuu wa Serikali ili kuipa kipaumbele katika mipango ya maendeleo katika ngazi zote. Baadhi ya maeneo ya kipaumbele katika Programu hii ni pamoja na:- Kuhamasisha jamii na wadau

katika kupanda na kutunza miti bilioni 2 na hekta 100,000 za bustani za kijani kwa mwaka; Kuwezesha urejeshwaji na uhifadhi wa ardhi ya kilimo, ardhi-oevu, misitu, na nyanda za malisho zilizoharibiwa kiasi cha hekta milioni 1 kwa mwaka; Kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa angalau Taasisi 13,000; Utekelezaji wa miradi 35 ya biashara ya kaboni katika sekta ya Usafirishaji, Misitu, na Nishati safi na Usimamizi wa Taka; na Kuchangia utekelezaji wa Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani (2023–2030) unaolenga kupanda miti Milioni 3 kila mwaka.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** Programu hii inatarajiwa kuzinduliwa katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani tarehe 5 Juni, 2026. Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa muda wao kwa ajili ya kutoa maoni yao yaliyosaidia kuboresha programu hii.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na uzinduzi wa programu hiyo, shughuli nyingine zitakazofanyika katika Wiki ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira ni pamoja na: Utoaji wa elimu kwa umma kuhusu masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi; Shughuli za kielelezo za uhifadhi wa mazingira; na Maonesho ya teknolojia na mbinu mbalimbali za uhifadhi wa mazingira zinazotekelezwa na wadau mbalimbali. Shughuli hizo zitahusisha Wizara, Idara na Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi, Asasi za kiraia, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Washirika wa Maendeleo na wananchi kwa ujumla.

**107.** ***Mheshimiwa Spika****,* nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuutangazia umma kuwa Wiki ya Mazingira itumike ipasavyo kama jukwaa la kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa vitendo. Wananchi wahamasishwe kushiriki katika upandaji miti, usafi wa mazingira, matumizi ya nishati safi, na kuzingatia sheria na kanuni za mazingira.

**i) Utekelezaji wa Miradi ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi iliratibu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kama ifuatavyo:

**i) Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo Ikolojia, Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai Tanzania**

**109.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka wa fedha 2025/26, Ofisi imeendelea na utekelezaji wa Mradi huu unaolenga kuimarisha usimamizi jumuishi wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibiwa ili kujenga uhimilivu wa mifumo-ikolojia na jamii kwa ujumla nchini Tanzania. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF). Mradi unatekelezwa katika Mikoa ya: Iringa (Halmashauri ya Wilaya ya Iringa); Mbeya (Halmashauri ya Wilaya za Mbeya na Mbarali); Njombe (Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe); Katavi (Halmashauri ya Wilaya za Tanganyika na Mpimbwe); na Rukwa (Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga). Kiasi cha shilingi bilioni 5.028 kilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: Ujenzi wa mfereji wa umwagiliaji; muindombinu ya kuwezesha ufugaji wenye tija; urejeshaji wa misitu na ardhi; mipango ya matumizi bora ya ardhi; na shughuli mbadala za kiuchumi ambazo ni rafiki kwa mazingira.

**ii) Mradi wa Kuanzisha Bustani ya Kijani Katika Eneo la Swaswa, Dodoma**

**110.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka wa fedha 2025/26, Ofisi imeendelea na utekelezaji wa mradi huu unaolenga kuboresha mandhari ya eneo la Bwawa la Swaswa kwa lengo la kuongeza uhimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, na kuwezesha kufanyika kwa shughuli za kiuchumi. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani na za nje kupitia Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF). Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na; Kukamilisha Tathmini ya Athari

kwa Mazingira (TAM) na kupata Kibali cha Mazingira; na Kupatikana kwa Mkandarasi ambaye ataanza shughuli za ujenzi.

### iii) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea na utekelezaji wa Mradi huu unaolenga kujenga uwezo wa Kitaasisi kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Utekelezaji wa Itifaki ya Montreal ambapo hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha shilingi milioni 250 kilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zifuatazo: Kutoa mafunzo kwa maafisa wa Idara za Serikali na mawakala wa forodha katika mipaka ya Holili, Horohoro, Tunduma na Bandari ya Tanga na Dar es Salaam pamoja na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius K. Nyerere kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa vifaa na kemikali zinazoweza kusababisha uharibifu wa tabaka la ozoni na ongezeko la joto duniani; Kutoa mafunzo kwa mafundi mchundo wa viyoyozi na majokofu kuhusu namna bora ya kuhudumia vifaa hivyo; na Ununuzi wa mashine za kunasa na kurejeleza gesi chakavu za majokofu na viyoyozi katika Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya, Vyuo vya Elimu ya Ufundi stadi vya Zanzibar, Chang'ombe, Kilimanjaro, Morogoro, Kigoma, Lindi, na Arusha. Vilevile, kupitia mradi huu Ofisi imeandaa Mpango wa Taifa wa Usimamizi na uondoshaji wa kemikali chakavu nchini.

### iv) Mradi wa Kujenga Ustahimilivu wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Mkoani Kigoma

**112.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kujenga Ustahimilivu wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Mkoani Kigoma. Lengo la mradi ni kuboresha mifumo ikolojia na kuimarisha ustahimilivu wa jamii dhidi ya mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Kigoma na kuchangia kuboresha mazingira. Mradi huu unatakelezwa katika

Halmashauri ya Wilaya za Kasulu, Kibondo na Kakonko. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuajiri timu ya uratibu wa mradi na Ununuzi wa vitendea kazi.

**v) Mradi wa kuimarisha jamii na mifumo ikolojia katika kustahimili athari za mabadiliko ya tabianchi wenye Ukanda wa misitu ya miombo Tanzania Bara na maeneo kame ya Zanzibar.**

**113. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, Ofisi imeanza utekelezaji wa mradi huu unaolenga kupunguza na kuimarisha uhimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi katika jamii pamoja na mifumo ikolojia kwenye ukanda wa Misitu ya Miombo Tanzania Bara na maeneo kame Zanzibar. Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia 2025 hadi 2029 kwa gharama ya Dola za Marekani 4,416,210 sawa na shilingi 10,598,904,000.00, fedha kutoka Mfuko wa Dunia wa Mazingira kupitia Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO). Mradi huu unatekelezwa katika Mikoa saba, mitatu (03) ya Tanzania Bara ambayo ni Tabora (Sikonge), Katavi (Nsimbo) na Rukwa (Nkasi) na minne (04) ya Zanzibar ambayo ni Unguja Kaskazini (Kaskazini B), Unguja Kusini (Kusini), Pemba Kaskazini (Micheweni) na Pemba Kusini (Chakechake).

**vi) Mradi wa Ujenzi wa Kuta za kuzuia Maji ya Bahari katika Fukwe za Mikindani – Mtwara na Sipwese Pemba.**

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea na ujenzi wa kuta na Matuta kwa ajili ya kuzuia maji ya bahari kuingia kwenye makazi na mashamba pembezoni mwa fukwe za Mikindani Mtwara na Sipwese Pemba. Ofisi imepokea kiasi cha shilingi milioni 392 kwa ajili ya kukamilisha shughuli za mradi ambapo ujenzi umefikia asimilia 95 kwa upande wa Sipwese na asilimia 75 kwa upande wa Mikindani.

### vii) Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais

115. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kutekeleza mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. Kwa mwaka 2025/26, kazi zilizofanyika ni ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli II, Makazi ya Oysterbay (Dar es Salaam) na Kilimani Dodoma.



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi akikagua ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais iliyopo Mtaa wa Luthuli, Posta Jijini Dar es Salaam Januari 29, 2026.***

## 3) MASUALA YA UCHUMI WA BULUU NCHINI

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Uchumi wa Buluu ni moja ya maeneo mapya ya kimkakati yenye mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za bahari, maziwa, mito, mabwawa, maji chini ya ardhi na maeneo oevu kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi, kuboresha maisha ya jamii na hifadhi ya rasilimali za Uchumi wa Buluu. Maeneo haya yana fursa kubwa za kuongeza uzalishaji, kukuza biashara na uwekezaji, kutoa ajira kwa vijana na wanawake, kuimarisha usalama wa chakula, pamoja na kuongeza mchango wa sekta husika katika Pato la Taifa.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 imetambua sekta ya Uchumi wa Buluu kuwa ni sekta ya mageuzi katika kufikia malengo ya Dira hii. Hatua hii ni dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuhakikisha Uchumi wa Buluu unakuwa nguzo muhimu ya uchumi shindani, jumuishi na endelevu.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024 na Mkakati wake wa Utekelezaji kwa kuweka mfumo wa uratibu wa shughuli za Uchumi wa Buluu ikiwemo kuanza maandalizi ya Mpango wa Matumizi endelevu wa Maeneo ya Maji (Marine Spatial Planning - MSP).




**Kuratibu Utekelezaji wa Shughuli za Uchumi wa Buluu**

119. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Serikali imeanzisha Kitengo cha Maendeleo ya Uchumi wa Buluu na Uratibu chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Hatua hii imeimarisha uratibu wa shughuli za Uchumi wa Buluu nchini na kuweka msingi wa usimamizi jumuishi wa sekta zote zenye mnasaba na Uchumi wa Buluu.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uratibu huo kwa ngazi za kisekta, Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Uchumi wa Buluu kupitia Kamati za maamuzi kwa ngazi ya Makatibu Wakuu na Mawaziri. Vilevile, Ofisi imewateua Maafisa Viungo wa Uchumi wa

Buluu katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, ambao wamekuwa na mchango mkubwa katika kurahisisha mawasiliano, usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Uchumi wa Buluu nchini.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na kuanzishwa kwa mifumo hiyo ya uratibu, Serikali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi na wataalamu kwa kuwawezesha kushiriki mafunzo ya kikanda na kimataifa, ambapo wataalam watano waliwezeshwa kushiriki mafunzo kuhusu uandaaji wa Mpango wa matumizi endelevu wa Maeneo ya Maji yaliyofanyika Zanzibar tarehe 24 Novemba hadi 03 Disemba, 2025; na Kushiriki kwenye makongamano na Warsha za Uchumi wa Buluu. Lengo la hatua hizi ni kupata wataalamu wenye uwezo wa kusimamia kwa ufanisi Mipango, Sera na Mikakati ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu nchini.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ajenda ya Uchumi wa Buluu inaeleweka vyema kwa Viongozi Wakuu wa Serikali na kusimamiwa kikamilifu, Ofisi iliratibu warsha ya mafunzo kwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, na Manaibu Makatibu Wakuu iliyofanyika tarehe 4 Desemba, 2025 kwa ajili ya kupata uelewa kuhusu fursa za kifedha zinazotolewa na Umoja wa Ulaya kupitia Taasisi zenye ithibati ya Umoja wa Mataifa na taasisi za fedha ikiwemo Benki za NMB, CRDB na KCB. Aidha, warsha hii ililenga kutoa msisitizo kwa Viongozi kufuatilia utekelezaji wa Miradi inayotekelezwa kupitia Wizara na Taasisi zao. Vilevile, wanufaika wa fursa hii ni wananchi kupitia vikundi vinavyoratibiwa na Wizara za kisekta zenye mnasaba na Uchumi wa Buluu.

123. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kuimarisha ushirikiano wa masuala ya Uchumi wa Buluu baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Ofisi iliratibu Kikao cha Mashirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kilichofanyika tarehe 13 Februari, 2026 ambapo mikakati ya ushirikiano iliyoafikiwa ni pamoja na:- Kuendeleza na kuratibu tafiti jumuishi za Uchumi wa Buluu kati ya SJMT na SMZ; Kufanya maandalizi na utekelezaji wa miradi ya pamoja katika shughuli za

Uchumi wa Buluu; Uandaaji wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji (*Marine Spatial Planning – MSP*); Ushiriki wa pamoja katika Mikataba na Majukwaa ya Kikanda na Kimataifa yanayohusu Uchumi wa Buluu; na Kujengeana uwezo, kubadilishana taarifa, uzoefu na mbinu bora za utekelezaji wa shughuli za Uchumi wa Buluu kwa pande zote mbili.

### b. Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji (Marine Spatial Planning - MSP)

124. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa matumizi endelevu ya rasilimali za Uchumi wa Buluu, katika mwaka 2025/26 Serikali imeanza mchakato wa kuandaa Mpango wa Matumizi Endelevu wa Maeneo ya Maji. Mpango huu ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha rasilimali za bahari na maji baridi zinatumika kwa tija, kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi, kuboresha maisha ya jamii na hifadhi ya rasilimali za maji kwa lengo la kupunguza migongano ya matumizi na kufungua fursa mpya za uwekezaji.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizofanyika ni pamoja na: Kuandaliwa kwa Taarifa ya Tathmini ya Hali ya Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji Tanzania; Kuandaliwa kwa Mkakati wa Ushirikishwaji wa Wadau katika Kuandaa na Kutekeleza wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji wa mwaka 2026–2035; na Mpango Kazi wa Maandalizi ya Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji wa mwaka 2025–2030.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya majaribio ya uandaaji wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji katika Halmashauri za Wilaya ya Mkinga Mkoani Tanga, pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga Mkoani Pwani. Lengo la miradi hii ni kupata uzoefu wa kitaalam na kiutekelezaji utakaoisaidia nchi kuandaa kwa ufanisi Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji na kupunguza changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wake.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** Napenda kutumia fursa hii kuwahimiza wadau wote kushiriki kikamilifu katika zoezi la uandaaji wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji, kwa kuwa huu ni mpango shirikishi utakaosaidia kuondoa migongano ya matumizi ya rasilimali zilizopo ndani ya maji, kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za Uchumi wa Buluu na kuwezesha ukuaji wa uwekezaji katika sekta mbalimbali za Uchumi wa Buluu.

### c. Elimu kwa Umma kuhusu Masuala ya Uchumi wa Buluu

128. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Uchumi wa Buluu kupitia vyombo vya habari, makongamano, semina, warsha na maonesho ya kitaifa na kimataifa. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuratibu Kongamano la Tatu la Kimataifa la Uchumi wa Buluu lililofanyika Jijini Dar es Salaam na kukutanisha wataalam na watafiti kutoka ndani na nje ya nchi kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kutangaza fursa za Uchumi wa Buluu.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Ofisi iliratibu na kufanikisha Kongamano la kwanza la Kitaifa la Wadau wa Uchumi wa Buluu (National Blue Economy Stakeholders Conference - NBESC) lililofanyika tarehe 10 hadi 11 Septemba, 2025 Jijini Dar es Salaam. Kongamano hilo lililenga kujadili fursa, changamoto na mikakati ya kuendeleza sekta ya Uchumi wa Buluu nchini pamoja na kutambua hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kuimarisha sekta ya Uchumi wa Buluu.




***Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais Bw. Abdallah Hassan Mitawi (katikati) akiongoza Kongamano la Kitaifa la Wadau wa Uchumi wa Buluu lililofanyika jijini Dar es Salaam Septemba 10 hadi 11, 2026.***

130. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha elimu kuhusu Uchumi wa Buluu inawafikia wadau wengi zaidi, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa Umma kupitia Mikutano, Semina, Warsha mbalimbali ambazo zilirushwa kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio, runinga na mitandao ya kijamii ambapo elimu kuhusu fursa, umuhimu na wajibu wa kila mdau katika kukuza sekta imeendelea kutolewa kupitia kaulimbiu isemayo "Uchumi wa Buluu na Tanzania Tuitakayo".

### 4) MASUALA MENGINE YALIYOTEKELEZWA

131. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na Ofisi kwa kipindi cha mwaka 2025/26 ni pamoja na: Kuendelea kusimamia masuala ya utawala na usimamizi wa rasilimali watu ikiwemo utoaji wa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi.

### 5) BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

132. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Mipango, Miongozo na

maelekezo mbalimbali ya viongozi wa Serikali. Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Baraza lilitekeleza shughuli zifuatazo:

**a) Uzingatiaji na Usimamizi wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191**

**i) Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira**

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi,2026 Baraza lilifanya kaguzi katika miradi 3,408 ikijumuisha viwanda, migodi (yakiwemo machimbo ya mchanga na kokoto), mitambo ya gesi na mafuta na nishati ya umeme, machinjio ya wanyama, kumbi za starehe, nyumba za ibada, hoteli, mabomba ya mafuta, maghala ya kemikali na taka zenye madhara, vituo vya mafuta, masoko, madampo, hifadhi ya vyanzo vya maji, mashamba, mifumo ya maji taka, Taasisi za elimu na afya, maghala ya kuhifadhi kemikali na taka hatarishi, majengo ya biashara na makazi pamoja na miradi mingine ya maendeleo nchini.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya kaguzi hizo ni pamoja na kuongezeka kwa uzingatiaji wa Sheria na ubora katika hifadhi ya mazingira kwa maeneo yote yaliyokaguliwa. Hii imetokana na ongezeko la utoaji elimu na ushauri kuhusu uhifadhi wa mazingira na uzingatiaji, uwekaji mifumo thabiti ya kuhifadhi taka ngumu, kuboresha mifumo ya kutibu majitaka na udhibiti wa hewa chafu. Hata hivyo, miradi 137 sawa na 4% ya miradi iliyokaguliwa ilibainika kutozingatia sheria na hivyo wahusika walichukuliwa hatua stahiki za kisheria. Kutokana na kaguzi hizo, kumekuwa na ongezeko la wawekezaji wanaojisajili kwa ajili ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na kaguzi za mazingira kutokana na uhamasishaji na ufuatiliaji unaofanyika.



***Watalaam wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Ilala jijini Dar es Salaam, Februari 25, 2026 wakifanya ukaguzi wa mazingira pamoja na kutoa elimu ya Uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira viwandani.***

**i) Udhibiti wa Taka Hatarishi**

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Baraza limeendelea kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Udhibiti wa Taka Hatarishi za mwaka 2019 na marekebisho yake ya mwaka 2021. Katika kipindi hicho, jumla ya maombi 224 ya vibali vya usimamizi wa taka hatarishi yalipokelewa, ambapo vibali 212 vilitolewa sawa na asilimia 95. Vilevile, Baraza lilipokea maombi 28 ya uteketezaji wa taka hatarishi na kusimamia uteketezaji na udhibiti wake ambapo kiasi cha tani 15,572.7 ziliteketezwa. Taka hizo ni pamoja na:- Dawa zilizokwisha muda wake, vifaa tiba vilivyokwisha muda wake pamoja na mabati ya ASBESTOS.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako Tukufu, niwakumbushe watu binafsi na Makampuni yanayojihusisha na biashara ya taka hatarishi kuzingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zilizopo ili kutunza mazingira.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Kanuni ya Kupiga Marufuku Matumizi ya Mifuko ya Plastiki, Baraza limeendelea

kudhibiti matumizi ya mifuko hiyo, ambapo hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya tani 60 zimekamatwa na kati ya hizo tani 40 zimeteketezwa na tani 20 zilizobaki zinasubiri taratibu za kuteketezwa.



***Watumishi kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Ziwa Victoria Mashariki kwa kushirikiana na Mamlaka za Ulinzi na Usalama wakiwa wamekusanya mifuko ya plastiki iliyokamatwa na kuhifadhiwa katika vituo mbalimbali vya polisi baada ya kesi zake kukamilika kisheria, zoezi lililofanyika kuanzia Februari 13, 2026.***

**ii) Kushughulikia Malalamiko ya Umma Kuhusu Uchafuzi na Uharibifu wa Mazingira**

138. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2025/26, Baraza limeshughulikia malalamiko ya wananchi kuhusu uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake. Hadi Machi, 2026, Baraza limepokea jumla ya malalamiko 179 kuhusu masuala mbalimbali ya kimazingira, ikiwemo kelele zilizozidi viwango vilivyowekwa. Kati ya hayo, malalamiko 162 sawa na asilimia 91 yalishughulikiwa ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu kwa walalamikiwa waliotenda makosa kwa mujibu wa sheria na kanuni za uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

**b) Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Ukaguzi wa Mazingira**

**i) Miradi Iliyosajiliwa**

139. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kusimamia usajili wa miradi ya maendeleo kwa ajili ya kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Ukaguzi wa Mazingira ambapo jumla ya Miradi 1,471 ilisajiliwa. Kati ya hiyo, miradi 1,180 ilisajiliwa kwa ajili ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na miradi 291 kwa ajili ya Ukaguzi wa Mazingira. Kwa kipindi hicho, jumla ya miradi ipatayo 1,030 imeidhinishwa kupata vyeti ambapo miradi 903 ni ya tathmini ya athari kwa mazingira na 127 ni miradi ya ukaguzi wa mazingira.

**c) Usajili na Uratibu wa Utendaji Kazi wa Wataalam Elekezi wa Mazingira**

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Baraza limesajili na kutoa vyeti vya utendaji kazi kwa wataalam elekezi wa mazingira. Hadi Machi, 2026, Baraza limepokea na kuchakata jumla ya maombi 453 ya usajili, vyeti vya utendaji kazi wa wataalam elekezi wa mazingira pamoja na uhuishaji wa vyeti vya utendaji kazi wa wataalam elekezi wa mazingira (Usajili 147, Utendaji 120 na uhuishaji 186). Kati ya maombi hayo, jumla ya wataalam elekezi wa mazingira 51 walioomba usajili waliidhinishwa na Bodi na orodha kuwasilishwa kwenye mamlaka husika. Vilevile, Baraza lilitoa vyeti 193 vya usajili na utendaji kazi wa wataalam elekezi wa mazingira.

**d) Utekelezaji wa Ajenda ya Taifa ya Tafiti za Mazingira (Tafiti na Tathmini)**

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti wa Mazingira (NERA) yenye lengo la kutoa mwelekeo wa kitaifa kwa wadau wa kufanya tafiti za mazingira ili kuwawezesha kuandaa programu, miradi na shughuli mbalimbali za kitafiti kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele ya Kitaifa yaliyomo kwenye ajenda na Dira ya Taifa ya Maendeleo, DIRA 2050.

**142. *Mheshimiwa Spika,*** warsha kwa ajili ya kupitia rasimu ya NERA ya mwaka 2026–2036 ilifanyika Mkoani Morogoro kuanzia tarehe 29 hadi 30, Januari, 2026 ikijumuisha Kamati ya Taifa ya tafiti za Mazingira. Aidha, NERA imeidhinishwa na Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Kupitia Ajenda hii, Baraza linaratibu utekelezaji wa tafiti na miradi ya mazingira kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele sambamba na masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira yaliyoainishwa kwenye DIRA 2050.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** Ajenda iliyoandaliwa imezingatia jukumu la tafiti za mazingira na tathmini ya mifumo ikolojia. Maeneo ya kipaumbele ya tafiti ni pamoja na: Usimamizi wa taka na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira; Uhifadhi na Usimamizi Jumuishi wa rasilimali za maji; Usimamzi wa matumizi ya ardhi; Uhifadhi wa Bioanuai; Uhimilivu na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; Usimamizi wa masuala ya kijenetiki; na Matumizi ya teknolojia katika usimamizi wa mazingira na maendeleo ya uchumi na mazingira.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha uwezo wa nchi wa utafutaji wa rasilimali fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya hifadhi ya mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Baraza limefanya jitihada za kuhuisha Ithibati ili kuwezesha kupata fedha kupitia Mfuko wa kuhimili athari za Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Fund). Katika hatua hii, napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Baraza limefanikiwa kukamilisha hatua hii na hivyo kukidhi vigezo vya kupokea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na athari za maporomoko ya ardhi ambazo zimekuwa zikijitokeza katika maeneo mbalimbali hapa nchini kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, Baraza limefanya jitihada ya kuainisha maeneo yenye changamoto hususan katika maeneo ya milima na kufanya tathmini ya mifumo ikolojia ili kubaini njia sahihi ya kukabiliana na changamoto hizo. Hadi kufikia Machi, 2026 Baraza limefanya tathmini kwenye milima ya Kawetere na Livingstone (Mbeya), milima ya Mambamiamba (Kilimanjaro) na safu za milima ya Chinyami (Dodoma). Aidha, tathmini hizo zitatumika kuandaa mipango ya usimamizi wa

mazingira kwenye maeneo hayo. Vilevile, uandaaji wa Mpango jumuishi wa usimamizi wa mazingira wa mlima Kawetere umekamilika.

**e) Uandaaji Maandiko Dhana na Mapendekezo ya Miradi**

146. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kuandaa maandiko mbalimbali ya miradi kwa ajili ya kutafuta fedha za kusaidia shughuli za kuhifadhi mazingira. Hadi kufikia Machi, 2026, Baraza limeandaa maandiko saba (7) ikijumuisha maandiko kamili ya miradi minne (4) pamoja na maandiko dhana matatu (3). Maandiko hayo yamejikita zaidi katika eneo la Mabadiliko ya tabianchi.

f) **Kuandaa Nyenzo na Miongozo ya Mazingira**

147. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeandaa Mwongozo unaosaidia katika ukusanyaji wa taarifa za taka zinazozalishwa viwandani. Mwongozo huu ni mahsusi katika kusaidia utambuzi, ukusanyaji wa takwimu, uainishaji na uwasilishaji wa taarifa za taka za viwandani.

g) **Uratibu na Matokeo ya Miradi inayotekelezwa na Baraza**

148. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kuratibu miradi mbalimbali ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira ikiwemo mradi wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki kwa Wachimbaji Wadogo wa Madini ya Dhahabu ambapo shughuli zifuatazo zimefanyika:- Ujenzi wa kituo cha teknolojia mbadala wa zebaki, Kata ya Msalala Wilaya ya Kahama Shinyanga; Ujenzi wa mialo 8 ya mfano ya uchenjuaji salama kwa kutumia zebaki katika mikoa ya Geita, Mwanza, Singida, Shinyanga na Mbeya; na ujenzi wa kituo cha elimu kuhusu zebaki katika Mkoa wa Geita. Ujenzi huu wa kituo cha elimu umekamilika kwa asilimia 90. Vilevile, mradi huu umesaidia kuimarisha maabara za taasisi nne (4) ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Tume ya Madini; na Taasisi ya Jiolojia na

Tafiti za Madini nchini. Pamoja na matokeo hayo, mradi huu umetoa elimu ya matumizi salama ya zebaki, athari zake katika afya ya jamii na teknolojia mbadala kwa zaidi asilimia 30 ya wachimbaji wadogo nchini.

149. ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limetekeleza mradi wa kujenga uwezo wa Taifa wa kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, EMA, kwa kununua gari lenye vifaa vya maabara *(Mobile Laboratory)*. Gari hili lina vifaa vya kusaidia kuchukua sampuli na kufanya vipimo vya ubora wa hewa na maji katika maeneo husika. Vilevile, Baraza linasimamia utekelezaji wa miradi minne (4) ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambapo miradi hii inatekelezwa na wadau mbalimbali nchini. Lengo la miradi hiyo ni kuongoa mifumo ya ikolojia na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika mikoa ya Kaskazini Unguja (Kaskazini B), Pemba Kaskazini (Wete), Dodoma (Kongwa na Bahi); Singida (Manyoni); Tabora (Nzega na Igunga); na Mara (Bunda).




***Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Semesi (katikati mwenye miwani) akipokea mfano wa ufunguo kama ishara ya makabidhiano ya maabara inayotembea iliyofadhiliwa na Serikali ya Sweden katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam Februari 19, 2026.***

### h) Elimu kwa Umma

150. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26, Baraza limefanikiwa kuendesha programu 78 za mazingira kupitia redio jamii na taifa, programu 52 za runinga, makala maalumu tatu (3) za

televisheni, habari 151 za runinga, habari 109 za redio na taarifa 563 zilisambazwa katika mitandao mbalimbali ya kijamii. Aidha, habari 278 zilichapishwa kwenye magazeti, vipeperushi 384 vya kielektroniki vyenye jumbe za mazingira vimeandaliwa na kuhuishwa kwenye mitandao ya kijamii ya NEMC, picha mjongeo 26 na mikutano sita (6) ya waandishi wa habari.



***Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dkt. Immaculate Semesi akifafanua jambo wakati wa kikao cha uwasilishwaji wa Taarifa ya Bajeti kwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, jijini Dodoma Machi 23, 2026.***

### 6) KITUO CHA TAIFA CHA KURATIBU KABONI

151. ***Mheshimiwa Spika***, Kituo cha Kitaifa cha Kuratibu Kaboni, kimeanzishwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 iliyofanyiwa marekebisho kupitia Sheria Namba Na. 5 ya Mwaka 2025 na kupewa Majukumu ya: Kuratibu masuala yanayohusiana na gesijoto na Biashara ya Kaboni; Kuwa Msajili wa miradi ya kaboni; Kuweka Mfumo wa Ufuatiliaji, Utoaji wa Taarifa na Uthibitishaji wa Gesijoto; Kutoa Mafunzo na uhamasishaji kwa wadau, Kufuatilia utekelezaji wa Kanuni za Biashara ya Kaboni; na Kuweka Mipango ya kukuza uwekezaji na ushirikiano wa kimataifa katika Biashara ya Kaboni nchini.



***Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Ofisi ya Makamu wa Rais, Balozi Baraka Luvanda (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Afisa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji Kaboni (NCMC), Bi. Kathryn Kigaraba pamoja na Watendaji wa Kituo hicho wakati wa ziara ya kikazi kituoni hapo mkoani Morogoro Machi 04, 2026.***

152. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni, kimeendelea kuratibu na kuimarisha usimamizi wa Biashara ya Kaboni nchini ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Muundo na Majukumu ya Kituo sambamba na Uratibu wa Biashara ya Kaboni yalifanyika tarehe 19 Januari, 2026 katika ukumbi wa Bunge Dodoma; Kuwajengea uwezo wa kufanya biashara ya Kaboni taasisi na wadau mbalimbali ikiwemo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Aidha, elimu kwa umma kuhusu biashara ya kaboni imeendelea kutolewa kupitia njia mbalimbali ikiwemo mitandao ya kijamii.

153. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Kituo kilitekeleza shughuli zifuatazo: Usajili wa miradi 22 ya Biashara ya Kaboni ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na hivyo idadi ya miradi iliyosajiliwa kufikia 99. Miradi hiyo imegawanyika katika sekta mbalimbali, ambapo

asilimia 49.5 ipo katika sekta ya Misitu, asilimia 40.4 katika sekta ya Nishati, asilimia 3 katika sekta ya Kilimo, asilimia 2 katika sekta ya udhibiti wa taka, na asilimia 1 sekta nyingine.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2026 halmashauri 24 kati ya 184 zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa biashara ya kaboni. Halmashauri nne (4) za Tanganyika, Kiteto, Karatu na Mbulu zinapokea fedha kwa ajili ya utekelezaji miradi ya maendeleo; Halmashauri sita (7) za Bukoba, Misenyi, Muleba, Ngara, Karagwe,kyerwa na Biharamulo fedha za biashara ya kaboni hutolewa kwa wananchi moja kwa moja ambapo wananchi 16,908 wananufaika; na halmashauri 13 za Mpwapwa, Kilosa, Liwale, Gairo, Kongwa, Tunduru, Mvomero, Morogoro, Longido, Monduli, Namtumbo, Kilolo na Monduli ziko kwenye hatua mbalimbali kwa kufanya tathimini na kuandaa maandiko ili kuendelea na biashara ya kaboni kwa mwaka 2026/27.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa wito kwa Halmashauri zote nchini kukitumia Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni kwa ajili ya ushauri, uratibu na usimamizi wa miradi ya kaboni ili kuhakikisha miradi hiyo inazingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa, inaleta manufaa halisi kwa wananchi, na inalinda rasilimali za mazingira kwa uendelevu. Aidha, Halmashauri zinahimizwa kushirikiana kikamilifu na wadau mbalimbali wakiwemo sekta binafsi na jamii za wananchi ili kuongeza wigo wa miradi ya kaboni, kuimarisha uwazi katika mikataba, na kuhakikisha mapato yanayotokana na biashara ya kaboni yanachangia ipasavyo katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa biashara ya kaboni inaendeshwa kwa uwazi na fursa zilizopo zinatumika ipasavyo na kuleta tija na manufaa kwa wananchi, Serikali iliunda Kamati ya Wataalamu iliyopewa majukumu ya kushauri kuhusu mikakati madhubuti ya kuimarisha usimamizi wa biashara ya kaboni; kubaini na kutoa mapendekezo ya kushughulikia changamoto zilizopo au zinazoweza kujitokeza katika biashara ya kaboni.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi, ikiwemo kuimarisha mifumo ya kidijitali ya usajili na ufuatiliaji wa miradi, kujenga uwezo kwa wataalam wa halmashauri, na kuhakikisha kuwa biashara ya kaboni inakuwa chachu ya ukuaji wa uchumi wa Taifa, uhifadhi wa mazingira, na ustawi wa wananchi wetu.

158. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na ukweli kuwa Biashara ya Kaboni ni dhana ngeni kwa wananchi, ninaomba nitoe rai kwa umma kutumia ipasavyo Kituo cha Uratibu wa Kaboni nchini ili kupata ushauri wa kitaalamu na miongozo stahiki kuhusu biashara hiyo ikiwa ni pamoja na uandaaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati yenye fursa ya biashara ya Kaboni ambayo siyo tu inachangia ukuaji wa uchumi lakini pia uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



***Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni (NCMC) Bi. Kathryrn Kigaraba akifafanua jambo wakati wa kikao cha uwasilishaji wa taarifa kuhusu muundo na majukumu ya NCMC kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, jijini Dodoma Januari 19, 2025.***

## 7) CHANGAMOTO NA UTATUZI

### a) Changamoto

159. ***Mheshimiwa Spika,*** mbali na mafanikio makubwa yaliyopatika katika mwaka 2025/26, Ofisi ilipitia changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizo ni pamoja na: Uelewa mdogo wa masuala yanayohusu chimbuko, misingi, historia na fursa za Muungano. Hii inatokana na uhalisia kuwa idadi ya watu waliozaliwa baada ya Muungano ni zaidi ya asilimia 75.

160. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa hifadhi na usimamizi wa Mazingira changamoto zilizopo ni pamoja na: Jamii kutozingatia kikamilifu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake; Uelewa mdogo kuhusu umuhimu wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na mabadiliko ya tabianchi na biashara ya kaboni; Uwepo wa mnyororo mrefu wa biashara ya kaboni unaojumuisha madalali wengi na kusababisha kupungua kwa mapato halisi; Utegemezi mkubwa wa rasilimali za mazingira kwa baadhi ya jamii nchini katika kujipatia kipato na kujikimu bila kuzingatia hifadhi ya mazingira.

161. **Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine ni ukosefu wa Mpango wa Matumzi Endelevu ya Maeneo ya Maji (MSP) kunakosababisha kutonufaika vyema na fursa zilizopo katika sekta za Uchumi wa Buluu; na uelewa mdogo wa jamii kuhusu fursa za Uchumi wa Buluu na namna ya kunufaika nazo; na kuongezeka kwa matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za Uchumi wa Buluu kunakosababisha uharibifu wa rasilimali za maji.

### a) Utatuzi wa Changamoto

162. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na Changamoto hizo kwa mwaka 2025/26, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano na fursa zake, uzalendo na mshikamano wa Kitaifa hususan kwa vijana. Hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na: Kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa Mazingira hususan uzingatiaji

wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake pamoja na biashara ya kaboni; na Kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za uhifadhi na usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Vilevile, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira limeendelea kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa miradi inayokiuka taratibu zilizowekwa. Kuanzisha rejesta ya kidijitali na mifumo ya kisasa ya upimaji, utoaji na uthibitishaji wa taarifa ili kuongeza uwazi, ufanisi na kuimarisha nafasi ya nchi katika soko la kaboni kimataifa.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kukamilika kwa utafiti wa awali kuhusu maandalizi ya mpango wa matumizi endelevu wa maeneo ya maji; Kukamilika kwa nyenzo zitakazotumika kuandaa MSP ikiwemo Mwongozo wa Mpango wa Matumizi ya Rasilimali za Maji, Mkakati wa Ushirikishwaji Jamii katika Uandaaji wa MSP; Kuandaa mpango wa kitaifa utakaosaidia katika uandaaji MSP; Kufanyika kwa miradi ya majaribio ya upangaji wa maeneo ya maji katika Halmashauri za Wilaya ya Mkinga (Tanga) na Mkuranga (Pwani); na kutoa elimu kwa jamii kuhusu fursa zilizopo katika sekta za Uchumi wa Buluu.

## D. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27

164. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na bajeti ya Ofisi kwa mwaka 2026/27 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo: DIRA 2050; Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu wa Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31); Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021; Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024; Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025; Mpango Mkakati wa Ofisi (2026/27 - 2030/31); Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2026/27; Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi; na Maagizo ya Viongozi wa Kitaifa.

## E. SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA NA OFISI KWA MWAKA 2026/27

### 1) MASUALA YA MUUNGANO

165. ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2026/27, Ofisi itaendelea kutekeleza jukumu lake la kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano kwa masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuendelea na utekelezaji wa mpango Kabambe wa Elimu kwa umma kuhusu Muungano ambao pia unahusisha maandalizi ya ujenzi wa vituo vya Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano (MAKAVAZI) na Msafara wa Muungano (Muungano Caravan); Kuendeleza tafiti kuhusu uelewa wa Vijana katika masuala ya Muungano Tanzania Bara na Zanzibar; Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo zinazotekelezwa pande mbili za Muungano; Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano ikiwemo kukamilisha utatuzi wa hoja za Muungano na kuhamasisha fursa za Muungano; Kuratibu Vikao vya ushirikiano baina ya Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano za SJMT na SMZ; Kufanya ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Masuala 22 ya Muungano; Kuandaa Maadhimisho ya Miaka 63 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; na Kuzijengea uwezo Kamati za Usimamizi wa Fedha za Mfuko wa Jimbo; Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Zanzibar; na Watendaji wa Halmashauri kuhusu uendeshaji na usimamizi wa fedha za Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.

### 2) HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEVU WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

166. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2026/27, Ofisi imepanga kuratibu na kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuratibu utekelezaji wa Dira ya 2050 katika masuala yanayohusu hifadhi na usimamizi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi ikiwemo utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Kimkakati ya Mazingira Endelevu Tanzania; Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa

ya Mazingira 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; Kuratibu Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032); Kuimarisha uratibu na utekelezaji wa masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira katika Wizara za Kisekta, Taasisi, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau mbalimbali wa mazingira ikiwemo kuimarisha upatikanaji wa taarifa kupitia mifumo ya kielektroniki; Kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira; na Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Hifadhi ya mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka huu Tanzania inatarajiwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 12 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi. Mkutano huo unategemewa kufanyika tarehe 06 - 09 Oktoba, 2026 Jijini Dar es Salaam. Aidha, Mkutano huo unatarajiwa kuleta manufaa katika nyanja mbalimbali ikiwemo kupata fursa za miradi na uwekezaji; kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa; na kutangaza bidhaa mbalimbali za kiasili zinazotengenezwa hapa nchini.

### 3) URATIBU WA SHUGHULI ZA UCHUMI WA BULUU

168. ***Mheshimiwa Spika;*** katika kutekeleza Dira 2050, Ofisi itaendelea kuratibu na kusimamia sekta zenye mnasaba na Uchumi wa Buluu ili kuhakikisha Malengo yaliyokusudiwa na Dira 2050 yanafikiwa kwa kuweka mazingira wezeshi ya Uwekezaji katika sekta ya Uchumi wa Buluu.

169. ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2026/27, Ofisi itaendelea kuimarisha mfumo wa uratibu wa shughuli za Uchumi wa Buluu kwa kuandaa Mwongozo wa uratibu pamoja na kuandaa Mpango Kabambe wa Uwekezaji katika sekta za Uchumi wa Buluu (Blue Economy Investment Masterplan) ili kuwezesha utekelezaji madhubuti wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024 na Mkakati wake wa Utekelezaji. Lengo ni kuhakikisha kuwa sekta ya Uchumi wa Buluu inachangia kikamilifu kwenye Pato la Taifa.

170. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpangokazi wa Maandalizi wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji (2025-2030), Ofisi imejipanga kuanza na Maeneo ya Kitaifa ya maji bahari (Territerial Water) ambapo kwa mwaka 2026/27, Ofisi itaratibu maandalizi ya Mpango kwa kukusanya takwimu na taarifa za msingi, kufanya tathmini ya kiikolojia na kutambua matumizi ya kibinadamu katika maeneo ya maji, pamoja na kuendesha kampeni za elimu kwa umma na uhamasishaji kuhusu mpango huo. Kukamilika kwa mpango huu kunatarajiwa kuongeza mchango wa sekta ya Uchumi wa Buluu katika Pato la Taifa, ikiwemo kukuza uchumi wa Nchi, kuboresha maisha ya jamii, kuhifadhi rasilimali za Uchumi wa Buluu katika kupanua wigo wa ajira na kupunguza migongano ya matumizi ya rasilimali za maji kwa wanufaika.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu masuala ya Uchumi wa Buluu kupitia makongamano ya kitaifa na kimataifa ya wadau wa Uchumi wa Buluu; Kujenga uwezo wa watalaam kuhusu Uchumi wa Buluu; Kuratibu programu za elimu kwa umma kwa wadau mbalimbali ikiwemo Kamati za Bunge, Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa na jamii kwa ujumla.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2026/27, Ofisi itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta za Uchumi wa Buluu kwa kutumia utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kuongeza mitaji, teknolojia, ubunifu na ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati.

## 4) KAZI NYINGINE ZITAKAZOTEKELEZWA NA OFISI

173. ***Mheshimiwa Spika***, kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi kwa mwaka 2026/27 ni pamoja na: Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutekeleza majukumu yake; Kusimamia masuala ya Utawala na Menejimenti ya Rasilimaliwatu; Kuratibu maandalizi ya maandiko na nyaraka mbalimbali za Ofisi; Kuandaa Mpango na Bajeti ya Ofisi na taarifa za utekelezaji wa mipango mbalimbali; Kuelimisha umma kuhusu Majukumu, Sera, Mikakati na Programu zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais; Kutoa

huduma ya ushauri wa masuala ya kisheria; Kufanya kaguzi za fedha zilizopokelewa na matumizi yake; Kusimamia utekelezaji wa mifumo ya manunuzi na kutoa taarifa; Kuandaa taarifa za mapato na matumizi ya Fungu 26 na 31; Kufanya Ufuatiliaji na Tathimini ya utekelezaji wa Sera, Mikakati, Mikataba ya Kimataifa pamoja na Programu zinazohusu Muungano, Mazingira na Uchumi wa Buluu; na Kuandaa, Kusimamia Mifumo na Kutoa Msaada wa Kitaalamu katika masuala ya TEHAMA.

### 5) KURATIBU UTEKELEZAJI WA MIRADI NA SHUGHULI WEZESHI ZA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

#### a) Utekelezaji wa Miradi

174. ***Mheshimiwa Spika**,* Kwa mwaka 2026/27, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kama ifuatavyo:

#### i. Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai

175. ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo kuu la mradi ni kuimarisha usimamizi jumuishi wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibiwa ili kujenga uhimilivu wa mifumo-ikolojia na jamii kwa ujumla nchini Tanzania. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2026/27 ni pamoja na: Kujenga miundombinu ya mifugo ikiwemo majosho, mabirika, na mabanio katika Halmashauri saba (7) zinazotekeleza mradi ambazo ni Mbeya, Iringa, Tanganyika, Mpimbwe, Sumbawanga, Wanging'ombe na Mbarali; Kununua na kufunga mifumo ya gesi ya kupikia katika Halmashauri tano (5) za Wilaya (Mbeya, Iringa, Tanganyika, Mpimbwe na Sumbawanga); Kukamilisha ununuzi na uwekaji wa mitambo ya uchakataji wa mazao kwa ajili ya kuongeza thamani katika viwanda vidogo sita katika Halmashauri za Iringa, Wanging'ombe, Mbarali, Sumbawanga, Mpimbwe, na Tanganyika; na Kuanzisha vitalu saba (7) vyenye jumla ya miche 2,100,000 katika Halmashauri saba (07) za Wilaya (Mbeya, Iringa, Tanganyika, Mpimbwe, Sumbawanga, Wanging'ombe na Mbarali).

### ii. Mradi wa Kujenga Ustahimilivu wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Mkoani Kigoma

176. ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuboresha mifumo ikolojia itakayoongeza ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Kigoma na hivyo kuchangia moja kwa moja kuboresha mazingira katika eneo husika. Katika mwaka 2026/27 shughuli za mradi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: Kuandaa Mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji 20; Kufanya tathmini ya migogoro ya ardhi na kubuni mbinu za kupunguza migogoro hiyo; Kuainisha na kupima maeneo kwa ajili ya kupanda miti; Kujenga miundombinu ya uvunaji maji na kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za umwagiliaji; Kuotesha miti hekari 12,000 kwa njia ya kilimo mseto; Kufanya manunuzi ya vifaa na vitendea kazi vya Ofisi; Kujenga miundombinu ya kudhibiti mafuriko na mmomonyoko wa ardhi katika maeneo yenye idadi kubwa ya watu ili kupunguza athari na kuhifadhi mazingira; Kutekeleza Mipango ya Usimamizi Shirikishi ya Misitu ya Jamii; Kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi na kilimo kinachohifadhi mazingira na ufugaji wa nyuki; Kutoa mafunzo kwa Viongozi wa Vijijiji, Kata na Wilaya kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi; na Kutoa elimu kwa wakulima, Maafisa Ugani wa Wilaya kuhusu kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi.

### iii. Mradi wa kuimarisha jamii na mifumo ikolojia katika kustahimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye Ukanda wa misitu ya Miombo Tanzania Bara na maeneo kame Zanzibar

177. ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kupunguza athari na kuimarisha uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika jamii zinazozunguka maeneo ya misitu ya Miombo Tanzania Bara na maeneo kame Zanzibar. Katika mwaka 2026/27 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: Ununuzi wa vifaa vya kuchakata, kufungasha na kutunza malisho ya mifugo na mbegu katika maeneo ya utekelezaji wa mradi; Kujenga jengo kwa ajili ya kukusanya, kuchakata na kuzalisha mbegu za miti na mazao; Kujenga manzuki kwa ajili ya kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya nyuki; na Kuanzisha vitalu vya miti katika ngazi ya vijiji

upande wa Tanzania Bara; na Kufanya Mapitio ya Mkakati wa Mazao yasiyo ya Mbao Zanzibar.

iv. **Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Babati**

178. ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kurejesha ikolojia ya Ziwa Babati lililoathiriwa kutokana na shughuli za kibinadamu. Katika mwaka 2026/27 shughuli zitakazotekelezwa zinajumuisha:- Kubaini na kuweka mipaka ya kudumu katika ziwa; Kupanda miti ili kuzuia mmomonyoko wa udongo; Kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Matumizi wa rasilimali za Maji; Kubainisha shughuli mbadala za kujikimu kwa jamii zinazozunguka maeneo ya ziwa; na Kutoa mafunzo kuhusu udhibiti wa magugu maji kwa jamii zinazozunguka eneo la ziwa.

v. **Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Chala na Ziwa Jipe**

179. ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuimarisha ikolojia na usimamizi endelevu wa Ziwa Chala na Ziwa Jipe. Katika mwaka 2026/27 shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: Kuhamasisha mbinu za asili zinazotumika kuondoa magugu maji katika Ziwa Chala na Ziwa Jipe; Kufanya mapitio ya sheria ndogo zinazosimamia Ziwa Chala na Jipe; Kubainisha njia mbadala za kujikimu kwa jamii zinazozunguka katika maeneo ya ziwa; na Kukuza uelewa wa jamii kuhusu usimamizi endelevu wa Ziwa.

vi. **Mradi wa Bustani ya Kijani Katika Eneo la Swaswa Mnarani, Dodoma**

180. ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuanzisha eneo lenye mandhari ya kijani na mazingira safi katika eneo oevu la Swaswa Mnarani Jijini Dodoma. Kwa kipindi cha mwaka 2026/27 shughuli zitakazotekelezwa ni:- Kuwezesha uchimbaji wa kisima kimoja; Kuweka miundombinu; na Kuwezesha ujenzi wa jengo la kupumzika na Bwalo la Chakula.

vii. **Program ya kujenga uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (SCALE)**

181. ***Mheshimiwa Spika,*** Program hii inatekelezwa katika Halmashauri 65 (54 Tanzania bara na 11 Zanzibar). Baadhi ya Halmashauri hizo ni pamoja na: Buhigwe, Nsimbo, Chemba, Kilolo, Chake Chake, Mkoani, Kaskazini A, na Kaskazini B. Programu hii inatekelezwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI. Lengo la progamu hii ni kujenga uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kupitia programu hii jamii itahusika moja kwa moja katika kuibua miradi mahsusi inayolenga kutatua changamoto za mazingira na kuongeza uhimilivu dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi zilizojitokeza katika maeneo yao. Kwa kipindi cha mwaka 2026/27 kazi zilizopangwa kutekelezwa zinajumuisha: Ununuzi wa gari moja kwa ajili ya mradi; Kuandaa na kufanya mapitio ya Miongozo na Mikakati mbalimbali ikiwemo Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi; Kujenga uwezo wa jamii kuhusu uibuaji na uandaaji wa miradi ya mabadiliko ya tabianchi; Ukusanyaji wa takwimu za mabadiliko ya tabianchi na uandaaji wa taarifa; Kufanya ufuatiliaji na tathmini katika ngazi ya Serikali za Mitaa zinazotekeleza program; na Kujenga uwezo kwa Halmashauri 54 kuhusu nyenzo za mazingira katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

viii. **Programu ya Mageuzi ya Kimkakati ya Mazingira Endelevu Tanzania**

182. ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi kwa kuongeza uoto wa kijani kupitia upandaji miti na kuboresha usimamizi wa mazingira. Kwa mwaka 2026/27 shughuli zilizopangwa ni kuwezesha wadau mbalimbali na jamii kuotesha na kutunza miti bilioni 2 na kuanzisha hekta 10,000 za sehemu za kijani (green parks).

**b) Utekelezaji wa Shughuli Wezeshi**

**i. Kujenga Uwezo wa Kitaifa wa Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi**

183. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/27 shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa: Kuandaa Taarifa ya awali itakayobainisha wadau, mpangilio wa kitaasisi na mifumo ya kisheria kuhusu mabadiliko ya tabianchi na Warsha ya wadau kwa ajili ya kupitia taarifa hiyo; Kuwezesha mfumo wa kitaifa wa ukusanyaji wa taarifa za mabadiliko ya tabianchi utakaojumuisha moduli za uzalishaji wa gesijoto (GHG Inventory), ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mchango ya Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (NDC) pamoja na taarifa za fedha za mabadiliko ya tabianchi; Kuratibu warsha mbili (2) za mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo wadau mbalimbali kuhusu matumizi ya kutumia mfumo wa kitaifa wa taarifa za mabadiliko ya tabianchi; na Kufanya manunuzi ya vifaa vya Ofisi.

**ii. Kujenga Uwezo wa Kitaasisi Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomomonyoa Tabaka la Ozoni**

184. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Ofisi imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: Kufanya mafunzo kwa mawakala wa forodha 200 na watekelezaji wengine wa sheria; Kufanya mafunzo kwa Mafundi mchundo 250 wa viyoyozi na majokofu kuhusu njia bora za kuhudumia vifaa hivyo bila kuathiri Tabaka la hewa ya Ozoni; Kufanya mafunzo kwa mawakala wa forodha 500 kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa gesi na vifaa vinavyodhibitiwa chini ya Itifaki; Kufanya mafunzo kwa maafisa ugavi na ununuzi 120 kuhusu matakwa ya Itifaki ya Montreal; Kuratibu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni; na Kuandaa nyenzo za uelimishaji umma kuhusu hifadhi ya tabaka la ozoni.

## 6) MIRADI MINGINE ITAKAYOTEKELEZWA

### i. Mradi wa Ujenzi na ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais

185. ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la mradi huu ni kuwezesha shughuli za ujenzi na ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Luthuli I na II Dar es Salaam, na makazi ya Makamu wa Rais Oysterbay Dar es Salaam na Kilimani Dodoma.

### ii. Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano

185. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unalenga kurahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za masuala ya Muungano, kuhifadhi kumbukumbu, na kuongeza uelewa kuhusu Muungano wa Tanzania kwa jamii hususan vijana. Kwa kipindi cha mwaka 2026/27 Ofisi imepanga kuanza shughuli za awali za utekelezaji wa mradi kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar.

## 7) BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

187. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2026/27 Baraza litaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuendelea kuratibu, kusimamia na kushauri utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Mikakati ya mazingira kwa lengo la kudhibiti athari za uharibifu na uchafuzi wa mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; Kuratibu mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira ili kuhakikisha miradi yote ya maendeleo inajumuisha masuala ya mazingira kabla ya kuanza utekelezaji; Kusajili na kusimamia utendaji wa wataalamu elekezi wa mazingira; Kutoa elimu na kuhamasisha jamii na wadau kuhusu umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kuzingatia miongozo ya usimamizi wa mazingira kwa maendeleo endelevu na Kufanya tafiti mbalimbali za mazingira ili kuongeza uelewa wa mifumo ikolojia na kuhifadhi bioanuai.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na: Kufanya tathmini katika mifumo ikolojia ya milima, maeneo oevu, vyanzo vya maji, bahari na pwani, mmomonyoko wa fukwe, hali halisi ya bioanuai, ili kubaini hali ya mazingira, kutambua changamoto zilizopo, na kusaidia uhifadhi na usimamizi endelevu wa rasilimali asilia; Kutoa elimu kwa jamii, wadau na wawekezaji kuhusu umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa maendeleo endelevu; Kudhibiti vyanzo vikuu vya uchafuzi wa mazingira; Kuimarisha usimamizi wa taka hatarishi; Kutekeleza mkakati madhubuti wa kudhibiti kelele na mitetemo inayozidi viwango vilivyowekwa kisheria; Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034); na kuimarisha uwezo wa kitaasisi kwa kuboresha mazingira ya kazi, ikiwemo kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu Njedengwa na Ofisi za Kanda.

8) **KITUO CHA TAIFA CHA KURATIBU KABONI**

189. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni kitaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha uratibu wa biashara ya kaboni nchini pamoja na uanzishaji wa kituo kama ifuatavyo:- Kuanzisha na kusimamia rejesta ya kidigitali ili kuongeza ufanisi wa usajili na ufuatiliaji wa miradi ya Kaboni; Kwenda kujifunza uendeshaji wa rejesta za kidigitali za miradi ya Kaboni kwenye Nchi zinazofanya vizuri; na Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Biashara ya Kaboni kupitia Mikutano, Warsha, Semina na Mafunzo kwa Makundi Maalum, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na: Kuongeza wigo wa usajili wa miradi ya kaboni ili kulinda mazingira na kuongeza kipato kwa jamii na Serikali; Kuratibu ukamilishaji wa miradi iliyosajiliwa ili iweze kufikia malengo yaliyokusudiwa; Kukamilisha mfumo wa Kidigitali wa Upimaji, Utoaji wa Taarifa na Uthibitishaji (Measurement, Reporting and Verfication – MRV) ili kurahisisha na kuweka uwazi katika uendeshaji wa biashara ya kaboni; na Kuimarisha uratibu wa biashara ya kaboni kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli nyingine ni pamoja na Kufanya tafiti na kutoa ushauri kuhusu uanzishaji, usimamizi na uendeshaji wa biashara ya kaboni; Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi mbalimbali ya biashara ya kaboni inayoendelea na kutoa ushauri wa kitaalamu; Kusimamia utekelezaji wa Sheria, kanuni na miongozo zinazosimamia uendeshaji wa biashara ya kaboni nchini; Kusimamia mgawanyo wa mapato yatokanayo na biashara ya kaboni kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na miongozo ya biashara ya Kaboni; Kuhuisha kanuni na miongozo ya biashara ya kaboni ili iweze kuendana na wakati na kuleta tija kwa jamii na taifa kwa ujumla; Kuimarisha usimamizi wa vihatarishi, utawala na udhibiti wa ndani ili kuhakikisha malengo ya taasisi yanafikiwa; Kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato kupitia ubunifu mbalimbali katika biashara ya Kaboni Nchini ikiwemo kuanzisha hisa za kijani na buluu kupitia biashara ya Kaboni; na kuanzisha mchango wa uzalishaji wa kaboni nchini hasa kwenye usafiri wa Maji na Anga kwa vyombo vinavyotoka nje ya Tanzania.

## F. HITIMISHO NA SHUKRANI

192. ***Mheshimiwa Spika***, Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2025/26 yamechangiwa na ushirikiano mzuri kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Sekta binafsi, Taasisi za Fedha nchini, Asasi Zisizo za Kiserikali za ndani na nje ya nchi; na Wadau mbalimbali.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee ninaomba kutoa shukrani kwa wadau wafuatao: Serikali za Norway; Sweden; Denmark; Japan, Uingereza; India; Korea Kusini; na Ufalme wa Saudi Arabia, Oman, na Qatar. Wengine ni pamoja na: Umoja wa Ulaya (EU); Benki ya Dunia (WB); Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF); Mfuko wa Kimataifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (AF); Mfuko wa Kusaidia Nchi zinazoendelea kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (LDCF); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Shirika la Maendeleo la Jumuiya ya Madola (FCDO); Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ); Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO); Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF); Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP); Shirika la Mazingira la

Umoja wa Mataifa (UNEP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Huduma za Miradi (UNOPS); Shirika la Chakula Duniani (WFP); na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO).

194. ***Mheshimiwa Spika,*** wadau wengine ni pamoja na: Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo - IFAD; Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Mitaji ya Maendeleo (UNCDF); Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF); Mfuko wa Utekelezaji wa Mkataba wa Montreal; Mfuko wa Dunia wa Bioanuai (GBFF); The Good Neighbours Global Impact Foundation; Korea Investment Securities; Kamisheni ya Umoja wa Afrika; Sekretarieti za Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusiana na mazingira na mabadiliko ya tabianchi; Wadau wengine ni pamoja na: TNC, TRC, CRDB, NBC, NMB, Azam Marine, TBC, TADB, ZFF, TFF, UpEnergy Tanzania, BRAC Maendeleo Tanzania, Save the Children na CORUS International.

195. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia fursa hii kuwaomba Washirika wa Maendeleo na Wadau wengine kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuimarisha Muungano, hifadhi na usimamizi wa Mazingira na mabadiliko ya tabianchi na Uchumi wa Buluu kwa maendeleo endelevu.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** Baada ya shukrani hizo kwa washirika wa maendeleo, ninaomba sasa nichukue nafasi hii kumshukuru **Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa (Mb.),** Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwa ushirikiano na msaada mkubwa anaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

197. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kumshukuru **Dkt. Richard Stanslaus Muyungi,** Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Ndugu **Abdallah Hassan Mitawi,** Naibu Katibu Mkuu (Muungano), **Balozi Baraka Haran Luvanda,** Naibu Katibu Mkuu (Mazingira), **Mhandisi Mwanasha Rajabu Tumbo,** Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), **Dkt. Albina Andrew Chuwa,** Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni (NCMC), **Dkt. Immaculate Sware Semesi,** Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) **na Bi.**

**Kathryn Kigaraba,** Afisa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni Nchini (NCMC), Menejimenti na Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, NEMC na NCMC kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima kubwa na ya kipekee ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kikwajuni, Zanzibar kwa kunipa heshima ya kuwawakilisha tena hapa Bungeni kwa kipindi cha nne mfululizo. Aidha, ninakishukuru sana Chama Cha Mapinduzi kwa kunipa heshima ya kugombea tena katika Jimbo la Kikwajuni, Zanzibar. Ninawaahidi wananchi wa Kikwajuni na Chama Cha Mapinduzi utumishi wenye ari, bidii, weledi, heshima na utiifu.

199. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwisho lakini sio kwa umuhimu napenda kuishukuru familia yangu pendwa nikianza na Mke Wangu Kipenzi Thania Ali Abdulla na watoto wetu, Riziki Hamad Masauni, Asha Hamad Masauni, Bareek Hamad Masauni na Basit Hamad Masauni kwa upendo wao unaonipa nguvu ya kutekeleza majukumu yangu vyema.

## G. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/27

200. ***Mheshimiwa* Spika,** ninaomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 23,297,959,000.00** kwa ajili ya matumizi ya Fungu 26 (Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais). Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,297,959,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 22,000,000,000.00** ni Matumizi Mengineyo.

201. ***Mheshimiwa Spika***, aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 76,686,837,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Fungu 31. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 38,371,992,000.00** ni Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 4,875,325,000.00** ni Mishahara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, **Shilingi 7,096,050,000.00** ni ruzuku ya mishahara kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na **Shilingi 26,400,617,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 38,314,845,000.00.** Kati ya fedha

hizo, **Shilingi 14,402,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 23,912,845,000.00** ni fedha za nje.

## H. HITIMISHO

202. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha, Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ni www.vpo.go.tz.

203. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na kuungwa mkono. Nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba, na Sheria ili aweze kusoma taarifa ya Kamati. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo. Washa *mic* ili uendelee. Msaidie hapo.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA, NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, ili kwa niaba ya Mwenyekiti na Wajumbe wote niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba, na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, ninaomba taarifa yote ya Kamati iwekwe kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa Mezani kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba, na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira katika Masuala ya Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadiro ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana vijana nchini Tanzania kwa imani yao kwangu kama mwakilishi wao. Pia, ninamshukuru *Comrade* Mohamed Ali Kawaida, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi Taifa kwa usimamizi mzuri wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba pia nifikishe salamu zangu kwa Mwenyekiti wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi Taifa, Mheshimiwa Mama Mary Chatanda kwa malezi yake makubwa na mazuri kwetu sisi wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, kwa kugawanyika katika sehemu kuu tano kama zilivyoainishwa katika ukurasa wa pili wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Kamati kufanya uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 unatokana na masharti ya Kanuni ya 121(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025. Kanuni hiyo inaelekeza utekelezaji wa bajeti ya mwaka unaoishia, na makadirio ya mwaka unaofuata kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati imezingatia masharti hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi huo, Kamati ilipokea, kujadili, na kuchambua jumla ya mafungu mawili ambayo ni

Fungu 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira katika masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, hususan katika masuala ya Muungano na Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais umeangazia maeneo makuu manne ambayo ni: -

(a) Utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(b) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti ya matumizi ya kawaida na bajeti ya maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026;

(c) Ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026; na

(d) Uzingatiaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Makamu wa Rais inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vya mpango wa bajeti mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza vipaumbele hivyo, ofisi hiyo inatekeleza majukumu mbalimbali. Baadhi ya majukumu hayo ni kumwezesha Makamu wa Rais kutekeleza ipasavyo jukumu kuu la Kikatiba la kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kuratibu masuala ya Muungano yapatayo 22 kama yalivyoainishwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi kuhusu utekelezaji wa vipaumbele hivi na kubaini kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano imeendelea kutekeleza vipaumbele hivyo kupitia kazi mbalimbali kwa ufanisi. Kwa mfano, Kamati ilibaini kuwa Wizara

imeendelea kushughulikia hoja mbalimbali za Muungano ambazo wakati mwingine zilibatizwa jina la kero za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa kuwa, katika kero 25 kero 22 zimeshapatiwa majawabu na kubaki na kero tatu tu, ambazo nazo jitihada za kuzipatia majawabu zinaendelea vizuri. Jambo hili ni kubwa kwani linadumisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafanikio hayo, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Waziri wake Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, kwa jitihada kubwa wanazoendelea kuzifanya katika kuboresha Muungano huu ambao ni mojawapo ya tunu za Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Makamu wa Rais katika mafungu yake mawili iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 38.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida yanayojumuisha mishahara ya *OC* pamoja na ya miradi ya maendeleo. Hadi mwezi Februari, 2026, ofisi hiyo kwa ujumla wake ilikuwa imepokea shilingi bilioni 33.3, sawa na 87.4% ya fedha zote zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji wa bajeti hiyo kwa kila kifungu ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, fungu Fungu Na. 26 liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 19.9. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 18.8 ni kwa ajili ya *OC* na shilingi 1.1 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Februari, 2026, Fungu 26 lilipokea jumla ya shilingi 13.4, sawa na 67% ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 12.87 ni kwa ajili ya *OC*, na shilingi 542.42 ni kwa ajili ya mishahara. Kwa ujumla kiwango cha utekelezaji wa bajeti kwa fungu hili kilizingatia matakwa ya kibajeti ya kuoanisha kiasi kilichopokelewa na muda wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo zaidi kuhusu mapokezi ya fedha za bajeti kwa Fungu Na. 26 yanapatikana katika ukurasa wa saba hadi nane wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu Na. 31 liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 18.16, ambapo shilingi bilioni 16.46 ni za matumizi ya kawaida, ikijumuisha shilingi bilioni 3.1 ya mishahara, na shilingi bilioni 13.34 za OC. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ziliidhinishiwa shilingi bilioni 1.7. Hadi kufikia Februari, 2026, Fungu 31, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano ilipokea jumla ya shilingi bilioni 19.89.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10.97 sawa na 66.7% ya lengo ni za matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 2.2 ni mishahara na OC ni shilingi bilioni 8.7. Kwa upande wa fedha za maendeleo zilizopokelewa ni shilingi bilioni 8.9 sawa na 524% ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa kupokelewa fedha za maendeleo kwa kiasi kikubwa zaidi kulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo kupokea nyongeza ya fedha kwa ajili ya utaratibu wa shughuli za Uchumi wa Buluu, kufuatiwa kuanzishwa kwa kitengo hicho baada ya kuanza utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kuwa kupokelewa kwa fedha za maendeleo zaidi kulizingatia ushauri wa Kamati uliotolewa mwezi Aprili, 2025 wakati Kamati ilipowasilisha maoni yake kuhusu utekelezaji wa bajeti ya ofisi hii ya mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imezingatia na kutekeleza ushauri uliotolewa na Kamati kwa wakati, Kamati inatoa pongezi kwa jitihada hizo na kusisitiza kuwa uzingatiaji wa ushauri unaotolewa na Kamati katika kipindi cha muda mfupi liwe ni jambo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha ukaguzi wa miradi, Kamati ilitembelea na kukagua mradi mmoja unaotekelezwa na ofisi hii. Mradi huu unahusu ujenzi wa jengo la ghorofa sita ya Ofisi ya Makamu wa Rais, unaotekelezwa katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa ofisi hiyo ulianza tarehe 10 Novemba, 2021 na ulitakiwa kukamilika tarehe 9 Novemba, 2023. Hata hivyo, mradi haukukamilika katika muda huo na hivyo kuongezewa muda hadi tarehe 30 Machi, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wakati Kamati ilipotembelea mradi huu tarehe 18 Machi, 2026 kukiwa zimebaki siku 12 tu kumalizika kwa muda wa nyongeza, utekelezaji wake ulikuwa umefikia 94.5%. Kwa ujumla mradi huo unagharimu shilingi bilioni 24.38. Katika kiasi hicho, shilingi bilioni 22.64 ni kwa ajili ya mkandarasi wa ujenzi SUMA JKT, shilingi milioni 934.69 ni kwa ajili ya msimamizi wa mradi Shirika la Nyumba *(NHC)* na shilingi milioni 811.54 ni kwa ajili ya usanifu wa ujenzi uliotekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 18 Machi, 2026 jumla ya shilingi bilioni 22.99 zilikuwa zimeshatolewa na Serikali na kulipwa kwa wakandarasi wanaotekeleza mradi huu. Katika kiasi hicho, kampuni ya ujenzi SUMA JKT ilikuwa imeshalipwa shilingi bilioni 21.52 sawa na 95% ya gharama ya mkataba. *NHC* ilikuwa imeshalipwa shilingi milioni 664.65 sawa na 71% ya gharama za mkataba na *TBA* ilikuwa imeshalipwa shilingi milioni 811.54 sawa na 100% ya gharama za mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokagua mradi huu ilielezwa kuwa ujenzi wake ulikuwa umefikia 94.5%, licha ya asilimia hiyo ukaguzi wa Kamati ulibaini kuwa kazi nyingi zilikuwa hazijakamilika kwa 100%, jambo lililoashiria kuwa bado kuna kazi kubwa ya kumaliza kazi hizo ili jengo hilo lianze kutumika. Hivyo basi, Kamati ilipata mashaka kuhusu ujenzi wa jengo hilo kukamilika katika muda wa siku 12 zilizokuwa zimebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuhusu mradi kutokukamilika ilipofika Novemba, 2023 hadi kupelekea kuongezewa muda wa nyongeza wa zaidi ya miaka miwili, yaani hadi tarehe 30 Machi, 2026 Kamati ilijulishwa kuwa jambo hilo lilisababishwa na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ucheleweshwaji wa malipo ya mkandarasi, kuchelewa kwa baadhi ya vifaa vya ujenzi vilivyoagizwa nje ya nchi na kusuasua kwa mkandarasi SUMA JKT kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua changamoto hiyo, Kamati ilielezwa kuwa hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwemo mkandarasi SUMA JKT kubadili timu ya awali iliyokuwa inatekeleza mradi huo, timu ya kutoka kanda ya kaskazini na kuleta timu mpya ambayo ni timu ya kutoka kanda ya kusini, ambayo ilielezwa kuwa imekuwa ikifanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa licha ya jitihada hizo, miradi ya majengo ya ofisi inayotekelezwa na mkandarasi SUMA JKT ikiwemo majengo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria yanayojengwa Mwanza na Mji wa Serikali Mtumba Dodoma hayajakamilika licha ya muda wa utekelezaji kufika mwisho, hata baada ya muda kuongezwa na mkandarasi kulipwa fedha kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hali ni tofauti kwa miradi kama hivyo inayotekelezwa na mashirika mengine, hususan miradi ya ujenzi wa majengo ya ofisi katika Mji wa Serikali Mtumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kuwa ujenzi wa baadhi ya miradi hiyo iliyotolewa kwa SUMA JKT ikiaminika kuwa Shirika hilo litakamilisha miradi hiyo kwa wakati, hali ambayo imekuwa tofauti kutokukamilika kwa jengo hilo kwa wakati kumesababisha watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kusongamana katika ofisi ndogo ikiwemo kutumia majengo ya kupanga kama ofisi ya kumbi za mikutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuchelewa huko kumepelekea ofisi hiyo kutumia jumla ya shilingi milioni 62.5 kwa mwaka kwa ajili ya pango la ofisi na mikutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutokuendelea kuchelewa kwa mradi na kusababisha Serikali kupata hasara kwa siku za usoni, kutokana na baadhi ya miradi iliyotekelezwa na SUMA JKT kuchelewa kukamilika kadri ilivyopangwa. Ni mtazamo wa Kamati kuwa SUMA JKT ijengewe uwezo ili iweze kukamilisha miradi yote inayokabidhiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uwezeshaji huo uendane sambamba na kutatua changamoto zinazokwamisha ukamilishaji wa miradi inayokabidhiwa kwa kampuni hiyo licha ya washitiri kulipa kwa wakati fedha za kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Ofisi ya Makamu wa Rais katika mafungu yake mawili; Fungu 31 na Fungu 26 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 50.465 kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kiasi hicho ni zaidi ya kiasi cha shilingi bilioni 12, sawa na ongezeko la 32.43% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 ambayo ilikuwa shilingi bilioni 38.1. Ofisi hii kwa mwaka ujao wa fedha inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 23.3 Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambayo ni mishahara na *OC*. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.3 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 22 ni kwa ajili ya fedha za *OC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa fungu 26 bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 imeongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 3.5 sawa na ongezeko la 16.8% dhidi ya bajeti ya mwaka unaoisha. Katika ongezeko hilo, mishahara imeongezeka kwa kiasi cha shilingi milioni 231 sawa na 21.6% na bajeti ya *OC* imeongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 3.1 sawa na 16.5% ya ongezeko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na. 31, Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027 katika masuala ya Muungano inaomba kuidhinishiwa jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 27.167 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 23.46 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo ndani yake kuna fedha za mishahara shilingi bilioni 3.7 na fedha za *OC* ni shilingi bilioni 19.69. Aidha, kiasi kinachoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 3.7 ambazo zote ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa fungu 31, Bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 katika masuala ya Muungano imeongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni tisa sawa na ongezeko la 49.6% dhidi ya bajeti ya mwaka unaoisha. Katika ongezeko hilo mishahara imeongezeka kwa kiasi cha shilingi milioni 656 sawa na 21% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka unaoisha, wakati bajeti ya fedha za OC imeongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 6.35 sawa na 47.6%. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa shilingi bilioni mbili, sawa na 117.6%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada za kutenga fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa 100%. Maelezo zaidi kuhusu Makadirio ya bajeti ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yanapatikana katika ukurasa wa 16 hadi 20 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kusaidia Serikali katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshamlipa mkandarasi anayejenga Ofisi ya Makamu wa Rais katika Mji wa Serikali Mtumba kiasi cha fedha sawa na 95% ya fedha zote kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi huo. Wakandarasi wengine wanaotekeleza miradi kama hiyo katika eneo hilo wameshakamilisha na kukabidhi kazi hizo licha ya wakandarasi wote kuanza ujenzi wa majengo hayo yanayofanana kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais linalojengwa na kampuni ya SUMA JKT, bado halijakamilika na kutokamilika huko kunasababisha Serikali hasara na kuathiri utendaji wa watumishi wa ofisi hizo. Ili kuhakikisha mkandarasi huyu anatekeleza wajibu wake ipasavyo, Serikali ianze kumtoza fedha za kuchelewesha mradi huo kwa kuzingatia makubaliano yao ya mkataba wa ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi, idadi kubwa ya wananachi wa Tanzania wamezaliwa baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, uliofanyika mwaka 1964.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Muungano huo una manufaa mengi na ni moja ya tunu ya Taifa, Kamati inashauri kwamba ili kuendelea kukuza uzalendo wa nchi yetu ikiwemo kulinda, kuheshimu, kupenda na kuenzi Muungano huo, Serikali ihakikishe inaanza ujenzi wa vituo vya kumbukumbu na nyaraka za Muungano katika Mji wa Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar kama ilivyopangwa ili watu waweze kufika kwenye vituo hivyo kwa ajili ya kujifunza historia ya Muungano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za bajeti zinazotengwa kila mwaka katika Ofisi ya Makamu wa Rais, zimeendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili Muungano wetu. Aidha, utatuzi huo umekuwa na mafanikio makubwa ambapo kero 22 kati ya kero 25 zimepatiwa ufumbuzi na hivyo kubaki na kero tatu tu. Kamati inashauri kwamba, Muungano wetu ufikie kiwango cha kuwa ni jambo la fursa pekee badala ya kuongelea habari za kero. Serikali ihakikishe inazipatia ufumbuzi kero tatu za Muungano zilizobaki na kuzuia kuzaliwa kwa kero nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja wapo ya maeneo mapya ya kiuchumi yanayochipukia nchini ni Uchumi wa Buluu. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano ilianzisha kitengo cha Uchumi wa Buluu ili kuweza kuratibu na kuwawezesha wananchi wanaohitaji kujishughulisha na Uchumi wa Buluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha wananchi wa pande zote za Muungano wananufaika na uanzishwaji wa kitengo hicho, ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali iendelee kukiwezesha kitengo hicho kifedha na rasilimali nyinginezo ili kiweze kuwasaidia wananchi wa pande zote za Muungano katika kupenda na kuwekeza kwenye Uchumi wa Buluu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo anaulinda Muungano kwa vitendo na kuendelea kutatua changamoto zote za Muungano wetu. Pia, tunampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa usimamizi makini wa hoja za Muungano na Mazingira nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati pamoja na kuwasilisha vizuri Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa ushirikiano aliokuwa anaipatia Kamati na kwa niaba ya Kamati. Ninamtakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yake mapya ya Naibu Waziri TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kumpongeza na kumkaribisha Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Kamati inamkaribisha na inamtakia kila la heri katika kazi zake za kumsaidia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia wakiongozwa na Katibu Mkuu wa ofisi hiyo Dkt. Richard Stanslaus

Muyungi, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Abdallah Hassan Mitawi na Naibu Katibu Mkuu Mazingira, Balozi Baraka Haran Luvanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu, likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya **Kanuni ya 121 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, natumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja

na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya **Kanuni ya 145** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 kwa kugawanyika katika Sehemu kuu Tano kama ifuatavyo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, misingi na muundo wa taarifa hii;
(b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuangazia mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;
(c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi katika masuala ya Muungano kwa mwaka wa fedha 2026/2027;
(d) Sehemu ya Nne inahusu Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; na
(e) Sehemu ya Tano ni hitimisho ikijumuisha shukrani.

### 1.3 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika, Uchambuzi na Maoni ya Kamati kuhusu** Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira ya mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa fedha 2026/2027 unatokana na masharti ya **Kanuni ya 121(4)** ikisomwa kwa pamoja na **vifungu 6(2)(c) na 7 (1)(a)** vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni na vifungu hivyo vimeweka masharti yanayoelekeza Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii katika masuala ya Muungano kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

## 1.4 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua jumla ya mafungu mawili (2) ambayo ni:-

(a) **Fungu 26** - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais; na
(b) **Fungu 31** - Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira katika masuala ya Muungano.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0. UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA UZINGATIAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

## 2.1 Vipengele vya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** katika vikao vya Kamati vilivyoketi tarehe 9 na 26 ya mwezi Machi, 2026, Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Taarifa za Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira (katika masuala yanayohusu Muungano na Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais) kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hizo ziliwasilishwa na **Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni (Mb),** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). Uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa hizo umeangazia maeneo makuu manne (4) ambayo ni: -

(a) Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Utekelezaji wa vipaumbele hivyo;
(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026;
(c) Ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026; na
(d) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kupitia Taarifa ya Kamati wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### 2.1.2 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Utekelezaji wa vipaumbele hivyo

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Makamu wa Rais inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Bajeti ulioidhinishwa mwaka 2025/2026. Katika kutekeleza vipaumbele hivyo, Ofisi hiyo inatekeleza majukumu mbalimbali. Baadhi ya majukumu hayo ni kumwezesha Makamu wa Rais kutekeleza ipasavyo jukumu kuu la kikatiba la kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuratibu masuala ya Muungano yapatayo ishirini na mbili (22) kama yalivyoainishwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kuimarisha ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa vipaumbele hivi. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa kupitia kazi mbalimbali, Wizara imeendelea kutekeleza vipaumbele hivyo kwa ufanisi. Kwa mfano, Kamati ilibaini kuwa Wizara imeendelea kushughulikia na kutatua masuala mbalimbali ambayo awali yalikuwa yanahesabiwa kuwa ni kero kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, na kupelekea idadi ya hoja hizo kupungua kwa kiasi kikubwa. Kutokana na mafanikio hayo, **Kamati kwa dhati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Waziri wake Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni (Mb),** kwa jitihada kubwa wanazoendelea kuzifanya katika kuboresha muungano huu ambao ni mojawapo ya tunu za Taifa.

### 2.1.3 Upatikanaji wa Fedha za Bajeti kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Makamu wa Rais katika mafungu yake mawili ili idhinishiwa jumla ya shilingi **38,106,589,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi mwezi Februari, 2026, Ofisi hiyo kwa ujumla

wake ilikuwa imepokea shilingi **33,310,479,792.77** sawa na **asilimia 87.41** ya fedha zote zilizoidhinishwa.

Katika kushughulikia bajeti ya Ofisi hii, Kamati imeangazia mapokezi ya fedha hizo fungu kwa fungu katika vipengele vya matumizi ya kawaida ambayo inajumuisha mishahara (PE) na matumizi mengineyo (OC), pamoja na fedha kwa ajili ya maendeleo. Tathmini ya utekelezaji wa bajeti hadi februari, 2026 kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo: -

### 2.1.4 Fungu Na. 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais

**Mheshimiwa Spika**; Katika mwaka wa fedha 2025/26
Fungu 26 liliidhinishiwa jumla ya Shilingi **19,946,399,000.00** Kati ya fedha hizo, Shilingi **18,879,500,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi **1,066,899,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE).

**Mheshimiwa Spika**; Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026, Fungu 26 limepokea jumla ya kiasi cha shilingi **13,417,088,666.64** sawa na asilimia **67** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi **12,874,666,666.64** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), na shilingi **542,422,000.00** ni kwa ajili ya mishahara. Hali ya mapokezi ya fedha hadi Februari, 2026 inaoneshwa katika **Jedwali Na. 1** kama ifuatavyo: -

**Jedwali Na. 1: Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 kwa Fungu 26**

| MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | FEDHA ZILIZOPOKELEWA | % YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| OC | 18,879,500,000.00 | 12,874,666,666.64 | 68 |
| MISHAHARA | 1,066,899,000.00 | 542,422,000.00 | 51 |
| **JUMLA** | **19,946,399,000.00** | **13,417,088,666** | **67** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa, hadi kufikia Februari 2026 Fungu 26 limepokea jumla ya shilingi **13,417,088,666.64** sawa na **asilimia 67** ya bajeti. Hali hiyo inaonesha kuwa, mapokezi ya fedha kwa Fungu 26 yalizingatia matakwa ya kibajeti kwa, kwani kiwango kinachotakiwa kupokelewa hadi wakati huo ni **asilimia 66.7**.

### 2.1.5 Fungu Na. 31 - Ofisi Makamu wa Rais- Muungano

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Fungu 31 liliidhinishiwa jumla ya Shilingi **18,160,190,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 16,460,190,000.00** ni za Matumizi ya Kawaida, ambapo **Shilingi 3,115,273,000.00** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na **Shilingi 13,344,917,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo iliidhinishwa **Shilingi 1,700,000,000.00**.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu mapokezi ya fedha tathmini inaonesha kuwa, hadi kufikia Februari, 2026 Fungu 31-Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ilipokea jumla ya shilingi **19,893,391,126.13**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **10,973,271,518.00** ni matumizi ya kawaida, sawa na **asilimia 66.7** ya lengo. Katika fedha za kawaida zilizopokolewa, zinajumuisha mishahara shilingi **2,226,718,600.00** na fedha za matumizi mengineyo shilingi **8,746,552,918.00**. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, zilipokelewa Shilingi **8,920,119,608.13,** sawa na **asilimia 524.7** ya lengo. **Jedwali Na. 2** linaonesha ufafanuzi huo kama ifuatavyo: -

Jedwali Na.2: **Upatikanaji wa Fedha hadi Februari, 2026 kwa Fungu 31**

| Eneo | Kiasi Kilichoidhinishwa | Kiasi kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Mishahara (PE) | 3,115,273,000 | 2,226,718,600 | 71.47 |
| Matumizi mengineyo-OC | 13,344,917,000 | 8,746,552,918 | 65.54 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jumla Ndogo | 16,460,190,000 | 10,973,271,518 | 66.67 |
| Maendeleo | 1,700,000,000 | 8,920,119,608.13 | 524.71 |
| **Jumla Kuu** | **18,160,190,000** | **19,893,391,126.13** | **109.54** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muuungano na Mazingira na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha katika Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni wa kutosheleza. Kwa mfano, fedha za maendeleo zilipokelewa kiasi sawa na asilimia **524** ya lengo tarajiwa. Kamati ilielezwa kuwa, kupokelewa kwa kiasi kikubwa zaidi kulitokana na kupokelewa fedha za ziada shilingi **5,720,119,608.13** kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa Ofisi pamoja na Makazi ya Makamu wa Rais yaliyopo Dodoma na Dar es Salaam. Aidha, shilingi **1,500,000,000.00** zilipokelewa kwa ajili ya uratibu wa shughuli za uchumi wa buluu kufuatia Serikali kuanzisha kitengo hicho, ambacho awali hakikuwepo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kupokelewa kwa fedha za maendeleo kwa asilimia 524 kulizingatia misingi ya kibajeti na ushauri wa Kamati uliotolewa mwezi Aprili, 2025 wakati Kamati ilipowasilisha Maoni yake kuhusu Utekelezaji wa bajeti ya Ofisi hii ya Mwaka 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka
2025/2026.

Kamati katika taarifa yake, ilitoa ushauri kwamba Serikali ihakikishe fedha za maendeleo zilizotengwa zinatolewa kikamilifu ili kukamilisha utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa, ikiwemo kukamilisha kwa wataki mradi wa ukarabati wa Ofisi za Makamu wa Rais, ili ofisi hizo ziendane na hadhi ya Ofisi hiyo. **Kwa kuwa Serikali imezingatia na kutekeleza ushauri uliotolewa na Kamati kwa wakati, Kamati inatoa pongezi kwa jitihada hizo na kusisitiza kuwa uzingatiaji wa ushauri unaotolewa kwa wakati uwe suala endelevu.**

## 2.2 Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 18 Machi, 2026, Kamati ilitembelea na kukagua mradi mmoja unaotekelezwa na Ofisi hii. Mradi huo unahusu Ujenzi wa Jengo la ghorofa sita la Ofisi ya Makamu wa Rais unaotekelezwa katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma (**ambao ni Mradi Namba 6309**).

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa Ofisi hiyo ulianza tarehe 10 Novemba, 2021 ukilenga kukamilika tarehe 9 Novemba, 2023. Hata hivyo, mradi haukukamilika katika muda huo, na hivyo kuongezewa muda hadi tarehe 30 Machi, 2026. Aidha, wakati Kamati ilipotembelea mradi huu tarehe 18 Machi, 2026, ilielezwa kuwa utekelezaji wa mradi wake ulikuwa umefikia **asilimia 94.5**.

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa mradi huo unagharimu jumla ya shilingi **24,382,055,160.06**. Katika kiasi hicho, shilingi **22,635,818,859.42** ni kwaajili ya mkandarasi wa ujenzi-SUMA JKT, shilingi **934,693,333.3** ni kwa ajili ya msimamizi wa mradi-Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na Shilingi **811,542,967.34** ni kwa ajili ya usanifu wa ujenzi uliotekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA).

**Mheshimiwa Spika,** hadi tarehe 18 Machi, 2026, jumla ya shilingi **22,998,192,759.66** zilikuwa zimeshatolewa na Serikali na kulipwa kwa wakandarasi wanaotekeleza mradi huu. Katika kiasi hicho, Kampuni ya ujenzi SUMA JKT ilikuwa imeshalipwa shilingi **21,522,001,053.19** sawa na **asilimia 95** ya gharama za mkataba, NHC ilikuwa imeshalipwa shilingi **664,648,739.13** sawa na **asilimia 71** ya gharama za mkataba na TBA ilikuwa imeshalipwa shilingi **811,542,967.34**, sawa na **asilimia 100** ya gharama za mkataba.

Aidha, kuhusu Samani za kuwekwa katika ofisi hizo, Kamati ilielezwa kuwa mkataba wa ununuzi na ufungaji wa samani ulisainiwa tarehe 29 Januari, 2024 kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Kampuni ya *Jaffery Industry Ltd* kwa grahama ya **shilingi 2,114,338,278.** Katika kiasi hicho, ilielezwa kuwa mzabuni ameshalipwa malipo ya awali ya

shilingi **845,735,311.00** na ameshakamilisha uwasilishaji wa baadhi ya Samani ambazo zimehifadhiwa ili kusubiria kufungwa mara baada ya ujenzi wa jengo kukamilika. **Kwa kuwa kazi ya ujenzi bado haijakamilika, ni msisitizo wa Kamati kuwa samani zilizokwisha nunuliwa na kuwasilishwa, zitunzwe vizuri ili kuzuia kuharibika uharibifu au kupotea**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokagua mradi huu, ilielezwa kuwa ujenzi wake ulikuwa umefikia **asilimia 94.5**. Licha ya asilimia hiyo, ukaguzi wa Kamati ulibaini kuwa kazi nyingi zilikuwa hazijakamilika kwa asilimia mia moja, jambo lililo ashiria kuwa bado kuna kazi kubwa ya kumalizia kazi hizo. Kutokana na sababu hiyo, Kamati ilipata wasiwasi kuhusu ujenzi wa jengo hilo kukamilika ifikapo tarehe 30 Machi, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa, sababu za kuchelewa kukamilika kwa mradi huo ni pamoja na mkandarasi kuongezewa muda wa mkataba wa ujenzi, ucheleweshaji wa malipo ya mkandarasi, kuchelewa kwa baadhi ya vifaa vya ujenzi vilivyoagizwa nje ya nchi na kusua sua kwa timu ya ujenzi ya Mkandarasi-SUMA JKT.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutatua changamoto hiyo, Kamati ilielezwa kuwa hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwemo mkandarasi SUMA JKT kubadili timu ya awali iliyokuwa inatekeleza mradi huo (timu kutoka kanda ya kaskazini) na kuleta timu mpya (timu kutoka kanda ya kusini) ambayo ilielezwa kuwa imekuwa ikifanya kazi vizuri.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, licha ya jitihada hizo, miradi ya majengo ya Ofisi inayotekelezwa na Mkandarasi SUMA JKT ikiwemo majengo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria yanayojengwa Mwanza na mji wa Serikali Mtumba-Dodoma hayajakamilika licha ya muda wa utekelezaji kufikia mwisho hata baada ya muda kuongezwa. Aidha, hali ni tofauti kwa miradi kama hiyo inayotekelezwa na Mashirika mengine, hususan miradi ya ujenzi wa majengo ya Ofisi katika mji wa Serikali Mtumba. Kamati inatambua kuwa, ujenzi wa baadhi ya miradi hiyo ilitolewa kwa SUMA JKT ikiaminika kuwa shirika hilo litakamilisha miradi hiyo kwa wakati, hali ambayo imekuwa tofauti. Kutokukamilika kwa jengo hilo

kwa wakati, kumesababisha watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kusongamana katika ofisi ndogo ikiwemo kutumia majengo ya kupanga kama ofisi na kumbi za mikutano. Vilevile, kuchelewa huko kumepelekea Ofisi hiyo kutumia jumla ya **shilingi 92,500,000.00** kwa mwaka kwa ajili ya pango la Ofisi na mikutano.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuepukana na hasara na athari hizo, Kamati ilielezwa kuwa, ofisi inaendelea kumsimamia mkandarasi kwa ukaribu ili aweze kukamilisha ujenzi wa jengo hilo na watumishi kuhamia. Aidha, kutokana na matarajio hayo, katika mwaka 2026/2027, fedha kwa ajili ya kukodi pango la Ofisi na kumbi za mikutano kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais zimetengwa **shilingi 10,300,000.00** tu badala ya **shilingi 92,500,000.00** zilizokuwa zikitengwa kwa mwaka. Kufanya hivyo kumeokoa fedha za Serikali kiasi cha **shilingi 82,200,000.00** kwa kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutokuisababishaia Serikali hasara kwa siku za usoni kutokana na baadhi ya miradi inayotekelezwa na SUMA JKT kuchelewa kukamilika kadiri ilivyopangwa, **ni mtazamo wa Kamati kuwa, SUMA JKT ijengewe uwezo ili iweze kukamilisha miradi yote inayokabidhiwa kwa wakati. Aidha, uwezeshaji huo uendane sambamba na kutatua changamoto zinazokwamisha ukamilishaji wa miradi inayokabidhiwa kwa Kampuni hiyo, licha ya washitiri kulipa kwa wakati fedha za kutekeleza miradi hiyo.**

### 2.3 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Baadhi ya mapendekezo ilikuwa ni kutolewa kikamilifu kwa fedha za maendeleo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, tarehe 26 Machi, 2026; Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo katika mafungu yote mawili kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Mafungu hayo ni Fungu 26 linalohusu Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 linalohusu Ofisi ya Makamu wa Rais – katika masuala ya Muungano. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika eneo moja ambalo ni Makadirio ya mapato na matumizi kutokana na Ofisi hii kutokuwa na makusanyo ya maduhuli.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, Ofisi ya Makamu wa Rais katika mafungu yake mawili inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **50,465,088,000.00** kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kiasi hicho ni zaidi kwa kiasi cha shilingi **12,358,499,000.00**, sawa na ongezeko la asilimia **32.43** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2025/2026 ambayo ilikuwa shilingi **38,106,589,000.00**. Tathmini ya uchambuzi kuhusu fungu kwa fungu ni kama ifuatavyo: -

### 3.1 Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais -Fungu 26

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 23,297,959,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 1,297,959,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na **shillingi 22,000,000,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** kwa ulinganisho kati ya bajeti ya mwaka 2025/2026 na bajeti ya 2026/2027; bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi 3,351,560,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 16.80** dhidi ya bajeti ya mwaka unaoisha. Katika ongezeko hilo, Mishahara imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi 231,060,000.00** sawa na asilimia **21.66** na bajeti ya Matumizi mengineyo (OC) imeongezeka kwa kiasi cha Shilingi **3,120,500,000.00** sawa na asilimia **16.53**. Mchanganuo huo unaoneshwa katika **jedwali Na. 3** kama ifuatavyo:-

Jedwali Na. 3: **Ulinganisho wa bajeti ya Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027 Fungu Na. 26**

| **OFISI BINAFSI YA MAKAMU WA RAIS- FUNGU 26** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **FEDHA** | **CHANZO** | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO** | **ASILIMIA** |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | OC | 18,879,500,000 | 22,000,000,000 | 3,120,500,000 | **16.53** |
| | MISHAHARA | 1,066,899,000 | 1,297,959,000 | 231,060,000 | **21.66** |
| **JUMLA KUU** | | **19,946,399,000** | **23,297,959,000** | **3,351,560,000** | **16.80** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira na usanifu wa Kamati*

### 3.2 Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano)-Fungu 31

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, kupitia Fungu 31 katika masuala yanayohusu muungano inaomba kuidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Shilingi27,167,129,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **23,467,129,000.00.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kiasi kinachojumuisha mishahara **Shilingi 3,772,212,000.00** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 19,694,917,000.00.** Aidha, kiasi kinachoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni **Shilingi 3,700,000,000.00** ambazo zote ni fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ulinganisho kati ya bajeti ya mwaka 2025/2026 na bajeti ya 2026/2027, bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 kwa Fungu 31 kwenye masuala ya muungano imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi 9,006,939,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 49.6** dhidi ya bajeti ya mwaka unaoisha ambayo ilikuwa **shilingi 18,160,190,000.00**.

Katika ongezeko hilo, Mishahara imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi 656,939,000.00** sawa na asilimia **21.09** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka unaoisha, wakati bajeti ya Matumizi mengineyo (OC) imeongezeka kwa kiasi cha Shilingi **6,350,000,000.00** sawa na asilimia **47.58.** Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo imeongezeka kwa shilingi **2,000,000,000.00** sawa na **asilimia 117.65**. Mchanganuo huo unaoneshwa katika **jedwali Na. 4** kama ifuatavyo:-.

**Jedwali Na. 4: Ulinganisho wa bajeti ya Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027 - Fungu Na. 031**

| **OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)- FUNGU 31** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **FEDHA** | **CHANZO** | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO** | **ASILIMIA** |
| **MAENDELEO** | NDANI | 1,700,000,000 | 3,700,000,000 | 2,000,000,000 | **117.65** |
| | NJE | 0 | 0 | 0 | **-** |
| | **Jumla ndogo** | **1,700,000,000** | **3,700,000,000** | **2,000,000,000** | **117.65** |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | OC | 13,344,917,000 | 19,694,917,000 | 6,350,000,000 | **47.58** |
| | MISHAHARA | 3,115,273,000 | 3,772,212,000 | 656,939,000 | **21.09** |
| | **Jumla ndogo** | **16,460,190,000** | **23,467,129,000** | **7,006,939,000** | **42.57** |
| **JUMLA KUU** | | **18,160,190,000** | **27,167,129,000** | **9,006,939,000** | **49.6** |

***Chanzo:*** *Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira na usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho hapo juu unaonesha kuwa nyongeza kubwa ya fedha imeelekezwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo, ambapo fedha zimeongezwa kwa **asilimia 117.65**. Aidha, fedha zote zilizoongezwa ni fedha za ndani. **Kamati**

**inaipongeza Serikali kwa jithada za kutenga fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa asilimia mia moja. Ni rai ya Kamati kuwa, Ofisi hii iendelee na jitihada hizo katika miaka ijayo**.

## SEHEMU YA NNE

## 3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia majadiliano ya kina na uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ili kusaidia katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo: -

(a) Serikali imeshamlipa mkandarasi anayejenga Ofisi ya Makamu wa Rais katika mji wa Serikali Mtumba kiasi cha fedha sawa na **asilimia 95** ya fedha zote kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi huo. Wakandarasi wengine wanaotekeleza miradi kama hiyo katika eneo hilo wameshakamilisha na kukabidhi kazi hizo licha ya wakandarasi wote kuanza ujenzi wa majengo hayo yanayofanana kwa wakati mmoja. Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais linalojengwa na Kampuni ya SUMA JKT bado halijakamilika, na kutokukamilika huko kunaisababishia Serikali hasara na kuathiri utendaji wa watumishi wa Ofisi hizo. Ili kuhakikisha mkandarasi huyo anatekeleza wajibu wake ipasavyo, Serikali ianze kumtoza fedha za kuchelewesha mradi huo kwa kuzingatia makubaliano yao ya mkataba wa ujenzi.

(b) Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi, idadi kubwa ya Wananachi wa Tanzania wamezaliwa baada ya Muungano wa Tanganyia na Zanzibar uliofanyika mwaka 1964. Kwa kuwa Muungano huo una manufaa mengi na ni moja ya tunu ya Taifa, Kamati inashauri kwamba ili kuendelea kukuza uzalendo wa nchi yetu ikiwemo kulinda, kuheshimu, kupenda na kuenzi Muungano huo, Serikali ihakikishe inaanza ujenzi wa vituo vya Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano katika miji ya Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar kama ilivyopangwa ili watu waweze kufika kwenye vituo hivyo kwa ajili ya kujifunza historia ya Muungano huo.

(c) Fedha za bajeti zinazotengwa kila mwaka katika Ofisi ya Makamu wa Rais zimeendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazoukabili Muungano wetu. Aidha, utatuzi huo umekuwa na mafanikio makubwa ambapo kero 22 kati ya kero 25 zimepatiwa ufumbuzi, na hivyo kubakia kero tatu (3) tu. Kamati inashaurii kwamba, ili muungano wetu ufikie kiwango cha kuwa ni jambo la fursa pekee badala ya kuongelea habari za kero, Serikali ihakikishe inazipatia ufumbuzi kero tatu za Muungano zilizobakia na kuzuia kuzaliwa kwa kero nyingine.

(d) Mojawapo ya maeneo mapya ya kiuchumi yanayochipukia nchini ni uchumi wa buluu. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) ilianzisha kitengo cha uchumi wa Buluu ili kuweza kuratibu na kuwawezesha wananchi wanaohitaji kujishughulisha na uchumi wa buluu. Katika kuhakikisha wananchi wa pande zote za Muungano wananufaika na uanzishwaji wa kitengo hicho, ni ushauri wa Kamati kwamba Serikali iendelee kukiwezesha kitengo hicho kifedha na rasilimali nyinginezo ili kiweze kuwasaidia wananchi wa pande zote za Muungano katika kupenda na kuwekeza kwenye uchumi wa buluu.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. - **Mjumbe**
4. Mhe. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb - **Mjumbe**

| | | |
|---|---|---|
| 5. Mhe. Aziza Sleyum Ally, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 7. Mhe. Asha Hussein Saleh, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 8. Mhe. Esther Edwin Malleko, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 9. Mhe. Maryam Ussi Yahya, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 10. Mhe. Nassoro Rashid Nassoro, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 11. Mhe. Dkt. Neema Peter Majule, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 12. Mhe. Nyamizi Simon Mhoja, Mb | - | **Mjumbe** |
| 13. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 14. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 15. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb | - | **Mjumbe** |
| 16. Mhe. Timida Mpoki Fyandomo, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 17. Mhe. Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mb | - | **Mjumbe** |
| 18. Mhe. Yohana Stephen Msita, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 19. Mhe. Zena Maulid Katambo, Mb. | - | **Mjumbe** |
| 20. Mhe. Hussein Nassoro Amar, Mb. | - | **Mjumbe** |

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mhe. Mhandisi, Hamad Yussuf Masauni, Mb. – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati pamoja na kuwasilisha vizuri makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Aidha, naomba kumpongeza Mhe. Dkt. Festo Dugange (Mb) aliyekuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, kwa ushirikiano aliokuwa anaipatia Kamati na kwa niaba ya Kamati, ninamtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake mapya ya Naibu Waziri TAMISEMI. Aidha, natumia fursa hii kumpongeza na kumkaribisha Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo (Mb), kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Kamati inamkaribisha na inamtakia kila la kheri katika kazi zake za kumsaidia Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara, pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Richard Stanslaus Muyungi, Naibu Katibu Mkuu-Muungano Ndg. Abdallah Hassan

Mitawi na Naibu Katibu Mkuu-Mazingira, Balozi Baraka Haran Luvanda.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leornard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

**21 APRILI, 2026**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON G. KISWAGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 ninaomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa taarifa hii umezingatia masharti ya kanuni ya 145 kuhusu muundo wa taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu: sehemu ya kwanza inahusu

utangulizi ambayo inahusisha msingi wa muundo wa taarifa, na sehemu ya pili ni kuhusu uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; na sehemu ya tatu inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Serikali na mwisho itakuwa ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa kazi ya uchambuzi, namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake. Kanuni za Kudumu za Bunge 2025 zimeweka masharti yanayoitaka Kamati kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026, (Kanuni ya 121 (1)) na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ili kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, (Kanuni ya 120 (2))

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulijulisha Bunge lako kwamba Kamati ilitekeleza jukumu lake kwa kuzingatia matakwa ya kanuni hizi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi. Madhumuni ya taarifa hii ni kuliwezesha Bunge kujadili hotuba ya Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira iliyowasilishwa mapema leo hii ili kuliwezesha Bunge kufanya kazi hiyo inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imebainisha uchambuzi katika maeneo yafuatayo: hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati katika mwaka wa fedha 2025/2026; hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026; hali ya upatikanaji wa fedha za matumizi hadi kufikia mwezi wa Februari, 2026; hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mipango iliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ikilinganishwa na utekelezaji kwa mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtindo uliotumika kufanya uchambuzi unajumuisha kulinganisha na hali ilivyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Njia ya ukokotoaji wa asilimia ilitumika kubaini hatua iliyofikiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha na uwezekano wa mipango kwa mwaka wa fedha unaokuja. Kwa utaratibu huo, Bunge linaweza kujiridhisha na uwezekano wa mipango iliyolengwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa kutumia uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi kuhusu utekelezaji na ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Wakati wa majadiliano ya hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha 2025/2026, tarehe 24 Aprili, 2025 Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo katika maeneo matano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Maeneo yote Matano ya ushauri yanaendelea na utekelezaji na hakuna ushauri uliokamilika kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yanayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:-

(i) Ushauri kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kupata fedha kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa shughuli za hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imejulishwa kuwa, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026, hadi kufikia Februari, 2026 jumla ya shilingi 15,564,262,675.16 zimepokelewa sawa na 52.3% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ikilinganishwa na Shilingi 13,713,367,233.00, sawa na 44% ya fedha iliyopokelewa mwaka wa fedha 2024/2025 katika kipindi hicho.

(ii) Ushauri mwingine ni kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepokea taarifa kuwa, hatua iliyofikiwa ni kuandaliwa kwa andiko dhana la Mapendekezo ya Kuanzisha Mamlaka ya Taifa ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kuwasilishwa kwenye ngazi za maamuzi kwa ajili ya kupata idhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumaini ya Kamati ni kwamba Serikali itatekeleza ahadi ya kuwasilisha Muswada husika.

(iii) Ushauri mwingine ni kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, kupitia Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni, kuendelea kuhamasisha Vijiji vingi zaidi kujihusisha na biashara ya Kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeelezwa kuwa, kazi ya kuhamasisha vijiiji na halmashauri zenye misitu kujiunga katika biashara hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri unapotolewa Bungeni unalenga kuboresha shughuli za umma kwa maslahi ya wananchi. Serikali inapozingatia ushauri huo inatimiza azma ya kuboresha ustawi wa wananchi kama ilivyoshauriwa Bungeni. Aidha, kwa kuchelewa kuzingatia ushauri, hatari yake ni kutoboresha shughuli za umma kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi kuhusu Mambo yaliyobainika wakati wa Ziara ya Ukaguzi; Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 kwa kutembelea na kukagua utekelezaji wa mradi mmoja, kati ya miradi tisa ya Maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mmoja uliotembelewa na kukaguliwa ni Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo Ikolojia kwa Ajili ya Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bionuai Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi huo, katika Kijiji cha Kipera, Kata ya Nzihi Mkoani Iringa mnamo tarehe 12 Machi, 2026. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira, kwa ruzuku ya Dola za Marekani 11,205,872.00 sawa na shilingi bilioni 28 za Kitanzania. Mradi huo unatekelezwa katika kata tatu ambazo ni Nzihi, Izazi na Migoli. Vilevile unahusisha Vijiji nane ambavyo ni Ilalasimba, Magubike, Kipera, Makuka, Mnadani, Migoli Mtera na Makatapola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mradi huu ni kuimarisha usimamizi wa pamoja wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibiwa, ili kujenga uhimilivu wa mifumo ikolojia na jamii kwa ujumla. Utekelezaji wa mradi huu, hadi kufikia Februari, 2026 ilifikia 85%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini baadhi ya mafanikio kama ifuatavyo:-

(i) Kuongezeka kwa kiasi cha maji kilichotiririka kwenye mfereji mkuu na kuwezesha wakulima kuwa na uhakika wa maji ya umwagiliaji;

(ii) Kupungua kwa migogoro baina ya watumiaji wa maji kwenye eneo la umwagiliaji;

(iii) Ongezeko la eneo linalomwagiliwa kutoka hekta 70 kwa mwaka 2022 hadi hekta 256 kwa mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mradi, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo:-

(i) Kuchelewa kukamilika kwa ukarabati ambapo kilometa 11.5 hazijakamilika hivyo kusababisha hekta 248 kutofikiwa na maji.

(ii) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu biashara ya Kaboni;

(iii) Kutokuwa na Mabwawa madogo madogo kwa ajili ya kuvuna maji kwa kipindi cha mvua;

(iv) Miundombinu hafifu ya barabara kuelekea mashambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawapongeza wananchi wa Kijiji cha Kipera, Ipwasi, Ndorobo Iringa kwa kuachana na shughuli za ukataji miti na wameanza kujishughulisha na shughuli za kilimo cha umwagiliaji na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2025/2026; Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Serikali Fungu 31 kwa tarehe 23 na 24 Machi na kubaini changamoto zifuatazo:-

(i) Mabadiliko ya Sera za Kimataifa kwa baadhi ya nchi kujitoa katika uchangiaji wa Mifuko ya Kimataifa ya Mazingira;

(ii) *NEMC* kutokuwa Mamlaka kamili kisheria kunasababisha kushindwa kutimiza majukumu yao kikamilifu;

(iii) Kutokuwepo kwa ushirikiano wa karibu kwa Wadau wa shughuli za Mazingira. Wadau wanaohusika na mazingira ni pamoja na Sekta ya Maliasili na Utalii, Kilimo, Nishati, Madini, Mifugo, Viwanda, Maji na Ardhi;

(iv) Uelewa Mdogo kwa Wadau na wananchi kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; na

(v) Upungufu wa watumishi wa *NEMC* unaosababisha kushindwa kutimiza majukumu kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi kuhusu Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; Hali ya upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida; Uchambuzi wa Kamati wa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati umebaini kuwa mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha unaarifu kuwa Makadirio

ya Matumizi ya Kawaida hadi Februari, 2026 ni wa kuridhisha kwenye Matumizi ya Kawaida.

(i) Hadi Februari, 2026, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ilipokea kiasi cha 65.1% ya bajeti kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiwango hicho cha upatikanaji wa fedha kinaendana na hali halisi ya utekelezaji wa bajeti. Kiasi kilichopatikana ni shilingi 8,074,540,835.84 kati ya shilingi 12,398,024,000.00. Fedha zilizopokelekwa inakaribia wastani wa juu wa 66.5% unaopaswa kufikiwa katika kipindi hiki;

(ii) Mishahara iliyoidhinishwa kwa Idara ya Mazingira imepokelewa kwa 59.3%, *NEMC* 65.5% matumizi ya uendeshaji ni 66% ya matumizi ya kawaida. Uwiano wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya mishahara unaridhisha na unaendana na matumizi ya malipo ya mishahara kwa kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo hadi Februari, 2026; Matokeo ya Uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa miradi unaonesha kuwa, jumla ya fedha iliyopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Mazingira hadi Februari, 2026 ni 43%. Asilimia hii ni ndogo ikilinganishwa na muda uliobaki. Hali hiyo ni dalili ya wazi kwamba upo uwezekano wa baadhi ya Miradi ya Mazingira haitokamilika kama ilivyokusudiwa kufikia Juni, 2026.

(i) Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo usioridhisha, kulikosababisha kushindwa kukamilika kwa baadhi ya miradi;

(ii) Fedha za ndani zilizopangwa hadi Februari, 2026, ni 47% tu ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo;

(iii) Fedha za nje kwa ajili ya Miradi ya Mazingira zilizopatikana ni 42% ya bajeti iliyoidhinishwa;

(iv) Baadhi ya Miradi ambayo haikupokea fedha kabisa kama ilivyoidhinishwa na Bunge, ni Mradi wa Mfano, wa

ukijanishaji na upendezeshaji wa Jiji la Dodoma, Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Babati, Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Chala na Jipe, Mradi wa kujenga Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Mandhari ya Mkoa wa Kigoma Tanzania na Mradi wa kuboresha Mandhari ya eneo la Bwawa la Swaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo Kamati ina maoni kuwa, upatikanaji wa fedha kwa kiwango hicho unaweza kuathiri utekelezaji wa miradi. Aidha, msukumo wa fedha za ndani kwa miradi ya mazingira unahitaji kuongezewa mkazo zaidi. Taarifa iliyopokelewa kwenye Kamati inaonyesha kuwa, baadhi ya Miradi ambayo haikupokea fedha ilitegemea zaidi fedha za nje. Kielelezo Na. 2 kinatoa picha ya hali ya upatikanaji wa fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ulifanyika kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka huo wa fedha. Umakini zaidi uliwekwa katika maeneo yafuatayo:-

(a) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na

(b) Makadirio ya matumizi kwa ajili ya Mishahara kwa Idara ya Mazingira na *NEMC* na uendeshaji wa shughuli zinazohusu masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti Fungu 31; Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi 49,519,708,000. Kati ya fedha hizo shilingi 14,904,863,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 34,614,845,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida; Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 14,904,863,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha

hizo, shilingi 1,103,113,000.00 ni fedha za Mishahara kwa Idara ya Mazingira, shilingi 7,096,050,000.00 Fedha za Mishahara kwa *NEMC* na shilingi 6,605,700,000.00 ni kwa Matumizi mengineyo, kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2026/2027, imeongezeka kwa shilingi 2,506,839,000.00 sawa na 20% ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha unaoisha wa 2025/2026 ambapo bajeti hiyo ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa shilingi 12,398,024,000.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza kuajiri watumishi wa kutosha ili kuipa *NEMC* uwezo wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027; Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, imetengewa jumla ya shilingi 34,614,845,000.00 kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 10,702,000,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 23,912,845,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Maendeleo katika mwaka wa fedha 2026/2027, imeongezeka kwa takribani shilingi 17,255,266,000.00 sawa na 99% ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa:-

(a) Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 imeongezeka kwa 99% ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha;

(b) Bajeti ya Fedha za Nje imeongezeka kwa 40% huku Bajeti ya ndani ikiongezeka kwa 268% ikilinganishwa na fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Maendeleo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. Ni matarajio ya Kamati kwamba, Serikali itatoa fedha zote ili kuliwezesha Bunge kufanya shughuli kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati; Lengo kuu la Taarifa hii ni kubainisha maoni na ushauri wa Kamati ili kuwezesha majadiliano ya Bunge. Kamati inaamini kuwa maelezo yaliyotolewa ndani ya Taarifa hii yatakuwa na msaada muhimu kwa Bunge. Pamoja na majadiliano kuhusu hoja hii, upo umuhimu wa kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa katika Taarifa hii kwa lengo la kuboresha shughuli za umma zinazohusu usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira – Fungu 31 kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, ninaomba kubainisha Maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Ongezeko la Bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa shilingi 17,255,266,000.00 sawa na 99%. Kamati imeelezwa kuwa, ongezeko la fedha hizo litaongeza ufanisi katika utoaji elimu kwa umma kuhusu uhifadhi wa Mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hilo. Ongezeko hilo litakuwa na maana iwapo fedha hizo zitatolewa kwa wakati;

(ii) Uelewa Mdogo wa Wadau na Wananchi kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191, kunakwamisha juhudi za Serikali katika kuhifadhi mazingira na kukosa ufanisi katika kufanya tathmini ya athari kwa Mazingira;

(iii) Kutokuwepo kwa ushirikiano wa karibu kwa Wadau wa Mazingira kunakwamisha shughuli za usimamizi na uhifadhi wa mazingira;

(iv) *NEMC* kutokuwa Mamlaka kamili kisheria kunakwamisha utekelezaji bora wa majukumu yake kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191;

(v) Mabadiliko ya Sera za Kimataifa na baadhi ya nchi kujitoa katika uchangiaji wa Mifuko ya Kimataifa ya Mazingira kunakwamisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za utekelezaji wa miradi;

(vi) Kutokamilika kwa Mfereji wa Kilimo cha Umwagiliaji Katika Kijiji cha Kipera, kunasababisha upotevu wa maji njiani;

(vii) Uelewa mdogo wa wananchi kwenye biashara ya hewa ukaa/kaboni na uhaba wa fedha unakwamisha jitihada za kupambana na uharibifu wa mazingira; na

(viii) Upungufu wa Watumishi na vitendea kazi kwa *NEMC* kunasababisha kushindwa kutimiza kikamilifu majukumu yao ya kusimamia utunzaji wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza Serikali kwamba, izingatie maoni yanayotolewa na Bunge ili kuimarisha utendaji kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushauri wa Kamati; kwa msingi huo, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenendo Usioridhisha wa Utoaji wa Fedha za Miradi 2025/2026; Mabadiliko ya Sera za Kimataifa na baadhi ya nchi kujitoa katika uchangiaji wa mifuko ya Kimataifa ya Mazingira ni moja ya changamoto inayosababisha fedha za miradi kutokutolewa kwa wakati;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kwamba:-

(i) Kuweka Mkakati wa muda mrefu utakaowezesha kuimarisha upatikanaji wa mapato ya ndani katika utekelezaji wa Miradi ya Mazingira nchini;

(ii) Kufanya Makadirio ya bajeti kutokana na vyanzo vya uhakika vya fedha na zipatikane kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; Moja ya changamoto inayoikabili *NEMC* ni kutokuwa na nguvu kamili ya Kimamlaka katika suala la uendelezaji na usimamizi wa shughuli za mazingira nchini, jambo linalopunguza kasi ya uratibu bora katika usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali, kuharakisha mchakato wa kuleta Bungeni Muswada utakaowezesha Marekebisho ya Sheria ya Baraza kuwa mamlaka kamili yenye uwezo ulioimarishwa wa kusimamia kwa ufanisi masuala ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano duni kwa Wadau wa Mazingira; Moja ya changamoto inayoikabili *NEMC* ni kutokuwa na ushirikiano wa karibu na Wadau wanaohusika na shughuli za Mazingira, jambo ambalo linaleta changamoto katika kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali:-

(i) Kuchukua hatua stahiki ili kuwezesha ushirikiano wa wadau wote wanaohusika kwa karibu na shughuli za mazingira;

(ii) Kuondoa changamoto ya ucheleweshaji wa kupata vibali vya matumizi ya fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo baada ya kukamilisha taratibu za kimkataba; na

(iii) Ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa fedha za usimamizi wa Mazingira, *NEMC* ipate tozo kutoka kwa Wadau ambao shughuli zao zinaweza kuleta athari za moja kwa moja katika utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Biashara ya Hewa Ukaa (Kaboni) kwa Wananchi; hii ni njia bora ya kupunguza athari za uharibifu wa

Mazingira na mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo maeneo yenye misitu mikubwa na maeneo ya bahari nchini (kupunguza athari za uchafuzi wa bahari);

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kwamba, kupitia Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni, iendelee kutoa elimu na msaada wa kitaalam ili kuhamasisha vijiji vingi zaidi kujihusisha katika biashara ya kaboni na kuleta chachu ya maendeleo katika vijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukiukwaji wa Sheria na Kanuni ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; Moja ya changamoto katika usimamizi na utunzaji wa Mazingira, ni jamii kutokuzingatia sheria husika na kanuni zake jambo linalosababisha matokeo yasiyoridhisha kwenye masuala ya utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kwamba, elimu iendelee kutolewa kwa wananchi kuhusu uzingatiaji wa sheria kuanzia ngazi za vijiji na ianzishe programu maalum ya kuhifadhi misitu maeneo tofauti tofauti kulingana na ukubwa wa tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa watumishi *NEMC*. Imebainika moja ya changamoto inayoikabili *NEMC* ni uhaba wa watumishi na vitendea kazi. Ni jambo linalosababisha baraza kushindwa kutimiza majukumu yake kwa ufanisi. Kamati inaishauri Serikali ione namna bora ya kuongeza watumishi na vitendea kazi ili *NEMC* iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, kwa namna ya kipekee ninaendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuaminiwa na Bunge kupata nafasi ya kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yameendelea kutolewa mara kwa mara ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninamshukuru pia Naibu Spika kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako pamoja na

Wenyeviti wote wa Bunge kwa kumsaidia Mheshimiwa Spika kufanikisha kwa ufanisi Vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Kutokana na muda sitataja majina yao, ninaomba yaingie kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Hamad Yusuph Masauni, Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; na Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa ushirikiano katika uwasilishaji wa makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Richard Stanslaus Muyungi kwa ushirikiano walioupatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard kwa umakini na weledi katika kuratibu Shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kiukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende pia kuwashukuru wananchi wa Kalenga kwa kunirudisha mahali hapa mara ya pili, lakini na kuendelea kuniombea ili niendelee kutekeleza majukumu yangu kiufanisi na ninawaahidi kwamba sitawaangusha, nitaendelea kuwasemea kuhakikisha tunasukuma gurudumu la maendeleo kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana familia yangu na mke wangu kwa kuniombea na kunivumilia ninapokuwa katika kazi ya kutekeleza majukumu ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA 2026/2027 KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 121 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 145 kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu Tatu (3): -

(i) Sehemu ya 1 inahusu utangulizi ambayo inahusisha msingi na muundo wa taarifa;

(ii) Sehemu ya 2 ni kuhusu uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

(iii) Sehemu ya 3 ni Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Serikali; na Hitimisho.

## 1.2 Msingi wa Kazi ya Uchambuzi

### 1.2.1 Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira unatokana na Kifungu cha 6 (6) (b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, 2025. Vifungu hivyo vinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025, zimeweka masharti yaliyoitaka Kamati: -

(i) Kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Kanuni ya 120(1)); na

(ii) Kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ili kulinganisha na Makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. (Kanuni ya 120 (2)).

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulijulisha Bunge lako kwamba Kamati imetekeleza jukumu lake kwa kuzingatia matakwa ya kanuni hizi za Bunge

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Madhumuni ya Taarifa hii ni kuliwezesha Bunge kujadili Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira aliyoiwasilisha mapema leo hii. Ili kuliwezesha Bunge kufanya kazi hiyo inavyostahili, Taarifa hii inabainisha uchambuzi katika maeneo yafuatayo:

(i) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iii) Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Matumizi hadi kufikia Mwezi Februari, 2026;

(iv) Hatua iliyofikiwa katika Utekelezaji wa mipango iliyowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(v) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ikilinganishwa na utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika,** Mtindo uliotumika kufanya uchambuzi unajumuisha kulinganisha na hali ilivyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadiro kwa Mwaka 2026/2027. Njia ya ukokotoaji wa asilimia imetumika kubaini hatua iliyofikiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha na uwezekano wa Mipango kwa Mwaka wa fedha unaokuja. Kwa utaratibu huo, Bunge linaweza kujiridhisha na uwezekano wa mipango inayolengwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa kutumia uzoefu uliopatikana kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**2.2 Uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Ushauri Uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa majadiliano ya hotuba ya Bajeti ya OMRM kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, tarehe 24 Aprili, 2025, Kamati ilitoa Ushauri na Mapendekezo katika maeneo Matano. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Maeneo yote Matano ya ushauri yanaendelea na utekelezaji, na hakuna ushauri uliokamilika kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni yanayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:-

(i) **Ushauri kuhusu OMRM kupata fedha kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa shughuli za hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Miradi ya Maendeleo.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imejulishwa kuwa, kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/26, hadi kufikia Februari, 2026 jumla ya **Shilingi 15,564,262,675.16** zimepokelewa sawa na asilimia **52.3** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ikilinganishwa na Shilingi **13,713,367,233.00** sawa na asilimia **44** ya fedha iliyopokelewa Mwaka wa Fedha 2024/25 katika kipindi hicho.

(ii) **Ushauri mwingine ni kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepokea taarifa kuwa, hatua iliyofikiwa ni kuandaliwa kwa andiko dhana la Mapendekezo ya Kuanzisha Mamlaka ya Taifa ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kuwasilishwa kwenye ngazi za maamuzi kwa ajili ya kupata idhini.

**Mheshimiwa Spika**, katika suala hili itakumbukwa kwamba, wakati wa Bunge la 12 (mkutano wa 18) Bunge lako tukufu, lilifanya marekebisho madogo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 ambapo Serikali iliahidi kuwasilisha Mswada wenye marekebisho makubwa yatakayoongeza ufanisi katika usimamizi wa Mazingira na

mabadiliko ya tabianchi. Hivyo ni matumaini ya Kamati kwamba, Serikali itatekeleza ahadi ya kuwasilisha Mswada husika.

(iii) **Ushauri mwingine ni kuhusu OMRM kupitia Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni (NCMC), kuendelea kuhamasisha Vijiji vingi zaidi kujihusisha na biashara ya Kaboni.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeelezwa kuwa, kazi ya kuhamasisha Vijiiji na Halmashauri zenye Misitu kujiunga katika biashara hiyo inaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Ushauri unapotolewa Bungeni unalenga kuboresha shughuli za umma kwa maslahi ya Wananchi. Serikali inapozingatia ushauri huo inatimiza azma ya kuboresha ustawi wa Wananchi kama inavyoshauriwa Bungeni. Aidha, kwa kuchelewa kuzingatia ushauri, hatari yake ni kutoboresha shughuli za umma kwa wakati.

## 2.3 Uchambuzi Kuhusu Mambo Yaliyobainika Wakati wa Ziara ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 kwa kutembelea na kukagua utekelezaji wa mradi mmoja, kati ya miradi 9 ya Maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** mradi mmoja uliotembelewa na kukaguliwa ni Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo Ikolojia kwa Ajili ya Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bionuai Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea mradi huu, katika Kijiji cha Kipera kata ya Nzihi Mkoani Iringa mnamo tarehe 12.03.2026. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF), kwa ruzuku ya Dola za Marekani **11,205,872.00** sawa na Shilingi **bilioni 28** za Kitanzania. Mradi huo unatekelezwa katika kata 3 ambazo ni Nzihi, Izazi na Migoli . Vilevile unahusisha vijiji 8 ambavyo ni Ilalasimba, Magubike, Kipera, Makuka, Mnadani, Migoli Mtera na Makatapola.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la mradi huu ni kuimarisha usimamizi wa pamoja wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibiwa, ili kujenga uhimilivu wa mifumo ikolojia na jamii kwa ujumla. Utekelezaji wa mradi huu, hadi kufikia Februari, 2026 ni **asilimia 85.**

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo, Kamati ilibaini mafanikio yafuatayo: -

(i) Kuongezeka kwa kiasi cha maji kinachotiririka kwenye mfereji mkuu na kuwezesha wakulima kuwa na uhakika wa maji ya Umwagiliaji;

(ii) Kupungua kwa migogoro baina ya watumiaji wa maji kwenye eneo la umwagiliaji;

(iii) Ongezeko la eneo linalomwagiliwa kutoka Hekta 70 kwa Mwaka 2022 hadi Hekta 256 kwa Mwaka 2025;

(iv) Wakulima 475 wamenufaika na Kilimo cha Umwagiliaji;

(v) Wakulima kuongeza tija ya uzalishaji wa zao la mpunga kutoka tani 1.3 hadi tani 2.5 kwa ekari na mradi wa ujenzi wa ghala la kuhifadhia na kusindika nafaka;

(vi) Uharibifu wa mazingira umepungua kwa kuwa, wakulima wamekuwa na uhakika wa kilimo cha umwagiliaji na ufugaji wa Nyuki pamoja na ng'ombe Wa Maziwa, kama chanzo cha uhakika cha mapato;

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mradi, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo:-

(i) Kuchelewa kukamilika kwa ukarabati wa Skimu ambapo Kilomita **11.5** hazijakamilika hivyo kusababisha hekta **248** kutofikiwa na maji ya umwagiliaji;

(ii) Uelewa mdogo wa Wananchi kwenye biashara ya hewa ukaa / Kaboni;

(iii) Kutokuwa na Mabwawa madogo madogo kwa ajili ya kuvuna maji kipindi cha mvua;

(iv) Miundombinu hafifu ya barabara kuelekea mashambani.

**Mheshimiwa Spika** Kamati inawapongeza Wananchi wa kijiji cha Kipera Ipwasi Ndorobo Iringa kwani wameachana na shughuli za ukataji miti na wameanza kujishughulisha na kilimo cha umwagiliaji na ufugaji wa Ng'ombe wa maziwa.

**2.4 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2025/2026.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Serikali **Fungu 31** kwa tarehe 23 &24 Machi, na kubaini baadhi ya mafanikio yafuatayo :-

(i) Ofisi imewezesha upatikanaji wa fedha kiasi cha **Dola za Marekani 651,000** sawa na **Shilingi bilioni 1.5** za kuwezesha utekelezaji wa maazimio ya mikataba ya kimataifa ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kupitia Sekretarieti zake;

(ii) Ofisi imeendelea na maandalizi ya maandiko dhana kumi na moja (11) kwa ajili ya kupata fedha kupitia Mifuko mbalimbali ya Mazingira na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo, fedha zitakazotengwa katika awamu ya tisa (09) ya Mfuko wa Mazingira wa Dunia;

(iii) kupitia Mfuko unaoshughulikia upotevu na hasara itokanayo na athari za Mabadiliko ya Tabianchi, Ofisi imeanza maandalizi ya maombi ya fedha kiasi cha Dola za Marekani **milioni 20** sawa na shilingi **bilioni 51**;

(iv) Katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya kupikia, Machi 24, 2023 Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais ilipiga marufuku matumizi ya kuni na

mkaa kwa taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 na kuanza kutumia nishati safi ya kupikia. Hadi kufikia Februari, 2026 jumla ya Taasisi 1,301 zimeanza matumizi ya nishati safi ya kupikia

(v) Kuratibu Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

(i) Mabadiliko ya Sera za Kimataifa na baadhi ya nchi kujitoa katika uchangiaji wa mifuko ya Kimataifa ya Mazingira;

(ii) NEMC Kutokuwa Mamlaka kamili kisheria kunasababisha kushindwa kutimiza majukumu yao kikamilifu;

(iii) Kutokuwepo kwa ushirikiano wa karibu kwa Wadau wa shughuli za Mazingira. Wadau wanaohusika na mazingira ni pamoja na Sekta ya Maliasili na Utalii, Kilimo, Mifugo, Viwanda, Maji, Ardhi, Nishati na Madini ;

(iv) Uelewa Mdogo wa Wadau na Wananchi Kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; na

(v) Upungufu wa watumishi wa NEMC na vitendea kazi kunakosababisha kushindwa kutimiza majukumu yao kikamilifu.

**2.5 Uchambuzi Kuhusu Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2025/2026**

**2.5.1 Hali ya upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati wa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati umebaini kuwa mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha unaarifu kuwa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida hadi Februari, 2026 ni wa kuridhisha kwenye Matumizi ya Kawaida.

**Kielelezo Na. 1 kinatoa picha ya hali hiyo ya upatikanaji wa fedha za matumizi ya Kawaidak ama ifuatavyo:-**

(i) Hadi Februari, 2026 Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira ilipokea asilimia **65.1** ya bajeti kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiwango hicho cha upatikanaji wa fedha kinaendana na hali halisi ya utekelezaji wa bajeti. Kiasi kilichopatikana ni Shilingi **8,074,540,835.84** kati ya Shilingi **12,398,024,000.00.** Fedha iliyopokelewa inakaribia wastani wa juu ya **asilimia 66.5** unaopaswa kufikiwa katika kipindi hiki.

(i) Mishahara iliyoidhinishwa kwa Idara ya Mazingira imepokelewa kwa **asilimia 59.3**, NEMC **asilimia 65.5** matumizi ya uendeshaji ni **asilimia 66** ya matumizi ya kawaida. Uwiano wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya Mishahara unaridhisha na unaendana na matumizi ya malipo ya mishahara kwa kila mwezi.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kwamba inaendelea kuongeza idadi ya watumishi** kwa **NEMC na kuboresha maslahi yao ili kuwawezesha kufanya majukumu yao kwa ufanisi.**

**Kielelezo 1: Mchanganuo wa Fedha za Mishahara zilizotengwa na Kupokelewa**

| **FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA ZILIZOPOKELEWA HADI FEBRUARI 2026** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha iliyotengwa 2025/26** | **Fedha zilizopokelewa** | **% ya Fedha iliyopokelewa** | **Kiasi kilichotumika** |
| Mishahara Idara ya Mazingira | 1,117,037,000.00 | 662,504,000.00 | 59.3 | 662,504,000.00 |
| Mishahara NEMC | 6,675,287,000.00 | 4,373,917,142.72 | 65.5 | 4,373,917,142.72 |
| OC (OMR) | 4,605,700,000.00 | 3,038,119,693.12 | 66.0 | 3,037,961,465.50 |
| **JUMLA** | **12,398,024,000.00** | **8,074,540,835.84** | **65.1** | **8,074,540,835.84** |

Chanzo: **Randama ya Bajeti 2026/2027 Fungu 31**

### 2.5.2 Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo hadi Februari,2026

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya Uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa miradi yanaonesha kuwa, jumla ya fedha iliyopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Mazingira hadi Februari, 2026 ni asilimia **43.** Asilimia hii ni ndogo ikilinganishwa na muda uliobaki. Hali hiyo ni dalili ya wazi kwamba upo uwezekano wa baadhi ya Miradi ya Mazingira haitokamilika kama ilivyokusudiwa kufikia Juni, 2026;

(i) Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo usioridhisha, kunasababisha kushindwa kukamilika kwa baadhi ya miradi;

(ii) Fedha za ndani zilizotolewa hadi Februari 2026, ni **asilimia 47** tu ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo;

(iii) Fedha za nje kwa ajili ya Miradi ya Mazingira zimepatikana kwa **asilimia 42** ya Bajeti iliyoidhinishwa;

(iv) Baadhi ya Miradi ambayo haikupokea fedha kabisa kama ilivyoidhinishwa na Bunge, ni Mradi wa Mfano, wa ukijanishaji na upendezeshaji wa Jiji la Dodoma, Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Babati, Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Chala na Jipe, Mradi wa kujenga Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Mandhari ya Mkoa wa Kigoma Tanzania na Mradi wa kuboresha Mandhari ya eneo la Bwawa la Swaswa;

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo Kamati ina maoni kuwa, upatikanaji wa fedha kwa kiwango hicho unaweza kuathiri utekelezaji wa miradi. Aidha, msukumo wa fedha za ndani kwa miradi ya mazingira unahitaji kuongezewa mkazo zaidi. Taarifa iliyopokelewa kwenye Kamati inaonyesha kuwa, baadhi ya Miradi ambayo haikupokea fedha ilitegemea zaidi fedha za nje.

Kielelezo Na. 2 kinatoa picha ya hali ya upatikanaji wa fedha za Maendeleo

**Kielelezo 2: Mchanganuo wa Fedha za Maendeleo zilizopokelewa na kutumika**

| Idara | Aina ya Matumizi | Fedha zilizoidhinishwa | Fedha Zilizopokelewa | Fedha zilizotumika | % iliyopokelewa | % iliyotumika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mazi-ngira** | Fedha za Ndani | 2,902,000,000.00 | 1,357,241,839.32 | 1,357,241,839.32 | 47 | 100 |
| | Fedha za Nje | 14,457,579,000.00 | 6,132,480,000.00 | 3,716,090,000.00 | 42 | 61 |
| **JUMLA KUU** | | **17,359,579,000.00** | **7,489,721,839.32** | **5,073,331,839.32** | **43** | **68** |

**Chanzo: Randama ya Bajeti 2026/2027 Fungu 31**

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, ulifanyika kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka huo wa fedha. Umakini zaidi uliwekwa katika maeneo yafuatayo;

(a) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na

(b) Makadirio ya matumizi kwa ajili ya Mishahara kwa Idara ya Mazingira na NEMC na uendeshaji wa shughuli zinazohusu masuala ya mazingira (OC).

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa maeneo hayo unafanyika kwa kuzingatia ahadi iliyotolewa kwa Wananchi kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2025, DIRA 2050, Mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2026/27 na Maelekezo mengine ya Viongozi.

### 3.1 Vipaumbele vya Baraza kwa Mwaka 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, vipaumbele vya Baraza kwa Mwaka 2026/2027 vimeandaliwa kwa kuzingatia malengo makuu yalioainishwa kwenye mpango Mkakati wa Baraza kama ifuatavyo: -

(i) Baraza kuwa mamlaka kamili yenye uwezo ulioimarishwa wa kusimamia kwa ufanisi masuala ya mazingira;

(ii) Kuratibu mchakato wa TAM ili kuhakikisha miradi yote ya maendeleo inajumuisha masuala ya mazingira kabla ya kuanza utekelezaji;

(iii) Kusajili na kusimamia utendaji wa wataalamu elekezi wa mazingira;

(iv) Kuratibu, kusimamia na kushauri utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, miongozo na mikakati ya mazingira kwa lengo la kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;

(v) Kufanya tafiti mbalimbali za mazingira ili kuongeza uelewa wa mifumo ya ikolojia, kuhifadhi bioanuwai, na kusaidia maamuzi sahihi ya usimamizi endelevu wa mazingira; na

(vi) Kuimarisha mfumo wa kisheria na uratibu wa utekelezaji wa viwango vya mazingira (Kanuni mbalimbali); Kudhibiti vyanzo vikuu vya uchafuzi wa mazingira (plastic na taka hatarishi).

### 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti FUNGU 31

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 49,519,708,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 14,904,863,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 34,614,845,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

### 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 14,904,863,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,103,113,000.00** ni fedha za Mishahara kwa Idara ya Mazingira, **Shilingi 7,096,050,000.00** Fedha za Mishahara kwa NEMC na **Shilingi 6,605,700,000.00** ni kwa Matumizi mengineyo, kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.3.**

**Kielelezo 3: Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida Fungu 31 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 026/2027**

| ULINGANISHO WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA FUNGU 31 KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA 2026/2027 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **AINA YA MATUMIZI** | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO** | **ASILIMIA** |
| Mishahara Idara ya Mazingira | 1,117,037,000.00 | 1,103,113,000.00 | - 13,924,000.00 | - 1.25 |
| Mishahara NEMC | 6,675,287,000.00 | 7,096,050,000.00 | 420,763,000.00 | 6 |
| OC | 4,605,700,000.00 | 6,705,700,000.00 | 2,100,000,000.00 | 46 |
| **Jumla** | **12,398,024,000.00** | **14,904,863,000.00** | **2,506,839,000.00** | **20** |

**Chanzo. Randama ya Bajeti 2026/2027 Fungu 31**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi katika kielelezo hicho unaonesha kuwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imeongezeka kwa Shilingi **2,506,839,000.00** sawa na asilimia **20** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha unaoisha wa 2025/2026 ambapo Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa **Shilingi 12,398,024,000.00**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza kuajiri Watumishi wa kutosha ili kuipa NEMC uwezo wa kutekeleza majukumu yake.

### 3.4 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 OMRM, imetengewa jumla ya **Shilingi 34,614,845,000.00** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 10,702,000,000.00** ni fedha za ndani, na **Shilingi 23,912,845,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 imeongezeka kwa takribani **Shilingi 17,255,266,000.00** sawa na **asilimia 99** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha**. kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 4.**

**Kielelezo 4: Ulinganisho wa Bajeti ya Fedha za Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027**

| ULINGANISHO WA BAJETI YA MAENDELEO FUNGU 31 KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA 2026/2027 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Aina ya Matumizi** | **BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** | **BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2026/2027** | **Ongezeko** | **Ongezeko** |
| Fedha za ndani | 2,902,000,000.00 | 10,702,000,000.00 | 7,800,000,000 | 268.78 |
| Fedha za nje | 14,457,579,000.00 | 23,912,845,000.00 | 9,455,266,000 | 40 |
| **Jumla** | **17,359,579,000.00** | **34,614,845,000.00** | **17,255,266,000.00** | **99** |

**Chanzo: Randama ya Bajeti 2026/2027 Fungu 31**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa:

(a) Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027 imeongezeka kwa **asilimia 99** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha;

(b) Bajeti ya Fedha ya Nje imeongezeka kwa **asilimia 40** huku Bajeti ya ndani ikiongezeka kwa **asilimia 268** ikilinganishwa na fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Maendeleo kwa OMRM. Ni matarajio ya Kamati kwamba, Serikali itatoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kama ilivyopangwa

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la Taarifa hii ni kubainisha maoni na ushauri wa Kamati ili kuwezesha majadiliano ya Bunge. Kamati inaamini kuwa maelezo yaliyotolewa ndani ya Taarifa hii yatakuwa na msaada muhimu kwa Bunge. Pamoja na majadiliano kuhusu hoja hii, upo umuhimu wa kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa katika Taarifa hii kwa lengo la kuboresha shughuli za umma zinazohusu usimamizi wa mazingira.

### 4.2 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya OMRM – **Fungu 31** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, naomba kubainisha Maoni ya Kamati kama ifuatavyo: -

(i) Ongezeko la Bajeti ya Maendeleo ya OMRM kwa Shilingi **17,255,266,000.00** sawa na **asilimia 99.** Kamati imeelezwa kuwa, ongezeko la fedha hizo litaongeza ufanisi katika utoaji elimu kwa umma kuhusu uhifadhi wa Mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hilo. Ongezeko hilo litakuwa na maana iwapo fedha hizo zitatolewa kwa wakati;

(ii) Uelewa Mdogo wa Wadau na Wananchi Kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191, kunakwamisha juhudi za

Serikali katika kuhifadhi mazingira na kukosa ufanisi katika kufanya tathmini ya athari kwa Mazingira (TAM);

(iii) Kutokuwepo kwa ushirikiano wa karibu kwa wadau wa Mazingira kunakwamisha shughuli za usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira;

(iv) NEMC kutokuwa Mamlaka kamili Kisheria kunakwamisha utekelezaji bora wa majukumu yake kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191;

(v) Mabadiliko ya Sera za Kimataifa na baadhi ya nchi kujitoa katika uchangiaji wa Mifuko ya Kimataifa ya Mazingira kunakwamisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za utekelezaji wa miradi;

(vi) Kutokamilika kwa Mfereji wa Kilimo cha Umwagiliaji Katika kijiji cha Kipera, kunasababisha upotevu wa maji njiani;

(vii) Uelewa mdogo wa Wananchi kwenye biashara ya hewa ukaa / Kaboni na uhaba wa fedha unakwamisha jitihada za kupambana na uharibifu wa mazingira; na

(viii) Upungufu wa Watumishi na vitendea kazi kwa NEMC kunasababisha kushindwa kutimiza kikamilifu majukumu yao ya kusimamia utunzaji wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza Serikali kwamba, izingatie maoni yanayotolewa na Bunge ili kuimarisha utendaji kwa manufaa ya Wananchi.

### 4.3 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo, Kamati inashauri mambo yafuatayo: -

### 4.3.1 Mwenendo Usioridhisha wa Utoaji wa Fedha za Miradi 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, Mabadiliko ya Sera za Kimataifa na baadhi ya nchi kujitoa katika uchangiaji wa mifuko ya Kimataifa ya Mazingira ni moja ya changamoto inayosababisha fedha za miradi kutokutolewa kwa wakati;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kwamba,

(i) iendelee kuweka Mkakati wa muda mrefu utakaowezesha kuimarisha upatikanaji wa mapato ya ndani katika kutekeleza Miradi ya Mazingira nchini;

(ii) kufanya Makadirio ya bajeti kutokana na vyanzo vya uhakika vya fedha na zipatikane kwa wakati.

### 4.3.2 Marekebisho Kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira

**Mheshimiwa Spika**, moja ya changamoto inayoikabili NEMC ni kutokuwa na nguvu kamili ya Kimamlaka katika suala la uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Mazingira nchini, jambo linalopunguza kasi ya Uratibu bora katika Usimamizi wa Mazingira;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali , kuharakisha mchakato wa kuleta Bungeni Mswada utakaowezesha Marekebisho ya Sheria ya Baraza kuwa mamlaka kamili yenye uwezo ulioimarishwa wa kusimamia kwa ufanisi masuala ya mazingira.

### 4.3.3 Ushirikiano duni kwa Wadau wa Mazingira

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto inayoikabili NEMC ni kutokuwa na ushirikiano wa karibu na Wadau wanaohusika na shughuli za Mazingira, jambo ambalo linaleta changamoto katika kufikia malengo yaliyokusudiwa;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali,

(i) kuchukua hatua stahiki ili kuwezesha ushirikiano wa wadau wote wanaohusika kwa karibu na shughuli za mazingira;

(ii) kuondoa changamoto ya ucheleweshaji wa kupata vibali vya matumizi ya fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo baada ya kukamilisha taratibu za kimkataba; na

(iii) Ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa fedha za usimamizi wa Mazingira, NEMC ipate tozo kutoka kwa Wadau ambao shughuli zao zinaweza kuleta athari za moja kwa moja katika utunzaji wa mazingira.

**4.3.4 Biashara ya Hewa Ukaa (*Kaboni)* kwa Wananchi**

**Mheshimiwa Spika,** hii ni njia bora ya kupunguza athari za uharibifu wa Mazingira na mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo maeneo yenye misitu mikubwa na maeneo ya bahari nchini (kupunguza athari za uchafuzi wa bahari);

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kwamba, kupitia Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni (NCMC), iendelee kutoa elimu na msaada wa kitaalam ili kuhamasisha vijiji vingi zaidi kujihusisha katika biashara ya kaboni, na kuleta chachu ya maendeleo katika vijiji husika.

**4.3.5 Ukiukwaji wa Sheria na Kanuni ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191;**

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto katika usimamizi na utunzaji wa Mazingira, ni jamii kutokuzingatia sheria husika na kanuni zake jambo linalosababisha matokeo yasiyoridhisha kwenye masuala ya utunzaji wa mazingira;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kwamba, elimu iendelee kutolewa kwa wananchi kuhusu uzingatiaji wa Sheria, pia ianzishe programu maalum ya kuhifadhi misitu maeneo tofauti tofauti kulingana na ukubwa wa tatizo.

### 4.3.6 Upungufu wa Watumishi wa NEMC

**Mheshimiwa Spika,** imebainika moja ya changamoto inayoikabili NEMC ni uhaba wa watumishi na vitendea kazi, ni jambo linalosababisha Baraza kushindwa kutimiza majukumu yake kwa ufanisi;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali ione namna bora ya kuongeza watumishi na vitendea kazi, ili NEMC iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa Kuaminiwa na Bunge kupata nafasi ya kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yameendelea kuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira. Aidha, namshukuru Naibu Spika, kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha kwa ufanisi vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Prof. Pius Zebhe Yanda, Mb - **Makamu**
3. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb, - Mjumbe
4. Mhe. Patali Shida Patali, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Eng. Ramadhani Hamza Singano, Mb - Mjumbe
6. Mhe. George Venance Lugomela, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Haiderali Hussein Gulamali, Mb - Mjumbe

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Mhe. Azza Hillal Hamad, Mb | - Mjumbe |
| 9. | Mhe. Thomas Maganga Kampala, Mb | - Mjumbe |
| 10. | Mhe. Martha Festo Mariki | - Mjumbe |
| 11. | Mhe. Lutevele Nathan Dickson Mb | - Mjumbe |
| 12. | Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | - Mjumbe |
| 13. | Mhe. Asya Sharifu Omar, Mb | - Mjumbe |
| 14. | Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb | - Mjumbe |
| 15. | Mhe. Patrick Adkin Mwalunenge, Mb | - Mjumbe |
| 16. | Mhe. Jamal Ramadhan Mwinyi, Mb | - Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mecktridis Fratern Mdaku, Mb | - Mjumbe |
| 18. | Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb | - Mjumbe |
| 19. | Mhe. Sanya Jussa Jafari, Mb | - Mjumbe |
| 20. | Mhe. Zuena Athumani Masauni, Mb | - Mjumbe |
| 21. | Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb | - Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe Hamad Yussuf Masauni (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira na Mhe. Reuben Nhamanilo Kwagilwa (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa ushirikiano katika uwasilishaji wa Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Richard Stanslaus Miyungi kwa ushirikiano walioipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Lenard, kwa umakini na weledi katika kuratibu shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jackson Kiswaga, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA**
21 Aprili, 2026.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti, Mheshimiwa Kiswaga kwa taarifa hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kwenye hatua ya uchangiaji tutakuwa na wachangiaji wachache mchana huu kipindi hiki na wengine wengi watachangia jioni.

Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Najma Murtaza Giga atafuatiwa na Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii. Kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndiyo muweza wa yote katika ulimwengu wetu. Pia, ninakishukuru Chama Cha Mapinduzi chini ya uongozi thabiti wa Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia, nivishukuru vikao vyote ambavyo vimekaa vya uteuzi hadi kupitisha jina kufika Kamati Kuu na kuweza leo kuwa Mbunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu ambao wapo sehemu mbalimbali katika nchi hii Wilaya zote za Nchi hii ya Tanzania. Ni ahadi yangu kwamba yale ambayo nimeahidi nitaendelea kuyatekeleza kwa ambavyo Mwenyezi Mungu atanijalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sasa nitumie fursa hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na timu yake yote ya Mawaziri waliohudumu katika Ofisi hii ya Rais, Muungano na Mazingira ambapo sasa hivi yupo ndugu yetu,

Mheshimiwa Hamad Yusuph Masauni pamoja na timu yake yote ya watendaji katika Ofisi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya kama ambavyo Kamati imeeleza mafanikio yamepatikana sina haja ya kuyarejea. Kazi iliyofanywa ni kubwa, changamoto 25 kuondolewa zikabaki tatu, siyo kazi ndogo. Hatuna budi kuipongeza Serikali kwa juhudi hizi inazochukua kuboresha au kulinda na kuudumisha muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kabisa maono ya viongozi wetu wote kuanzia Awamu ya Kwanza hadi hii ya Sita wana uelewa, wanathamini na kutambua umuhimu wa muungano wetu ikiwa ni tunu pekee na muungano pekee ambao unaheshimiwa na kuthaminiwa Barani Afrika na duniani kwa ujumla, ndiyo maana jitihada hizi zilifanyika kuanzia Awamu ya Kwanza hadi ya sasa hivi ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani hiyo itujengee Watanzania na sisi tuweke *mindset* zetu vizuri Watanzania wote na kuthamini, kuuenzi na kuuheshimu Muungano wetu ikiwa Bara la Afrika na dunia kwa ujumla inatambua Muungano wetu ni muungano wa kipekee ambao umedumu kwa zaidi ya miaka 60 ukiwa umedumisha Taifa moja lenye amani, utulivu na mshikamo. Je, sisi Watanzania kwa nini tusijivunie na Muungano wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika siku hii ya leo ninaomba niishauri Serikali yetu sikivu, pamoja na maoni mazuri yaliyotolewa na Kamati ya kuunda vituo, Zanzibar, Dar es Salaam na Dodoma, ninaongeza mchango wangu ili kuboresha kama si bajeti hii, lakini ninajua tunaweza kupata njia mbadala ya kutafuta fedha. Tushirikiane na Wizara ya Elimu, tuhakikishe kama ambavyo tunafundisha Somo la Historia kwa mambo mengine ambayo mara nyingi tumekuwa tukishauri katika Bunge letu, suala la uraia, uzalendo, maadili ya Taifa letu sambamba na suala la Muungano wetu lihusishe katika mitaala ya elimu kwa kiwango tutakachoona inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu haiwezekani kwamba Bara letu la Afrika nje ya nchi yetu, duniani kwa ujumla waelewe kama ni Muungano wetu ambao umeunda nchi mbili huru na kupata dola moja, muungano wa pekee duniani ambao umedumu kwa muda mrefu kuliko muungano wowote duniani, iwe sisi Watanzania hatuuelewi na kuuthamini, uthaminiwe na nchi za nje. Itakuwa ni jambo la ajabu na aibu kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri huu ninauelekeza tushirikiane na Wizara ya Elimu tulifanye hili jambo liwe mahsusi kwa Taifa letu. Kama ambavyo tunamuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Abeid Aman Karume wa Zanzibar na thamani ya Muungano wetu ambao umeanzishwa na waasisi hawa iendelee kudumu vizazi na vizazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tupo mahali si pabaya sana, lakini kutoendelea kuelewa thamani ya muungano wetu namna ambavyo umeundwa na ambavyo unaendeshwa kwa kizazi kilichopo ambacho hakijazaliwa wakati wa muungano kunaweza kwenda kuhatarisha muungano wetu miaka ya mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri huu mdogo ambao ninahisi ni muhimu sana kwa siku ya leo ninaomba wauchukue na kuufanyia kazi. Vinginevyo mimi ni muumini wa muungano na nitaendelea kumwomba Mwenyezi Mungu hadi mwisho wa uhai wangu muungano huu udumu miaka hata elfu ikiwezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Abood.

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa hii fursa, lakini vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri sana na yenye mwelekeo mzuri sana kwa Taifa letu kwa maana ya Muungano wetu. Vilevile,

nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuhakikisha kwamba muungano wetu unakuwa imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ninataka nianze kwanza na muungano. Muungano wetu una miaka 62 sasa kwa siku tano zinizokuja, sasa ina maana gani? Ukiangalia Bunge letu hapa wengi wetu kama siyo 90% au 99% tumezaliwa baada ya muungano na hii ina maana kubwa sana kwa Taifa letu. Tafsiri yake maana yake ndiyo ukomavu wenyewe wa muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, picha tuliyonayo hapa ndiyo picha ambayo ipo nje ya Bunge hili kwa wananchi. Kwa hiyo, wananchi wengi wamezaliwa baada ya muungano na ndiyo tafsiri ya uimara wa muungano wetu. Wamarekani wana *phrase* moja katika *constitution* yao nitaisoma kwa Kisukuma: *"In order to form a perfect union."* Maana yake nini? Hata baada ya miaka 200 ya Muungano wa Marekani, *they are still perfecting their union*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maana yake nini kwa Mheshimiwa Waziri? Ni kwamba, kazi ya muungano *is a working progress* na wakati mwingine tunapitiwa sana vitu ambavyo ni *very trivial*, vitu vidogovidogo tunavitumia kuhoji misingi ya muungano na ni jambo ambalo kwa Watanzania ninafikiri ni vizuri sana tukajikumbusha kwa hilo na kujipongeza kwamba Muungano huu miaka 62 sasa hivi tukiwa *very strong*, tukiwa imara kama Taifa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kizazi, vijana wetu, ninafikiri Bunge letu 90% ni vijana. Wajue kwamba tunapozungumzia umoja wa Taifa hili na amani ya Taifa hili kifungashio chake ni Muungano. Ninataka nirudie hili inawezekana pengine halijasikika vizuri. Unapozungumzia umoja wa Taifa hili na amani ya Taifa hili, kifungashio chake *(package yake)* ipo ndani ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana katika mambo haya tunapokuwa tunajikumbusha. Mheshimiwa Waziri Muungano ni *working progress*, tusiogope kufikiri *especially* katika

mambo ambayo yanatuimarisha kimuungano, kwa sababu uimara wa kiuchumi ndiyo uimara wa muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo yanaweza yakajitokeza, pengine yapo nje ya yale ambayo ni kati ya kimuungano. Kwa mfano, suala la utalii yawezekana kabisa… na hili nilikuwa ninaliulizia, silizungumzii kinadharia, nilikuwa ninaulizia kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwamba hivi watalii wanapokuja 100 Zanzibar, wangapi wanakuja bara. Ukiangalia katika *ratio* wapo ambao wanakuja ku-*spend* muda Zanzibar baada ya hapo wanakuja safari lakini kuna watu ambao wanakuja safari baada ya hapo wanaenda Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Maana yake kama kuna ujenzi wa *infrastructure* ambazo zinaweza kutupa uimara kwa sababu ndiyo maana ya ku-*leverage* muungano wetu, tufanye tusiogope kwa sababu mambo fulani ambayo tumekubaliana haya hatujakubaliana. Tukae chini tuone kama kuna *infrastructure* au kuna mambo ya kufanya kuimarisha Zanzibar ili tuweze kupata watalii wengi kwa bara, basi tufanye hayo mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili nijikite kwenye mazingira na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwa uzuri sana kwamba mazingira ni nguzo katika nguzo tatu za Dira yetu ya 2050, ni nguzo tatu. Maana yake ukiondoa nguzo moja yale ambayo tunatarajia kuyafikia katika Dira 2050 hatuwezi kuyafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ina maana gani Mheshimiwa Waziri katika Wizara yako? Maana yake Wizara yako inatoa uamuzi au inapelekea kuwa mwamuzi kama Dira hii tutaifikia au hatutaifikia. Sasa yapo mambo ambayo ni ya msingi yamezungumzwa kwa upande wa mazingira na umeyazungumza hapa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo; la kwanza, kuimarisha mazingira yetu na hili ni suala mtambuka. Sasa kuna mengine unaweza ukazungumza kwa upande wako, lakini upimaji wa ardhi ndani ya nchi unalenga katika kulinda mazingira yetu. Kwa hiyo, hili

maana yake ni kwamba Wizara yetu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na Wizara ya Ardhi lazima kuwepo na *proper coordination* kuhakikisha kwamba tunakuwa na upimaji wa matumizi sahihi ya ardhi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu huo ni mwanzo mzuri wa kuhakikisha kwamba tunatunza mazingira yetu. Kuna suala ambalo Mheshimiwa Rais amekuwa akili-*champion* sana la nishati safi na hii ninafikiri kama ni jambo ambalo tutaweza kumkumbuka sana Mheshimiwa Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan kuanzia akiwa bado Makamu wa Rais na sasa hivi akiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la nishati safi pamoja na mambo mengine ambayo ametoka kuya-*champion*. Suala hili ni muhimu sana tukalikazania na ni vizuri tukawa na *focus* kwamba yapo maeneo pengine tuwe na *focus* kama ile ya, ninafikiri kuna mpango wa kaya zile ambazo hazijiwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri katika ku-*target* kwa ajili ya kuhakisha kwamba progamu hii inafanya kazi kukiwa na *focus* ya maeneo fulani fulani. Kuna baadhi ya maeneo yanaweza pengine kuwa na nafuu zaidi kiuchumi, lakini maeneo ambayo yapo *disadvantage* tuwe na *focus* kubwa sana. Ninashukuru katika hili nimekuwa mfaidika, Bariadi Vijijini tumeletewa majiko mengi sana kwa ajili ya nishati safi na wananchi wangu wanafurahia, ninajua kuna awamu nyingine inakuja na kwa hilo ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kulizungumzia kuna suala la *carbon credit*, suala la *carbon credit* ukiangalia nchi yetu kwa maana ya *national park* na mapori tengefu *almost* karibu 32% ya nchi yetu. Kwa maana nyingine kwamba tuna *advantage* kubwa sana kama nchi ku-*leverage* katika hili na Wizara ya Fedha waone kama ni *opportunity* ya ku-*utilize*, kama ni sehemu mojawapo ya ku-*finance* baadhi ya miradi yetu hasa ambayo inahusiana na mazingira.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kadogosa…

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, huyu atakuwa ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa hii nafasi. Kwanza kabisa ninapenda kuipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa inayofanya katika kuhakikisha mazingira ya nchi yetu yanahifadhiwa, lakini pia kwa kusimamia shughuli zote zinazohusu Muungano. Ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninajielekeza kwenye upande wa mazingira. Juhudi kubwa zinafanywa katika kuhifadhi mazingira ya nchi yetu, pia kukabiliana na matatizo ya mabadiliko ya tabianchi. Ninachoomba na kusisitiza hii Taasisi ya *NEMC* ifanyiwe haraka kupewa mamlaka ili iwe nguvu ya kusimamia mazingira na mabadiliko ya tabianchi, iwe na nguvu za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapohapo ninashauri kwamba Mfuko wa Mazingira utafutiwe vyanzo vya uhakika ili kuwe na fedha za uhakika katika kukabiliana na matatizo ya kimazingira na matatizo ya mabadiliko ya tabianchi, tuwe na fungu la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyoona sasa hivi mabadiliko ya tabianchi yanaathiri mambo mengi, yanaathiri miundombinu na yanaharibu rasilimali za nchi hii. Kwenye mabadiliko ya tabianchi lazima twende sambamba na kuhifadhi uoto wa asili. Ukataji wa miti umekuwa ni mkubwa sana na kuharibu uoto wetu wa asili, ambapo huu uoto wa asili tunauhitaji kwa mambo mengi yakiwemo utafiti na mambo ya kujua dawa zetu za asili lazima tuwe na hifadhi ya uoto wa asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali mbaya ya kimazingira inachangia kuharibu nchi yetu kwa misingi kwamba, kwa mfano, maeneo ya Pwani ya Tanzania sasa hivi bahari inakuwa na inakwenda kula nchi kavu, inatoka inapanda, inashuka chini. Yaani inatoka baharini inashuka chini na baadhi ya maeneo tayari yameshaanza kuathiriwa na mabadiliko haya ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mifano duniani, kuna baadhi ya visiwa havipo tena kwenye ramani ya dunia, vimeshafukiwa na bahari. Kwa hivyo, ni lazima tuangalie kwamba tuna Tanzania iliyokamilika pamoja na visiwa vyake vinabaki kuwa urithi wa Taifa hili na tusije tukavipoteza visiwa hivi kutokana na matatizo ya kimazingira, ibaki Tanzania na uhalisia wake kama ilivyoumbwa na Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza kwenye upande wa upandaji miti. Serikali inafanya juhudi kubwa, inatenga fedha nyingi katika upandaji miti, lakini sasa lazima tuhakikishe tunaotesha miti. Kwa sababu kuipanda ni suala lingine na kuiotesha ni suala lingine. Kuiotesha ni kuisimamia ile miti ikakua na ikatoa faida. Ninashauri hapa, ikiwezekana kuwe na mashindano katika vijiji na halmashauri, waliootesha miti ikakua na hapo ukubwa wake na kuihifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili iwe changamoto vijiji vyetu na halmashauri na taasisi nyingine ziwe na ari ya kupanda miti ili Tanzania iwe Tanzania ya Kijani. Ukitua kwenye ndege uone miti *green* badala ya kuona mabati yamepangana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninajielekeza kwenye Muungano. Tumebakisha siku tano tu kutimiza miaka 62 ya Muungano wetu. Ni safari ndefu, tumeanza mbali, tumepitia misukosuko mbalimbali, tumepitia changamoto mbalimbali, lakini bado Tanzania ipo imara, Watanzania wapo imara, Taifa lipo moja lenye upendo, lenye mshikamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu umeasisiwa kwa misingi yake, misingi ya undugu, upendo, mshikamano, maridhiano

na kustahamiliana. Ninawapongeza viongozi wote wa awamu zote kuanzia Waasisi wa Muungano huu hadi kufikia leo kuhakikisha kwamba muungano huu unadumu, Taifa linakuwa moja lenye umoja, juhudi zao, maarifa yao, ustahamilivu wao, viongozi wetu hao ndiyo leo wametufikisha hapa pamoja na sisi Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu ni tunu ya Taifa hili na muungano huu ndiyo unatufanya tuwe na tunu kubwa ya amani na utulivu. Kwa hivyo, kuna kila sababu na kila haja ya kuutetea na kuulinda kwa vitendo muungano wetu ili tuendelee kuwa na tunu hizi za taifa ambazo zinatupa umoja na mshikamano wa kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu ninakubaliana na wazo la Wizara na Kamati hizi. Kuna changamoto kubwa ya Ofisi za Muungano kwa upande wa Zanzibar. Ninaishauri Serikali iendelee kutenga bajeti ili kuweza kujenga zile ofisi za sekta za muungano kwa upande wa pili wa muungano ili kuwe na majengo yenye heshima na yenye hadhi ya sura yenyewe ya muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ukomavu wake, maono yake, kwa kusema kwamba kwa awamu hii au mwaka huu Sherehe za Muungano zisifanyike na badala ya fedha zile kutumika kwa sherehe zikatengeneze miundombinu iliyoharibiwa na mvua kubwa zilizojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko kwa Mheshimiwa Rais wetu ni mapenzi kwa wananchi wake na ni mapenzi kwa nchi yake kuona wananchi hawapati tabu, hawapati changamoto zozote na wanaishi kwa furaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine, ninawapongeza kwamba turejeshe ile ligi ya muungano. Ligi ile vijana wanaipenda na wanaifurahia sana ambayo kwa miaka mingi kombe lile la muungano halikuwepo, sasa hivi linaendelea kufanyiwa kazi na mashindano yanaendelea.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho, wachangiaji wengine wataendelea mchana. Tutakaporudi tutaanza na Mheshimiwa Haji Amour Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Ali Mbarouk na Mheshimiwa Profesa Pius Zebhe Yanda, wengine watatajwa kadri tunavyoendelea.

Tuna matangazo machache, kwanza kuwatambua wageni ambao tunao. Mheshimiwa Waziri Mhandisi Hamad Yusuph Masauni, Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ana wageni wengine hawa ni Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasadizi na Wakuu wa Vitengo kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na taasisi zake.

Pia, kuna viongozi mbalimbali kutoka taasisi zenye nasaba na masuala ya mazingira: Mkuu wa Chuo cha Mazingira *(IEDCS)* na mwingine ni mwakilishi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa *UNDP* na viongozi mbalimbali wa CCM kutoka Zanzibar lakini na Vijana wa *Green Samia*. *(Makofi)*

Vilevile, kuna Madiwani na Masheikh kutoa Wilaya ya Mjini Zanzibar. Pia, ana ndugu mbalimbali na jamaa. Hawa ni wa Mheshimiwa Waziri, wako sehemu mbalimbali wamekaa kwenye jukwaa letu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tangazo lingine ni kwa Waheshimiwa Wabunge, mnakumbushwa kwamba, kwa wale ambao hawajachukuwa mchele, zoezi linaendelea baada ya kikao hiki, kuanzia muda huu.

Baada ya hayo, ninasitisha Bunge mpaka Saa 11.00 jioni.

**21 APRILI, 2026**

*(Saa 7.04 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tunaanza na Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Said Ali Mbarouk, Mheshimiwa Profesa Pius Zebhe Yanda ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Wizara yetu hii, Ofisi ya Rais, Muungano. Kwanza, kabla ya yote ninampongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, kuweza kulijenga Taifa letu hili na kutuletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Balozi Dkt. Nchimbi, akiwa kama ni Mtendaji Mkuu katika Wizara yetu hii, Ofisi ya Rais, Muungano. Tatu, ninampongeza Waziri wetu Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni kwa namna ambavyo anafanya kazi zake hizi za Ofisi ya Rais, Muungano. Tatu, ninawapongeza watendaji wote wa Wizara hii, wakifuatia Makatibu

Wakuu wote, Manaibu Katibu Wakuu, pamoja na kurugenzi zake zote zilizopo katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika mchango wangu, hasa kwa upande wa Muungano. Tukiwa tunajadili Hotuba ya Wizara ya Muungano na Mazingira, ninajikita zaidi kwa upande wa Muungano. Tukija kwenye historia ya Muungano wetu wa Tanzania, sisi Watanzania tunasema kwamba, tumebahatika, tuna Muungano ule wa kimaumbile. Ninasema kwamba, tuna Muungano wa kimaumbile kwa sababu, kabla ya Muungano huu tulikuwa tuna mahusiano ambayo ni ya kidamu, tuna mahusiano ya kibiashara na tuna mahusiano ya mambo mbalimbali kabla ya kuja kwa Muungano wetu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri kuja kwa waasisi wetu wawili, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Rais wa kwanza wa Zanzibar, Amani Abeid Karume, wao wakaanzisha na kuimarisha rasmi Muungano wa Tanzania kwa kuziunganisha nchi mbili, Tanganyika na Zanzibar, kuwa kitu kimoja. Nikasema kwamba, viongozi wetu wawili hawa, wao ndiyo waliokuja kuuimarisha Muungano na nikasema kwamba, wamekuja kuuimarisha Muungano kwa sababu, Muungano wenyewe upo kimaumbile. Sasa wao wakaamua kwa dhamira ya pamoja kwa mujibu wa sera za vyama vyao; Sera ya Chama cha *TANU* pamoja na Sera ya *Afro-Shiraz Party,* kwa umoja wao wakatuunganisha na kwa makubaliano yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hivyo, maana yake kabla ya kuunganisha vile vyama, waliunganika wao kama nchi na bahati nzuri nchi zetu sisi pamoja na kwamba, zimeungana kimaumbile, lakini baadaye nchi zetu hizi zikaja zikaungana kwa mujibu wa *surface* zetu zote mbili kwa kuchukua mchanga wa Tanganyika na mchanga wa Zanzibar na kuuchanganya mahali pamoja. Kitu ambacho wakati mwingine ninawaambia watu, mtu yeyote yule ambaye anataka kuvunja Muungano labda akazibague zile chembe za mchanga, achukue chembe za Zanzibar moja moja, pamoja na zile za Tanzania Bara, upande wa Tanganyika, aseme hizi tayari ninazibagua, kitu ambacho hakitawezekana katu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tuna ile tafsiri ya kuzungumza, kuimarisha Muungano. Katika nadharia yangu ninasema kwamba, katika kizazi chetu hiki tulichonacho sisi hatuimarishi Muungano, tunatakiwa kuboresha Muungano kwa sababu, tayari umeimarika. Kitu ambacho kimeimarika, maana yake husemi sasa unakiimarisha, kitu kilichoimarishwa unasema hiki sasa hivi tunakiboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, sisi sote kwa sasa hivi, maana yake Watanzania, hatuimarishi ila tunaboresha Muungano. Ninazungumza hivyo kwamba, tunaboresha Muungano, siyo kuimarisha kwa sababu, utasikia kuna kitu kinachoitwa changamoto. Kwa kweli, Watanzania sisi hatuna changamoto, *in such*, isipokuwa tuna ule uboreshaji wa Muungano na kila kitu ambacho kina hitilafu, kinatakiwa kuboreshwa na maboresho yetu ndiyo yatakayoweza kutuweka mahali pamoja. Ndugu zangu, viongozi wenzangu, Wabunge wenzangu, Muungano ni Tunu ya Taifa na Muungano ndiyo umoja wetu Watanzania. Hakuna hata mmoja kati yetu sisi atakayesema mimi sitaki Muungano kwa sababu ya faida ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la Muungano lina faida nyingi tu ambazo zipo. Kuna faida za kiuchumi za moja kwa moja, kuna faida za kisiasa na kuna faida za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia suala la kisiasa, maana yake ni kuviunganisha vyama vyetu viwe vya kitaifa na tuwe tunafanya mambo yetu pamoja. Nini maana yake kwenye upande wa kisiasa? Maana yake ni Muungano wetu unaimarika siku hadi siku katika mazingira ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za kiuchumi ni kwamba, tunafanya biashara kwa pamoja na tunatembeleana kila mahali. Suala la fedha, tuna fedha za pamoja na kila kitu chetu kinakuwa ni cha pamoja. Hiyo yote maana yake nikasema katika masuala ya kiuchumi tunatumia sarafu moja, tuna bandari moja na tunakusudia kuwa na mfumo mmoja wa bandari, *TRA* na mambo mengine

maana ni ya pamoja. Ni kitu ambacho kinaweza kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia suala la Muungano, nije kidogo katika suala la Mfuko wa Jimbo kwa upande wa Zanzibar. Kwa upande wa Zanzibar, Wizara hii ya Muungano na Mazingira ndiyo ambayo *answerable* kwa Mfuko ule wa Jimbo. Tumekaa vikao karibu viwili, kati yetu sisi na Viongozi wa Wizara, kwa ajili ya kujadili suala la Mfuko wa Jimbo. Ninashauri tu kwamba, katika Mfuko wa Jimbo yapo mapungufu katika ule Mfuko na hii Wizara maana yake ndiyo ambayo inatakiwa kutusimamia sisi kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ambayo imekuwepo ni kwamba, zile fedha zina mlolongo mkubwa sana mpaka sisi Wabunge kuweza kuzipata. Sasa ni vyema tubadilishe ile Sheria ya Mfuko wa Jimbo, tupunguze ule mlolongo, pamoja na kwamba kule kuna waratibu, lakini ni vyema, wakaratibu wenyewe kama ni jukumu lao mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na huo Mfuko wa Jimbo kuwepo, pia ninaishauri Wizara kwamba, kwa wakati ambao tumefika kwa sasa hivi kule Zanzibar, ni vizuri zaidi tukajenga ofisi ambayo itakuwa inajumuisha shughuli zetu zote za Kimuungano zitakazosimamia masuala ya uratibu na mengine, ambayo yatakuwa kule Zanzibar, ili kurahisisha hii milolongo yote ambayo imekuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, ninamwangalia Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuniangalia sana, ninaunga mkono hoja. Ninasema ahsante sana na ninaipongeza sana Wizara kwa kazi nzuri na hotuba yao nzuri, ambayo wameileta hapa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, wachangiaji bado tunao wengi tutakwenda kwa dakika nane nane.

Tunaendelea na Mheshimiwa Said Ali Mbarouk na Mheshimiwa Profesa Pius Zebhe Yanda ajiandae.

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya ya kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza ndugu yangu, Mheshimiwa Waziri, ametuletea hotuba ya bajeti yake. Ninaomba nianze kwa kusema kwamba, tunaambiwa muasisi wa Muungano wetu, Baba wa Taifa, Hayati Nyerere, alikuwa tayari kuahirisha uhuru wa Tanganyika mpaka majirani zake wapate uhuru kwa pamoja, ili kuunda Jumuiya ya Afrika ya Mashariki yenye nguvu *(Federation of East African Countries)*. Hilo lilikuwa jambo zuri sana, lakini kwa sababu, halikuwa, sisi wa Zanzibar Mzee wetu, Mzee Karume akaamua tuanze na pengine wenzetu wangeweza kuiga. Bahati mbaya miaka 62 sasa hakuna hata nchi moja miongoni mwa jirani zetu aliyeraghbika kujiunga nasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri tujitahidi, kama waasisi wa Muungano, tuwashawishi, ili waweze kujiunga nasi kwa sababu, umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Wenzetu wa Jumuiya ya Ulaya Mwaka 1958 walianza na nchi sita, baadaye wakaanzisha *European Union,* sasa wana nchi 27. Sisi Muungano wetu wa nchi mbili wa miaka 62, wao miaka 68 tayari ziko nchi 27. Sasa huko ndiyo kufanikiwa kwa Muungano, unaanza na kidogo, lakini baadaye wengine wanaiga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninashauri kwamba, jitihada zifanywe na wenzetu watuige, wa-*join* katika Muungano huu; wenzetu wa Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Congo, Malawi, Zambia, Msumbiji, Shelisheli na Comoro, tungekuwa na Muungano mmoja mkubwa na wenye nguvu sana. Kwa hiyo, hatujachelewa, jitihada zifanyike za kibalozi, ili kuona kwamba, tuna Muungano wa nchi hizi, lakini hatuwezi kufika hapo kwanza mpaka Muungano ambao tunao mafanikio yake yawe yanavutia wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Jumuiya ya Ulaya, nchi zile 27 zilijiunga kwa sababu, waliona mafanikio makubwa ya zile nchi sita zilizoanzisha. Kwa hiyo, na sisi tujitahidi kuleta mafanikio makubwa ya kiuchumi ndani ya nchi hizi mbili, ili tuweze kufika hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea na Mheshimiwa Waziri, amezungumza suala la Kero za Muungano. *Paragraph* ya 28 naona; zilikuwa 25, tayari 22 zimefanyiwa kazi, bado tatu, lakini kwa maoni yangu hizo tatu ndiyo wazee wa kero na hatuwezi kuendelea kuwa na Muungano huu tukiwa na kero za miaka mingi sana, zitazaa mgogoro na mgogoro ni hatari katika umoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii ambayo amesema Waziri, suala la mgawanyo wa mapato yaliyokuwa hisa za Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki. Hii kuanzia mwaka 1965 mpaka leo ni zaidi ya miaka 60, sisi Zanzibar nchi hii tuna uchumi mdogo, tungetegemea mapato haya yatusaidie sana kuendesha bajeti ya Serikali, lakini miaka 60 hisa, mapato, aah!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, hii inasikitisha na ninadhani hili linahitaji tuambiwe Serikali ina mpango gani? Maana hii lugha aliyotumia Waziri mimi si ya kwanza kuisikia, kwamba, bado tunaendelea na tupo mbioni, tutakamilisha! Hii si ya kwanza kumsikia Mheshimiwa Yussuf Masauni, kuna Mawaziri wengine wa Muungano, lugha hii hii tumeweza kuisikia. Sasa ninahisi hili, sisi wa Zanzibar, linatuumiza kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni lile ambalo, ninamshukuru sana Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, alituongoza kwa muda wa miaka 21. Mwaka wa 20 kabla ya kung'atuka, katika Katiba, alifanya usia kwa maana ya kwamba, alianzisha Kifungu cha Katiba cha Kugawanya Mapato ya Muungano, Mfuko wa Pamoja, Akaunti ya Pamoja ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1984 sasa ni miaka 42, Serikali zilizofuata zimeshindwa kutekeleza hili! Sasa Baba wa Taifa tunahitaji kumuenzi kwa vitendo. Mzee alikuwa na nia njema kwa sababu, anajua mambo ya fedha, mambo ya mapato katika umoja yana

mitihani yake, ndiyo maana akaanzisha Kikatiba. Ndani ya Katiba ya Muungano, kifungu hiki ili wanavyoacha madaraka, wanaofuata waweze kuendeleza ili twende na Muungano wetu.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa Mheshimiwa Said Ali. Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge anazungumzia mambo yanayohusu mapato na fedha. Anasema miaka 41 Serikali imeshindwa kupeleka fedha, lakini ni vizuri angetueleza miaka ya awamu ya ngapi, awamu ya ngapi! Mwaka fulani hazikwenda, mwaka fulani hazikwenda! Anapozungumza kwa ujumla hivyo, anaweza kuwa anapotosha mapato halisi yanayokwenda kule kwa sababu, hana uhakika na hayo mapato. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Said Ali, unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei. Ninachosema ni mzee wetu alianzisha Kikatiba kifungu cha kuanzisha Akaunti ya Pamoja ya Mapato. Tokea mwaka 1984 leo ni mwaka 2026, miaka 42 kifungu hiki hakijatekelezwa, ndiyo ninachozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo sisi Zanzibar tuna imani, tuna dhana, tuna maoni kwamba, tunakosa mapato mengi ya kuendesha nchi. Kwa hiyo, ninashukuru Mheshimiwa Waziri amesema suala hili linatekelezwa, lini? Tubaki tu kusubiri tena miaka mingapi mingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali inaendelea kuzungumza, nina hakika mwakani Mheshimiwa Waziri atakuja na maelezo kama hayo. Kwangu ninaomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kwa mwaka huu wa fedha, masuala haya yanayohusu mapato ya Zanzibar amekusudia kuyatekeleza lini na kwa kiasi gani cha fedha? Atuambie shilingi ngapi za fedha amezitenga katika bajeti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala limalizwe kwa sababu, linatuathiri sana kwa maslahi ya upande wa pili wa Muungano.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Said Ali. Kwa hiyo, hujaunga mkono hoja?

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaunga mkono mpaka nisikie majibu ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Ungeunga mkono halafu ungepata majibu mazuri. *(Kicheko)*

Tunaendelea. Mheshimiwa Profesa Pius Zebhe Yanda, Mheshimiwa Asha Hussein Saleh ajiandae.

**MHE. PIUS Z. YANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Nitajikita zaidi kwenye upande wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nianze kwa kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mwanamazingira namba moja, hilo linaonekana wazi kwa kuwepo kwa Dira ya 2050. Kama haitoshi nguzo namba tatu ni nguzo mahsusi kwa ajili ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, haya ni maono yake yaliyowezesha kuwa na nguzo ambayo ipo *dedicated* kwa ajili ya mabadiliko ya tabianchi na mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo pia linaonekana wazi kwamba, hiyo ni nguzo muhimu kwa sababu jambo lolote lile linalofanyika kama ni la kimaendeleo kwa vyovyote vile ni lazima kuwe na *checks and balances* ambayo ni masuala ya mazingira kuhakikisha tuna maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekti, ninaomba pia niipongeze Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi kubwa ambayo inaifanya kuhakikisha kwamba misingi ya usimamizi bora wa mazingira inawekwa sawa. Ofisi imeandaa miongozo mbalimbali ambayo inasaidia usimamizi

wa mazingira. Pia ninaomba kwa namna ya pekee nimpongeze Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni kwa hotuba nzuri ambayo inaakisi Dira ya 2050 na ni mwanzo mzuri katika juhudi za kuweza kutekeleza nguzo Namba Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaomba pia nirejee kwa nini mazingira ni muhimu. Uhifadhi wa Mazingira ni msingi wa ustawi wa Watanzania wote, tukumbuke kwamba inabidi tutembee kwenye kauli mbiu inayosema tunza mazingira, yakutunze. Hilo ni muhimu na lazima tukumbuke pia kwamba mazingira tumeyarithi kwa mababu na mabibi zetu, sisi ni wasimamizi tu, kwa lugha ya Kiha tunaita *custodians* lakini kesho na keshokutwa ni lazima vizazi vijavyo viweze kutumia mazingira kama yalivyo kwa ajili ya maisha yao. Kwa hiyo, tunao wajibu wa kuhakikisha kwamba mazingira yanasimamiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikirudi kwenye uharibifu wa mazingira. Tunashuhudia mfumo wa mvua unabadilika, tunaona mafuriko zaidi, tunaona ukame, lakini pia tunaona mmomonyoko wa udongo na mambo mengine yote, hayo yote ni matokeo ya uharibifu wa mazingira katika ngazi mbili. Kwenye ngazi moja tunazungumzia mabadiliko ya tabianchi ambayo binadamu wametoa mchango mkubwa sana na ndiyo maana tunaathirika na athari tunazoziona sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yanayotuzunguka na shughuli zetu tumetoa mchango mkubwa sana katika matatizo tunayoyaona sasa hivi, tumezungumzia suala la uharibifu wa Barabara, kwa nini tuna mafuriko makubwa sasa hivi ukilinganisha na siku za nyuma, kwa nini tunaona vyanzo vya mito vinaanza kukauka hasa wakati wa kiangazi. Hayo ni mambo ambayo inabidi tuweze kujiuliza na bahati nzuri sisi wenyewe tunayo majibu kwa sababu ndiyo tumechangia katika hayo matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kusema hayo ninaomba niseme jambo moja kwamba, pamoja na juhudi ambazo zimefanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais, katika kuandaa mikakati, kuandaa mipango, miradi na hata kuweze kutafuta fedha za

kutosha kutoka kwa wafadhili, lakini bado inaonekana wazi kwamba hili tatizo ni kubwa. Hiyo imedhihirika wazi kwenye hotuba ya Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais wakati anawasilisha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo ambalo lipo wazi ni suala la uratibu, kwamba ni kweli tunajua sekta mbalimbali, Wizara mbalimbali zimeweza kuhuisha masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Kwenye upande wa sera na upande wa mipango na mikakati kila kitu kinaonekana vizuri lakini uhalisia ni kwamba utekelezaji hauko sawa. Sasa tujihoji kwa nini haya yanaendelea hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta sasa kila sekta inafanya mambo yake kwa lugha ya wenzetu tunaita *in silos*, kila Wizara inafanya mambo yake, tunasahau yale ambayo tumesema tutatekeleza kwa kadri ya miongozo inayotoka Ofisi ya Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inakuja kutuletea jambo moja kwamba sasa kunahitaji kuwe na ufuatiliaji wa karibu, tuone *compliance* wa kila sekta kuhakikisha kwamba mazingira ni *part and parcel* ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika nchi hii. Tunalifanyaje, hili ni jambo ambalo tunahitaji tujadiliane, jambo la msingi zaidi ni kule chini ambako tunafanya utekelezaji, tuhakikishe kwamba kuna mikakati mahsusi kila utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa wananchi tuweze kuzingatia suala la usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika, kila sekta ina *component* ya usimamizi wa mazingira, kwa nini tusiwe na *coordinated efforts*, uratibu wa karibu kwenye ngazi za Halmashauri ili kwamba hizi nguvu zote ziweze kuwekwa kwa pamoja. Tuangalie kwamba pia isije ikawa utekelezaji wa shughuli za sekta moja unaathiri sekta nyingine au unaishia kuathiri mazingira. Kwa hiyo, hayo yote yangeweza kuchujwa kwenye *planning level* kwenye ngazi ya wilaya ninafikiri haya yote tunaweza tukayatatua, kwa sababu kwenye ngazi ya kitaifa sera zipo, miongozo ipo, sasa ni nini kinaleta shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Ofisi ya Makamu wa Rais ni tufanye kazi ya ziada, tuone ni jinsi gani kuwe na *vertical coordination* pia na *horizontal coordination*. Nikimaanisha turatibu juu lakini tuweze kuwa na uratibu wa kutoka juu kwenda chini mpaka kwenye *level* ya halmashauri. Tukiweza kufanya hivyo nina uhakika tutaweza kupunguza au kujitahidi kupunguza hizi athari tunazoziona sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Asha Hussein Saleh na Mheshimiwa Mwinyi Jamal Ramadhan ajiandae.

**MHE. ASHA HUSSEIN SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi jioni hii ya leo kuweza kuchangia Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwanza kabisa ninapenda kumpongeza Rais Samia, pamoja na Rais Mwinyi kwa kazi zao nzuri wanazofanya hakika mwenye macho haambiwi tazama. Ninapenda pia kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyotuletea hapa leo yenye manufaa mazima ya mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie mambo matatu katika ofisi hii. Jambo la kwanza nitachangia katika sehemu ya Muungano, jambo la pili nitachangia mazingira na uchumi wa buluu na jambo la tatu nitachangia katika Mfuko wa Jimbo. Ni dhahiri kabisa ofisi hii ni ya kupongezwa katika suala la Muungano kama Waziri alivyosema kwamba ametatua hoja 22 katika hoja 25, jambo hili siyo dogo, ni la kupongezwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anastahiki kupongezwa zaidi kwa kazi kubwa alizozifanya kwani ameweza upeleka gawio katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar linalofikia shilingi bilioni 48.5. Gawio hili likijumuisha *PAYE*, likujumuisha misaada kutoka nje na gawio la Benki Kuu *(BOT)*. Kwa kweli asilimia 48.5 hili ni jambo la kupongezwa kabisa kwa kuwasilishwa katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapohapo katika suala la Muungano. Vizazi vyetu vinavyokuja kusema kweli watakuwa wanaelewa Muungano, lakini hawatoelewa zaidi. Ni vema kama mwenzangu alivyosema ni kusomeshwa katika ule upande wa Zanzibar, sijui kwa upande wa Bara kama lipo katika *syllabus* suala la kusomeshwa Muungano, lakini kwa Zanzibar ni bora nalo likaingizwa sehemu ya Muungano ili vizazi vinavyokuja wakauelewa Muungano wetu na wakaweza kuudumisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi kwa Waziri la kuanzisha haya matamasha au makongamano ili wananchi watakapokwenda kutembelea katika yale maeneo ya maonesho, wananchi wakienda kutembelea katika yale maonesho wakiona kazi zilizofanywa za Muungano na zinazoendelea, basi tutadumisha huu Muungano na wananchi watazidi kuupenda Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nijielekeze Mheshimiwa Waziri amesema kwamba ametatua hoja 22 na zimebaki hoja tatu, basi aendelee na watendaji wake kufanya hili jambo zuri ili kuweza kumaliza hizi hoja tatu zilizobaki ikiwemo hii hoja ya kikatiba iliyokuwepo ya Mfuko wa Pamoja wa Fedha. Kwa hiyo atumie busara zake, hekima zake ili aweze kutatua pia hoja hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo kwenye suala la Muungano sasa nijielekeze katika suala la mazingira na uchumi wa buluu. Kwa upande wangu katika Jimbo langu, basi nimwombe Makamu wa Rais aweze kutembelea katika Jimbo la Fuoni ili aweze kujionea hali ya mazingira katika Bonde la Dangamizini, pamoja na kutembelea eneo la Fuoni Kibondeni akawaona wajasiriamali au wavuvi wadogowadogo wanaojikwamua kiuchumi, wanaokwenda kule baharini kwenda kuvua kaa, akawaona jinsi gani shida zao na tabu zao wanazozipata katika kujikwamua kiuchumi ili kuwapatia mafunzo, kuweza kuwapatia vifaa pia vya uvuvi pamoja na kuwapatia boti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze katika Mfuko wa Jimbo. Kama mwenzangu pale Mheshimiwa Haji alivyosema basi nimwombe tu Mheshimiwa Waziri kwa makusudi mazima kama hali hii

ya Mfuko wa Jimbo na shida hizi zinazotukuta Wabunge katika huu Mfuko wa Jimbo, basi kwa busara zake na hekima zake, bora atuletee hapa tuje turekebishe au vifungu vya sheria vilivyopo turekebishe ili viweze kukaa sawa, nasi tuweze kwenda na wakati katika huu Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwinyi Jamal Ramadhan.

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni ya leo kwa kupata nafasi hii kuzungumza. Pili, nichukue nafasi kuwashukuru viongozi wote wa kitaifa akiwemo Mwenyekiti wa Chama changu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Dkt. Emmanuel Nchimbi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Mwigulu Nchemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mara ya kwanza ninachangia, pia ninashukuru viongozi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja wa Chama changu Cha Mapinduzi Wilaya pamoja na wananchi wote wa Jimbo la Bumbwini kwa kunipa ushirikiano, kwa kunipa nafasi hii ili kuja kuwatetea wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Waziri kwa kuanza vizuri katika bajeti muhimu sana ya nchi yetu, yenye uti wa mgongo wenye maslahi ya Taifa letu, yenye msingi wa dira yetu, yenye umoja, mshikamano na ari kubwa ya maendeleo yetu. Tukiwa tuna miaka 62 sasa ya Mapinduzi yapo mambo yamefanyika, tunayapongeza yale yaliyofanyika mazuri, lakini kuna mambo mawili, matatu tunaomba Waziri ayatazame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kule kwetu Zanzibar tuna kituo cha bahari kuu cha uvuvi ambacho kimejengwa Fumba. Kile kituo kwa sasa hakionekani kama kinawasaidia sana Wazanzibari kwa sababu kimekosa taaluma na Wanzibari kujua nini umuhimu wake kabisa. Sasa tunamwomba Waziri katika hilo aangalie sana ili kuweza kupata maslahi wananchi na kujua na taaluma ielekezwe zaidi ili kuweza kupata manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kwa sababu tunaelekea katika uchumi wa buluu *(blue economy)*. Waziri katika bajeti yake mwaka huu kaona, imekuja katika mwaka wa kwanza huu tunaona vizuri sana, tuipongeze Serikali kwa kuliona hili jambo muhimu sana. Wananchi wa kwenye maeneo matatu haya ni mambo muhimu, kwanza hiyo *blue economy* tukiitizama hasa katika ile tunazungumza kwenye Kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiitizama kaboni ya buluu inayotokana na Bahari, hilo ni jambo muhimu sana na ukitizama kwenye mitandao unaona hasa jambo hili lina thamani kubwa na linaingiza fedha nyingi katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu tuna Muungano na Zanzibar tumejaaliwa kabisa kutumia bahari ipasavyo vizuri sana, sasa tunaona akija Waziri hebu atuambie kati ya kuanzisha hili suala la biashara ya kaboni na Zanzibar kwa sababu tuna Wizara ya Mazingira ushirikiano kati Bara na Zanzibar upoje, katoa mchango upi na Zanzibar inanufaika vipi na ushirikiano upoje. Mheshimiwa Waziri akija atuambie ili tuone, tujue kwamba sasa tunakwenda vizuri katika kuutekeleza Muungano wetu na maslahi yanapatikana kwa wananchi wote wa pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, tunapozungumzia Muungano wa miaka 62. Muungano huu sote tukiuzungumzia tunajua na kila mmoja aliyesimama hapa anatoa historia, lakini tumpongeze Waziri pale alipokuja na hoja kwamba sasa tunaenda kujenga kituo ambacho kitatuelezea historia yetu na makumbusho ya Muungano. Mheshimiwa Waziri jambo hilo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaulizana kule ukienda sasa, watu wetu wakienda pale Kisonge pana mnara wa kumbukumbu ya Mapinduzi, lakini Muungano wetu mzuri na sifa nzuri tunazozitaja hakuna kituo kinachoainisha, hicho kituo kikiwepo kitatusaidia sana na kitakuza utalii, watalii wetu watakuja kusoma historia ya nchi yetu ilivyo tutaondoka na hilo deni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumuunge mkono Rais wetu Samia wa Jamhuri ya Muungano, hiki kituo kikijengwa akiwa anaongoza yeye katika huu utawala kitaleta tija sana na fahari kwetu. Mheshimiwa Waziri anapaswa alisimamie jambo hili na kuhakikisha tukija bajeti ya mwakani, basi atuambie tumefikia wapi na kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni elimu kwenye Mazingira. Mazingira tunayapigia mfano, sote tunahitaji mazingira, uhai wetu sisi ni mazingira, lakini bado katika eneo hili hatujafanya vizuri. Sasa tunaomba Waziri aone mkazo katika hili eneo tuweze kufika mahali. Kwa nini, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika siku ya kuazimisha sherehe yake ya kuzaliwa anakwenda anaonekana kwa dhahiri kabisa ameelekeza suala hili la kupanda miti, lakini hii Serikali kuna Wizara nyingine inatoa vibali vya kukata miti na huku tuna mipango ya kuanzisha biashara ya kaboni. Tunaomba walitizame hili jambo, Wizara hizi zikae zijue asili, tujue hii tofauti iko wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo ni la muhimu sana, tunapoangalia mazingira tunayaangalia vipi, yapo mazingira yanachafuka, lakini kwenye eneo la kuweka sana rasilimali za fedha hasa kwenye suala la madini, eneo hili tuwekee sheria maalum na tupate tozo ambazo zinatoka kwenye madini kwenda moja kwa moja kwenye Wizara ya Mazingira kama ni faini kati ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo tumeliona na Waziri amelitaja lakini Mwenyekiti wa Kamati amelitaja ni kuhusu suala na *NEMC*, hebu hii *NEMC* sasa tumalize hili tatizo, tumwombe Waziri aje na sheria sasa tumalize ili tuipe meno hii taasisi iweze

kufanya vizuri ili mambo yetu yaende vizuri kabisa, tufike mahali sasa tumalize tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la elimu kwenye mazingira, tunasema huko zamani wazazi wetu, wazee na shuleni kwetu mazingira yalikuwa yakifundishwa. Sasa kwenye eneo hili kwenye elimu haliko vizuri, tutafute njia sasa kuona sasa mtaala wa kufundisha mazingira ili nchi yetu ifike salama baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, ninaipongeza sana bajeti yake. Mimi kwa niaba ya wananchi wa Bumbwini ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwinyi Jamal Ramadhan. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. George Venance Lugomela na Mheshimiwa Asya Sharif Omar, ajiandae.

**MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa hii fursa ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii muhimu ambayo tuko nayo hapa. Kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuleta maendeleo ya nchi hii. Tunafahamu kwamba Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiye mwanamazingira namba moja; na ameendelea kutoa miongozo ya usimamizi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kupanda miti siku ya *birthday* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Makamu wa Rais Dkt. Emmanuel John Nchimbi, tunafahamu kwamba ndiye mkuu wa ofisi hii ya hoja tunayoijadili leo. Kwa hiyo miongozo yake pamoja na maelekezo yake pia yamo kwenye hoja ambayo tunaijadili leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nimpongeze Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa kazi kubwa anayoifanya. Waziri Mkuu ndiye kiongozi wa shughuli za kila siku za Serikali, kwa hiyo maana yake ni kwamba, hata tunayojadili kwenye hoja ya leo pia Waziri Mkuu ana maelekezo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Waziri wa sekta hii Mheshimiwa Hamad Masauni kwa hotuba aliyoiwasilisha hapa na kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuhakikisha kwamba mazingira yanatunzwa, lakini pia Muungano unalindwa. Nimpongeze pia Naibu Waziri wa sekta hii, Mheshimiwa Reuben Kwagilwa kwa kazi kubwa anayoifanya kumsaidia Mheshimiwa Waziri. Niwapongeze pia watendaji wote, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu wawili, Wakurugenzi pamoja na watendaji wote katika sekta hii ya Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajielekeza zaidi katika sekta ya mazingira. Sekta ya mazingira ni pana, lakini pia sekta hii ni changa. Kwa maana ya kwamba ni kuanzia katikati ya miaka ya 90 ndipo mazingira yameanza kutiliwa mkazo. Maana yake ni kwamba kazi kubwa imefanyika. Sheria ya mazingira ilikuja 2004, kazi kubwa imefanyika; lakini bado kuna mambo mengi kwa sababu tunashuhudia uharibifu wa mazingira na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzijuzi tumeona maporomoko yaliyotokea kule Kyela, lakini miaka kadhaa iliyopita tuliona maporomoko yaliyotokea kule Manyara. Ukiangalia vizuri utaona kwamba haya pia pamoja na mabadiliko ya tabianchi lakini yana uhusiano na mazingira, ukataji wa miti na uondoshaji wa uoto wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza mchango wangu katika eneo la mazingira. Changamoto kubwa ninayoiona katika sekta hii ya mazingira, hatujaweza kuwa na vyanzo vya kutosha vya mapato kuwezesha sekta hii isimamiwe vizuri. Ukiangalia idara ya mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, fedha nyingi inazotegemea kwa ajili ya kuendesha shughuli zake za maendeleo ni kutoka kwa wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na changamoto ya sera za wafadhili kubadilika, wakati mwingine kuchelewa kutolewa kwa fedha hizi baadhi ya miradi haitekelezwi; kwenye taarifa ya Kamati hilo limebainishwa. Kwa hiyo maana yake tunahitaji kufikiria namna ya kuongeza mapato katika sekta hii ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kuwa Baraza la Usimamizi wa Mazingira linajiendesha kwa tozo na faini mbalimbali ambazo linatoza katika kutekeleza shughuli zake; lakini bado hela inayopatikana haitoshi kuendesha shughuli za mazingira kwa upana wake na ukubwa wa tatizo hili. Kwa hiyo, ninaomba nipendekeze maeneo machache ambayo tunaweza tukayatilia mkazo na kuweza kupata fedha kwa ajili ya kusimamia shughuli za mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mfuko wa Mazingira *Environmental Trust Fund;* lakini Mfuko huu bado vyanzo vyake vya mapato ni vidogo na haviwezi kukidhi haja ya usimamizi wa shughuli za mazingira hapa nchini. Kwa hiyo, ninashauri tuongeze wigo wa tozo kama vyanzo vya mapato kwa ajili ya Mfuko wa Mazingira na fedha zinazopatikana zitumike kwa ajili ya usimamizi wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wachafuzi wengi wanaochafua mazingira yetu. Imeelezwa hapa habari ya migodi, lakini pia vipo viwanda ambavyo vinachafua mazingira. Kuna baadhi ya viwanda vina mitambo ya kutibu majitaka lakini vingine havina. Maana yake ni kwamba, wanatiririsha majitaka kwenye mazingira. Ninafahamu kwamba *NEMC* wamekuwa wakitoza tozo kwenye maeneo haya, lakini viwanda vingi havijafikiwa na migodi mingi bado inatiririsha majitaka na maeneo mengine hatuwezi kuyafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NEMC* inashindwa kuwafikia kwa sababu, *NEMC* iko kwenye kanda peke yake, haiko kwenye mikoa na wala haiko kwenye wilaya. Kwa hiyo, wanashindwa kuweza kuwa mahali ambapo matatizo haya yametokea. Wanaweza kuwakamata wachache lakini wengi wanachoropoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili tunayo ile kanuni inasema *polluter pays principle,* mchafuzi lazima alipe. Ninashauri *NEMC* isimamie hili na fedha inayopatikana sehemu yake iende kwenye Mfuko wa Mazingira ili kuwezesha fedha kwa ajili ya usimamzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo eneo ya uchumi wa kijani *(green economy)*, hili ni eneo ambalo tukiliboresha makampuni yanaweza yakawekeza katika kufanya uchumi wetu uwe wa kijani. Kwa hiyo, takataka zile tuanazokusanya nyingi zinaweza zikabadilishwa kuwa nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo miongozo isimamiwe vizuri ili tuweze kuwa na kampuni nyingi ambazo zinaweza kugeuza taka kuwa nishati au tunaita urejelezaji wa taka katika maeneo mbalimbali na hivyo taka zile zisiweze kuchafua mazingira yetu. Vilevile kampuni zile zinaweza kutoa ajira pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo pia eneo la biashara ya kaboni. Biashara ya kaboni inazidi kukuwa duniani na nchi yetu bado haijaweza kutumia fursa ya biashara ya kaboni vizuri; kwa maana ya *carbon credit*. Tunayo misitu mingi katika maeneo mbalimbali nchini ambayo inafyonza ile hewa ya ukaa; na kwa mujibu wa makubaliano tunaweza tukapata fedha kwa ajili ya kutunza ile misitu. Fedha zile zikipatikana zitatoa motisha kwa wananchi wetu ili wasiharibu misitu kwa sababu wanajua kwamba wanapata kipato kwa kutunza misitu. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo litiliwe mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwamba kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeona kwamba amelitaja hili. Sambamba na hilo, kile kituo cha kuratibu biashara ya kaboni, *National Carbon Monitoring Centre,* tunaomba kiimarishwe ili kiweze kuratibu biashara hii pamoja na kutoa elimu kwa wananchi na taasisi mbalimbali kuhusu fursa ambazo tunaweza kuzipata katika biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika biashara ya kaboni siyo misitu peke yake. Tunafahamu kwamba nishati safi inapunguza hewa ya

ukaa ambayo ndiyo kaboni yenyewe. Maana yake ni kwamba, juhudi anazozifanya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuhakikisha kwamba tunatumia nishati safi maana yake ni kwamba, tunaweza tukapata fedha kutoka kwenye Mifuko ya Mabadiliko ya Tabianchi kwa kupunguza hiyo hewa ya ukaa. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo linahitaji kutiliwa mkazo ili tuweze kuongeza mapato kwenye...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho dakika moja tu, ninaomba niongee kwamba, elimu kwenye jamii inabidi itiliwe mkazo ili kuweza kudhibiti mazingira yetu vizuri. Kwa sababu wananchi wakielewa maana yake ni kwamba watatekeleza sheria bila shuruti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mheshimiwa Martha Festo Mariki, ajiandae.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, na mimi ninakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira; ninakushukuru sana. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo nikaweza kusimama hapa katika Bunge letu hili Tukufu la Kumi na Tatu, ninashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nianze kwanza kwa pongezi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nimpongeze kwa namna anavyoendelea kutuongoza wananchi wake, lakini kwa namna anavyoendelea kutambulika katika nchi yetu kitaifa na kimataifa duniani. Hongera sana kwa Mama Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza pia Makamu wetu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, lakini pia nimpongeze sana Waziri wetu Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba, tunampongeza sana. Kwa kweli Waziri Mkuu anatutia moyo na anatutia nguvu kwa namna anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu. Hili ni fundisho, kwamba na sisi wasaidizi wake tukaze buti na tunamwahidi tutaendelea kuunga mkono jitihada hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mwenyekiti wangu wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania, Mama Mary Chatanda. Nina kila sababu ya kumshukuru kwa sababu amenilea vizuri, ametufunza vizuri wanawake leo tumeweza kusimama hapa kuweza kuchangia hotuba hii ya bajeti. Ni upendo wa kutulea vizuri wanawake sisi, tukaweza kuisemea mema Serikali yetu kwa sababu ya inayoyafanya na hatubahatishi. Tunachangia hotuba hii ya bajeti kutokana ana kazi nzuri za Mheshimiwa Dkt. Samia. Ni lazima wanawake tuwe mstari wa mbele na tutaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri wangu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Waziri Hamad Masauni. Waziri Masauni ni msikivu na ni mwelewa. Mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, anatuongoza vizuri sana, tunakwenda naye vizuri kwenye hii Wizara. Amekuwa akichangia vizuri katika kuwasilisha hoja zake na sisi tumeweza kuzichangia vizuri kuisaidia Serikali yetu. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na *insha Allah* Mwenyezi Mungu atamsaidia kwenye hili la kumsaidia Mama Samia. Anachokifanya ni haki yake kwa sababu anaitumikia nchi yake kwa utii, naye Mwenyezi Mungu atamsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mchango wangu utakuwa na mambo mawili. Moja, suala la Muungano, lakini la pili suala la nishati safi na salama. Nianze mchango wangu kwenye jambo la nishati safi na salama. Nichukue nafasi hii nimpongeze sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara, lakini balozi namba moja kwa kutunza mazingira, lakini kwa kuongoza vizuri nishati safi na salama nchini. Dkt. Samia amekuwa wa mfano kwenye jambo hili na ndiyo maana sisi Wajumbe wa Kamati tumepata nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba, kutokana na nguvu zake zile za kuhakikisha kwamba nishati safi na salama inatumika kwenye nchi yetu, leo wamekwenda kufaidika mama lishe na baba lishe kwenye nchi yetu hii. Wajasiriamali walio wengi tayari wamenufaika na nishati safi na salama, wameweza kujinyanyua katika hali zao za kiuchumi kutoka walipokuwa na sasa walipo; tunamshukru sana Mheshimiwa Rais. Kwa kweli, Mheshimiwa Rais anatuwakilisha vyema na anatuendesha vyema kwenye nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema, kwamba nishati safi na salama kwenye nchi ni jambo muhimu. Tutaendelea kusema, kwamba ni mahali petu wananchi, sote tuunge mkono jitihada hizi za Mheshimiwa Rais na jitihada za Waziri wetu anazozifanya katika Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajasiriamali wengi, wakiwemo wanawake walikuwa na afya mgogoro kwa kutokutumia nishati safi na salama, lakini Mama Samia amekuwa mkombozi, leo akina mama wanauza biashara wakiwa wanang'ara, wanameremeta unaona raha kununua chakula chao. Hii ni jitihada ya Dkt. Samia, amemwezesha mwanamke wa Kitanzania, amemwezesha kijana wa Tanzania kufanya biashara zake katika hali ya afya njema na hali ya usafi. Ahsante Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuwa rahisi, watu walikuwa wakitumia matumzi ya kuni, ndipo aje afanye biashara zake. Vilevile wanawake wenzetu walikuwa wakikaa kwenye foleni hospitali kutokana na kuharibika macho; leo Mama Samia amekwenda kuwajengea uwezo, akawatoa walikokuwa. Tunamshukuru Dkt. Samia na wala hatuchoki, hatuchoki kumshukuru kwa mazuri na mema anayoendelea kutufanyia wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, kabla sijatoa ushauri wangu kwa Serikali, ninaomba nilizungumzie jambo la Muungano. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa zile kero ambazo ameweza kuziondosha, zimebaki chache, tatu tu. Niseme kwamba, hakuna jambo rahisi, hata nyumbani kwako huyamalizi yote kwa

wakati mmoja, itakuwa jambo la nchi? Tutaendelea kuulinda Muungano wetu, tutaendelea kuutetea Muungano wetu kwa gharama yoyote kwa bei yoyote hauvunjiki, na tuna kila sababu ya kusema hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waende Kariakoo Dar es Salaam, tunaongoza Wazanzibari kwa biashara, tume-*invest*, halafu ndiyo unitoe kwenye Muungano? Haiwezekani! Muungano tutaendelea kuulinda kwa sababu ni tunu yetu tuliyoachiwa na wazee wetu wa CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kutoa ushauri kwa Serikali yangu sikivu na Tukufu. Tuna *VETA* kila wilaya katika nchi yetu. Sasa, kama itapendeza kwa Serikali yetu, ni vizuri vijana na wanawake wenzetu kupatiwa ujuzi wa kuzalisha majiko sanifu. Haya yatasaidia kuzalisha kipato kwao, lakini pia yataongeza kutoa fursa kiuchumi na kuondokana na maisha tegemezi ya kusubiri ajira za Serikali yetu peke yake. Kama Serikali yetu inavyotaka, inatoa fursa, sasa ni wakati vijana kujiajiri na pia wanawake wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu. Ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asya Sharif Omar. Nilimtaja Mheshimiwa Martha Festo Mariki na Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano ajiandae.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia fursa ili niweze kuchangia katika mada iliyoko mezani. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyetujalia uzima na afya njema mpaka siku ya leo nimeweza kusimama hapa ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya; lakini pia wasaidizi wake wanaomsaidia akiwepo Makamu wa Rais, pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu. Pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri wetu wa Wizara hii, kwa kazi nzuri nayoifanya ya

kumsaidia Mheshimiwa Rais, vilevile ninampongeza kwa hotuba nzuri aliyoitoa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza moja kwa moja katika mchango wangu na nitaanza katika kuchangia katika suala la hewa ya ukaa. Biashara ya hewa ya ukaa katika nchi yetu ya Tanzania, bado haijawa wazi, ni kwa sababu Serikali bado haijatafuta masoko ya uhakika kwa ajili ya kufanya biashara hiyo. Mfano sisi Wilaya yetu ya Tanganyika ndani ya Mkoa wangu wa Katavi tunafanya biashara hii na halmashauri nyingi nchini zimekuwa zikija kujifunza katika mkoa wetu wa Katavi Wilaya ya Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba biashara hii bado haijawa na uwazi kutokana na kwamba masoko ya uhakika bado hayajapatikana. Hivyo niiombe sana Serikali yangu iweze kutafuta masoko ya uhakika kwa sababu hata sisi Wilaya ya Tanganyika inavyoonekana baada ya mimi kuwa Mjumbe wa Kamati ya Maji na Mazingira, wale watu wanaofanya biashara ile ni *middle man* ambao kwa kweli biashara hii imesababisha kutokuwa na uwazi. Hata wananchi pia tumekuwa hatuna uelewa nini kinachopatikana kutokana na biashara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali ikitusaidia kupata masoko ya uhakika kupitia halmashauri zetu ambapo watu watafanya biashara hii tutakwenda kuwa wanufaika kwa sababu sisi Wilaya ya Tanganyika tayari ni mfano kupitia biashara hii. Tumeweza kujenga vituo vya afya vya kisasa na hivyo tunaamini katika nchi yetu ya Tanzania iko mikoa mingi ambayo ina misitu mizuri na wenyewe wanaweza kufanya biashara hii na wenyewe wakaweza kunufaika na wananchi wakapata jitihada za kuweza kutunza misitu hususan misitu ile ya asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali vilevile iondoe kuchelewesha kutoa vibali kwa wafanyabiashara wanaofanya biashara hii ya hewa ukaa. Mfano, katika msitu wetu wa Tongwe Wilaya ya Tanganyika, pia Msitu wa Nkamba ni misitu ambayo tulikuwa tunatarajia kufanya biashara hii ya hewa ukaa, lakini mpaka sasa vibali vimekuwa

vikicheleweshwa, hivyo kusababishia halmashauri kupoteza mapato mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaokaa katika maeneo yale kwa kweli wamekata tamaa hata ya kutunza misitu ile ambayo ni ya asili. Tunatambua biashara hii inafanyika, lakini misitu yetu inaendelea kutunzwa. Badala ya watu kukata miti watu wamekuwa wakihamasika kuitunza misitu kwa sababu wameona sasa misitu ni fursa kwao ya kuwapatia kipato lakini kuleta maendeleo katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la *NEMC*. Tunaiomba sana Serikali iweze kuharakisha *NEMC* iweze kuwa mamlaka kamili kwa sababu tunatambua *NEMC* inafanya kazi kubwa na nzuri, lakini mpaka sasa *NEMC* imekuwa ikisuasua kutokana na kwamba bado haijawa mamlaka kamili. Sasa hatutaki *NEMC* iwe na visingizio. Sote ni mashahidi tumeendelea kushuhudia kwamba kuna ucheleweshwaji wa vibali katika kufanya biashara. Tunatambua kwamba biashara nyingi ili zifanyike ni lazima *NEMC* waweze kutoa vibali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano watu wanataka waanzishe *petrol station* lakini vibali vimekuwa vikisuasua. Tunachoiomba Serikali *NEMC* iweze kupewa mamlaka kamili ili itakapokuwa inafanya vibaya tuweze kuihoji, tuweze kuwauliza nini kinakwamisha kwa sababu tunatambua hata Dira ya maendeleo ya mwaka 2025 mpaka 2050 inasema kwamba 70% itatokana na *private sector*. Sasa sekta binafsi wanakwamishwa mara nyingi na *NEMC* kutokana na kwamba…

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnzava, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpa taarifa mzungumzaji. Pamoja na mchango wake mzuri,

ninataka nimpe taarifa kwamba ni sahihi ili *NEMC* iweze kufanya kazi vizuri ni lazima iwe mamlaka kamili. Hata majirani zetu kwa maana ya nchi zote ambazo zinatuzunguka, vyombo vyao vya kusimamia mazingira kwa sasa ni mamlaka kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua mfano wa Kenya kupitia Sheria ya Usimamizi na Uratibu wa Mazingira Na.8 ya Mwaka 1999, Kenya wana mamlaka, lakini Rwanda hivyo hivyo wana mamlaka inaitwa *REMA* na Uganda *the same* wana mamlaka kamili ambayo inasimamia shughuli za mazingira kama ilivyokuwa *NEMC* kwa upande huu wa Tanzania. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa hiyo. Tukiwezesha *NEMC* kuwa mamlaka kamili ni uhakika kwamba itakwenda kufanya kazi nzuri. Sote tumeshuhudia pia uharibifu katika maeneo mbalimbali. Mfano, katika sekta ya madini kule wachimbaji wamekuwa wakifanya uchafuzi katika mazingira, lakini *NEMC* wanashindwa kuwa na kauli moja kwa sababu bado haijawa mamlaka kamili kuna mwingiliano wa kimaslahi. Hivyo tunasema kwamba *NEMC* ikiwa mamlaka kamili itaweza kuendelea kuwawajibisha wale wote wanaofanya uchafuzi wa mazingira, lakini itafanya kazi zake vizuri. Hivyo ni muhimu sana *NEMC* ikawa mamlaka kamili ili iweze kufanya kazi zake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na suala la mazingira. Hapa nichukue nafasi hii kumpongeza sana kinara namba moja wa mazingira katika Taifa letu la Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mama yetu kwa kazi nzuri anayoifanya kuhakikisha kwamba anayatunza mazingira na ameonyesha mfano. Hata siku ya leo tumeona kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kukutana na mama lishe na baba lishe kwa ajili ya kuwapatia mitungi kwa ajili ya nishati safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kweli amekuwa kinara wa kuhakikisha kwamba nishati safi na salama inakuwa kipaumbele

katika Taifa letu la Tanzania na kuhakikisha kwamba matumizi ya nishati chafu katika Taifa letu yanakwenda kukomeshwa katika Nchi yetu ya Tanzania na katika maeneo yetu na hata katika bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama huyu ndiyo kinara wa kuhakikisha kwamba nishati safi inafika katika maeneo yote. Pia, amekuwa akijipambanua kwa kuielezea na kwa kufanya vitendo na amekuwa akifanya hivyo kwa kukutana na makundi mbalimbali kuhakikisha kwamba suala la nishati safi ni kipaumbele kwani tunatambua kabisa waathirika wakubwa wa nishati chafu ni akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, akina mama waliokuwa wakitumia kuni kwenye kupikia ambao kwa kweli walikuwa wakiathirika kwa kiasi kikubwa, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akaamua kufanya kwamba jambo la nishati safi liweze kuwa kipaumbele katika nchi yetu ya Tanzania. Hivyo tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini tunampongeza kwa kuifanya siku yake ya kuzaliwa kuwa siku ya upandaji wa miti. Hilo ni jambo kubwa sana ambalo linasaidia kuendelea kutunza mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Festo Mariki, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano na Mheshimiwa Amour Seif Abdalla ajiandae.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi hii kwa kupata muda wa kuchangia wakati huu. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ndio mwingi wa rehema na anayetujalia hata uwepo wetu hapa. Suala la mazingira na Muungano ni mambo muhimu sana lakini nimshukuru sana kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu kipenzi Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hata ile Sera ya Mazingira ya Mwaka 1997 wakati akiwa huko kwa maono yake mazuri tayari 2021 tumepata sera mpya ambayo imeboresha zaidi masuala mazima ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa na kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais ambaye Hotuba hii ambayo ni jambo tunalolijadili liko chini ya Wizara yake Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa jinsi anavyoendelea kuitafsiri tabasamu ya Mama Samia Suluhu Hassan hasa anapopita kwa Watanzania na hili tumelishuhudia katika ziara zake mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana pia Waziri wa Ofisi hii ya Mazingira na Muungano ndugu yangu Mheshimiwa Injinia Masauni na Mheshimiwa Naibu Waziri wake ndugu yangu Mheshimiwa Ruben Kwagilwa jinsi anavyomsaidia Waziri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nilikuwa mtendaji niwashukuru watendaji wote wa *NEMC* kuanzia wa juu mpaka wa chini kwa kazi nzuri wanayoifanya na kumwezesha Mheshimiwa Waziri naye atuletee taarifa iliyonona na iliyopendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira ni suala mtambuka na ni suala ambalo limeongelewa pia katika vitabu vya Dini. Imenukuliwa katika Kitabu cha Isaya ya 32:19: "kwamba lakini mvua ya mawe itakunya (kwa maana itanyesha kwa lugha nyingine) wakati ambao wakati wa kupunguza miti ya msituni na huo mji utadhalilika." Hii ni dalili kwamba tunapochafua mazingira kuna madhara yanajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mvua nyingi itanyesha na mji udhalilike, maana yake kinyume chake kuna wakati tunapata ukame pia. Hata katika Quran imenukuliwa katika *Surat Nuur* aya ya 40

Mwenyezi Mungu anasema, akiyazungumzia mazingira, *“Dhwaharal fasad fiilbarri walbahar bimaaakasabat ay’yin naas.”* Ufisadi, uharibifu umeongezeka mno kuanzia bara na baharini kuanzia nchi kavu na majini kwa sababu ya mikono ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika andiko lingine Mwenyezi Mungu anasema katika Surat Yunus aya ya 44, *“Inna Allah laayadhrumu nnasa shaian walaakinna nnasa anfusahum yadhwirimun.”* Hakika Mwenyezi Mungu hajawahi kuwadhulumu watu bali nafsi zao wenyewe, maamuzi yao mabaya wenyewe, ndiyo yanawaletea madhara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye michango yangu ambayo nimeikusudia wakati huu. Jambo la kwanza ni jambo la kuboresha tozo katika Wizara hii ikiwepo na taasisi yake ya *NEMC*. Niungane na wenzangu waliotangulia wakiizungumzia ile *polluter pays principle* kwamba anayechafua mazingira lazima ashikwe tozo au mazingira yakichafuliwa lazima yalipiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa najiuliza mpaka najikuna kichwa. *NEMC* ana dude kubwa tumempa la kusimamia mazingira. *NEMC* ndiyo anawakagua watu wa migodi, *NEMC* ndiyo anawakagua watu wa gesi, *NEMC* ndiyo anawakagua wachimba mafuta na ana gharama kubwa hapo anaingia; kwa nini asiwe na tozo la uhakika? Kwani akipata asilimia moja moja tu si anayafanya mazingira yanakaa vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi akipata asilimia moja ya madini, akapata ya mafuta (wale wanaochimba visima vya mafuta) kwa sababu yeye ndiyo mkaguzi, akapata kwenye visima vya gesi hamwoni kwamba *NEMC* anaenda kufanya jambo kubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama *percent* zote hizi asilimia zote hizi zinaenda Wizara ya Fedha basi kama wanachukua moja kwa nini wasigawane na *NEMC*? Upo msemo mmoja wa kanuni ya dini unasema, *“maa laa yatiibul wajibu ilaabihi fahuwal waajib.”* Kinachosababisha wajibu utimie ndio wajibu wa kwanza kabla ya

wajibu wenyewe. Sasa kama tunataka *NEMC* awepo pale lazima tozo lake tulizungumzie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama shida ni sheria kwa nini isije hapa tukaisimamia Waheshimiwa Wabunge mpaka ikakaa sawa matozo haya yakamsaidia. Sioni kwa nini *NEMC* asipate tozo ya uhakika kwa sababu vyanzo vipo ni suala tu la kuweka sawa sheria kama ndiyo yenye shida. Hapa Mheshimiwa nimwombe Waziri hili alichukue kwa herufi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo wanaweza wakaongeza mapato ni kwenye biashara hii ya kaboni ya hewa ukaa (biashara ya *carbon* ambayo pia ndiyo hewa ukaa). Tunaitumia *carbon* kwa sababu ndiyo *reference*. Nchi 192 zilikaa katika itifaki ya Kyoto ya Mwaka 1997. Nyingine zilikataa, lakini mwaka 2015 kwenye yale Makubaliano ya Paris zote zilikubaliana hapa ndio msingi wa hewa ukaa ilipoanzia. Ni biashara kubwa ambayo elimu ni ndogo katika maeneo tunayoyaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwamba ipo mifano ya kuangalia katika Wilaya za Tanganyika na Nyanda za Juu Kusini kwa sababu tayari wameshaanza kupata pato hili. Kwa hiyo hili lielekezwe kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri jambo lingine kwamba hewa hukaa katika maeneo ya baharini ni zao kubwa sana kwa sababu miti ya mikoko huwezi ukailinganisha na misitu ya kawaida. Katika bahari, zao la hewa ukaa linaweza likawa ni mara tano au mara 10 zaidi ukisoma makala nyingi za kimazingira. Kwa hiyo, ina maana mpaka sasa hivi tumepoteza dola nyingi sana na trilioni nyingi sana za mazingira. Nishauri pia kwamba elimu ya hewa ukaa inatakiwa ifike kwa viongozi wa chini mpaka wa vijiji kwa sababu hawa ndiyo wabeba maono ya wale wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri lugha zitumike nyepesi. Unaweza ukatumia *carbon credit* isieleweke, lakini kwa nini usiseme, *"fedha zinazopatikana kwa utunzaji mzuri wa misitu na matumizi ya*

*hewa safi?* Kwa nini lugha kama hizo zisitumike ili kuhakikisha wananchi wanang'amua vizuri na kufikia malengo tunayoyakusudia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu isipopatikana basi pato la hewa ukaa au pato la biashara ya *carbon* tutalisikia na hatutafikia malengo. Kwa kuwa kuna wenzetu ambao wameshaanza, basi wengine wakajifunze huko ili tuhakikishe kwamba tunaendana na maono ya Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mdogo, lakini *NEMC* inakotokea imesonga mbele sana lazima tuisifie. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. Aliwahi kusema mwanafalsafa Dkt. Kwame Nkrumah wa Ghana akasema, "*those who would judge us merely by the heights we have achieved, would do well to remember the depth from which we started*." Wale wanaotupima kwa kimo tulichofikia wangefanya vizuri zaidi kama wangeanzia kwenye kina tulipoanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na mchangiaji anayefuata, ninaomba tuwatambue wageni waliopo Bungeni hapa jioni hii.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni wageni 21 ambao ni Machifu kutoka mikoa mbalimbali Nchini Tanzania. Hao ni wageni wa Mheshimiwa Spika ambao wageni hao wameongozwa na Mwene Antony Tadeo Kapufi wa Tatu. Karibuni sana machifu wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Amour Seif Abdalla na Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga ajiandae.

**MHE. AMOUR SEIF ABDALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza kabisa ninampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa yeye ni kinara namba moja katika kuhakikisha haya masuala ya mazingira yeye anakuwa ni mfano kwa kufanya kwa vitendo. Sote ni mashuhuda yeye ndiye anakuwa ni mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba anapanda miti kwa vitendo na anafika hadi *site* kwa ajili ya kuwahimiza wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii ya masuala ya Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulika na masuala ya Muungano na Mazingira, ninataka nichangie kwenye masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya mazingira Tanzania sisi tumepiga hatua kubwa sana. Kwa kuthibitisha hivyo ni kwamba juzi tu Mheshimiwa Masauni hapa amechaguliwa kuwa Makamu wa Rais katika Baraza la Mazingira la Umoja wa Mataifa. Asingechaguliwa huyu Mheshimiwa kama Tanzania haijafanya vizuri katika masuala ya mazingira. Kwa hiyo, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Hamad Masauni kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais katika Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme katika hotuba hii ya masuala ya Mazingira pamoja na Muungano pia nimependa katika hotuba hii dira yake inavutia kabisa inayosema, *"Tanzania yenye Muungano imara lakini vile vile endelevu katika mazingira salama, endelevu, uchumi wa bluu na uchumi jumuishi wa bluu."* Kwa hiyo, nimependa sana dira ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii ya mazingira na katika hotuba hii ya bajeti, ninaomba nichangie katika mazingira. Hata katika Jimbo la Wete ni muhanga wa masuala ya mazingira kwa Bandari yangu ya Wete, katika ile sehemu ambayo ni uchumi wa bluu ambayo imo humu kwenye hotuba katika gati ya wachuuzi na wavuvi wa Jimbo la Wete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mazingira ya pale ni mazingira ambayo yameshababishwa kutokana na mabadiliko ya tabia nchi ya bahari. Sasa inapelekea pale katika bandari ya wachuuzi watu hawafanyi kazi zao kwa inavyotakiwa kwa sababu mazingira si mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira ya Bandari ya Wete; bandari pale ni bandari ya pili ya ukusanyaji wa mapato kwa *TRA* na *ZRA* kwa Zanzibar. Hata hivyo, licha ya kuwa mazingira ya ile bandari si rafiki watu wanafanya kazi vizuri, lakini endapo kama Wizara hii itakwenda kuangalia vizuri katika mazingira ya ile gati kwa sababu imepelekea kutokana na hii tabianchi ya mabadiliko ya bahari imesababisha kina cha pale kuwa kidogo hadi inasababisha vyombo vingine vinashindwa kwenda pale. Vyombo hivyo vikishindwa kwenda katika Bandari ya Wete kutokana na mazingira mabovu tutakosa mapato mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaiomba Wizara hii iende ikaangalie pale, ikapeleke wataalam mahususi kabisa kwa ajili ya kuangalia Bandari ya Wete mazingira yake na mazingira ya Gati ya Wete, lakini vilevile na ile sehemu ya wachuuzi na wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu Bandari ya Wete ndiyo uti wa mgongo wa Kaskazini Pemba. Hivyo, mazingira yanasababisha hata maendeleo ya Mkoa wa Kaskazini Pemba na maendeleo katika Jimbo langu la Wete yanasuasua kwa sababu ya bandari kuwa ndiyo uti wetu wa mgongo pale hatuna kitu kingine ambacho kinasababisha uchumi wa Kaskazini ukue. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba Wizara hii na namwomba Mheshimiwa Waziri waende wapeleke wataalam pale wakaangalie hili suala ni la muda mrefu sana kwa sababu pale tunategemea *channel* nne katika ile bandari endapo kama mazingira yataboreshwa vizuri kabisa ile bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *channel ya Mombasa,* pale tunategemea sana Bandari ya Mombasa, tunategemea sana Bandari ya Tanga, tunategemea sana Bandari ya Unguja pamoja na

Dar es Salaam. Hivyo, mazingira kwa sasa siyo rafiki, ndiyo maana inasababisha mapato ni mengi, lakini hayatoshelezi. Hivyo, ninaiomba Wizara hii iende pale ipeleke wataalam ili uchumi wa mtu mmoja mmoja pale Wete ukue; lakini vilevile na kipato cha *TRA* na *ZRA* kizidi kuongezeka pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa haya mambo mazuri ambayo yameelezwa katika hotuba hii ya Makamu wa Rais, Mzingira na Muungano, ni mambo mazuri, ambayo yana dira nzuri, yameelezwa hapa na Mheshimiwa Waziri. Nami sina budi kusema kwamba ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amour Seif Abdalla ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga na Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme ajiandae.

**MHE. THOMAS M. KAMPALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mosi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu wa mbinguni kwa kuniwezesha leo siha njema kusimama mbele yako na kuchangia hotuba ya Waziri wa Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwa moyo wa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameonyesha kwa vitendo. Leo wakati ninakuja kuchangia hapa nimemwona mama huyu akigawa majiko kuonyesha ni namna gani alivyo *serious* na mambo ya mazingira, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumpongeza Waziri wa Mazingira na Muungano, ndugu yangu Hamad Yussuf Masauni kwa wasilisho zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunakubaliana mazingira ndiyo kila kitu. Uhai wetu sisi unahitaji mazingira, kilimo kinahitaji mazingira, afya zinahitaji mazingira, viwanda vinahitaji mazingira, kila kitu kinahitaji mazingira. Ukisikiliza wasilisho la Waziri ameongea, kwa mwaka Tanzania inapoteza hekta 469,420 za misitu. Kwa miaka

mitano tunapoteza hekta 250,000. Hizi hekta 250,000 ni sawa *square kilometer* 23,500. *Square kilometer* 23,500, Mkoa wa Mwanza una *square kilometer* 25,233. Kwa hiyo, kwa miaka mitano tunapoteza misitu yenye ukubwa wa Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumepitisha hapa mpango. Kwa kasi hii ya upotevu wa misitu ni kubwa ya kiwango hiki baada ya miaka 10 huu mpango hautakuja kutekelezeka. Nini ushauri wangu? Tumeongea sana hapa. Imefikia wakati sasa Serikali ifanye maamuzi. *NEMC* wamepewa jukumu kubwa sana, lakini *NEMC* amepewa jukumu ni sawa na nyoka wa kwenye ngoma. *NEMC* amepewa jukumu halafu hana meno lazima tukubaliane, umefika wakati sasa wa *NEMC* kuwa mamlaka kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye miji yetu mikubwa, ukienda vijijini kwenye kila eneo, tatizo kubwa ni uharibifu wa mazingira. Leo hii tunayoongea *NEMC* hana uwezo wowote wa kwenda sehemu akafika akakuta kuna eneo ambalo lina uharibifu mkubwa wa mazingira. Kwa mfano, kila siku huwa ninatolea mfano ukienda kwenye Mkoa wa Mwanza kila mwaka mvua zinaponyesha kuna *disaster* za mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kuangalia mafuriko mengi yanayotokea kwenye mikoa ya Mwanza na majiji makubwa changamoto kubwa ni shughuli za kibinadamu. Kwa mfano Mto wa Mkuyuni pale ukienda Mto wa Mkuyuni juzi tu kulikuwa kwenye mafuriko makubwa sana. Chanzo cha mafuriko yale ya Mto wa Mkuyuni vimetolewa vibali vya ujenzi, ule mto pembeni yake kumejengwa viwanda vikubwa, mbele ya daraja ukienda pale Mkuyuni utakuta kuna ghorofa limejengwa *NEMC* hana *mandate* ya kumwambia yule bwana avunje. Matokeo yake sasa *NEMC* kazi yake ni kutoa ushauri tu. Akifika anatoa ushauri na vifaini vidogo vidogo. Kama tunataka Taifa hili lipige hatua lazima tukubaliane *NEMC* sasa iwe mamlaka kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya kaboni; halmashauri zetu nyingi zimejipanga kuingia kwenye biashara ya *carbon* na hili jambo, Waziri Mkuu yuko hapa ni vizuri akasikiliza vizuri na akalichukulia hatua

tatizo la halmashauri nyingi kuingia kwenye biashara ya *carbon* ni *TFS*. *TFS* wamekuja kwenye halmashauri zetu, wamechukua misitu kila kwenye kijiji wameweka *GN*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye halmashauri zetu sisi tunaotoka vijijini kila sehemu ukizunguka *GN* za *TFS* na *TAWA* zimekuwa kama kombati ya jeshi. Sasa tukijipanga kuingia kwenye biashara ya *carbon credit* huku unakuta kuna zuio la *NEMC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikubaliki na hawa *TFS* sio kwamba wanakataa sisi tusiingie kwenye biashara ya *carbon credit* wana faida na hii misitu. Hapana, ukienda pale sasa hivi kwenye halmashauri zetu kuna kuna *contradiction* kati ya *TAWA* na *TFS*. *TAWA* wanahifadhi misitu, *TFS* wanakata misitu. Leo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anapiga magoti kupanda miti halafu huku kuna taasisi la Serikali kazi yake kukata miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubaliane *TFS* na *TAWA* wanafanya kazi moja ni sawa na Dula na Abdalla. Kuna sababu gani ya kuwa na taasisi nyingi? Hakuna sababu ya kufunga mpaka asiyekula panya. Lazima tukubaliane hapa hizi taasisi kila mmoja kama kuna majukumu ya *TFS* ni bora yakapelekwa *TAWA* kwa sababu sasa kule kijijini ni shida, *TFS* ni *disaster* kubwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nije kwenye kuchangia Muungano; ni muumini mkubwa sana wa muungano. Kwangu mimi Muungano ni Imani; mtu akiugusa Muungano mbele yangu ni sawa na kunishika bega wakati wa tafaruku ile. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu akigusa Muungano kwangu atakutana na matatizo makubwa kweli kweli. Muungano unazo faida nyingi sana ambazo kwa akili ya kawaida tu unaweza usizione, lakini napenda kueleza ni mmoja ya watu ambao wako tayari kulinda Muungano kwa nguvu zangu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali na Mheshimiwa Waziri aje na majibu lini *NEMC* itakuwa mamlaka kamili

na Mheshimiwa Waziri asipokuja na haya majibu shemeji yangu alikuwa pale juu, shemeji ninaondoka na mshahara wa mzee. Bila majibu ya lini *NEMC* itakuwa mamlaka ninapita na mshahara bila kujali matatizo yatakayotokea nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kupata nafasi ya kuchangia siku ya leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii nami kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyowasilisha leo hapa Bungeni. Ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais. Pamoja na hilo nitumie na fursa hii kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yeye akiwa mwana mazingira namba moja; yeye akiwa kinara wa nishati safi ya kupikia. Tanzania, Afrika na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uongozi wake thabiti Mheshimiwa Rais, ameonyesha maono yake na nia yake. Ameweka mikakati thabiti ya kusimamia suala la mazingira nchini. Katika hili tumemwona Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuliweka suala la mazingira kulipa kipaumbele ameliweka katika dira yetu ya maendeleo ya mwaka 2020 - 2050. Ili sasa suala la kuhifadhi, kulinda na kutunza mazingira lipewe kipaumbele kwa sababu ndiyo suala muhimu linotufikisha katika maendeleo na mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutambua suala la mazingira ndiyo nguzo

muhimu ya maendeleo ya Taifa letu amefanya mambo mbalimbali katika nchi yetu na anaendelea kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameiwezesha *NEMC* kupata maabara tembezi yaani *mobile laboratories* haijawahi kutokea katika nchi hii. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka historia ameipatia *NEMC* maabara hii ili kuweza kuiongezea uwezo *NEMC* kufanya udhibiti wa kina, uchambuzi wa mazingira, kusimamia suala la uchafuzi wa mazingira kwa kutumia ushahidi wa kisayansi. Hii ni historia katika nchi yetu na ndiyo maana Wabunge wengine wamesema nami ninaungana nao tunahitaji sasa mabadiliko ya kisheria. *NEMC* sasa ibadilike kutoka kuwa baraza na kuwa mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunayasema haya? Kwa uchache zipo sababu kadhaa; sababu ya kwanza, *NEMC* itakapobadilika kwenda kuwa mamlaka itaongezewa nguvu ya kisheria; pili, ufanisi wa kazi zake utaongezeka bila kuingiliwa na taasisi zingine; tatu usimamizi wa masuala ya mazingira utaongezeka; nne, uwajibikaji utaongezeka katika kusimamia sheria za mazingira bila kuwepo na mgongano na taasisi zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, utoaji wa vyeti vya tathmini ya mazingira utafanyika kwa uharaka bila kucheleweshwa; sita, hawategemei Mamlaka za Serikali za Mitaa au Jeshi la Polisi katika kutekeleza majukumu yao katika suala zima la udhibiti wa mazingira na kusimamia sheria; saba, kutaondoa migongano ya majukumu na wadau wengine kwa kutambua kuwa *NEMC* sasa ni mamlaka na hivyo itaongeza ushirikiano na taasisi zingine; nane, kutakuwepo na ulinzi wa mazingira kwani udhibiti wa uchafuzi na utupaji wa taka hovyo utafanywa kwa kiwango cha juu na mamlaka hii mpya ambayo utaundwa sio baraza mamlaka ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, hilo baraza litakapoundwa litapatiwa mamlaka kamili na hivyo *NEMC* itapata nguvu ya kuongeza mapato, itakuwa na mwonekano mpya, lakini na wawekezaji watakuwa na imani na baraza hili jipya ambalo litaundwa na mamlaka hii mpya ambayo itaundwa. Ulinzi wa

rasilimali za mazingira utakuwepo na utasimamiwa kwa uaminifu mkubwa na uwajibikaji mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuchelewa kuleta mabadiliko haya ya sheria katika Bunge lako hili Tukufu kunasababisha athari mbalimbali ikiwemo *NEMC* kuchelewa kutoa maamuzi ikiwemo kutoa vyeti na vibali mbalimbali kwa sababu ya mwingiliano na mlolongo mrefu sana. *NEMC* ikibadilika ikiwa mamlaka kutakuwa kuna *direct enforcement* ya sheria. Kwa kuchelewa kuleta mabadiliko haya ya kisheria, mwajibikaji hafahamiki ipasavyo, je, ni *NEMC*? Je, ni Mamlaka za Serikali za Mitaa? Je, ni polisi? Tunataka sasa *NEMC* iwe na nguvu na iwe na meno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuchelewa kuleta mabadiliko haya taswira ya *NEMC* inaendelea kudhohofika kwa wawekezaji. Vilevile kunakuwa kuna ongezeko la malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali. Sasa *NEMC* huyu ni *eyes on, hands off* hana nguvu. Tumwongezee nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayasema haya ili dira yetu ya mwaka 2020 - 2050 ili iweze kufikiwa kikamilifu na malengo yake yatekelezwe kamilifu, tunahitaji mabadiliko ya sheria hii iletwe Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ambaye ndiye kinara wa nishati safi ya kupikia, tunampongeza sana kwa kuleta hii ajenda ya nishati safi kwa Watanzania. Mafanikio makubwa yameonekana, leo hii takribani taasisi 3,350 zimehama kutoka kutumia nishati isiyo salama, sasa hivi inatumika nishati iliyo salama. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini na matumizi ya nishati safi ya kupikia yameongezeka kutoka asilimia 6.9 mpaka 23%, haijawahi kutokea!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira mazuri ya utekelezaji wa uchumi wa bluu. Usimamizi mzuri na uendelezaji wa uchumi wa bluu nchini tunauona. Rasilimali maji zinatumika kwa sababu ya mazingira mazuri aliyoyaweka Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali sasa iweke mfumo mzuri ili sasa rasilimali maji hii iweze kutumika vizuri. Ushauri mwingine kwa sababu ya muda; tunaona jitihada za upandaji miti zinafanyika nchini, lakini sasa tunashauri uwekwe mfumo mzuri wa kufuatilia ile miti inayopandwa je inakua? *Sustainability* ya ile miti inayopandwa iwepo lakini vilevile, biashara ya kaboni. Tunaipongeza sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha Kituo hiki cha Kitaifa cha Kuratibu Biashara ya Kaboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda umekwisha ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme. Nilimtaja Mheshimiwa Ali Hassan King na Mheshimiwa Joshua Nassari na Mheshimiwa Hija Hassan Hija, wajiandae.

Mheshimiwa Joshua Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi angalau kwa dakika mbili tatu niweze kuzungumza kwenye Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza, kwanza nitumie nafasi hii kulipongeza Bunge lako. Bunge hili la Kumi na Tatu kwa mara ya kwanza kwenye historia ya nchi yetu kwa siku nzima ya jana na mimi nikiwa ni Mbunge kijana ambaye niliwahi kuingia hapa ndani nikiwa Mbunge mdogo kuliko wote Tanzania, Bunge hili limeweka historia kwa kutumia siku nzima kujadili masuala ya vijana ndani ya Bunge, haijawahi kutokea tangu uhuru wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limewezekana pekee; hatuwezi kulipongeza Bunge tukaacha kumpongeza mbeba maono ambaye aliona kwamba kuna umuhimu wa nchi yetu kuwa na Wizara maalum na mahususi kwa ajili ya masuala ya maendeleo ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tumelilia kwa miaka mingi, tukaongea habari ya Baraza la Vijana, tukaongea habari ya namna gani, lakini Rais mwenyewe ameona kwamba siyo suala la Baraza tu ni habari ya kuwa na Wizara ambayo inahusika moja kwa moja na masuala ya vijana. Kwa hiyo, kwa hilo nianze kwa kulipongeza Bunge lako na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hayo maono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia habari ya vijana kwa mfano kama ambavyo tumefanya jana, *we are talking of future.* Tunaongea habari ya siku zijazo, miaka ijayo *future* ya nchi na dunia yetu hii ambayo tunaishi. Tunapozungumza habari ya *future* ya dunia hii, hatuwezi kuacha kuzungumzia habari ya mazingira. Mheshimiwa Kampala alikuwa anazungumza akasema kilimo kinategemea mazingira, akasema viwanda vinategemea mazingira na vitu vingine vingi alivyovitaja: siyo wanyama, siyo sisi wanadamu, siyo utalii, siyo nishati, sekta karibu zote zinategemea zinategemea mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwongezee Mheshimiwa Kampala niseme kwamba *future* yetu sisi, *future* ya nchi na *future* ya ulimwengu ambao tunaishi inategemea namna gani ambavyo tuta-*handle* mazingira yetu ya hapa duniani tunakoishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nipongeze kazi kubwa ambayo imefanywa na Wizara katika suala zima la utunzaji wa mazingira na usimamizi. Kwa dakika chache ambazo umenipa na sitazitumia zote, nitajikita kwenye jambo moja tu kwa sababu mengi yamezungumzwa *and I wouldn't like to repeat* yale ambayo yameshazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini ninazungumzia sana sana ni habari ya suala la *NEMC* hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza hili la Usimamizi wa Mazingira lilianzishwa mwaka 1983. Mimi ninayezungumza hapa nilikuwa sijazaliwa, lakini Baraza lile likaanza kazi mwaka 1986. Wakati huo ndiyo ninazaliwa, lakini sheria iliyotengenezwa ya mazingira ya wakati ule na mazingira ya sasa ni tofauti. Dunia imekwenda mbele ni zaidi ya *over 40 years* karibu miaka 50 na kitu sasa tangu wakati ule

lilipoanzishwa Baraza hili mpaka sasa hivi mazingira yamebadilika, mahitaji ya wakati yamebadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati dunia nzima tunazungumza habari ya mazingira, sisi tumebaki na taasisi ambayo haina meno, haina nguvu inaitwa Baraza. Sasa jamani kule kwetu mitaani kule tunakotoka tuna Mamlaka za Miji, Miji Midogo, Halmashauri zinasimamiwa na Mabaraza ya Madiwani, halafu leo kuna habari hapa ya kitaifa ambapo dunia nzima inaongea habari ya mazingira na nini tunaitengenezea Baraza. Kwa nini hatuna *Authority* kwa nini tusiipe mamlaka kamili kama ambavyo tumetoa kwenye mamlaka zingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wanyamapori tumewapa mamlaka kamili kutoka kuwa Idara. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Utalii ninakumbuka ilivyokuwa. Leo ukienda *TRA* ni mamlaka kamili, kwa nini haikuachwa ndani ya Wizara ya fedha kwamba Wizara ya fedha ndiyo ikakusanye mapato? Ikusanye kodi ikatengenezewa mamlaka kamili? Kwa nini leo suala la mazingira ambalo ni nyeti tunalizungumza ndiyo *future* ya dunia yetu, lakini tuna kaweka kama ni kakitu fulani tukaatamie kakae huko chini halafu huku juu ionekane Wizara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Wizara ni habari ya kutunga sera na usimamizi wa utekelezaji wa sera, lakini siyo kazi ya Wizara tena kazi hiyo hiyo iwe ndiyo kazi hiyo kwamba ni kama ya kuatamia mpaka majukumu ambayo yanapaswa yafanywe na mamlaka zingine ambazo zinapaswa ziachwe zifanye kazi hiyo. Hivi leo ungemwona Waziri wa Fedha yuko huko mtaani anakusanya kodi anafanya nini? Unamwona afisa, Katibu Mkuu unamwona nani. Inawezekana kweli hiyo? Au umwone Waziri wa TAMISEMI yuko kule mtaani kule anasimamia, anahangaika na nini na vyoo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye ugatuzi na ndiyo maana kuna halmashauri huko chini zinafanya. Ndiyo maana kuna vijiji zina Maafisa Ardhi wake. Ukienda leo kwenye kijiji wanaweza wakakutoa ardhi mpaka ekari 50 imepewa mamlaka kamili ukienda kwenye halmashauri hali kadhalika; lakini leo hii sisi Baraza hili la kwetu, Baraza

la Mawaziri limekaa wamezungumza kuhusu habari hii, lakini kila siku bado kuna mkwamo. Kiongozi wetu mkubwa kabisa wa nchi amezungumza na ametoa maelekezo na yeye akazungumza kabisa kuonesha nia ya kutaka kwamba sheria iletwe hapa, ibadilishwe ili watu hawa wa Baraza la Usimamizi wa Mazingira wawe ni mamlaka kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu kwenye Muungano huu Zanzibar wana Mamlaka inaitwa ni *ZEMA (Zanzibar Environmental Management Authority)* sisi tumebaki hivyo. Mataifa yote yanayotuzunguka yote yanazo mamlaka kamili, sisi tumeendelea kubaki hivo kwa nini? Yaani kigugumizi ni kitu gani? Nini kinachotufanya tuendelee ku-*lag behind, I don't see a reason*. Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa wameeleza faida ni zipi wameeleza na *pros* and *cons* …

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninaomba kabisa kabisa kwamba, leo kama alivyosema ndugu yangu Kampala na mimi niseme Mheshimiwa Waziri wetu Masauni yuko hapo asubuhi ametambulishwa na familia yake iko hapo …

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa Mheshimiwa Nassari

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba tu kumpatia Taarifa Mheshimiwa Mbunge mara *NEMC* itakapobadilishwa na kuwa mamlaka itapunguza *bureaucracy* na maamuzi yatafanyika kwa haraka. Ninaomba kutoa Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo ninaipokea kabisa kwa sababu *it goes in line with what I was saying*

na hatuongei hapa kwa sababu kuna maslahi au namna gani tunaongea hivi kwa sababu ni ukweli ulio wazi. Kama Mkuu wa Nchi mwenyewe ameona, Baraza la Mawaziri limekaa na limeridhia, kwa nini kila linapokuja Bungeni wanasema tutaleta sheria ya Bunge hili? Tutaleta Bunge lijalo, tutafanya Bunge lijalo, kwa nini tunakwenda hatua 10 mbele, tunarudi hatua nyingi nyuma halafu tunajipongeza? *Why?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii tumejadili kwa mfano tu kwenye Kamati yetu pale kuna mamlaka inaitwa *TTB* (Bodi ya Utalii Tanzania) ambayo kazi yake imewekwa kule ni kutangaza utalii, ni kufanya nini, lakini kwenye Kamati kule tukajikuta tunalalamika kwamba unajikuta yenyewe haipewi mamlaka kamili ya kufanya kazi hiyo wakati Rais anataka nchi yetu ifikishe watalii milioni nane. Mamlaka ile ambayo inapaswa ifanye kazi hiyo ya kutangaza inaendelea kuatamiwa, unakuta wanaotangaza ni zile taasisi *TANAPA*, sijui *TAWA* sijui nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunakwenda mbele tunarudi nyuma na hali kadhalika kwenye suala la mazingira tumeunda Baraza hili hapa, tangu miaka ya 1980 mpaka leo bado tunaliacha vilevile wakati dunia ndiyo ipo kwenye masuala ya mazingira, tunazidi kuachwa, tunazidi kubaki hapo tulipo wakati wenzetu wanapiga hatua, sisi tunarudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika hatua sasa Mheshimiwa Waziri Serikali ituletee sheria, hapa tufanye mabadiliko watu wa *NEMC* wapate mamlaka kamili ili waweze kufanya kazi kulingana na *mandate* ambayo itakuwa itatengenezwa na sheria husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nassari Joshua Nassari. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa upande wa Wabunge ni Mheshimiwa Hija Hassan Hija.

**MHE. HIJA HASSAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima na leo kwa mara ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa mchango wangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake uliotukuka na ambao unatuletea masilahi kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda ninaomba niwashukuru sana viongozi wangu wa Chama Cha Mapinduzi kwa ujasiri wao na uamuzi wao sahihi wa kuamua sasa kuwa mwana-CCM na kuwa Mbunge wa Jimbo la Kiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kiwani kwa uamuzi wao wa kutupatia kura wagombea wote wa Chama Cha Mapinduzi na kuwa washindi ndani ya Jimbo la Kiwani na hatimaye kuwa viongozi wa nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa mchango wangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo ametoa hotuba yake iliyoeleweka na ambayo ina kiwango. Ninamwelewa Mheshimiwa Masauni kwamba jambo hili halikuwa gumu kwake kwa sababu tumeuelewa uwezo wake wa kufanya kazi kwa mujibu na kwa maslahi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Dira ya Wizara hii eneo la Muungano sina shida nalo, liko sawa na tunaunga mkono kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri amezungumza. Kwa msingi huo na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani ninaomba tudumishe Muungano na tuutetee kwa nguvu zote kama alivyosema wenzetu hii ndiyo silaha pekee ambayo itafanya Tanzania kuishi katika amani na ustawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la mazingira ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Wizara yake kwa kutujengea tuta ambalo limejengwa eneo la Sepwese mpakani mwa Jimbo la Kiwani ambalo limenusuru sana athari ya kimazingira katika mashamba ya wakulima na leo hii wananchi wa Jimbo la Kiwani na Jimbo la Mtambile wamekuwa na unafuu mkubwa kwenye eneo hili la mazingira baada ya kujengwa tuto la Mheshimiwa Waziri chini ya Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba, kama kuna eneo ambalo limeathirika Pemba, basi ni Jimbo la Kiwani na ni kutokana na ujenzi wa miundombinu mbalimbali inayoendelea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kujenga barabara Pemba bila kuzungumza Kiwani. Huwezi kujenga miundombinu ya gati bila kuzungumza Jimbo la Kiwani hususan kwenye Wadi ya Muwambe. Nimwombe Mheshimiwa Waziri afanye ziara makusudi kuja kuangalia mazingira haya ili kufanya busara kwa ajili ya kuokoa wananchi wa Jimbo la Kiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kwa sababu ya muda kwenye suala la biashara ya *carbon*. Nimejaribu kufanya utafiti tangu asubuhi na kuona kwamba yale ambayo Mheshimiwa Waziri amekuwa akitueleza kwa kweli yako makubwa zaidi ambayo Mheshimiwa Waziri hajatupatia maslahi ya elimu ya wananchi wa Tanzania. Mara nyingi Mheshimiwa Waziri amekuwa akizungumzia biashara ya *carbon* kwa eneo la misitu ya ardhini. Mheshimiwa mwenzangu Mbunge hapa wa Mkoa wa Tanga amezungumzia juu ya suala la *blue carbon*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya utafiti mdogo hapa, nimeona kwamba biashara ya *carbon* inayotokana na misitu ya ardhini bei yake ni dola tano mpaka dola 25 kwa tani moja ya *carbon dioxide* ya biashara hii, lakini biashara ya *blue carbon* kwa tani hiyo hiyo kwa kipimo hicho hicho bei yake ni dola 45 mpaka 70. Maana yake nini? Kumbe biashara hii kwenye bahari kuu ina

thamani kubwa zaidi kuliko ili biashara hii kwenye misitu yetu ya ardhini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo Mheshimiwa Waziri ana kazi kubwa ya kufanya, lazima apambane na atuelekeze kwenye kufanya biashara hii mbele ya misitu ya ardhini na katika eneo la bahari. Watanzania wanahitaji kufanya biashara hii ili wajikwamua na umaskini wao na wajenge nchi yao, nchi yenye kipato cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie, Tanzania ina misitu hekta 160,000 na kwa mujibu wa utafiti huu kama misitu hiyo itawekezwa kwenye biashara hii maana yake Tanzania ina uwezo wa kupata dola milioni 320 kwa mwaka. Sasa kama hilo ni jambo sahihi, ni kwa nini Mheshimiwa Waziri asifanye juhudi na kuwekeza kwenye eneo hili kwa ajili ya kulinda uchumi wetu na kuongeza mapato ya Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri na ninaomba Wabunge wenzangu tupitishe bajeti hii ili tumpe nguvu Mheshimiwa Waziri apambane kutafuta fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye biashara ya *carbon* kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, ninaomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hija Hassan Hija. Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaenda kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kushiriki kwenye sehemu ya majumuisho ya mjadala wetu huu wa Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kunifanya kuja kumsaidia

Mheshimiwa Waziri wetu wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Vivyo hivyo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa maelekezo na mwongozo wakati wote ambao wamekuwa wakitupatia ndani ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo amekuwa kiongozi wa shughuli zetu za Serikali za kila siku. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo amekuwa mlezi mzuri kwa siku chache hizi ambazo nimekuwa Wizarani, lakini na kwa namna ambavyo ametupa uelekeo mpya wa Wizara yetu na kwa kupitia bajeti hii ambayo leo Waheshimiwa Wabunge tumesimama hapa kuwaomba waipitishe ili tuweze kuyatekeleza yale yote ambayo wameyachangia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wizara yetu hii tumepata michango ya Kamati zetu zote mbili pamoja na michango ya Wabunge takriban 20. Maoni yote ambayo yametolewa na Wabunge, ushauri wote ambao Waheshimiwa Wabunge wameutoa na kwa kweli maelekezo yote ambayo Bunge hili litayaridhia, chini ya uongozi wa Waziri wetu Mheshimiwa *Engineer* Masauni, tuwahakikishie kwamba tutakwenda kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, atakuja Mheshimiwa Waziri kufanya majumuisho ya jumla kwenye maeneo mengi, lakini kwa fursa hii ninaomba niseme machache sana na kwa muda mfupi sana. Imezungumzwa hapa kwamba kwenye Dira yetu ya 2050 mazingira yamewekwa kama sehemu ya nguzo zile tatu. Ni bahati mbaya sana kwamba kwa sababu zile nguzo mbili zinaeleweka hazikuzungumzwa hapa. Sasa ili tuilete maana kamili ya nguzo ya tatu ni vyema tukajua zile nguzo mbili zimezungumza nini kwenye Dira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguzo ya kwanza ili kufikia malengo ya Dira yetu 2050 inazungumzia uchumi imara, jumuishi na shindani. Nguzo ya kwanza ambayo inazingatia uchumi unaokuwa kwa kasi, lakini uchumi unaobebwa na sekta binafsi. Nguzo ya pili, inazungumzia uwezo wa watu, uwezo wa Watanzania na maendeleo ya jamii ya Kitanzania. Jamii ambayo ina uwezo wa kupata afya bora, elimu bora na ujuzi kwa ajili ya kuendana na soko

la ajira la dunia ya sasa na dunia hii tunayoizungumzia kwa miaka 25 ijayo sisi kama Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguzo ya tatu ndiyo hii ambayo tumezungumza sana Waheshimiwa Wabunge; uendelevu wa mazingira na ustahimilivu. Kwa nini nguzo hii imewekwa na waandishi wa Dira na tukakubaliana kama Taifa iwe sehemu ya nguzo tatu za Dira hii 2050? Imewekwa ili kusimamia rasilimali za Taifa kuhakikisha kwamba tunapotumia rasilimali zetu za Taifa tuzingatie kuzuia mabadiliko ya tabianchi. Sababu ya pili nguzo hii ya uendelevu wa mazingira na ustahimilivu imewekwa ili kuhakikisha matumizi endelevu ya mazingira na maendeleo ya sasa yasiathiri vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge na niwasihi sana watupitishie bajeti hii ili tukayasimamie mazingira. Mheshimiwa Waziri wetu, *Engineer* Masauni tumeshakaa pamoja ndani ya Wizara na wataalam wote na tumekubaliana kwa dhamana hii tuliyopewa ya kitaifa ya kusimamia mazingira na Taifa letu kwa ajili ya vizazi vijavyo tutakwenda kuifanya kazi hii kuliko wakati mwingine wowote ambao umewahi kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni *champion* wa uhifadhi na uendelevu wa mazingira ndani ya Tanzania, Afrika Mashariki na duniani, amesaini Kitabu hiki cha Dira yetu ya 2050 mpaka tukafikia kuongelea habari ya zile nguzo tatu. Anataka nguzo hizi tatu zituelekeze kwenye uchumi wa dola trilioni moja, la kwanza; pia, zituelekeze kwenye kuwahudumia Watanzania ambao mwaka 2050 inakadiriwa tutakuwa tumefikia milioni 118. Siyo hivyo tu, anataka wakati huo ukifika tuwe uchumi wa juu wa pato la kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, amezungumza Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa, wakati akiuzungumzia Muungano na nitamnukuu. Amesema, "*amani na umoja wa Taifa letu tunaouona kifungashio chake ni muungano.*" Sasa, dira yetu hii na mambo yote yatakayoenda kufanyika, mipango yote ya maendeleo ambayo tutaipitisha kwa miaka 25 kutokea sasa, kifungashio chake ni mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii tutakwenda kuifanya kwa weledi na wivu mkubwa na kwa kweli, ninawahakikishia zitakuwepo kelele za hapa na pale. Kusimamia urithi, kwa ajili ya kizazi kijacho haitakuwa kazi ya kupigiana makofi. Tuko tayari kuzibeba lawama, lakini tutatanguliza kutoa elimu kwa Watanzania wote watuelewe na baada ya kutoa elimu tutakwenda kusimamia misingi ya sheria na taratibu ambazo tumejiwekea, kama Taifa, katika kuyasimamia mazingira ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda katika kipindi ambacho mazingira hayatakuwa *a by the way thing*, itakuwa ni jambo la kwanza kabla ya mtu kuwaza jambo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Sasa, ninamkaribisha mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametujalia kukutana leo hapa kwa mara nyingine tena tukiwa wazima wenye afya. Ninaomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Uongozi mzima wa Bunge letu kwa kuendesha mjadala wetu wa leo wa Bajeti hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa weledi mkubwa toka asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kuwapongeza sana na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri. Wapo waliobahatika kusema, lakini kwa sababu ya muda, nina hakika wameyawakilisha vyema mawazo ya wengi na wale ambao pia, walichangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja kuhusiana na Muungano. Ninajua hoja nyingi zimezungumzwa, ziko ambazo tunaweza tukazitolea ufafanuzi sasa

hivi na ziko ambazo tutazichukua, kama maelekezo na kwenda kuzifanyia kazi. Ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge, zile ambazo hatutaweza kuzitolea ufafanuzi leo, tutazitolea ufafanuzi kwa maandishi. Vilevile, maoni yao yote mazuri na muhimu sana tutayafanyia kazi na tunayachukulia kwa uzito mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la Muungano, ninaomba nianze na hoja moja ya msingi sana ambayo baadhi ya wachangiaji, ninadhani mchangiaji mmoja, alizungumza. Kuna wachangiaji wengi walizungumza, lakini ninaanzia pale ambapo mchangiaji mmoja alizungumza kuhusiana na zilizokuwa zinaitwa Kero za Muungano, ambapo sasa sisi tunaziita Hoja za Muungano. Akaeleza kwamba kutokufanyiwa kazi kwa kero hizo ni moja ya sababu ya kuudhoofisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikubaliane naye kwamba, moja kati ya mambo ambayo yamevunja miungano ya baadhi ya nchi duniani, ikiwemo katika Bara la Afrika ambapo nchi nyingi sana zilijaribu kuungana, lakini hazikufanikiwa na hazikufika tulipofika, sisi leo tunaadhimisha miaka 62. Miongoni mwa sababu, moja, ilikuwa ni hiyo, zipo sababu nyingi, kwa mfano; kuna nchi ziliungana hazina mahusiano yoyote ya kihistoria, tofauti na sisi. Sisi historia ya pande hizi mbili za Muungano haikuanzia leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya pande mbili za Muungano wa watu wa nchi hii ya Tanzania wanaotokea upande wa Zanzibar na upande wa Tanzania Bara inaanzia hata kabla ya wageni hawajaja katika nchi hizi. Vilevile, historia yao inaendelea wakati wa ukoloni, lakini historia hiyo imeendelea vilevile kipindi cha mapambano dhidi ya ukoloni na hata wakati wa utumwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa hiyo utakumbuka kwamba, pande hizi za Muungano wakati zinapambania ukombozi wa nchi hii, Waafrika ambao walikuwa wakinyanyaswa katika nchi hizi waliunganisha nguvu na kuunda vyama vya siasa. Mnamo Mwaka 1929 Chama cha *African Association* cha iliyokuwa Tanganyika kiliundwa na hicho ndicho kilichosababisha mwaka 1954 kuundwa

kwa *TANU*, chama kilichosimamia na kuongoza mapambano ya ukombozi wa iliyokuwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Zanzibar, mnamo mwaka 1934 Chama cha *African Association* kimeundwa na ndicho kilichosababisha kuundwa kwa Chama cha *Afro Shiraz Party* mwaka 1957. Chama hicho ndicho kilichosimamia ukombozi wa nchi hii kwa hiyo, ushirikiano wa vyama hivi vya Waafrika unathibitisha mahusiano yaliyopo kipindi cha wakati wa ukombozi wa nchi hizi na hata pale ambapo vuguvugu la ukombozi, kupitia *PAFMECA*, mwaka 1958 ambapo Mzee Karume na Mwalimu Nyerere waliongoza mapambano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu suala la kihistoria hata suala la kijiografia; ninapongeza sana, kuna wachangiaji waliozungumza kwamba, Muungano huu ni urasimishaji uliofanywa na Mwalimu Nyerere wa kuwarudisha pamoja watu wa nchi hizi mbili ambao walikuwa pamoja toka karne na karne na kukataa mipaka ya mabeberu iliyowekwa na kuwagawa Waafrika kwa mipaka, pale Berlin, katika Karne ya 19. Kwa hiyo, Mwalimu Nyerere na Mzee Karume waligoma mipaka ya wakoloni wakaamua kutengeneza na kusimamia mipaka yetu wenyewe Waafrika, ambayo mpaka leo inadumu. Hata Mwaka 1886 wakati ambapo mamlaka ya Sultan ilirasimishiwa mipaka mipya ambayo leo hii tunaiona ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sababu zipo nyingi. Hata sababu ya matarajio, iko miungano iliyovunjika kwa sababu, matarajio ya wananchi hayakutimizwa; sisi matarajio hapa yametimia. Moja katika matarajio makubwa, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia kuhusu umuhimu wa amani, utulivu na umoja wa nchi yetu, kama ndiyo msingi mkubwa wa Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio ya wananchi wa nchi hii ni kuendelea kuishi katika amani, umoja, mshikamano na maendeleo, lakini vilevile hata matarajio ya ugawanaji wa madaraka. Hii inadhihirishwa na Baraza la Kwanza la Mwalimu Julius Kambarage

Nyerere mara baada ya kuungana. Wako watu wanasema kwamba, nchi hii mbali na kuungana leo wanataka kutugawa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere alithibitisha hilo hata katika uteuzi wake wa Baraza la Mawaziri la kwanza. Kulikuwa kuna Wizara tano ambazo Mawaziri wake walikuwa ni kutoka Zanzibar na Wizara hizo wala hazikuwa za Muungano. Kwa mfano; Wizara ya Viwanda, Madini na Nishati, Waziri wake alikuwa Kassim Hanga; Wizara ya Sheria na Katiba, Mzee Hassan Nassor Moyo; Wizara ya Habari na Utalii alikuwa Idris Abdul Wakil; Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Aboud Jumbe Mwinyi; Wizara ya Biashara na Uchumi, Abdulrahman Babu. Kati ya Mawaziri 23 aliamua kwa makusudi kuonyesha kwamba, nchi hii ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kitendo cha Zanzibar kuondoa *sovereignty* yake na kusainiwa Mkataba wa Muungano Taifa hili limeendelea kubaki kuwa moja na leo hii tunashuhudia Muungano wetu ukiendelea kudumu. Ukiachilia mbali masuala ya utamaduni ambao utamaduni wetu wananchi wa pande hizi mbili unafanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikirudi katika hoja ya msingi, nimeona niyagusie hayo, lakini hoja ya msingi ambayo ninataka niigusie ni kuhusiana na zilizoitwa kero. Ninaomba nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, Wahenga wanasema; mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Ninaona watu wengi wanatofautiana sasa hivi juu ya msemo huo wa wahenga, wanasema mnyonge asinyongwe na ni kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua fursa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ameweza kuondoa kero 11 katika kipindi chake. Leo hii tunavyozungumza kati ya kero 25 tumebakiwa na hoja tatu peke yake. Leo ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge walio wengi, wamelitambua na kulithamini hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii kuwaeleza ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wananisikia kwamba, haya siyo mafanikio madogo, ni mafanikio makubwa sana, ni mafanikio ambayo tunahitaji tujivunie na ni mafanikio ambayo yamewezesha kufanya Muungano wetu uwe imara zaidi. Waheshimiwa Wabunge, katika kero tatu zilizobaki, kero mbili tunatarajia kuzimaliza muda siyo mrefu na moja iko chini ya mamlaka yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili hili panapo majaaliwa tunataka tuwasilishe mabadiliko madogo ya sheria kuimaliza kero moja kati ya hizo zilizobaki. Kero hii ni ambayo inahusu usajili wa vyombo vya moto; tunatarajia, Waheshimiwa Wabunge wakiridhia na nina uhakika wataridhia kwa sababu wao watu ambao wanaamini kabisa juu ya dhamira ya dhati ya kuondoa hoja hizi, ili tuweze kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hoja nyingine moja na yenyewe tunatarajia katika kikao kijacho kitakachofanyika siku ya Tarehe 25, cha Kamati ya Pamoja ya Fedha, kwenda kuimaliza. Hivyo, kwa kipindi hiki tutakuwa tumemaliza kero 24 kati ya kero 25. Hayo siyo mafanikio madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero moja ambayo imezungumzwa inahusu masuala ya kifedha, ikiwemo masuala ya mgao wa hisa za iliyokuwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki, ambayo kuna madai kwamba, Zanzibar ilichangia hisa kwenye Benki ya Tanzania wakati wa uanzishwaji wake. Hivyo hoja iliyopo ni kwamba, mgao huo uzingatie hisa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii pamoja na Mfuko wa Pamoja wa Fedha, hoja hizi za kifedha zinahitaji umakini na utulivu wa hali ya juu. Hata hivyo, Waheshimiwa Wabunge, ikiwa Mama Samia ameweza kupunguza hoja 11 na hizi mbili tunatarajia kuzimaliza kwa kipindi cha miaka mitano ni imani yangu na hii moja itamalizika. Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana leo hii tumezungumza kwamba, sasa tunakwenda kufanya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu

wa Rais pamoja na Kamati kuwa, sasa siyo Wizara tena ya kuzungumzia hoja za Muungano, ni Wizara ya kuzungumzia fursa za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkakati wetu wa kuelekea kwenye fursa, ambazo ziko nyingi, bahati mbaya sana fursa hizi ambazo wananchi wa pande mbili wameendelea kufaidika nazo zimekuwa hazizungumzwi sana. Wakati umefika sasa wa kufanya kila linalowezekana, ili elimu hii iweze kufika kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo tumekuja na mpango kabambe wa elimu kwa umma kuhusu Muungano. Ninaomba tushukuru Bunge lako Tukufu kwa kuridhia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kuweza kuja kutoa semina kwa Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru sana, maoni yao mazuri waliyotoa pamoja na Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi, tutayazingatia. Tunaamini semina hii imeleta utofauti hata miongoni mwa Wabunge na kuongeza uelewa juu ya masuala mbalimbali ya Muungano, ikiwemo fursa zilizomo ndani ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivyo, mkakati huu unalenga katika mambo mengi. Tunajua kuna changamoto kubwa ya uelewa, hususan kwa vijana, kuhusu masuala ya Muungano. Hivyo, moja katika mkakati wetu huu kabambe utagusa maeneo ambayo yanawagusa vijana ili vijana hawa tuweze kuwarithisha Muungano wetu, waweze kuulinda Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo yanagusa vijana moja ni eneo la elimu. Ndiyo maana leo hii ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kutoa maoni yao kuhusu umuhimu wa kuingiza masomo ya Muungano katika mitaala. Ninataka niwajulishe katika hilo tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaeleza baadaye eneo la mitaala, lakini ninaomba nigusie kwenye mkakati huu kabambe. Moja ni suala la midahalo, semina, makongamano na mashindano mbalimbali yakiwemo ya insha, kupitia kwenye shule zetu, vyuo vyetu na

kadhalika kupitia mitandao ya kijamii. Maeneo ambayo vijana wanayatumia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge, kuingia katika mitandao ya kijamii ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais. Huko wataweza kujionea shughuli mbalimbali na kupata taarifa kuhusu Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika bajeti hii ni tumetenga fedha, kwa ajili ya kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, ambayo ameitoa wakati wa kampeni za uchaguzi wa kuanzisha makavazi. Hivi tunavyozungumza tumekamilisha ujenzi wa jengo letu lililopo Mtumba, ambapo tutakuwa tuna makavazi ya muda, lakini katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha, kwa ajili ya kujenga makavazi hapa Dodoma pamoja na Zanzibar. Tunaamini kwamba, makavazi hizi zitakapokamilika zitasaidia sana kuhifadhi nyaraka mbalimbali zitakazosaidia vijana wetu kupata taaluma mbalimbali kuhusiana na Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba, elimu hii kwa umma inafika kupitia mkakati wetu huu, vilevile kuna matamasha mbalimbali tunafanya. Kwa mfano, ninaomba kuchukua fursa hii kuwajulisha na kuwaalika Waheshimiwa Wabunge, siku ya tarehe 26 tutakuwa tuna tamasha la aina yake la Mtanzania, pale Dar es Salaam. Leo hii tunapozungumza, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu, tunazindua Ligi ya Muungano ambayo inafanyika pale Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, siku ya tarehe 3 tunatarajia kuzindua Msafara wa Muungano *(Muungano Caravan)* ambao utapita katika Wilaya na Mikoa yote ya Tanzania kufikisha elimu kwa wananchi wetu, hasa vijana kwa utaratibu ambao utakuwa ni kivutio kwa watu kuhamasika na kuwa na hamu ya kusikiliza. Waheshimiwa Wabunge siku ya tarehe 3 tutazindua mpango huo wa *Muungano Caravan* Dar es Salaam na itakuwa ni siku ya Jumapili; tunaomba sana ushiriki wa Wabunge, wao ni watu muhimu sana katika kudumisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda sitagusia maeneo mengine ambayo yanagusa watu wa aina nyingine, mikakati kwenye eneo la viongozi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa baada ya maelezo hayo kuhusu Muungano niende kwenye eneo la mazingira. Ninataka nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge juu ya changamoto ambazo wamezieleza kwamba, bado zinasumbua katika nchi yetu kuhusiana na mazingira. Kwa mfano, bado kumekuwa na ukataji miti hovyo, tunakiri juu ya hilo. Tunakiri bado majiji yetu siyo masafi, lazima tukiri hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakiri bado kuna uharibifu kwenye vyanzo vyetu vya maji, bado kuna viumbe vamizi, lakini bado kuna kelele zitokanazo na shughuli mbalimbali kwenye makazi ya watu na mambo mengine mengi, sisemi kwamba hakuna kazi iliyofanyika, nimeeleza kwenye hotuba yangu mafanikio ya hatua ambazo zimechukuliwa, lakini kama kweli tunataka tufikie Dira ya Miaka 50 ambayo imeweka suala la uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa tabianchi kama moja kati ya nguzo muhimu pamoja na maelekezo yaliyopo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM, ni lazima tufanye mabadiliko makubwa katika eneo zima la usimamizi wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Mheshimiwa Naibu Waziri, kuwahakikishia Wabunge kwamba tunatarajia bajeti hii itakapokuwa imepita na yale yote ambayo tumedhamiria kuyafanya mengine nimeyaeleza hapa, tunakwenda kukabiliana na changamoto hizi na uwezo wa kudhibiti na kuzimaliza changamoto hizi tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza na la muhimu sana ambalo ninaomba Waheshimiwa Wabunge walifahamu, kwamba tumeamua kuja na mpango mkakati, kabambe wa mageuzi ya kimkakati ya mazingira endelevu na tumeitengea bajeti tayari katika bajeti ya mwaka huu kwa kuanzia ni shilingi bilioni 3.5 na mpango huu tunatarajia tuuzindue siku ya mazingira Tarehe 5 Juni ambapo utahusisha maeneo kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika maeneo ambayo mpango huu unakwenda ku-*address* ni suala la kuhakikisha kwamba tunaikijanisha nchi yetu, kwamba tunakwenda kuhakikisha kwamba tunapanda miti na siyo kuipanda miti tu, lakini hata kuilinda na kuitunza. Mpango huu unakwenda kutoa majawabu juu ya baadhi ya kero zilizopo kwa Waheshimiwa Wabunge kwenye Majimbo yenu kuhusu viumbe vamizi. Mpango huu unakwenda kutoa majawabu katika masuala ya usafi na urejezwaji wa taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taka zinazozolewa hizi ni bidhaa, wakati umefika tuwe na mkakati kabambe wa kuhakikisha kwamba taka hizi tunazitumia vizuri kuzalisha *products* zenye tija kwa ustawi wa wananchi wetu. Mkakati huu unakwenda vilevile ku-*address* suala la urejeshaji wa ardhi pamoja na ardhi oevu bila kusahau biashara ya kaboni. Ili hayo yafanyike ni lazima tuwe na nyenzo, nyenzo zetu kuu ni taasisi zetu mbili, Taasisi ya Baraza la Hifadhi na Mazingira Tanzania *(NEMC)*, pamoja na Kituo chetu cha Kuratibu Biashara ya Kaboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kukuhakikishia kwamba maoni ya Wabunge ni ya msingi kuhusu namna ambavyo tutafanya kuisaidia *NEMC* iweze kutimiza majukumu yake vizuri, ndiyo maana tunaamua kufanya, kuliangalia suala la *NEMC* kwa mapana zaidi si katika eneo moja la sheria peke yake tunataka *NEMC* iwe ni chombo ambacho kinaweza kufanya kazi ya *enforcement* kwa wale wote ambao wanakiuka sheria za nchi yetu na ziwe na nguvu, uwezo, meno na makucha ya kusimamia hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusingependelea kufanya kazi zetu kwa kuzima moto kwamba leo Waziri kaenda kafanya ziara ya kushtukiza kwenye kiwanda kimoja, mpango huu unakwenda kutupatia ufumbuzi wa kudumu. Kwa hiyo ni Mpango ambao unataka tuifanye *NEMC* iwe ya kisayansi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, ninakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba wakati umefika sasa *NEMC* kuwa Mamlaka, jambo hilo haliepukiki. Waheshimiwa Wabunge katika Bunge hili Tukufu niliwahi kutoa ahadi hiyo na bahati nzuri Dkt. Samia

Suluhu Hassan amenirudisha katika Wizara hii, ninataka kuwahakikishia, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na Mwanasheria Mkuu ananisikiliza, Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa, *Chief Whip* yupo hapa, tunatarajia katika Bunge lijalo Mungu akipenda tuweze kuleta hapa sheria ya kuifanya *NEMC* iweze kuwa mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zote muhimu za kiserikali tumeshazifika, kwa hiyo kiu ya Waheshimiwa Wabunge ya kuifanya *NEMC* kuwa Mamlaka sasa inaenda kupata ufumbuzi muda siyo mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuifanya *NEMC* kuwa Mamlaka haitoshi, lazima tuiangalie *NEMC* juu ya mambo mengi mbalimbali. Kwa mfano, *NEMC* inahitaji kuwa na vitendeakazi vya kisasa ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri, tumejitahidi kwenye bajeti hii kuiwezesha *NEMC* kupata magari, tumejitahidi katika bajeti hii kuhakikisha kwamba mbali ya mipango mingine ya upatikanaji wa fedha kupitia kwenye miradi mbalimbali ambayo tunaisimamia, kuweza kuwa na mifumo na mitambo ya kisasa ambayo inaweza kuifanya *NEMC* ipate taarifa *in real time*, kwamba mahali popote ambapo kuna uchafuzi wa mazingira na ukiukwaji wa sheria, *NEMC* aweze kupata taarifa hapohapo na siyo kukimbizana, mifumo hii tayari ipo katika hatua za mwisho kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii tunatarajia kuanza, tunayo mahitaji ya *drone* karibu 13, tunaanza na *drone*s mbili, pia malengo yetu, *NEMC* tunataka kuipatia *helicopter*, tuipatie na boti, tuwapatie wafanyakazi na watendaji wenye uwezo wa kutosha kusimamia shughuli za mazingira, tukiyatimiza hayo hakuna sababu katika nchi hii kuona kuna mtu yeyote anakiuka Sheria za Mazingira, hakuna sababu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majiji yetu yatakuwa masafi kama yalivyo majiji mengine nchi zilizoendelea, hakuna mtu atapigiwa kelele katika mitaa, hakuna uharibifu wa vyanzo vya maji, hakuna changamoto yoyote inaweza itajitokeza. Kwa hiyo, ninataka kuwahakikishia, hayo mambo wanaweza wakaona ni magumu, lakini ni mambo ambayo yanawezekana na yanatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la watumishi tumeanza katika bajeti hii, tumepata vibali vya watumishi zaidi ya 103, si hatua ndogo. Ninajua bado mahitaji ni makubwa lakini si haba! Hata majengo ya ofisi, juzi nilikwenda kutembelea Jengo la *NEMC* – Geita, si ofisi tu ya *NEMC*, ni kituo cha umahiri. Tunataka Ofisi za Kanda zote 13 za *NEMC* ziwe vituo vya kimahiri, kama ilivyo Kituo cha Geita ambayo changamoto iliyopo katika Kituo cha Geita kuhusiana na uchafuzi wa mazingira ya wachimbaji madini wanaotumia zebaki, tunaweka kituo ambacho kitafanya *research* na kutafuta njia mbadala kwa wachimbaji wetu wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa pia ni sehemu ya kuweza kutoa elimu ya madhara ya matumizi ya kemikali hizo zenye athari na afya na mazingira. Kwa hiyo, lengo letu ni kwamba vituo kama kilichokuwepo Geita ambacho tunatarajia kukizindua hivi karibuni, viwe katika Kanda zote. Tukifanikiwa kuifanya *NEMC* ikaweza kusimama kisheria, kitaasisi, tutaweza kuwa na chombo imara kabisa ambacho kitatusaidia sana kabisa, kukabiliana na changamoto ya mazingira ambayo Wabunge mmeipigia kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyenzo yetu nyingine ni Kituo cha kuratibu biashara ya kaboni. Wabunge wamezungumza kwa uchungu na ninakubaliana na wao kwamba, eneo la fursa ya biashara ya kaboni bado hatujalitumia ipasavyo. Bahati nzuri Taifa letu lina fursa nyingi sana ambazo hazijatumika na bahati mbaya ni kwamba fursa hizi hazisimami, kadri ya dunia inavyokwenda mbele, inawezekana, kwa mfano, kama sasa hivi kuna teknolojia za kufyonza hewa ukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikitokea wakati teknolojia hizi zikisambaa, hakutakuwa na mtu anahitaji misitu yako iliyokaa haina kazi yoyote, kwa hiyo ni lazima tuchukue hatua sasa hivi. Nami ninataka kuwapongeza Wabunge, kwenye Bunge la Mwezi Machi mwaka jana, tulipitisha Sheria ya kukitambua rasmi kituo hiki, tunashukuru sana na jambo hilo limesaidia sana. Hata katika bajeti hii, tutafanya kazi kubwa sana ya kukiimarisha kituo chetu na tunataka bishara ya kaboni iwe ni katika vyanzo vitatu vikubwa vya mapato vya nchi, hayo ndiyo malengo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kituo chetu cha *NCMC* Tanzania kiwe kituo cha mfano Afrika. Hayo ndiyo malengo na dhamira yetu tunataka kituo hiki kitengeneze Dola bilioni mbili kwa mwaka. Hayo ndiyo malengo, Wabunge wanaweza wakaona ni malengo ambayo ni *very ambitious*, malengo ambayo ni ya kufikirika, lakini ni malengo ambayo yanawezekana kwa sababu fursa hizo zipo nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini kifanyike ili tuweze kutimiza malengo hayo. Jambo la kwanza nimeeleza kwamba sasa tuna kituo na hata watu wa nchi nyingine wanakuja kujifunza hapa kwa mfumo ambao tumeuanzisha sisi. Jambo la pili ambalo baadhi yao wamezungumza ni kuhakikisha kwamba tunazitumia fursa zote, iwe kwenye misitu, kilimo, taka, madini, miundombinu, usafirishaji na kwenye sekta zote tutumie fursa zilizopo kwenye biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ziko baadhi ya Wilaya wameshaanza kufanya biashara ya kaboni, lakini haturidhiki juu ya utaratibu uliopo sasa. Tunaamini kabisa kwamba tutaweza kupata fedha nyingi zaidi ikiwa tutaimarisha mifumo yetu ya *Registry* na *MRV* kwa ajili ya kuhakikisha biashara hii inakuwa ya uwazi na kwamba bei ya kaboni popote duniani, ndiyo bei hiyo hiyo mwananchi wa kwenye halmashauri yoyote anaipata moja kwa moja. Ndiyo maana tumepata shilingi bilioni tano katika bajeti hii kwa ajili ya kuimarisha mifumo hii. Kwa hiyo sasa, dhuluma kwa wananchi wa nchi hii inakwenda kukoma muda siyo mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kama nilivyoeleza kwenye *NEMC*, *NCMC* inahitaji wataalam, inahitaji *training*, hayo ni miongoni mwa mambo tumeyapa kipaumbele katika bajeti yetu ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, ninaomba uridhie nitoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wameziuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika hoja ambazo ziliwasilishwa ambayo ninaona ni vizuri nikaitolea ufafanuzi, ni kuhusu sekta ya

uchumi wa buluu. Kuna hoja kwamba tumeanzisha Kitengo cha Uchumi wa Buluu mwaka jana kuweza kuratibu na kuwezesha wananchi wanaohitaji kujishughulisha na uchumi wa buluu, wanufaike na uanzishwaji wa kitengo hicho. Hii ilikuwa ni hoja ya Kamati ya kwamba, Kamati inaona kuna haja ya kutuwezesha kituo hicho kifedha na kirasilimali ili kiweze kuwasaidia wananchi wa pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu umepokelewa. Aidha, Serikali zote mbili zimeendelea kushirikiana katika masuala ya uchumi wa buluu na tayari maeneo ya ushirikiano yameainishwa ikiwemo kuandaa miradi ya pamoja na kuandaa *Marine Special Plan*, mpango wa matumizi endelevu ya rasilimali ya maji, elimu kwa umma na mikataba ya kimataifa ambayo itanufaisha wananchi wa pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ninaomba kuwashukuru sana Mawaziri ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Wizara zenye mnasaba na uchumi wa buluu. Hivi karibuni mpango huu sasa unakwenda kupanga mifumo yetu kwa kuanzia ya bahari vyema ili kuepusha mgongano uliopo kati ya sekta moja na sekta nyingine, kwamba tuwe na maeneo tunajua kabisa, haya ni maeneo kwa ajili ya burudani na utalii, haya ni maeneo kwa ajili ya uvuvi, haya ni maeneo kwa ajili ya uchimbaji gesi na mafuta na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huo tumeutengea bajeti mwaka huu kwa mara ya kwanza na tunakwenda kuanza utekelezaji wake, ni hatua moja kubwa sana na ni hatua ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kuhusiana na suala lile ambalo nilisema nitalizungumza baadaye kuhusiana na kushirikiana na Wizara za Elimu kuweka suala la Muungano kwenye mitaala ya elimu na kuweka mashuleni elimu ya Muungano ili udumu vizazi na vizazi. Ushauri huu umepokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, majadiliano baina ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu

masuala ya Muungano kuingizwa kwenye mtaala wa elimu nchini, yanaendelea kufanyika na kwa kuanzisha kitabu cha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar 'Chimbuko, Misingi na Maendeleo', kitabu chenyewe hiki hapa, tutafanya jitihada Waheshimiwa Wabunge wakipate hiki kitabu ni kizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu hiki kimepata ithibati na kitatumika kama kitabu cha ziada katika shule za sekondari Tanzania Bara na Zanzibar. Hivyo, wataalam wanaendelea na utaratibu wa kurudufu kitabu hicho kwa ajili ya kukisambaza pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ninaomba kuitolea ufafanuzi, ni kuhusiana na ujenzi wa Ofisi za Muungano Zanzibar. Ushauri huu umepokelewa, aidha, taasisi 21 kati ya 33 zilizo na ofisi Zanzibar, zina majengo yenye hadhi na ni ya kudumu hivyo Serikali itaendelea kuzihimiza taasisi zilizopanga ofisi kujenga ofisi zao Zanzibar. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, malizia kuhitimisha hoja yako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ufafanuzi mwingine tuweze kuwasilisha kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa kuhitimisha hoja yako na kujibu maswali mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyauliza. Ninaona hoja imeungwa mkono, tutaendelea.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 26 – Ofisi ya Binafsi ya Makamu ya Rais**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..…………………………Sh. 23,297,959,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Fungu hili ndilo linaloshika mshahara wa Waziri na kwa utaratibu Vyama vya Siasa wenyewe wanaleta majina hapa kama kuna hoja mbalimbali Wabunge wanataka ufafanuzi. Kwa vile hatujapokea jina la mtu yeyote na muda umefika karibu na mwisho tunaingia kwenye *guillotine*.

**Fungu 26 – Ofisi ya Binafsi ya Makamu ya Rais**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…...…...…….………Sh. 23,297,959,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Division*…………………….…………...Sh. 7,158,091,600
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…...……..Sh.952,652,400

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*……..Sh. 2,091,335,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*……5,310,073,000
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*……..………………Sh. 825,879,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*…...Sh.1,011,276,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*……………………..Sh. 1,090,441,000
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit*……..………………Sh. 851,764,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*……..Sh. 934,474,000
Kifungu 2001 – *Union Secretariat*……..…………Sh. 4,310,073,073,000
Kifungu 3001 – *Blue Economy Development and Coordination Unit*…………………….Sh. 1,949,621,000
Kifungu 5001 – *Environment*…………………………Sh. 14,904,863,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 31- Ofisi ya Makamu ya Rais - Muungano**

Kifungu1001- *Administration and Human Resources* Division…………………………….……Sh. 3,700,000,000
Kifungu 5001 – *Environment*………………………....Sh. 34,614,845,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Hivyo, ninaomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsanteni. Hoja imeungwa mkono nitawahoji kwa mujibu wa Kanuni kuhusu Hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano ya kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kwa hivyo sasa ninatangaza rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 yamepitishwa na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninatumia fursa hii kwa dhati kabisa kumpongeza Waziri mwenyewe Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Naibu Waziri, timu yenu yote ya Makatibu pamoja na Wakurugenzi wa Mazingira, bila kusahau Kamati zetu za Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Kamati ya Maji na Mazingira, ambazo kwa pamoja zote zimeshirikiana kuchakata bajeti hii au mapendekezo haya ya bajeti na hatimaye leo hii

tumeweza kufika hapa na kuchambua hoja mbalimbali na kufikia hatma hii kwa mujibu wa Kanuni.

Kwa hivyo, ninasema tu, ninawatakia kila la kheri, tunaelewa sote michango yote Mheshimiwa Waziri umeipokea na mengi ambayo Waheshimiwa walikuwa wana kiu nayo umeyajibu kwa njia iliyokuwa chanya *(positively)* na wote wamesikia.

Kuhusiana na mazingira umeongea vizuri, tunashukuru. Kuhusiana na *NEMC* umefafanua zaidi vizuri kuliko ambavyo wametamani Waheshimiwa Wabunge, pia masuala ya Muungano, masuala ya elimu kwa umma umeyafafanua vizuri, ninaamini kwamba yote yatakwenda kufanyiwa kazi na Mwenyezi Mungu atatusaidia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaamini kabisa Muungano wetu kwa heshima kubwa ambayo tumeipata dunia nzima kwa miaka 62 hii ambayo inakaribia hivi sasa, utaendelea kudumu daima kwa amani, utulivu, mshikamano, upendo na umoja. Sasa hivi Waziri umesema hapa tunaondokana na kero, tunaondokana na changamoto tunakwenda kwenye fursa. Fursa ziko nyingi Zanzibar pamoja na udogo wake, tuna fursa nyingi, hata kutembelea Zanzibar ni fursa kwa Watanzania Bara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hivyo tunawakaribisha sana, kwa namna yoyote ile, udugu wetu utaendelea kudumu, udugu hauwezi kuvunjika kwa namna yoyote ile kwa sababu ni mpango wa Mwenyezi Mungu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, basi ninawatakia kila la kheri, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili Asubuhi.

*(Saa 1.43 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 22 Aprili, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*